*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 18 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Migugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu sasa aulize swali lake.

Na. 229

**Tatizo la Shule na Mabweni Kuungua Moto**

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi la mabweni na hata shule kuungua moto, hususan Tanzania Bara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na wimbi la shule kuungua moto na mwaka 2016 pekee kuanzia mwezi Januari hadi Disemba nchi ilikuwa na janga kubwa la kuunguliwa na shule za sekondari 29, zikiwemo mbili zisizo za Serikali na shule za msingi mbili ikiwemo moja isiyo ya Serikali.

Matukio hayo yalitokea mfululizo na hata shule nyingine kukumbwa na tatizo hilo zaidi ya mara moja. Mbaya zaidi, katika mwezi wa Agosti, 2016 kasi ya matukio ya shule kuungua moto iliongezeka ambapo kati ya tarehe Mosi hadi 12 Agosti, 2016 jumla ya shule za sekondari za Serikali tano ziliungua. Tumeshukuru Mungu mwaka 2017 matukio haya ya moto hayajatokea tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hakuna uhakika wa chanzo halisi cha matukio haya moto yanayojitokeza. Hata hivyo, inadhaniwa kuwa chanzo cha moto hususan katika shule kongwe ni hitilafu ya umeme iliyotokana na uchakavu wa miundombinu na hujuma kutoka kwa watu na vikundi visivyo na nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, majanga ya moto katika shule zetu yanaweza kudhibitiwa ikiwa wote kwa pamoja tutashirikiana kutambua na kudhibiti viashiria na vyanzo ambavyo huleta majanga hayo. Serikali imetoa maelekezo kwa Mikoa, Halmashauri na wadau wengine wa elimu ili kudhibiti majanga ya moto mashuleni ikiwa ni pamoja na uundwaji wa Kamati za kukabiliana na majanga katika ngazi ya Halmashauri na katika ngazi za shule husika kwa kushirikisha wadau muhimu wa elimu katika ngazi mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantakaje Juma, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, je, ni vikundi ngapi zilizochukuliwa hatua mpaka sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI….

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ni shule ngapi zilizochukuliwa hatua mpaka sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameonesha *concern* kubwa ya suala zima la janga la moto katika maeneo yetu. Hili nimelisema katika jibu langu la msingi takribani shule 29.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la chanzo nani alisababisha imeonekana maeneo mbalimbali ni hitilafu ya umeme, lakini bado hatujabaini hasa watu mahsusi ambao wameshughulika katika suala la kuhujumu miundombinu hii na ndiyo maana tumeunda Kamati hizi

shirikishi katika jamii zetu hasa katika ngazi za shule, lengo ni kuzuia baadae watu watakapobainika basi tuweze kuwachukulia hatua katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare swali la nyongeza.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri na kwa niaba ya Serikali, kwamba matukio ya moto ambayo yanatokea katika shule, yamekuwa pia yakitokea katika maeneo mbalimbali yakisababisha maafa makubwa. Lakini tatizo kubwa ambalo limeonekana kuchangia maafa kuwa makubwa ni pale ambapo vikosi vyetu vya Zimamoto vinapofika kwenye eneo la tukio na vikishafika pale magari yanaonekana yanakuja tu, labda kuja kutembea yanakuwa hayana maji na wala hawana vifaa, matokeo yake wakati mwingine wamekuwa wakiambulia kipigo au matusi kutoka kwa wananchi wenye hasira kali.

Je, Serikali inasemaje juu ya hili na wamejipangaje kuliondoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kunachangamoto nyingi ambazo panatokea maendeleo na zenyewe zinajitokeza. Kwa mfano, miji inapokua majengo yanapojengwa, kuna maeneo mengine yanakuwa hayajatoa *provision* za magari ya kisasa kuweza kufanya kazi ile ya zimamoto.

Kwa hiyo, sasa hivi tunashirikiana na Wizara zingine zinazohusika ili tuweke *provison* hizo ambazo zitawezesha wenzetu wa zimamoto waweze kufanya hivyo. Lakini pia hilo jambo alilolisema lilishajitokeza maeneo mengi tumechukua hatua kuweza kuhakikisha kwamba, magari yanakuwa yako *standby* na vitendea kazi vyote vinavyotakiwa kwa ajili ya kwenda kuzima moto ili wasije wakafika kwanza halafu

wakajikuta kwamba walikuwa na upungufu wa vitendeakazi vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelizingatia na hata tulivyopitisha kwenye bajeti tulilielezea jinsi ambavyo tunakiunda upya kikosi kile kiweze kuwa na vitendeakazi vinavyostahili kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya aina hiyo aliyoyasema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge kabla sijamuita Mbunge mwingine maswali ya nyongeza naomba sana yawe mafupi kwa sababu Wabunge tuko wengi na kila mtu anaomba nafasi ya maswali. Kwa hiyo, uende moja kwa moja kwenye swali usianze kutoa hadithi ndefu wakati mwenye swali la msingi ameshamaliza. Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini shule za Serikali hawaweki *provision* ya kuwa na *fire extinguisher* ambayo inaweza ikatumika mara tu kama huduma ya kwanza wakati magari ya zimamoto yanaposubiriwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukiangalia kesi hizi za majanga ya moto na siyo shuleni peke yake hata katika maeneo mbalimbali, ni kwa sababu katika kipindi kirefu tulikuwa tumejisahau kuweka *fire extinguisher.* Ndiyo maana sasa tumetoa maelekezo katika shule zetu mbalimbali miongini mwa vitu ambavyo tunatakiwa tuviweke viwe vya msingi ni suala la *fire extinguisher.* Hata hivyo, katika ujenzi wa mabweni yetu, zamani mabweni yalikuwa yakifunguka yanafungukia ndani, hata janga la moto likitokea watoto wanavyogombania kufungua mlango kumbe ndiyo wanazidi kuufunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika suala la *specification* tukasema na mabweni yetu sasa hivi yote milango inafungukia kwa nje ili kwamba inapotokea hatari ya moto basi watoto wakiwa wanatoka mlangoni, iwe ni rahisi sana kuweza katoka katika eneo lile pindi janga la moto linapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni agizo letu na ninaomba niwasihi sana ni waagize Wakurugenzi wote katika Halmashauri zetu kuhakikisha katika maeneo ya shule zetu zote zinakuwa na *fire extinguisher as a back up strategy,* endapo moto unapotokea, wakati unasubiria kupata magari ya kuzima moto yaje, tuwe na mbinu mbadala wa kuweza kudhibiti moto mapema zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali.

Kwa kuwa ukiangalia shule nyingi zilizoungua, chanzo kikuu huwa ni vibatari au mshumaa, hii ni kwa sababu ya kukosekana kwa umeme; kwa kuwa Serikali imeshatoa maelekezo kwamba kila sehemu yenye taasisi kama shule na sehemu nyingine muhimu umeme upite, lakini mpaka leo baadhi ya sehemu wamekosa haki hiyo ya kupelekewa umeme. Je, Serikali inasemaje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba shule zote katika Halmashauri zote kwa nchi nzima tumeshaanza sasa kuchukua *stock taking* kuona shule za msingi na sekondari ambazo zimekamilika ili zipelekewe umeme kupitia mradi wa *REA* ambao umeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie kwamba Halmashauri

zote kwa kutumia nafasi hii, Wakurugenzi wote ambao hawajafanya hivyo niwaagize wafanye hivyo ili mradi utakapofika waweze kupitishiwa umeme haraka sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel swali fupi.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa Mikoa iliyoathirika na tukio hili la uchomaji wa shule za sekondari, waathirika wakubwa ni wanafunzi. Ningependa tu Waziri atufahamishe kwamba ni hatua gani za haraka zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaendelea na masomo badala ya kuziacha shule hizo kwa muda mrefu pasipo kupewa msaada wowote na badala yake ni wananchi ndiyo wanaojitolea na wasamaria wema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa Mikoa ambayo ilipata janga la moto. Tukumbuke kwamba janga hili liliikumba maeneo mbalimbali. Bahati nzuri unafahamu wewe ni mwenyeji wa Mkoa wa Mbeya, shule yetu ya Iyunga, Mbeya kulikuwa na sintofahamu kubwa sana, lakini ni nini tumekifanya katika maeneo mbalimbali. Tulichokifanya kama Serikali si kwamba Serikali ilikuwa inaangalia hivi na kuacha, hapana. Tumefanya harakati maeneo mbalimbali hasa kutumia Halmashauri husika na ngazi Mikoa na Serikali Kuu. Ndiyo maana wanaofahamu kama mashahidi katika Mkoa wa Mbeya, shule ya Iyunga na mimi nilikuwepo *site* moto ule ulivyokuwa umewaka pale, tumefanya kazi kubwa sana shule yote ya Iyunga pale imebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule ya Mpwapwa kwa Mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje nimefika pale *site* hivi sasa

bweni tunamaliza kulipaua. Pia maeneo mbalimbali harakati hizi zinaendelea, lakini tunaenda awamu kwa awamu, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Amina Mollel kwamba Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Arusha bahati nzuri wakati moto unawaka Monduli nilikuwepo pale. Nilienda na nilifanya tathmini hiyo, lengo kubwa ni kwamba tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo sehemu yenye mapungufu yote tutashirikiana na jamii husika kuondoa tatizo hili la watoto wetu ili wasikose maeneo ya kukaa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Kiwengwa sasa aulize swali lake.

Na. 230

**Ukaguzi wa Hesabu za Balozi Nje ya Nchi**

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI** aliuliza:-

Taasisi za Muungano zinafanyiwa ukaguzi na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Je, ni mara ngapi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeshirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukagua Taasisi za Ubalozi zilizoko nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Kiwengwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambapo majukumu ya ofisi hii yameainishwa katika Ibara ya 143(2) ya Katiba hiyo, ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi angalau mara moja

kila mwaka na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali, Bunge na Mahakama. Aidha, majukumu hayo pia yameanishwa katika kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa Balozi unafanyika chini ya Fungu 34, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, kwa kuwa na Ofisi zote za Ubalozi ni sehemu ya Fungu 34. Hivyo basi, ukaguzi wa Balozi kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Muungano unafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar majukumu yake yameanishwa kwenye Ibara ya 112(3) ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kutokana na maelezo hayo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kila moja ina mipaka yake ya kufanya ukaguzi. Jukumu la ukaguzi wa taasisi za Muungano lipo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijawahi kumhusisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ukaguzi wa Balozi au ukaguzi wowote ule kama wa Umoja wa Mataifa kwa sababu hakuna ulazima wa kufanya hivyo kikatiba na kisheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali swali la nyongeza.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa taasisi hizi za Ubalozi ni taasisi za Muungano

je, haoni ipo haja sasa ya kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar katika kukagua taasisi hizo?

Pili, kwa kuwa tuna mahusiano mazuri katika taasisi hizi za Muungano, yeye Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hajaona ulazima; je, haoni sasa imefika wakati wa kushirikiana na kuonesha Muungano wetu huu unadumu na kuondosha kero ndogo ndogo ambazo zinatokezea kama hizi za kutokushirikishana? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali yetu na lengo lake kwa Muungano ni kuudumisha Muungano wetu katika kila nyanja, kama alivyosema Mheshimiwa Rais wetu katika sherehe za Muungano za mwaka huu 2017 kwamba Serikali yetu inaupenda Muungano na tutaulinda kwa ngazi zote na nguvu zote, hiyo itabaki hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo jukumu hili la ukaguzi ni la Kikatiba na Kisheria. Ofisi zote za Muungano hukaguliwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini akiona inafaa Mkaguzi huyu anaweza kumshirikisha Mkaguzi yule. Tuelewe tu kwamba kikatiba na kisheria siyo lazima, lakini kimahusiano anaweza akafanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongezea katika majibu mazuri kabisa yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha, kwamba pamoja na mgawanyo wa majukumu ya kikatiba na kisheria kuhusu mamlaka za ukaguzi maeneo na taasisi zinazopaswa

kukaguliwa, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakaguzi hawa na Wadhibiti Wakuu wa Serikali zote mbili wanashirikiana kwa karibu sana katika kubadilishana uzoefu, pia kujenga uwezo wa kitaasisi hasa kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Zanzibar. Hilo ndilo ambalo tunalihimiza na tunalisisitiza lamahusiano na ushirikiano wa taasisi za pande zote mbili hata katika masuala ambayo siyo ya Muungano.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali swali la nyongeza.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha za Mfuko wa Jimbo hazijawahi kukaguliwa Zanzibar na kwa kuwa hakuna utaratibu wowote kwa sababu Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiwezi kukagua Hazina ya Zanzibar.

Je, fedha za Mfuko huu wa Jimbo zitakaguliwa lini na kwa utaratibu gani? (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ya Mfuko wa Jimbo uko utaratibu kwamba hizi zinazoingia Bara na zile zinazoingia Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, hili kuna utaratibu wa wazi kule Ndugu yangu Mheshimiwa Ngwali nadhani tukifanya *consultation* na wenzetu kutoka Baraza la Wawakilishi tutakuja kuona ni jinsi gani wanafanya kule utaratibu mzima wa usimamizi wa fedha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba Baraza la Wawakilishi litakuwa linafanya kazi yake kwa mujibu wa utaratibu unaotakiwa, ili fedha hizi ziweze kutumiwa kama inavyokusudiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo,

Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi sasa aulize swali lake.

Na. 231

**Haja ya Serikali Kuwekeza katika Michezo Michache**

**MHE. ALLY SALEH ALLY** aliuliza:-

Tanzania imesajili michezo kadhaa ambayo huingia kwenye medani ya Taifa kiushindani lakini kote huwa ni mashamba yanayozaa visingizio.

(a) Je, Serikali haioni haja sasa ya kujipinda katika michezo michache kiushindani Kimataifa?

(b) Je, kama kukiwa na uamuzi huo inaweza kuwa michezo ipi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesajili michezo mbalimbali kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, ili timu au mchezaji aweze kushiriki katika mashindano ya kimataifa kama vile michezo ya *Olympic* na michezo mingine, lazima awe amefikia viwango vilivyowekwa na mashirikisho ya kimataifa. Serikali inatoa mwanya kuibua na kukuzwa kwa vipaji katika michezo mbalimbali bila upendeleo. Suala la kufanya vizuri katika mashindano linategemeana na viwango vya uelewa, mazoezi, mafunzo na uzoefu katika mchezo husika.

Aidha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatoa msaada wa hali na mali kufanikisha timu ama

mchezaji aliyefikia viwango kushiriki michezo ya Kimataifa ikiwa taarifa na taratibu zinazingatiwa tangu ngazi za awali. Kitendo cha kuchagua michezo kadhaa kinaweza kupelekea kupoteza vipaji ambavyo havijavumbuliwa na kukuzwa kufikia kushiriki mashindano kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Serikali itaendelea kuhamasisha michezo yote kupitia vyama vya michezo kwa sababu kila mchezo unaweza kushiriki kiushindani. Hii inasaidia kutoa fursa kwa wanamichezo wenye vipaji tofauti kuweza kushiriki katika michezo ya kimataifa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Mheshimiwa Mbunge ni mazuri kwa maana ya kujikita katika michezo ile ambayo tunadhani itaweza kusaidia Taifa kufanya vizuri katika ushindani kimataifa, hili litawezekana kwa kusaidia timu ama mchezaji aliyefuzu, kwani katika hali halisi huwezi kuamua kuwa huu ndio mchezo unaoweza kufanya vizuri bila kupata viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niseme kuwa kwa sasa bado utaratibu huu hatujaanza kuutumia na kwa hiyo sio rahisi kujua ni michezo gani kwani kila mchezo unaandaliwa kwa kufuata taratibu na viwango husika na matokeo mazuri yanapatikana kwa kuibua na kukuza vipaji. Kwa kuchagua michezo kadhaa tutakatisha tamaa ukuaji wa vipaji katika michezo mingine. Lakini bado iko fursa kama wadau kufanya upembuzi wa kina na kuja na maoni juu ya michezo gani tuipatie kipaumbele kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh Ally swali la nyongeza.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwamba katika hali halisi inavyoonesha kwamba Tanzania haijawahi kuwakilishwa nje ya michezo ya kuogelea, mpira wa miguu,

riadha, ngumi katika ile michezo ambayo huwa inataka *qualifications,* lakini moja ya tatizo kubwa ni *choice* ya michezo yenyewe na pili ni ufadhili wa michezo yenyewe. Mimi siamini kwamba Serikali ndiyo isimamie kufadhili michezo kwa sababu ina-*priority* nyingi.

Je, Waziri haoni kwamba wakati umefika sasa kuja na mwongozo au sera ya namna ya *corporate* Tanzania kuchangia katika michezo? Kwa mfano Uingereza *British lottery* ndiyo inayodhamini *Olympic system* nzima ya Uingereza. *(Makofi)*

Swali la pili, ipo michezo ambayo kwa gharama zake na kwa uenezi wake ni rahisi sana kuenea, mchezo *chess investment* kubwa wanayotaka ni *chess board* ambayo in-*cost* labda dola sita au dola saba, baada ya hapo ni kuwa-*train* tu watoto au vijana.

Je, Serikali inaweza kushaurika kwamba huu ni mmoja kati ya mchezo ambao unaweza kuwa kipaumbele katika Taifa, kwa sababu hauna gharama na kwa sababu unaweza ukaenea katika hali ya haraka katika nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ally Saleh Ally kwa jinsi alivyo mdau mkubwa katika maendeleo ya michezo na amekuwa akichangia sana sana masuala ya michezo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lake la kwamba kuna michezo ambayo haijawahi kuwakilishwa Kimataifa, nitoe mfano tu kwamba kwa mchezo wa kuogelea nchi yetu imeshawahi kuwakilishwa, kuna vijana ambao walishawahi kwenda Canada na wakaiwakilisha nchi yetu, tuliwapa bendera na mmoja alishika namba nne, lakini pia hata riadha, walishawahi kuwakilisha nchi yetu kimataifa na

mmojawapo ni Simbu na anamfahamu. Ndugu Simbu ameshawahi kutuwakilisha Kimataifa na Serikali huwa inatenga bajeti kwa ajili ya hawa, lakini hatua za awali huwa zinafanywa na *Tanzania Olympic Committee* ambapo inawaandaa wale wachezaji na fedha zinatoka *Olympic* Kimataifa na wanapofuzu sasa kushiriki mashindano yale Kimataifa ndipo Serikali inapowawezesha. Mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga fedha na wanariadha wetu waliweza kuiwakilisha Tanzania katika michezo ya *Olympic.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwongozo wa ushiriki wa sekta binafsi tunakubaliana na hilo lakini tunakwenda hasa na sera kwa sababu, sera yetu inatutaka kusimamia michezo sio tu kwa kuegemea kutambulika Kimataifa, tunasimamia michezo kwa madhumini mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuimarisha afya, afya ya Watanzania kwa ujumla, pia kudumisha amani, umoja, mshikamano na upendo, vilevile kuhakikisha kwamba tunatambulika kimataifa kama anavyosema na kumjenga Mtanzania kuwa jasiri, kukabiliana na matatizo mbalimbali. Kwa hiyo, yako masuala ya msingi ambayo yanatupelekea Serikali kusimamia michezo.

Kwa upande wa mchezo anaoupendekeza wa *chess* katika swali lake la pili, tunapenda sana kutoa wito kwa wananchi wote kwa wananchi wote kwamba pale ambapo kuna michezo wanayoiona ni mipya na inafaa kuingizwa katika sekta ya michezo na hasa katika shule za msingi na sekondari, ili wanafunzi wetu waweze kujifunza, tunahimiza kwamba wananchi kama hao, Walimu ambao wanaweza kufundisha michezo hiyo wajitokeze ili waweze kufundisha kwa sababu, Azimio la Michezo la Umoja wa Mataifa la mwaka 1978 linahimiza wananchi wafanye ile michezo wanayoiweza, michezo wanayoipenda, michezo ambayo wana amani nayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Kiwelu swali la nyongeza.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Timu yetu ya Serengeti imeendelea kufanya vizuri huko ilipo, ningependa kujua Serikali imetenga kiasi gani, kwa ajili ya kuisaidia timu yetu hii ili iweze kufanya vizuri na kurudi na kombe hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza sana Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri sana. Ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba timu hii ya Serengeti haijaibuka tu, tumeanza nayo miaka mitatu iliyopita, kwa kushindanisha vijana wa chini ya umri wa miaka kumi na tano, tukapata timu bora, tumeilea hiyo timu na kuhakikisha kwamba inashiriki kwenye mashindano ya kimataifa kabla ya hizi mechi 22 ambayo haijapata kutokea toka historia ya nchi hii, yote hii huu ni uwezeshaji na uwekezaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nisisitize kwamba *figure* kamili yaani ni kiasi gani tumetumia kama Serikali tutaiandaa tumpe Mheshimiwa Mbunge, lakini Serikali imejitoa kwa hali na mali kuhakikisha kwamba timu hii inatuletea ushindi katika mashindano haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Katimba swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii niulize swali la nyongeza.

Kwa niaba ya vijana wote wa Tanzania ambao wanaweza kuwa wanufaika wakubwa sana wa michezo naomba kuuliza swali la nyongeza lifuatalo:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kwamba ni wakati muafaka wa kuwa na shule maalum kwa ajili ya kukuza vipaji katika michezo kama *sports academy*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninampongeza kwa kuwatetea vijana kimichenzo, kama alisikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha bajeti yake ya mwaka 2017/2018 ni kwamba tumedhamiria. Serikali sasa hivi imekwishatenga shule takribani 55 ambazo ziko katika Mikoa yote ya Tanzania, hizi ndizo ambazo tutazichukulia kama ndizo *academy* zetu. Vilevile michezo ya UMISETA, michezo ya UMITASHUMTA itasaidia sana kuibua vipaji, hata hivyo tunashirikiana sana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba michezo inafundishwa katika ngazi zote za elimu tangu awali, sekondari na vyuoni. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maria Kangoye swali la nyongeza.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na kwa niaba ya vijana wa Kitanzania ningependa kujua ni lini Serikali itarudisha programu ya michezo katika shule zetu za sekondari na msingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza katika suala zima la shule hizi, juzi tumezindua michezo ya UMISETA hapa rasmi, bahati nzuri Kitaifa tumezindulia hapa Dodoma, tuna shule zipatazo 55.

Hata hivyo, tumetoa maelekezo maalum kwa Ofisi za Mikoa yote sasa programu ya michezo sasa imeishaanza kurudi mashuleni na tumetoa maelekezo kwamba Maafisa Michezo wote waweze kuwezeshwa katika Mikoa yote na

katika Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba tunaibua vipaji katika michezo ya watoto wa shule za msingi na watoto wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie kwamba Serikali imeshalichukua suala hili na sasa liko katika utekelezaji. Tunawashukuru sana wenzetu wa CocaCola ambao mwaka huu wanafadhili michezo hii ya UMISETA hapa Tanzania, nayo imeishaanza vizuri na tunashukuru sana kwa kweli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fredy swali fupi.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni miongoni mwa watu ambao ni washabiki na wapenzi wa ngoma za asili, pamoja na kwamba wewe ni mpenzi wa ngoma za asili, hata huku Dodoma kuna ngoma za asili zinaitwa Chigogo.

Je, Serikali imejipangaje kuwezesha wale wote ambao wanaanzisha ngoma za asili katika mashindano hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Mawaziri sioni mtu anayetaka kusimama, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali lake liko nje ya michezo, lakini liko ndani ya Wizara yetu ni ngoma za asili.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi wote waendelee kuenzi ngoma za

asili, hata vyombo vya habari tunavihamasisha ili viweze kupiga ngoma za asili katika vipindi vyake kwa zile asilimia 60 za *local content* ambazo zimepewa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri hilo swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa ubunifu, ujasiri na uthubutu kuanzisha mashindano ya ngoma zetu za utamaduni katika Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilivyoanza hili Waheshimiwa Wabunge ilikuwa kwa Wilaya mbili tu, Wilaya ya Rungwe na Kyela sasa imepanuliwa zaidi kuhusisha Mkoa mzima na Mikoa ya jirani. Ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote katika maeneo yenu tusisubiri Serikali ianzishe hayo, hebu tufuate mfano alioutoa Naibu Spika, wote tuanzishe hayo mashindano. Sisi kama Serikali tutasaidia kuboresha hizo ngoma zetu za utamaduni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 232

**Sera ya Elimu ya Mwaka 2014**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Sera ya Elimu ya mwaka 2014 inaeleza wazi kuhusu mitaala na utaratibu wa masomo katika elimu ya msingi (kidato cha kwanza - nne) na inasema watoto wa kidato

cha kwanza – pili watasoma masomo yote ya sayansi na wanapoingia kidato cha tatu watachagua masomo wayatakayo kutokana na uwezo wao.

(a) Je, Waziri alipata wapi mamlaka ya kutangaza kuwa vijana wote wa elimu ya msingi hada kidato cha nne kusoma masomo yote ya sayansi?

(b) Je, kuna utafiti gani uliofanyika na matokeo kuonesha haja ya vijana wote kusoma sayansi yaani kemia na fizikia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Pili kipengele cha 4(1) na 5(f) cha Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1995 inampa Mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Elimu kutangaza jambo lolote lenye maslahi kwa Taifa kutokana na hali halisi iliyopo kwa wakati huo. Kwa sasa kuna haja kubwa ya kuhamasisha ongezeko la wanasayansi kulingana na hali halisi ya mahitaji. Kwa mfano, kuna upunfufu wa walimu wa sayansi na hisabati 24,716, upungufu wa walimu 355 wa masomo ya ufundi katika shule za sekondari za ufundi na mafundi sanifu wa maabara wa shule takribani 10,000. Moja ya jukumu kuu la Waziri ni kuhamasisha wanafunzi katika elimu ikiwa ni pamoja na kuchukua masomo ya sayansi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) taarifa mbalimbali zikiwemo za kimazingira halisi *(evidence based)* zinathibitisha juu ya upungufu wa

wataalam wa sayansi, mfano kwa upande wa afya, ili kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua inatakiwa kina mama hao wahudumiwe na matabibu wenye ujuzi lakini hawapo wa kutosha, Wizara imekuwa ikihamasisha wanafunzi kuchukua masomo ya Sayansi ili kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haijatoa waraka wowote unaowataka wanafunzi wote kusoma masomo ya sayansi, badala yake imejikita katika kuimarisha miundombinu ya maabara, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kupeleka walimu wa sayansi shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa sana na majibu ya Wizara. Suala kwamba tuna wataalam wachache wa sayansi, sikubaliani nalo kwa sababu hivi karibuni tu Mheshimiwa Rais alikuwa ameishatoa kibali madaktari wetu 500 kwenda kufanya kazi nchini Kenya. Vilevile tunatambua kwamba kuna manesi wengi wako mitaani hawajaajiriwa kwa sababu ya kukosa vibali.

Mheshimiwa Naib Spika, kwa hiyo, swali langu la msingi ninataka kuuliza ni kwamba ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri alitoa tamko na mimi nashukuru kwamba umesema waraka bado haujatoa na ninajua kwamba *government moves with papers*. Kwa kuwa masomo ya sayansi najua ni muhimu sana na kwa kuwa kwa bajeti ya mwaka huu ukiangalia tuna upungufu wa maabara nyingi sana, vilevile ili kumfanya mtoto asome sayansi inabidi kuwe na madarasa mazuri. Kwa mwaka huu tuna upungufu wa madarasa 158,000 na Serikali imesema inaweza ikajenga madarasa 2,000, hii ina maana itachukua miaka 79 kuweza kukamilisha hayo madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama lengo la Serikali ni kufanya watoto wetu wasome sayansi, nini mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanajenga mazingira mazuri na sio tu kutoa matamko wanafunzi wasome sayansi?

Swali la pili, kwa kuwa tunatambua kwamba nchi hii haihitaji tu wanasayansi bali pia inahitaji wengine, kwa mfano mameneja wanahitajika watu waliosoma, *lawyers* kama Mheshimiwa Naibu Spika na wengine, ni kwa nini sasa Serikali isihamasishe pia wanafunzi wasome masomo mengine kwa bidii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara yetu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ieleweke bajeti zote za Wizara zinapitishwa na Bunge lako Tukufu na Bunge hili linao uwezo mkubwa sana wa kusema jambo hili lipewe kipaumbele au jambo hili lisubiri kidogo, kama ambavyo tumeona kwenye Wizara ya Maji wote kwa pamoja tumesema iongezewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikijitahidi sana kuhakikisha inatafuta wafadhili kila kona ya dunia kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo hilo. Mfano ni madarasa ambayo yamejengwa mwaka huu zaidi ya madarasa 2,000, vyoo tulivyojenga na hali hiyo itaendelea kufanyika hivyo. Pamoja na kwamba kwa upande wako Mheshinimwa Waziri Kivuli unaona hakuna upungufu wa wanasayansi, nataka nikuhakikishie kutokana na mikakati ya Serikali ya kutaka uchumi uwe uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda unaendeshwa na sekta tofauti tofauti, kwenye kiwanda utahitaji watu wa afya, kwenye kiwanda utahitaji watu wa ujuzi wa ufundi, kwenye kiwanda utahitaji mambo mengi, lakini hali kadhalika kwenye sehemu zetu za

kuhudumia afya zinahitaji wataalam wa aina hiyo. Kwa hiyo, ukiangalia kwa mapana yake huwezi ku-*plan* kwa kuangalia leo unaangalia kwa mapana, sisi tunaona iko haja kubwa sana ya wanafunzi wetu kuchukua masomo ya sayansi kwa wingi zaidi ili kukidhi maeneo ambayo bado yana upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni pamoja na hiyo ya kusema kwamba tunatamka tamka, niseme tu kwamba suala siyo kutamka, unapohamasisha lugha unayotumia ni yoyote inayowezeshwa kutoa hamasa kwa wale vijana na wakafanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani swali la pili la nyongeza yako naomba limenitoka kidogo, kama unaweza ukarudia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uzime *microphone* yako ili aweze kuzungumza. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba labda awe pia anaandika wakati mtu anauliza ili isimletee shida. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili niliuliza kwamba kwa sababu nchi hii nadhani pia ameshalijibu amechanganya kwamba kwa sababu tunahitaji wataalamu mbalimbali ni kwa nini pia Serikali isihamasishe masomo mengine, kwa sababu hatuhitaji tu wanasayansi tunahitaji *variety* ya watu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi mbali ya hayo niliyomjibu ninayo ya kumuongezea na nilikuwa nataka nijue kama na wewe bado unakumbuka swali lako vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanafunzi katika maeneo mengine Wizara yetu haijajikita kwenye sayansi peke yake. Kwa mfano sasa hivi tunaendelea kuona namna

ambavyo tunaweza hata tukaingiza somo la kuwezesha wanafunzi katika masuala ya moyo *(mindset)*. Unakuta mtu anao uwezo wa kufanya jambo lakini kwa sababu tu kimoyo hajawa tayari anashindwa hata kusoma. Kwa hiyo, kuna masomo mengi pamoja na hilo, lakini haya ya sayansi tumeyapa kipaumbele kutokana na uhaba wake mkubwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata taabu kidogo maana yake na mimi ni mwalimu, iwapo Serikali tutaacha kwenda kwenye *specialization* na tukafanya watoto wote wakasoma sayansi. Mimi nina wasiwasi kwamba tutapata wanasayansi wabovu zaidi.

Je, Serikali haioni kwamba *specialization* ni *important* kuliko ambavyo sasa tunakwenda kumfanya kila mtoto asome sayansi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *specialization* inaanza na msingi na niseme tu kwamba tunawahitaji wataalam wa aina tofauti tofauti. Kuna hao *specialization* ambao wanakuwa wamekuwa *vertical* yaani anajikita katika eneo moja pia tunawahitaji wale ambao wanakua kimapana *(wide knowledgeable people)* ambao wanaweza wakaoanisha upande huu na upande huu. Kwa hiyo, katika ku-*specialize* kupo lakini lazima kuwe na msingi ni wa eneo gani ambalo huyu mtu atafanya *specialization*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari swali la nyongeza.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Swali langu lilitaka kufanana kidogo na Mama Anne Kilango na nikichukulia mwenyewe kuwa mfano, lakini kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekwishajibu labda nilisogeze mbele kidogo kwamba kama kweli lengo letu ni kuongeza idadi ya wanasayansi kwenye nchi hii na hususan walimu wa masomo ya sayansi kwenye shule zetu, ni kwa nini basi ile Programu ya Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali ya Chama hiki cha Mapinduzi ambayo ilianzisha *program* maalum kwa ajili ya watoto, Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kutengeneza walimu wengi wa sayansi kwenye nchi hii, ni kwa nini basi watoto wale walifukuzwa mwaka jana tena kwa polisi na mbwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TAKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wale hawakufukuzwa kwa sababu wako kwenye vyuo kumi ambavyo wanaendelea na masomo yao na bado Serikali inaendelea kuwalipia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lilikuwa linafanana kabisa na swali la Mheshimiwa Anne Kilango, amekwishauliza sidhani kama naweza kuendelea kuuliza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu imerithi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kutoka Wizaraya Afya. Je, kwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msaginya kilichoko Jimbo la Nsimbo, Mkoa wa Katavi, kuna mkandarasi miaka miwili amesimama kazi anaidai Serikali. Je, Serikali ina mpango gani wa kumlipa ili kukamilisha ukarabati wa majengo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mkandarasi anadai, kimsingi kama ambavyo mnafahamu vyuo hivi vimeletwa kwenye Wizara yetu katika kipindi cha mwaka huu wa fedha unaoishia. Tunachofanya ni kwanza kuvitembelea na kuweza kuviangalia viko katika hali gani, kama kuna Mkandarasi alikuwa anafanya kazi eneo hilo na hakulipwa, Wizara tunao wajibu wa kumlipa lakini baada ya kufanya uhakiki na kujua kwamba kazi aliyoifanya inafanana na uhalisia na aweze kulipwa kwa kadri ya kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando sasa aulize swali lake.

Na. 233

**Mkataba wa Ushirikiano baina ya Tanzania na Cuba katika Sekta ya Afya**

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI** aliuliza:-

Moja kati ya maeneo yaliyomo kwenye mkataba wa ushirikiano baina ya Tanzania na Cuba (1986) ni pamoja na kuimarisha sekta ya afya.

Je, ni kwa kiasi gani Tanzania imefaidika na utekelezaji wa mkataba huo katika sekta ya afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Jimbo la Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishirikiana na Serikali ya Cuba katika mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya afya tangu 1986, ambapo mkataba ulisainiwa kati ya Serikali hizi mbili. Kupitia mkataba huo, Serikali ya Tanzania imekuwa ikipokea Madaktari Bingwa kutoka Cuba ambao wamekuwa wakifanyakazi katika hospitali za Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya, Hospitali ya Tumbi na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari hawa wamekuwa wakitoa huduma mbalimbali za Kibingwa kwa wananchi na kuwajengea uwezo madaktari wanaofanya nao kazi katika hospitali hizo. Aidha, kwa kushirikiana na kampuni ya *Labiofarm* ya Cuba, Serikali imeweza kujenga kiwanda cha kutengeneza viuadudu vya kibaiolojia yaani *biolarvicides* kwa ajili ya kuua viluilui vya mbu waenezao malaria. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iligharamia ujenzi wa kiwanda hicho na Serikali ya Cuba ilitoa msaada wa wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio yetu ni kuwa, wataalamu hao watawajengea uwezo Watanzania ili waweze kutengeneza bidhaa hizo bila kutegemea wataalam kutoka nje ya nchi kwa siku zijazo. Viuadudu hivyo vimeanza kutengenezwa kuanzia mwezi Disemba 2016, na kwa sasa uhamasishaji wa Halmashauri mbalimbali nchini kununua bidhaa hizo umeanza. Endapo viuadudu hivyo vitatumiwa vizuri vitasaidia kupunguza mbu waenezao malaria na hivyo kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Othman swali la nyongeza.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswala mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, pamoja na kuhamasishwa Halmashauri mbalimbali kununua dawa hizi zinazotengenezwa na kiwanda hiki, Wizara ya Afya ni mteja mkuu ambaye alitegemewa kununua dawa hii inayozalishwa na kiwanda hicho, lakini wameshindwa kutokana na kukosa pesa, jambo ambalo limepelekea kiwanda kutafuta wateja kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Naibu Waziri atueleze hapa imekuwaje Wizara kutokutenga pesa kwa ajili ya kuwanusuru Watanzania ambao wanasumbuliwa na ugonjwa huu wa malaria hapa nchini?

Swali la pili,kwa sababu teknolojia hii ya kuzalisha viuadudu vya kuulia viluilui vya mbu ni mpya hapa Tanzania na Bara zima la Afrika, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza ni maeneo gani katika Jamhuri yetu ya Tanzania wamewahi kuchukua angalau sampuli ya kiwanda kile na kuweza kuifanyia majaribio ili kuweza kujua ubora wa dawa hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba arudie swali la pili walikuwa wanapiga makofi, sikumsikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Othman Haji naomba urudie swali lako la pili.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwa sababu teknolojia hii ya kuzalisha viuadudu vya kuulia viluilui vya mbu wanaoeneza malaria ni mpya hapa Tanzania na Bara zima la la Afrika.

Je, Wizara imewahi angalau kwenda kuchukua sampuli kule kiwandani na kuweza kuifanyia majaribio na kuweza kujua ubora wa hii dawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nitaanza na swali la pili kwamba je, Wizara imewahi kwenda kuchukua *sample* kwenye kiwanda kile na kuzifanyia utafiti?

Kwanza naomba nimhakikishie kwamba teknolojia ya *biolarvicides* kuingia hapa nchini na kukubalika kutumika kuna mchakato mrefu wa kisayansi ambao umefuatwa.

Kwa hivyo, katika hatua hii ambapo inazalishwa kwa wingi wala hakuna haja ya kufanya utafiti wa majaribio, kwa sababu pale mwanzoni wakati ugunduzi wa teknolojia unafanyika zilifanyika tafiti ambazo kisayansi zinajulikana kama *clinical tries* za kubaini *efficacy* ya *biolarvicide* ambayo inatumika lakini pia kubaini kama kuna *any emergency ya resistance* yaani usugu dhidi ya *biolarvicide* yenyewe ambayo inatumika na hatimaye ikafikiwa kuthibitishwa kwamba ni teknolojia ambayo ni *effective.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano walipoanza kufanya tafiti hizi miaka hiyo ya zamani walitumia *bacteria* ambaye anajulikana kama *bacillus sphaericus* katika hatua za awali mpaka wakafikia mwisho wakakamilisha uchunguzi na ikaonekana kwamba *bacillus sphaericus* ana-*develop resistance* kiurahisi sana, wakahama wakaweka *bacillus thuringiensis vara israelensis* ambayo ni *second generation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumuweka huyu *bacillus* wa aina ya pili yaani kwa kifupi *BTI* ikaonekana kwamba yeye ni *effective* zaidi kuliko yule wa kwanza. Kwa hivyo, ikaonekana kwamba sasa tutumie *generaly BTI* kwa ajili ya *biolarvicide.* Kwa hivyo ni teknolojia ambayo

imethibitishwa na haina shaka, na sisi Tanzania tunapaswa kujivuna kwa kuwa tuna kiwanda hicho hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kiwanda kile kitazalisha *full capacity* yake *biolarvicides* lita milioni sita. Malengo hasa ya kuanzisha kiwanda kile sio kwa ajili ya Tanzania peke yake, ni kwa ajili ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika na dunia ambazo zitakuja kununua *biolarvicide* hapa nchini. Kwa mfano mpaka sasa tayari tuna nchi za Serbia, tuna nchi ya Cuba, yenyewe tuna nchi za Sweden, tuna nchi ya Niger ambazo zimenunua *biolarvicide* kutoka Tanzania, kwa sababu kuanzia hiyo mwezi Desemba, 2016 mpaka sasa tumezalisha lita milioni mbili na tumeuza kwenye hizo nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hapa Tanzania Halmashauri takribani tano zimeonesha nia ya kununua, Halmashauri mbili zimekwisha nunua japokua kwa kiasi kidogo na zimekwishatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwapongeze Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ambao wao walikuwa ni wa kwanza kwa Halmashauri za hapa nchini kununua *biolarvicide.* Kwa hiyo swali lake la msingi linasema kwamba Wizara ya Afya tungepaswa tununue si sahihi kwa sababu malengo ni sisi kuwezesha kiwanda kile kuwepo na baada ya hapo Halmashauri ziweke kwenye bajeti zao wao wenyewe waweze kununua pale kadri ambavyo wanahitaji. Ndiyo maana tunaendelea na uhamasishaji wa Halmashauri zote nchini kununua *biolarvicide* kwa ajili ya *control* ya malaria.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu hayo bado mna maswali. Mheshimiwa Antony Komu swali la nyongeza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa ugonjwa wa malaria ni ugonjwa ambao

unaongoza kwa kuua katika nchi hii na ninaamini kwamba Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kupambana na malaria. Ni kwa nini Waziri asione kuna umuhimu wa fedha zote ambazo zimetengwa kwa ajili ya kupambana na malaria zikapelekwa kwenda kununua dawa za viuadudu Kibaha ili kupambana na malaria ikizingatiwa hicho kiwanda sasa hivi kimesimama kuzalisha kwa sababu ya kukosa soko la bidhaa zake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kwa nini tusichukue fedha zote tukapeleka kwa ajili ya kununua *biolarvicide* pale Kibaha kwa ajili ya Halmashauri zetu nchini. Hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu udhibiti wa malaria siyo kuua *larva* peke yake tunamu-*attack* adui mbu katika hatua nyingi tofauti tofauti, lakini pia tunamu-*attack* kile kijidudu chenyewe ambacho kinaambukiza malaria yaani p*lasmodium falciparum* katika hatua nyingi tofauti. Kwa hivyo, mikakati ni mingi ambayo inamlenga adui mmoja kwamba yule *vector* ambaye ni mbu *either* wa aina ya *anopheles* ama tunamu-*attack plasmodium* mwenyewe akiishaingia kwenye damu ndiyo *control* inakuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hatuwezi kutumia njia moja kumu-*attack* adui kwamba tunaua tu mazalia yaani *larvae* halafu tunasema basi ndiyo tumemaliza, hapana! Lazima kuwe kuna tiba. Kwa hiyo, ndiyo maana tuna mkakati wa kusambaza *ALU (Artemether* na *Lumefantrine combination)* nchi nzima na tunagawa bure ili tuue *plasmodium falciparum* ambaye yumo kwenye damu. Ndiyo maana tuna mkakati wa wajawazito, tunatumia *SP (Sulfadoxine Pyrimethamine)* kwa ajili ya kumuua mdudu mbu ambaye anawa-*attack* akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tuna *net* kwa ajili ya kuzuia mbu ambao wanapenda kuishi ndani ya nyumba na wanauma saa sita usiku kuambukiza malaria. Sasa tuna mikakati mingi, tunatumia *IRS – Indoor Residual*

*Spraying* kwa ajili ya kumu-*attack* mbu ambaye anapenda kubaki ndani ya nyumba, mchana hatoki nje anabaki ndani ili asiwepo. Kuna mikakati ya kumuua mbu kama atakuwa nje kwenye mzingira. Sasa hii ya kwenye mazingira ndiyo tunaona teknolojia hii mpya ya *biolarvicides* itatusaidia. Vinginevyo tungetumia *DDT. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushirikiano mzuri wa ndugu zetu hawa wa Cuba katika mambo ya tiba Tanzania, kwa kule Zanzibar ndugu zetu hawa walikuwa na programu maalum ya kuwafunza vijana wetu Udaktari na kwa kweli tayari sasa hivi *intake* mbili zimeshatoka, moja madaktari wanaendelea na kazi zao na wengine wako katika *internship* sasa hivi. Kwa kweli inaonekana kwamba wana mafanikio makubwa.

Je, kwa hapa Tanzania Bara programu hii imeanzishwa au imeshafikiriwa kuanzishwa kwa kuwatumia hawa ndugu zetu wa Cuba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza Cuba ni marafiki wa kihistoria wa Tanzania. *Comradeship* iliyotengenezwa na Fidel Castro na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni ya muda mrefu na imezaa matunda mengi katika nchi zote mbili, zaidi sisi tukiwa wafaidika kuliko wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushirikiano huo, Watanzania wengi, hususan kwenye fani hii ya afya wamepelekwa Cuba kwa ajili ya masomo na wamesoma

masomo ya ubingwa lakini pia katika nyakati mbalimbali hata wanajeshi wetu ambao wanahusika na mambo ya tiba na uokoaji pia wamepelekwa Cuba kwa ajili ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1986 ikaonekana kwamba isitoshe tu kuwa na *exchange* ya Watanzania kwenda kufundishwa kule Cuba mambo ya afya, ikaonekana kwamba tusaini mkataba mwingine ili waje hapa hapa watujengee uwezo. Kwa hivyo, harakati za kujenga uwezo zimekuwa zikifanyika kila mahali ambako madaktari wa Cuba wamekuwepo, pia wamekuwa wakifundisha katika vyuo vyetu hapa nchini, hivyo hata kwa Tanzania Bara tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza hapa, tuna Madaktari Bingwa kumi na moja wanaotokea Cuba ambao wapo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Natambua Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla wewe ni mtaalam na unafahamu kabisa kwamba katika *prevention* za malaria kuna *primary prevention* na kuna *secondary prevention,* nashukuru umeelezea vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri kiwanda cha viuadudu kama tutaweza kufanikiwa, dawa ikasambaa vya kutosha tuka-*control* wale *vector* kwenye hiyo *level* ya wale wadudu kutafuna *larva,* huoni kwamba tutakuwa tume-*eradicate* kabisa malaria na ni wajibu wa kila Hamashauri kununua zile dawa ili kusudi kile kiwanda kifufuke na tuweze kuzuia malaria? Ahsante sana.

**NAIBU SIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Anachokisema ni sahihi kabisa, tukitumia hii teknolojia ya *biolarvicides effectively* tunaweza tuka-*control* malaria na hatimae kuidhibiti kabisa katika muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukawa tupo *constrained* kibajeti na nadhani mkakati wetu kama nchi siyo kwa Wizara ya Afya kununua na kusambaza nchi nzima kwasababu majukumu yetu sisi kwakweli ni *prevention,* lakini pia tiba na mambo mengine na tuna *support* kwa kupitia pesa tunazozipata kutoka kwa wabia wa *PMI* pamoja na *Global Fund.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana hili suala la *biolarvicides* tunawahamasisha Halmashauri zote nchini kwa kutumia mapato yao ya ndani washiriki kwa kutenga pesa kwa ajili ya kununua hizi *biolarvicides* na kuzisambaza na kuzitumia kwenye maeneo yao. Sisi kama Wizara ya Afya tumekwishakutengeneza mwongozo wa namna ya wao kutumia teknolojia hii ku-*control* hawa *bio larvae* kwa kutumia *biolarvicides* katika maeneo yao. Kwa hivyo, sisi kazi yetu ni hiyo tu, kutoa mwongozo na tumekwishatoa. Sasa Halamshauri zote *including* Halmashauri ya Maswa mnunue. Wenzenu wa Kondoa wameshaweka *order,* wenzenu wa Songwe, Namtumbo, Mbogwe na Geita pia wameweka *order.*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo Halmashauri nyingine na ninyi mhamasishe kwa kutumia mapato yenu ya ndani muweze kununua *biolarvicides* kwa ajili ya *control* ya malaria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninayo matangazo machache hapa.

Tangazo la kwanza linahusu wageni, tunae mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Bulembo ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini ambalo sasa hivi ni

Wilaya ya Butiama na huyu ni Balozi Paulo Ndobo, karibu sana Mheshimiwa Balozi. *(Makofi)*

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu na wanafunzi, tunaamini mnaweza kujifunza kutoka hapa Bungeni mambo kadhaa na namna tunavyofanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Kepteni wa *volleyball* kwa wanaume Mheshimiwa Cecil Mwambe anawatangazia kwamba wachezaji wa *volleyball* kwa upande wa wanawake na wanaume wajiandikishe leo kwa ajili ya kuanza mipango ya mazoezi.

Waheshimiwa Wabunge, na hili nisisitize Wabunge wengi hapa mlisimama kwenye swali la michezo na wengine hata hamfanyi mazoezi popote lakini mlisimama kutaka kuuliza swali kwenye michezo. Sasa niwakumbushe tu, mlishasisitizwa hapa na Mheshimiwa Spika kwamba mfanye mazoezi, kwa hiyo nawakumbusha. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, lingine na la mwisho ni kuhusu maswali ya nyongeza. Kanuni zetu zinataka Waziri anapoulizwa swali ajibu swali kikamilifu, lakini Wabunge tunatakiwa kumpa fursa hiyo ya kujibu maswali kikamilifu kwa kukuuliza maswali yanayotokana na swali la msingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakipa Kiti wakati mgumu kumzuia Waziri kujibu swali kwanza kwa sababu kipindi hicho wapiga kura wenu wanakuwa wanaangalia. Kwa hiyo, kuna mawili *either* Kiti kikuzuie wewe unayeuliza swali na kiseme hilo swali halitokani na swali la msingi, kwa hiyo, achaguliwe mtu mwingine au kikusikilize halafu kimzuie Waziri kujibu hilo swali.

Sasa kwa sababu Kanuni zetu zinataka maswali yajibiwe kikamilifu basi Waheshimiwa Wabunge tutoe fursa hiyo kwa Serikali kutoa majibu kikamilifu kwa kuuliza maswali

ya nyongeza yanayotokana na maswali ya msingi. Ukitoka nje ya swali la msingi unaipungukia Kanuni yetu kwa sababu sasa huwezi kupewa majibu yanayotosheleza kwa kuwa Waziri atakuwa hajajipanga kujibu swali la namna hiyo kwa siku hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimewakumbusha ikitokea siku Mbunge ameambiwa swali lako haliendani na swali la msingi asijisikie vibaya ama Waziri akazuiwa kujibu hilo swali kwa sababu halitokani na swali la msingi basi Mheshimiwa Mbunge asijisikie vibaya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa anayetaka kuahirisha shughuli za Bunge. *(Kicheko)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1), (2) na kuendelea naomba nisisome, nisome ya kwanza; baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimuandikia Spika wa Bunge kuhusu tatizo la tembo Serengeti. Sasa hivi Wilaya yangu ina njaa kweli, wananchi wamelima mazao, yanakaribia kuvunwa, lakini mazao hayo yanashambuliwa na tembo kwa wingi makundi mengi kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila ninapomwambia Waziri wa Maliasili na Utalii hawana msaada wowote katika Wilaya

yangu ya Serengeti, hata kutupa tu lita moja ya mafuta hakuna! Tunasumbuka sisi Halmashauri kwa mapato ya ndani tunayoyapata kwenye minada, kwenye masoko.

Sasa ninaomba kutoa hoja kwamba shughuli za Bunge ziahirishwe kwa dakika kumi ili tujadili suala hili hapa ili tuweze kupata muafaka wa jambo hili la tembo ndani ya Wilaya ya Serengeti. Wananchi wangu wana njaa, wana matatizo makubwa, lakini Wizara hii huyu Waziri hawasikilizi kabisa. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja haitolewi kwa namna hiyo ya kutumia Kanuni ya 47. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba ukae, Waheshimiwa Wabunge halafu... sawa, naomba tufuate utaratibu tuliouweka kwenye Kanuni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Cecil Mwambe.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naombwa Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68, sitaisoma. Ninafahamu kwamba Tanzania ni Jamhuri iliyoundwa kwa kuunganisha Zanzibar pamoja na Tanzania Bara, Tanganyika wakati huo, lakini kuna mikoa zaidi ya 35 ndiyo inayofanya kuitwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kupata Mwongozo wako ili Waziri wa Fedha atueleze ni kwa nini unapoleta mzigo kutoka nchi za nje kupitia *border* ya Namanga kuleta Dar es Salaam haulipi kodi ya ziada, lakini unapoleta mzigo kutokea Zanzibar kuleta Dar es Salaam ambapo ni Mkoa wa Tanzania unatakiwa kulipa kiasi cha ziada? Hii inatuletea mkanganyiko mkubwa sana Watanzania. Tunaomba ufafanuzi wako. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Cecil Mwambe, kwa mujibu wa Kanuni 68(7) akitoa maelezo ambayo wote tumemsikia kuhusu kudaiwa kodi kwa vitu vinavyotoka Zanzibar kuingia Dar es Salaam ama kuingia Tanzana Bara. Ametoa maelezo yake kwamba nchi yetu kama ambavyo ina majirani wengi, vitu vikitoka nchi hizo vinafananishwa kana kwamba vinatoka nje ya Tanzania na kwa hivyo vinavyotoka Zanzibar na sisi tuna Muungano ni kana kwamba na vyenyewe vinatoka nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, suala hilo halijatokea hapa Bungeni. Kwa hiyo, Kiti hakitoi Mwongozo wowote kuhusu jambo hilo na ushauri tu kwa Mheshimiwa Cecil Mwambe hili jambo lilishaulizwa mara nyingi sana hapa ndani na kama majibu yanayotolewa na Serikali hayaridhishi basi ufuate utaratibu mwingine ambao utakupa wewe fursa ya kuweza kulifanya hili jambo kwa utashi unaopaswa pia kwa kufuata Kanuni zetu. Kwa hiyo, Kiti hakina Mwongozo juu ya jambo hili lililoombwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Mheshimiwa Marwa Chacha ametoa hoja ya kuahirisha Bunge na ametumia Kanuni ya 47. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kuna wengine mnazungumza ndiyo maana wakati wa kutumia hizi Kanuni tunarudia makosa yale yale kila wakati. Hoja ya Kuahirisha Bunge iko Kanuni ya 69.

Waheshimiwa Wabunge, Hoja ya Kuahirisha Bunge iko Kanuni ya 69. Kanuni ya 47 inazungumzia kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura na Mheshimiwa Chacha Marwa ametoa hoja yake akisema kwamba kuna jambo ambalo kwake yeye anasema ni la dharura, tembo wameingia katika Jimbo lake na Serengeti tunafahamu wote kwamba kuna mbuga yetu inayoitwa Serengeti, kwa hiyo Jimbo lake liko karibu sana na eneo hili na tembo hawa

wanakula mazao ya wananchi. Kwa hiyo, kwa maelezo aliyoyatoa anasema kuna njaa Serengeti kwa sababu tembo wanakula ama wamekula mazao ya wananchi kwa hiyo wamesababisha njaa. Kwa hivyo, nilimsihi asitoe hoja kwanza kwa kuwa Kanuni zetu zinataka mimi kwanza nimpe fursa ya kutoa hoja ikiwa nimeridhika kama hilo jambo ni la dharura ama hapana.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili la tembo kuwa maeneo mbalimbali ambayo wapo wananchi lipo nasi siku zote kwa sababu tembo wapo na wananchi wapo. Kwa hiyo, Wizara huwa inajibu mara nyingi hapa ndani kuonesha namna ambavyo kila mahali linapotokea tatizo inabidi likashughulikiwe wakati huo. Hapa juzi tu tumesikia kuna tembo walikuwa Chuo cha Dodoma na wataalam watoa maelezo kwamba pengine yale yalikuwa ni mapitio ya tembo kwa hiyo tembo wamekumbuka njia yao.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47 huwa inapaswa kusomwa na Kanuni ya 48, kwa sababu 47 ndiyo inayoruhusu kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura lakini 48 inasema masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura. Sasa jambo la dharura ili sisi tuweze kuahirisha shughuli zingine tujadili jambo hilo ni lile ambalo haliwezi kufanyiwa kazi kwa namna iliyo ya kawaida. Sasa hili la tembo kuingia Serengeti lina uwezo wa kushughulikiwa kwa taratibu zilizopo. Kwa hivyo, hatutaahirisha Bunge kwa ajili ya kujadili hoja ya Mheshimiwa Chacha Marwa.

Baada ya kusema hayo, nimetaarifiwa kwamba kuna Mheshimiwa mwingine alisimama kwa ajili ya Mwongozo, huo utakuwa ni Mwongozo wa mwisho halafu tutaendelea. Mheshimiwa Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa ruhusa yako kwa sababu Serikali iko hapa isikie kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumesikia suala la kuhusu ugonjwa wa Ebola na huu ugonjwa umethibitika kuwepo nchi ya Congo, nchi ya Congo na ukanda wa kwetu *Lake Tanganyika* na Jimbo la Kavuu kumekuwa na maingiliano wa watu ya kila siku. Naiomba Serikali iangalie ni namna gani itatoa udhibiti na kuelimisha wananchi wanaoingia ukanda ule ili kudhibiti ugonjwa huu, kwa sababu ni hatari sana kuliko UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wetu wa mwisho umetoka kwa Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe akitoa maelezo ambayo wote tumemsikia, hayahitaji Mwongozo wowote wa Kiti. Kwa hiyo, kama yeye alivyoomba kwamba Serikali imsikie, basi imekwisha kumsikia na nadhani Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi hilo jambo. Kwa hiyo, Kiti kwenye jambo hili hakina Mwongozo wowote.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na majadiliano ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Vyama mbalimbali kwa uwiano wao, kwa hiyo tutaanza na orodha kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa

Venance Mwamoto atafuatiwa na Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kupongeza Wizara hii kwa jinsi ambavyo kwa kweli wameandika vizuri, kama tungelipata muda mrefu wa kuweza kusoma hiki kitabu, nafikiri michango yetu ingepungua kwa sababu kimeandikwa vizuri sana na maeneo yote yameguswa, na ukisoma unaona kweli Serikali imedhamilia kutuingiza kwenye uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo leo kazi yangu kubwa hasa ni kushauri, lakini kabla sijaanza kushauri pia niipongeze Serikali jana nilitoa taarifa hapa kwa Waziri wa Kilimo kwamba kuna paka ameingia kule Ilula, amejeruhi zaidi ya watu saba na alikuwa anajeruhi sehemu ambazo anazijua yeye, jana timu imetumwa na kazi imefanyika, kwa hiyo, naipongeza hii Serikali kweli hapa kazi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mimi nitaenda kwenye ushauri, ukiangalia dhana nzima ya Serikali yetu tumejikita kwenye uchumi wa viwanda, walioteuliwa wataalamu kwenda kwenye Wizara ile wote ni makini, lakini kitu ambacho ninaomba ni kimoja nitatoa mfano, Wahehe mimi natoka Iringa, Mhehe na Mgogo, Mhehe akiongea Kihehe, Mgogo anaelewa na Mgogo akiongea Kigogo, Mhehe anamuelewa, tatizo linakuwa Mhehe anapotaka kuongea Kigogo na Mgogo anataka kuongea Kihehe wanapotea njia. Maana yangu ni nini, mwanasiasa ninyi wataalam wa Wizara hii ongeeni kitaalam, msianze kwenda kwenye siasa mkiongea kitaalam sisi wanasiasa tutajua mnachozungumza na sisi wanasiasa hatuwezi kuingilia kwenye utaalam wenu tutaongea kisiasa mtatuelewa, lakini tatizo linakuja pamoja na mipango mizuri tukiingiza siasa mtataka kuwa wanasiasa, mkiashaingiza siasa mipango yote mizuri itaaribika.

Kwa hiyo, naomba mjikite Mheshimiwa Mwijage nakufahamu vizuri, ulipokuwa unasoma Tosamaganga ulikuwa unaitwa kijiko cha jikoni hakiogopi moto, sasa huo moto wako kweli upeleke. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga viwanda, mwanzo ni ujenzi wa viwanda, unapojenga viwanda kuna vitu ambavyo unatakiwa uwe navyo ni pamoja na malighafi. Watu wa Mchuchuma ndugu yangu pale amezungumza sana tunajenga viwanda tumejitayarisha? Sasa ilikuwa ni wakati muafaka kuhakikisha chuma chetu kile tunakiandaa ili tuweze kukitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sasa wa kutumia malighafi nitatoa mfano mzuri, tupo kwenye ujenzi wa Makao Makuu ambapo kiasi kikubwa cha mbao zinatoka Wilaya ya Kilolo, mimi naomba Mheshimiwa Rais najua anasikiliza na anafuatilia, asilimia 75 zinatoka Kilolo na Mufindi, lakini miundombinu ya Wilaya ya Kilolo barabara siyo rafiki?

Sasa Wizara ya Viwanda naomba utoe ushauri kwa Wizara ya Miundombinu wahakikishe ile barabara inaweza kutengenezwa ili iwe rahisi kusafirisha mbao ambayo ni malighafi ya kujenga viwanda na itasaidia kupunguza gharama. Bila kufanya hivyo utakuwa hujatutendea haki. Mimi ninaomba tu Mheshimiwa Rais huko aliko anasikia siyo mbaya akiamua kuahirisha sikukuu moja zile fedha zikaenda zikajenga barabara ya kutoka Iringa mpaka Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ningependa kulisemea ni Ilula Wilaya ya Kilolo tumejenga Kiwanda cha Nyanya, lakini kiwanda cha nyanya kile nyanya tunalima sehemu oevu ambayo maji yanatuama ili tuweze kupata mazao vizuri, leo hii imekuja tafsiri mbaya sana wanasema kwamba wananchi wasilime kwenye vyanzo vya maji. Sasa tafsiri ya vyanzo vya maji Mheshimiwa January Makamba upo mimi nakuomba Jumapili nipo tayari hata kukuchangia hata mafuta uende, tatizo ni kubwa, sivyo vile ambavyo unafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu sasa hivi wananyanyasika tunaita kilimo cha vinyungu, Mheshimiwa Chumi amepiga kelele, Waheshimiwa wa Wilaya ya Mufundi wamepiga kelele na mimi napiga kelele, tusaidie kwa sababu tukilima nyanya ndizo ambazo tutapeleka kwenye kiwanda. Sasa hatujatengeneza miundombinu mizuri ya kuwawezesha watu wa Kilolo na sehemu nyingine waweze kuzalisha ili wapeleke kwenye kiwanda sasa hatujatengeneza miundombinu mizuri ya kuwawezesha watu wa Kilolo na sehemu nyingine waweze kuzalisha ili wapeleke kwenye kiwanda, bila kufanya hivyo uchumi utatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage shirikiana Mheshimiwa January Makamba nami namuomba ikiwezekana kama haiwezekani toa kauli waache kuwasumbua wananchi tuweke mipango kwanza. Shirikiana na watu wa kilimo watengeneze miundombinu ya umwagiliaji lakini leo unavyosema chanzo cha maji Wilaya ya Kilolo au Mkoa wa Iringa ambao unasifika nchi hii kwa kutunza vyanzo vya maji, sasa leo unavyokwenda kuwabugudhi ni sawa sawa ukiwa na kuku anayetaga mayai ya dhahabu ukimsumbua utakosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utusaidie katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ningependa kulizungumza Mheshimiwa ni mpango wa *SIDO*. Kwa kuwa tunakwenda kwenye viwanda, tujikite sasa kuhakikisha kwamba kila Wilaya angalau tunawatayarisha watu kwa kuwa na *SIDO,* kama usipowatayarisha watu ambao wanakwenda kwenye utekelezaji wa viwanda usitegemee kama tutapata chochote, lakini Mheshimiwa ninakusifu, ukiangalia na ukitaka kujua kazi nzuri ya Wizara yako ukienda ukurasa wa 107 kwenye malengo mambo yote mazuri yamezungumzwa humo kwa hiyo tujikite pake tusome na wengine wanabeza hapa wanasema viwanda havipo. Nenda kwenye ukurasa wa 167 utaona orodha ya viwanda, ukishaona orodha ya viwanda ambavyo viko kila mkoa nenda kwenye Mkoa wako kaulize.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kinatusumbua Mheshimiwa Waziri ni tafsiri ya viwanda, unaposema viwanda una maana gani, ndipo hapo ambapo kuna kuwa na ukakasi kidogo. Pia Mheshimiwa Waziri Mwijage, hivi viwanda ambavyo tunanaza kuna vingiine ambayo wanaweza kuanzisha Watanzania, leo hii ukienda pale kuna Wachina wanauza *juice*, wanauza *ice cream* wewe kama Waziri unasemaje, maana yake ni viwanda watakuambiwa ni viwanda vile. Kwa hiyo, utusaidie Mheshimiwa Mwijage vile viwanda ambavyo vinaweza kuanzishwa na Watanzania basi vianzishwe na Watanzania wenyewe bila kujali mambo yanakwenda vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la kilimo, Mheshimiwa Rais, anatuletea trekta nimesikia zaidi 2000 shirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kuna trekta zile ambazo zilitolewa mwanzo lakini leo hii wananchi wanaanza kunyang'anywa tena, hii haipendezi, tuweke tu mkakati mzuri kwamba wananchi wanazitumia zile trekta ili tuende kwenye kilimo.

Kiwanda cha ngozi mmezungumza vizuri, kwamba leo hii wafugaji nyama haina thamani, ngozi hazina thamani, ngozi ilikuwa inauzwa shilingi 4000 leo hii kwa kilo ngozi ni shilingi 2000 hazina thamani tena, sasa tusipoelekeza nguvu yetu kwenye viwanda kama hivyo matokeo yake tutaendeleza ugomvi wa wakulima na wafugaji wakati suluhu unazo wewe Mheshimiwa Mwijage.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie habari ya migogoro ya wakulima na wafugaji, mtu ambaye anaweza akatusaidia ni Waziri wa Viwanda kwenye jambo hili, ukishirikiana na Waziri husika, tukatenga maeneo haya ni ya viwanda, haya ni ya kilimo, haya ni ya mifugo ugomvi hautakuwepo na kutoa thamani kwenye mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Nyuzi, kwa mfano Kiwanda cha Pamba huwezi kujenga Iringa na ndiyo maana nilisema siasa, unaweza ukafanya siasa kikajengwa

Iringa, leo hii pale sisi Ilula mmetujengea kiwanda cha nyanya lakini bado tunahitaji kiwanda kwa ajili ya vitunguu, tunahitaji kiwanda kwa ajili ya *juice* na mambo mengine ili wananchi wale wapate ajira, lakini ukisema tu viwanda vijengwe halafu havina muungozo itakuwa ni shida. Pia kuna athari za viwanda kwa sababu kuna mambo ya hali ya hewa lazima kuzingatia, kwa sababu unaweza kukuta baadae tumefika mwisho hali ya hewa, mazingira yanachafuka na watu wanaanza kupata athari mbaya, sasa hilo pia uzingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ambalo ningependa kuzungumza ni kwamba tuangalie kwamba kiwanda hiki kinajegwa wapi na hiki kinajengwa wapi ili tuende sambamba na ukuaji wa uchumi kwa kutumia viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nikushukuru kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja iliyokuwa mbele yetu, na nitangulie kwa kuunga mkono hoja. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti pamoja na utekelezaji mzuri wa Ilani wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mkakati wa ujenzi wa viwanda ili Tanzania iweze kufikia hadhi ya nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hili ni jambo jema sana ni jambo lenye tija kwa uchumi wa nchi yetu Tanzania lakini ni ukombozi kwa mamilioni ya vijana wa Tanzania wa kike na wakiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa ya vijana wetu

wa kike na wa kiume wanaoingia kwenye soko la ajira sasa hivi ni ukosefu wa kazi, ujenzi wa viwanda maana yake viwanda vingi maana yake ni ajira nyingi. Tutawapa hadhi vijana wa Kitanzania watajisikia binadamu, watajisikia kuwa na heshima na wataweza kuchangia maendeleo ya nchi yao kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri katika Jimbo langu la Bagamoyo Serikali imetenga ardhi, jumla ya hekta 9,080 ama kwa kipimo cha ekari 22,700 hili ni kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika kata ya Zinga na kata ya Kiromo jumla ya vijiji vitano vitahusika na mradi huu. Tathmini imefanywa mwaka 2008 jumla ya wafidiwa 2,180 na kwa kipindi hicho thamani ya fidia ilikuwa shilingi bilioni 60, mpaka hivi sasa Serikali imelipa bilioni 26.4 kwa wafidiwa 1,155. Kwa hiyo, kuna wafidiwa 1,025 ambao bado hawajapata fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri mwaka 2008 mpaka leo mwaka 2017 ni jumla ya miaka kumi sasa. Mheshimiwa Waziri ungekuwa kule kijijini ujifanye wewe ni mzee kijijini kule Kagera mwaka 2008 shamba lako na nyumba limezuiliwa na Serikali ili liweze kufanywa mradi wa *EPZ* na ukazuiliwa kufanya maendelezo katika nyumba ile, ukazuiliwa kufanya maendelezo katika shamba lako, usubiri fidia kwa miaka kumi, fidia usiione. Mheshimiwa Waziri saa hizi baada ya miaka kumi hali ya nyumba yako ikoje, hali ya shamba lako ikoje, hali ya maisha yako kwa ujumla na familia yako ingekuwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo madhira ya wananchi wa Bagamoyo ambao tangu mwaka 2008 wamezuiliwa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, wako katika hali mbaya sana. Mimi kama Mbunge nashindwa kupita hawanielewi, hakuna jambo ambalo naweza nikawaambia wakanisikiliza. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri una fursa kubwa hii ya azma nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga viwanda, viwanda havijengwi hewani vinajegwa ardhini lazima ardhi hii iweze kulipiwa hivi sasa baada ya miaka kumi ili wananchi nao wajisikie nao wako katika nchi yao huru na wanaweza wakaendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujumuisha hoja yako unipe, ama utupe majibu mazuri na ya uhakika kwamba ni lini wananchi hawa wa Zinga, Kondo, Pande na Kiromo watalipwa fidia zao kwa sababu Mheshimiwa Waziri kwa madhira haya, wewe ni rafiki yangu na mimi nilishawahi kuwa kwenye Serikali nitaona aibu sana lakini nitakuwa sina namna nyingine bali kutangaza azma yangu ya kushikilia shilingi kama sitapata majibu ya uhakika, kwamba lini wananchi hawa watalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema pia katika hotuba yake kwamba fidia hizi inategemewa zitalipwa na mwekezaji mwenyewe jambo zuri, lakini Mheshimiwa Waziri niulize, kwa nini Serikali imebadilisha utaratibu, utaratibu ambao tumejiwekea kwamba fidia za ardhi ya wananchi wetu tulikuwa tunazilipa sisi wenyewe kama Serikali, mwaka 2012/2013 kwa ajili ya mradi wa *EPZ,* tulitenga shilingi bilioni 50 lakini zilitoka bilioni 10.9, mwaka 2013/2014 tulitenga bilioni tisa zikatoka bilioni tatu, mwaka 2014/2015 tulitenga shilingi bilioni saba, zikatoka bilioni saba zote na huo ndiyo ulikuwa utaratibu wakati wote tunaposema kwamba mwekezaji alipie fidia ya ardhi maana yake tunapunguza vivutio kwa wawekezaji hao na mitaji inatafutwa dunia nzima, unapopata mtu ana mtaji basi huyo ni wa kumshikilia na kimojawapo ni kigezo hiki ambacho Serikali inaweza ikalipia fidia zake kama tulivyokuwa tunafanya lakini pia nimuambie Mheshiwa Waziri hata kama mwekezaji atalipa fidia katika eneo hili eneo la *EPZ* ni hekta 9,080 na mwekezaji yule amesema ata *develop* hekta 3000 peke yake, hizi hekta 6000 zingine nani atalipia? miaka 10 baadae nani atalipia?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao wataendelea kuteseka, wananchi hawa wataendelea kuchukia Serikali yao, wananchi hao watashindwa kujiendeleza katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atueleze vizuri kwa nini tumefanya mabadiliko haya na uhakika upi

utakaotuwezesha wananchi hawa waweze kulipwa fidia zao kikamilifu na mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuelezea kwamba mradi huu wa *Special Economic Zone* Bagamoyo unajumuisha pia ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Bandari mpya ya Bagamoyo, bandari yenye uwezo mkubwa zaidi kushinda bandari yoyote katika mwambao wa Afrika Mashariki na kusema kweli ni mwambao wa Afrika nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 ndiyo kwa mara ya kwanza mwezi Septemba tulisaini MoU ya ujenzi wa bandari, na mwaka 2013 Machi, Rais Xi Jinping wa Serikali ya China na aliyekuwa Rais wa Tanzania, walishuhudia kutiwa saini kwa *framework agreement* ya ujenzi wa bandari hii, mwezi Machi 2013 mpaka leo ni mwaka wa tano sasa na ni mradi ambao umeshuhudiwa kuwekewa saini na Rais Xi Jinping, tena wakati ule ana wiki chache tu baada ya kuteuliwa kuwa Rais wa Taifa kubwa lile, huo ni mradi muhimu sana kwa nchi ya China. China ni rafiki zetu, China wamekubali kutusaidia, pesa ni ya kwao na tumesaini *framework agreement* Machi 2013 lakini mpaka sasa hivi miaka Mitano ni muda mrefu hatupaswi kukaa muda huo wakati mtaji tumeushikilia, mtaji huu kila mmoja ndani ya Bara la Afrika na nje ya Afrika wanautafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki tunaongea na *China Merchant Port* kipindi hiki hawa wa *China Merchant Port* wamekamilisha maongezi na Serikali ya Sri Lanka sasa hivi wanaendesha *Colombo International Container Terminal* wamekamilisha maongozi na Togo, wanaendesha *Lome Port Container Terminal,* wamekamilisha maongezi na Nigeria wanaendesha *Tincan Port Island Container Terminal* na wamekamilisha miradi kadhaa mingine ambayo kwa ukosefu wa muda sitaweza kuisema, kipindi hiki tangu 2012 mpaka leo tunajadiliana nao mpaka lini?

Mheshimiwa Waziri nakuomba utakapokuja hapa uweze kusema kwamba ni lini bandari hii itajengwa, lini tutakamilisha maongezi na *China Merchant Port?*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la bandari nalo pia lina mgogoro wa fidia, wananchi 687 walipunjwa fidia zao, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo alithibitisha hivyo na Mthamini Mkuu wa Serikali ameshafanyia tathimini tayari. Mheshimiwa Waziri ndani ya bajeti yako hakuna pesa za kuwalipa hawa wananchi, naomba utakapotoa majumuisho utuambie hawa wananchi 687 waliopunjwa fidia yao watalipwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala kubwa zaidi, katika kipindi hiki cha maandalizi Serikali iliwaahidi wananchi hawa jumla ya kaya 2000, kwamba itawahamishia mahali pengine na shule yao ya msingi ya Pande itajengwa huko, zahanati yao waliyojenga kwa nguvu zao wananchi na nguvu za wahisani itahamishiwa kule, Ofisi ya Serikali ya Kijiji itahamishiwa kule, nyumba zao za ibada, makanisa na misikiti itajengwa kule ili wawe na makazi mapya. Nyumba watajenga wenyewe lakini miundombinu hii ya jamii itajengwa kule, hili jambo halijatokea mpaka hivi sasa, na wananchi hawa wanaishi kwa wasiwasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara yako ya Viwanda ambaye wakati ule alikuwa *DG* wa *EPZA* anakumbuka safari zangu nyingi ambazo nilikuwa nimeenda kule *EPZA* kufuatilia jambo la makazi mapya.

Mheshimiwa Waziri utakapofanya majumuisho tafadhali chonde chonde uwaambie wananchi wa Bagamoyo hao wanaopisha bandari lini watapata makazi yao mapya ili waondoke pale na nchi yetu iweze kujenga bandari mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa muda ulionipa na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Umbula atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kupata fursa hii niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanyia nchi yetu katika sekta ya viwanda. Kama kweli kila mtu amesoma vizuri kitabu hiki, na mimi ni mara chache sana nasoma vitabu vya Wizara, lakini katika wizara hii nadhani kwa sababu nilikuwa najua kwamba nitachangia nimesoma vizuri sana; kusema kweli nia njema ya Serikali yetu baada ya kusoma kitabu hiki ya kuhakikisha kwamba inatuvusha kwenda uchumi wa kati na uchumi wa viwanda, nina hakika tutafikiwa hasa kwa takwimu ambazo zimesheheni katika kitabu hiki cha Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu nikianza na sekta ya viwanda, katika nchi yetu. Sekta ya Viwanda ni ya kimkakati, kwa nini nasema ni ya kimkakati? Si tu inaenda kupeleka nchi yetu katika uchumi wa kati lakini inakwenda kutatua changamoto nyingi ambazo nchi yetu na wananchi wetu wamekuwa wakipigia kelele sana, nikianza na migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na wafugaji. Kama tutazingatia maelekezo ya nia ya Serikali yetu katika kutupeleka kwenye viwanda, nina hakika wafugaji wetu wanakwenda kuachana na matatizo ya kuhangaika kugombania ardhi, kunyanganyana ardhi na wakulima kwa sababu azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaenda kujenga viwanda vya nyama, ngozi, pamoja na maziwa.

Kama tutapata viwanda hivi na mazao yote yanayotokana na mifugo nina hakika kwamba wakulima wetu wanakwenda kupunguza mifugo yao maradufu na matatizo ya kuhamahama na mifugo kuhakikisha kwamba nchi yetu sasa inafuga kwa namna ambayo wana uwezo wa kupata kunufaika kwa mifugo yao na nina hakika migogoro hiyo itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa wakulima. Wakulima wetu wamekuwa na matatizo makubwa ya kukosa masoko. Hamasa kubwa ya mkulima ni kumuhakikishia soko. Kama viwanda vyetu vitakwenda kuchukua malighafi ya kilimo nina hakika kwamba wakulima wetu watahamasika vilivyo, watalima kwa bidii, tena kwa ubora unaotakiwa ili malighafi ambazo zitatumika katika viwanda vyetu hivi vitokane na mazao ya kilimo. Kwa hiyo, nina hakika kwamba hata umasikini wa kipato ambao bado umekidhiri baina ya watanzania, umasikini pamoja na MKUKUTA I, II, III uliokuwepo bado umebaki palepale. Tutakapogusa sekta inayowaajiri watu wengi ambayo ni kilimo na ufugaji nina hakika umaskini utapungua maradufu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye *point* yangu ya kusema kwamba viwanda ni mkakati maalum wa kuvusha nchi yetu kuondokana na matatizo mbalimbali. Tutakuwa na biashara ya uhakika, tutakuwa tumepunguza umasikini kwa jinsi nilivyoeleza, kwa sababu sekta inayogusa watu wengi ni ya kilimo na ufugaji. Tutakuwa tumehamasisha pia vijana kujiunga na kilimo kwa hivyo tutakuwa tumeongeza ajira kwa wananchi wetu, lakini pia tutakuwa tumepunguza migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu biashara ya utalii. Katika biashara ya utalii nchi yetu bado haijanufaika kadri ambavyo inalingana na maliasili tuliyonayo, rasilimali tulizonazo katika sekta hii. Tunayo mapori mazuri sana katika nchi yetu ambayo hayapo kule duniani, tunao wanyamapori wazuri ambao hawapo katika nchi

mbalimbali, lakini nchi yetu bado haijanufaika kwa jinsi ambavyo tuna maliasili hiyo niliyotaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo amekuwa mbunifu ameona kama tutakuwa na maliasili ya aina hii, tuwe na mapori mazuri, wanyama wazuri, lakini kama watalii hawaji kwetu kuja kuangalia maeneo haya, bado hatutakuwa tumenufaika. Kwa hiyo, amekuwa mbunifu, na biashara ni ubunifu na viwanda ni mbunifu. Amenunua ndege ambazo atahakikisha watalii wetu watakuja Tanzania, watakuja kutembelea mapori niliyoyataja kwa ajili ya kuona wanyama wetu na hivyo uchumi wetu utakwenda kasi na kuhakikisha kwamba tunanufaika na sekta hiyo ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni ukurasa wa 23 imebeza ununuzi wa ndege. Kubeza sikatai kwa sababu ni kazi yao, lakini wabeze kwa takwimu. Mimi nimeeleza kwamba huo ni mkakati kwa sababu hata Biblia inasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Hayo ni maarifa ya kuhakikisha kwamba tunawaleta watalii nchini mwetu ili tunufaike na sekta yetu ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niweze kutoa ushauri kwa Serikali. Tozo katika sekta hii bado ni tatizo. Watalii wakisikia kwamba Tanzania wanatoza *VAT* kwenye huduma za utalii, bado kuna hatari ya kupunguza manufaa tutakayopata kwa sababu atakwenda katika nchi nyingine na sisi tutabaki kulalamika. Ninaomba Serikali yangu kama si tatizo kubwa iondoe tozo la *VAT* kwenye huduma za utalii ili tuweze kunufaika maradufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Benki ya Rasilimali *(TIB).* Benki hii iko Dar es Salaam, biashara ni mikopo, tunaomba Benki ya Biashara ifungue matawi yake katika mikoa mbalimbali ili wananchi wetu waweze kukopa, wakulima waweze kukopa ili waweze kupata mitaji ya kutosha kuweza kuendesha biashara zao. Ninaiomba Serikali yangu iweze kufikiria jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa Mkoa wangu wa Manyara. Mkoa wetu wa Manyara uko pembezoni na mkoa huu uchumi wake uko chini, lakini cha kushangaza ni kwamba tunayo mazao mengi ambayo mengine pia hayapo popote pale Tanzania. Kwa mfano zao la pareto, linalimwa kwa uchache sana kule kusini lakini mazao mengi ya pareto yanaozeana kwenye *godown* kwa sababu hakuna soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iweze kuangalia uwezekano wa kuanzisha kiwanda kule Bashnet ambako tunalima sana zao la pareto. Pareto ni zao zuri sana, dawa ya mbu ambayo ni *very effective* kuliko dawa zote, inaitwa *expel* inatengenezwa kutokana na pareto. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali iweze kutujengea kiwanda katika Mkoa wetu wa Manyara hususan Bashnet. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunalima vitunguu saumu. Vitunguu saumu ni zao ambalo kwa kweli ubora wake sina haja ya kueleza, lakini wakulima wanalima kwa kutumia zana duni, wakulima hawanufaiki kwa sababu, masoko bado yako chini. Ninaiomba Serikali yangu katika harakati hii ya kuanzisha viwanda hasa kujenga mkoa wetu wa Manyara ambao upo pembezoni na uchumi wake uko chini lakini una rasilimali nyingi iweze kutujengea kiwanda kule Mbulu ambako tunalima zao la vitunguu saumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza kidogo, maeneo ambayo yana mifugo mingi kanda ya kaskazini mkoa wangu wa Manyara, Wilaya ya Mbulu inaongoza kuwa na mifugo mingi, Wilaya ya Kiteto, Simanjiro na Hanang, lakini cha kushangaza kiwanda cha nyama kipo Arusha. Tunaiomba Serikali na sisi Manyara iweze kutujengea kiwanda cha nyama Mkoa wa Arusha ili wananchi wetu wafugaji waweze kunufaika kutokana na mazao yao ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa msisitizo kabisa mikoa ya pembezoni kama Manyara ni mikoa ambayo inalimwa mazao mengi kama mahindi, maharage na mazao

mengine ndiyo maana bodi nyingi za mazao yameanzishwa, bodi ya korosho, bodi ya katani, lakini sisi hatuna bodi huko. Lakini tunaomba *recognition* ya Serikali kuona kwamba mkoa wetu unazalisha mazao mengi ya biashara, tunaomba viwanda vielekezwe kule ili na sisi tuweze kunufaika na sekta hii ya viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya naomba kuunga mkono hoja, na nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa mara ya pili kujadili bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishatoa pole kwa wale ambao walifiwa kwenye maafa mbalimbali hivyo naomba niende moja kwa moja kwenye hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni lazima kwa ustawi wa wananchi wa nchi yoyote. Ninasema hivi kwa sababu viwanda na kilimo kwa pamoja ndivyo vinavyosaidia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi na maendeleo yake, huo ndio ukweli. Kwa hiyo, kama nchi haisisitizi viwanda na kilimo hakitaendelea kwa sababu kilimo kwa kiasi kikubwa kinasaidiana sana na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza Serikali na siipongezi tu kwa maneno na kwa vitendo kwa sababu sekta hii imekuwa kwa asilimia 7.8 ukilinganisha na ukuaji wake mwaka uliopita wa asilimia 6.5, na imekuwa ikikuwa hivi wakati zamani ukuaji wa viwanda ulikuwa chini. Ukuaji huu umetokana na sera nzuri ambayo kuna wengine walisema imekaa muda mrefu, Sera ya Maendeleo *(Sustainable Industrial Development)* ya mwaka 1996 mpaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa sera ni kukaa muda wa kutosha ili muda wa utekelezaji uwe unatosheleza. Kwa

hivyo, ninaomba niipongeze wizara hii kwa kuendelea kutekeleza sera hii ambayo kwa kiasi kikubwa inataka viwanda visambae nchi nzima na vifike hata kule pembezoni ili maendeleo ya nchi yawe na uwiano mzuri. Kwa hivyo, ni sera nzuri ninaomba tuendelee kuitekeleza, na mwaka 2020 utakapofika tutaifanyia kazi changamoto ili tuboreshe sera nyingine itakayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na sera hii *SIDO* imekuwa na *program* inayoitwa *MUVI* ambapo imetaka kila mkoa uwe na viwanda ambavyo una malighafi yake na ili uwiano wa maendeleo kwenye mikoa yetu iweze kufanana. Hii programu karibu itakwisha. Ninaomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ijiandae baada ya *MUVI* kutakuwa na nini? Kwa sababu mwenendo na mwelekeo wa *MUVI* ni mzuri sana. Unapokuwa na *specialization* kwa kila mkoa unawezesha kuwe na biashara kutoka mkoa hadi mkoa, na ndiyo baishara ya ndani itakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nitoe mfano kwa Wilaya yangu ya Hanang ambapo ilipangiwa kutengeneza kuwa na viwanda vidogo vya ngozi kwa sababu sisi ni wafugaji na mazao mengine yanayotokana na mifugo na Singida imepewa *specialization* ya mafuta ya alizeti kwa sababu inalima alizeti. Kwa hiyo, watu wa Singida watakuja kununua bidhaa za ngozi kwetu na sisi tunanunua mafuta kule. Tukiwa na utaratibu wa namna hii nchi nzima tutaendelea na maendeleo yatakuwa na uwiano mzuri, hakutakuwa na mahali ambapo patabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *MUVI* ifuatiliwe ili muda wake utakapokwisha tuwe na programu nyingine nzuri, na tumeifanya *program*; mimi nasema hivyo kwa sababu nilikuwa Wizara ya Viwanda; ili muda wake usiishe, huu si mradi ni programu na programu haina mwisho wake. Kwa hivyo ndugu zangu ninaomba sana tufanye hivyo ili tuongeze ajira kwa watu wetu, ili tuongeze mauzo ya nje. Nilipokuwa Wizara ya Viwanda tulikazana, kuna miaka miwili tulipita mauzo ya kwenda Kenya kuliko ununuzi wa bidhaa kutoka Kenya, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtajitahidi kutekeleza sera hii ya *sustainable Industrial Development* tutafika pazuri na hata tutaipita hii Kenya kwa sababu sisi tuna *resources* au maliasili nyingi kuliko hiyo Kenya ambayo inatupita kwa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili viwanda vilete manufaa nchini lazima tuwe na uwiano mzuri. Kwa sasa hivi kwa mujibu wa hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri viwanda vidogo sana ni asilimi 85, viwanda vidogo asilimia 14, viwanda vya kati asilimia 0.35, viwanda vikubwa asilimia 0.5 uwiano huuu si mzuri. Tunataka tuwe na uwiano mzuri wa viwanda vidogo kuwa vingi kama asilimi 65; vya kati vifuate na vikubwa hata vikiwa asilimia 5 haitakuwa mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano huu utatusaidia sana kuona kwamba malighafi zinatumika vya kutosha, itatufanya tuone kwamba mazao ya kilimo yanapata masoko kwa sababu viwanda ndio soko la uhakika la mazao ya kilimo. Vilevile itaajiri wananchi wengi. Hata hivyo ajira imeongezeka. Mwaka 2016 viwanda viliajiri watu 146,892 ukilinganisha na mwaka jana ambapo 139,000 waliajiriwa, kwa hivyo, *trend* ni kukua lakini ajira hii haitoshi na ndio maana nasisitiza umuhimu wa uwiano wa viwanda.

Ninaomba niongelee kidogo Kurasini *Logistic Center,* sijui mtakuwa mmefika wapi jamani. Tulianzisha *Logistic Center* ya Kurasini ili tuweze kuagiza vitu kwa *bulk purchases* na wafanyabiashara wa Kongo, Rwanda waje pale ili Kariakoo iwe Hong Kong ya Afrika, hilo ni moja. Hata hivyo kuna watu wanaogopa kwamba tutakuwa tunaagiza vitu kutoka China. Kutokana na *Logistic Center* tutajua mahitaji ya watu na nchi ambazo zinazunguka Tanzania na viwanda vitaanzishwa kwa haraka sana.

Kwa hiyo naomba sana *Logistic Center* ianze. Vilevile nataka tuongeze mauzo kwenda nje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nagu muda wako umemalizika.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini ninaomba Liganga ni kiwanda mama tukisisitize kianzishwe. Ninaunga mkono na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Kangoye, Mheshimiwa Catherine Magige ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais kwa ku-*revive dream* ya kuwa na *industries* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1967 Mwalimu Nyerere aliasisi dhana ya kuwa na viwanda, na *focus* ikawa *import substitution industries,* viwanda ambavyo baadaye vilikuja kufa. Kwenye bajeti ya mwaka jana nilimuahidi kaka yangu Mwijage, kwamba tutakutana na nilionesha mashaka yangu juu ya utekelezaji wa dhamira ya yeye kufikia yale ambayo alikuwa ametarajia, na leo tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, *vision* ya Rais ni kujenga uchumi wa viwanda ambao utalijenga Taifa hili kujitegemea, hii ndiyo *vision* ya Rais. Kwenye *battle field, Chief of Staff* na *Generals* wanachora vita kwenye meza, wanaoenda kupiganisha vita hii ni makamanda. Tuna tatizo kubwa la ku-*link vision* ya Rais na mikakati yetu ya kuweza kufikia malengo aliyokuwa nayo Mheshimiwa Rais ya kuwa na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mifano michache, kwa taarifa ya *BOT* ya mwezi Aprili, *manufacturing industry* imeshuka kutoka *1.4 million US Dollar* mpaka *817 million US Dollar,* maana yake tumepoteza dola milioni 500. *Re-Export* ime-*drop* kwa dola milioni 80, *fish and fish products* ime-*drop* kwa dola milioni 20, lakini *on the other hand credits*

kwenye *agro sector* zime-*drop* mpaka kufika *negative 9.2, transport and communication* zime-*drop by negative 21.6, building by negative 3, hotel and restaurant* ime-*drop by 7%. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *export of traditional crops,* bidhaa pekee iliyo-*grow* ni korosho na *not because of volume, because of price. Tobacco* imeshuka kutoka mwaka 2015, *three hundred and forty three million US Dollar* mpaka milioni 281 mwaka 2017 Machi. *Cotton* imeshuka kwa dola milioni 10, kahawa imeshuka kwa dola milioni tisa, karafuu imeshuka kwa dola milioni 13. *Sisal* ime-*grow only for one million US Dollar. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *capital goods, capital equipments. Capital goods* zimeshuka mpaka *negative 16.7, transport* imeshuka kwa *23.9, building 19.3, machinery 11.3, what is the problem? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *problem* ni *un-predictability* ya sera zetu za kodi. Nitatoa mfano wa Sheria ya Uwekezaji, kifungu namba 19. Sheria hii tumeibadilisha mwaka 2009 kwa kufuta utaratibu wa *deemed capital goods,* ikashusha *investiment.* Tukaibadilisha mwaka 2010;tukaibadilisha mwaka 2012; tunafuta na kurudisha, tukaibadilisha 2014 na tumeibadilisha mwaka 2015. *This is the same country* sheria ile ile, leo unweka *incentive* kesho unafuta. Mheshimiwa Mwijage hata ahubiri kwa Injili na Qurani, *we will never go through. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue mfano, *success* ya *industrialization* ni *private sector* na Mheshimiwa Rais amesema. Nimechukua kitabu cha miaka mitano cha mpango, hakuna hata *page* moja inayoongelea namna gani *private sector* itakuwa *included* kwenye *growth of economy of this country. The problem is a Ministry of Finance that is our biggest problem. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikupe mfano mwingine, ninayo Ripoti ya *World Bank* iliyoifanya Tanzania

*Micro Reform for Agri-Business.* Ili uanzishe kiwanda kidogo cha kuzalisha maziwa unatakiwa uwe na *documents* zifuatazo, upate *Incorporation Business Licence* kutoka *BRELA, Premise Registration, Equipment and Truck Registration, Product Testing and Registration, Staff Health Certificate, On Going Inspection, Import Permit/Export Permit, Weigh Measures;* ili uzipate hizi zinatakiwa zipite *BRELA, TFDA, TBS, Diary Board, OSHA, Ministry of Labour, Weigh and Measure, NEMC, all of these!* Nani anakuja kuwekeza hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, *Deputy Managing Director of International Monitory Fund* alikuwepo Tanzania, amesifia sana uchumi wetu kwa kipindi cha miaka 20, lakini amesema mambo matatu na naomba ninukuu:-

*"(i) It is essential to increase investiment in an effective way to address key bottlenecks in the economy and create more jobs."*

Mheshimiwa Naibu Spika, *our area to create jobs* ni ku-*link industrialization* na *agriculture,* tusipofanya namna hiyo hatuwezi ku-*create* kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa Wamachinga, na nimeongea na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameahidi kuipitia hii Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Leo tuna Sheria ya Fedha tuliyoifanyia mabadiliko mwaka 2012 ambayo inamtaka mfanyabiashara alipe *service levy* ya *0.3 percent.* Wewe ukiwa unauza *coca cola, double taxation* angalia hii. *Cocacola Kwanza* atalipa *service levy* kutokana na *turn over* na muuzaji wa Nzega anatakiwa alipe *0.3 on the same product* ambayo mmei-*tax from the producer* mnakuja kum-*tax from the agent* na mnakuja kum-*tax retail seller. How can we grow business like this? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, utazunguka *all over the world.* Nataka niwape mfano kuhusu *leather industry,* waliongea Waheshimiwa Wabunge hapa. Kuzalisha *one square feet* ya ngozi Tanzania ni senti 14 dola, Ethiopia ni senti 8, India ni senti 7, Pakistan ni

senti 8, *how can we compete?* Na *why,* kwa sababu, sisi tumeweka *export duty* ukizalisha ngozi Tanzania kui-*export* unalipia kodi, uki-*import chemicals* kwa ajili ya ku-*process* ngozi unalipa *25% tax,* unalipa *18% VAT, how can we grow? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kabisa nataka niiombe Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *there is no where in the World* una-*tax inputs.* Kodi zote lazima ziwekwe kwenye *output,* una-*tax* vipi *inputs!* Unaongeza *cost of production,* nani atawekeza? *BOT* imefanya mabadiliko kwenye mfumo wake wa *interest,* nani ataenda kukopa? *There is no way! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ripoti ya *BOT* inaonesha *lending* imeendelea kushuka kwa sababu hakuna sehemu ya kwenda kufanya biashara. Sasa hivi wanachinga tunakusanya kodi za Halmashauri vibaya mno, hawakui hawa watu, mkulima kodi, mmachinga kodi akianza kufanya biashara yake, mwekezaji kodi. Nataka niishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda toa *direction* dunia ijue.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefanyika Mkutano wa *IFC* juzi, *one week ago,* kujadili *emerging economies and where to put money* kwenye *private sector,* Tanzania inakuwa *discussed* ni *area* ambayo ni *unpredictable.* Leo mna sheria hii kesho akija Waziri huyu anabadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *there is no way* kama Wizara ya Fedha haitaelewa kwamba kodi ni *secondary, number one is creation of wealth and creation of job. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kiisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, muda wako umemalizika.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Maria Kangoye atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Gimbi Masaba ajiandae.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia afya na kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. Pia, niipongeze Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayofanya. Niipongeze pia Wizara hii ya Viwanda Biashara na Uwekezaji kwa kazi nzuri na jitihada zake katika kuijenga Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha programu ya kuwapa vijana 1,000 elimu ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi kutoka katika Chuo cha *DIT* Mkoani Mwanza na tayari 90 wamehitimu wiki iliyopita na wengine wanaendelea kujiunga na kozi hiyo. Pamoja na pongezi hizo bado ipo haja ya wanafunzi hawa kutafutiwa viwanda ambapo wataweza kufanya *internship.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali yangu, kipo kiwanda ambacho kilikuwa chini ya *Mwanza Tanneries* cha kutengeneza bidhaa za ngozi ambacho kilibinafsishwa na mwekezaji yule hajulikani hata alipo, lakini hata mashine zilizomo mle ndani zimeshatolewa. Nipende kuiomba Serikali yangu sikivu iweze kukirejesha kile kiwanda kwa Serikali, ili wanafunzi waweze kupata sehemu ya kufanyia *practicals,* na vile vile lakini waweze kupata sehemu ya kufanyia *internship* na kuajiriwa kama ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uwekezaji nchini si rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje, hivyo ipo haja ya Serikali kutengeneza mazingira mazuri. Mimi binafsi na-*declare interest* kwamba ni mmiliki wa kiwanda cha mavazi na taulo za kike. Ninapoongea hapa ninaongea kutokana na kile ninachokifahamu, ni ukweli kwamba hatutaweza kuijenga Tanzania ya viwanda kama hatutakaa na kupitia hizi kodi na tozo mbalimbali ambazo ni nyingi na zimekuwa zikiathiri uwekezaji ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo hizi na kodi zimesababisha bidhaa zetu kuwa za gharama kuliko hata zile zinazotoka nje. Haiwezekani leo mfanyabisahara ambaye ananunua pamba kutoka kwa wakulima inafika hatua ana-*prefer* kuuza nje ya nchi kwa sababu hatalipa *VAT.* Pamba hiyo hiyo ikienda nje inatengenezwa nguo, nguo zinaingia ndani bila kulipa *VAT,* sasa inakuwaje kwamba, viwanda vyetu viuziwe kwa wafanyabiashara wale watalipa *VAT* na sisi pia huku ndani tuuze na tulipe *VAT?* Ina maana hatutaweza ku-*compete* na masoko ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tunauona kwamba hata mbolea inayotoka Kenya leo hii ni ya bei ndogo ikifika nchini kuliko ile mbolea ambayo tunazalisha hapa. Kwa namna hii hatutaweza kutengeneza Tanzania ya viwanda. Suala hili liangaliwe kwa umakini kwa sababu sasa limeanza kuhamasisha wawekezaji wa ndani ya Tanzania kwenda kuwekeza katika nchi za jirani kwa sababu wanajua wakiwekeza kule wataleta bidhaa zao nchini na hawatalipa *VAT. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mashaka na kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote, lakini kama tunavyofahamu kwamba Wizara hii ni mtambuka na inahitaji *cooperation* kutoka katika Wizara mbalimbali kama ya Afya, Kilimo, Fedha, Nishati na nyinginezo. Hata hivyo bado inahitaji ushirikiano kutoka Taasisi mbalimbali za Kiserikali kama *TFDA, EPZA, TIC, NDC, SIDO, NEMC* na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu hapa ni urasimu mrefu. Kumekuwa na urasimu mrefu sana katika uwekezaji wa Tanzania ambao umekatisha tamaa viwanda vingi. Kwa mfano, mwekezaji wa kiwanda cha dawa atahitaji kwenda *TFDA, NEMC,* atahitaji kupitia kwa Msajili wa Kampuni, ataenda *TRA* na kote anakokwenda kunakuwa na muda mrefu wa kusubiria matokeo ambayo anataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuishauri Serikali kuliangalia hilo kwa ukaribu kwa sababu imesababisha sisi

kupoteza wawekezaji wazuri na wameenda kuwekeza katika nchi nyingine. Kwa mfano kiwanda cha *Omnicane* ambacho kilitaka kujengwa hapa Tanzania, lakini kutokana na urasimu huu na changamoto hizi nilizotaja hapo awali kimeenda kuwekeza Mauritius ambapo leo kimeajiri wafanyakazi 1,472 lakini kinazalisha umeme kutokana na makapi ya miwa *gigawatts* 717 ambayo ina-*produce* katika *community* inayowazunguka, lakini pia, kwa siku kina-*produce* sukari tani 8,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tulicheza karata mbovu kwa kweli, kwa sababu sisi ndio tungekuwa tunanufaika na haya. Tuki-*compare* kwa haraka haraka viwanda vyetu vikubwa ambavyo ni Kilombero na Mtibwa kwa mwaka vinazalisha sukari tani 80,000 ambayo ni *production* ya siku tatu ya Kiwanda cha *Omnicane.* Cha kushangaza zaidi pamoja na ukosefu wa sukari ya kutosha ndani ya nchi yetu na *experience* hiyo ambayo nimeitoa kutokana na kiwanda cha *Omnicane* bado tunaendelea kuweka mazingira magumu kwa viwanda ambavyo vinataka kuanzishwa hapa vya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni kule Tarime. Tarime kuna mwekezaji ambaye yupo tayari kufungua kiwanda cha sukari, lakini kumetokea vita iliyoanzishwa na Mbunge wa Tarime Vijijini ili kukwamisha kiwanda hiki kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hicho kikijengwa kitanufaisha wananchi wa Tarafa za Ingwe na Inchage ambavyo ni...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** ...ambavyo ni vijiji vinne vya Biswalu, Mrito Matongo na Kijiji cha Wegita...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maria Kangoye, kuna Taarifa. Mheshimiwa Esther Matiko!

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu spika, ningependa nimpe Mheshimiwa Maria Kangoye taarifa kwamba kwa sababu Mbunge wa Tarime Vijijini hayupo, na kwa sababu najua sakata lote kuhusiana na uwekezaji kwenye shamba la miwa kule Biswalu, ningependa tu nimpe taarifa kwamba Mbunge wa Tarime Vijijini hapingi uwekezaji, bali anataka *process* zifuatwe ili tuepushe yale ambayo yanatokea Nyamongo watu wanakufa, wanapokwa ardhi bila kufuata *process* za ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimpe hiyo Taarifa kwamba Mbunge, Madiwani na Halmashauri ya Tarime Vijijini haipingi uwekezaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maria Kangoye, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo siipokei kwa sababu hata wiki iliyopita wananchi wa vijiji hivyo vinne vya Biswalu, Mrito, Matongo na Wegita kijiji wanakotokea wanangu mimi Bhoke na Ryoba walikuja hapa Dodoma na mabasi mawili, wamekuja kuandamana na kuja kuonana na Waziri wa TAMISEMI. Na mimi nimekaa nao, nimepata taarifa hiyo, hata taarifa ya habari ilionesha hivyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Kwa hiyo, sipokei taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Ameshapewa taarifa kuhusu jambo hilo, Mheshimiwa Kangoye endelea.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana, huyu anapotosha watu hapa, si kweli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwanza usiwache *microphone,* unatakiwa usimame uonwe au umuandikie Spika. Ukiwasha wewe akiwasha na yule, akiwasha mwingine tutaweza kuwasiliana humu ndani? Naomba ukae, Mheshimiwa Kangoye malizia.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni matumaini yangu kwamba, muda wangu utalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki kitakapojengwa pale kitanufaisha tarafa za Ingwe na Inchage katika vijiji hivyo vinne ambavyo ni Biswalu, Mrito, Matongo na Wegita, kijiji ambacho wanangu wanatokea Bhoke na Ryoba. Pamoja na hayo yote kiwanda hiki kikijengwa kitatoa ajira kwa wananchi 15,000 lakini kitapunguza changamoto ya ukosefu wa sukari ndani ya nchi hii. Vilevile pia kitaongeza maendeleo katika vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuiomba Serikali yangu kuwa makini na suala hili iweze kuingilia kati na kusimamia, ili kiwanda hiki kiweze kuanzishwa kule Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote naomba niunge mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Catherine Magige atafuatiwa na Mhshimiwa Gimbi Masaba na Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwanza kabisa naomba sana niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais John Pombe Magufuli kwa kuendelea kutimiza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kuwa tunajenga Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiongea kila siku hapa kuhusu Kiwanda cha *General Tyre* cha Arusha nimeona kimetengewa pesa ili kianze, lakini ninachoomba je, tumejipangaje kuhusu viwanda vingine vinavyotengeneza matairi hasa vya nje? Je, Kiwanda cha *General Tyre* tumejipangaje ili kifanye biashara vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilikuwa naomba reli ya Tanga – Arusha mpaka Moshi. Reli hii itasaidia sana katika usafirishaji wa matairi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Arusha kuna viwanda vingi tu, kuna Kiwanda cha *Lodhia Plastic.* Kiwanda hiki kimeajiri Watanzania 700; ni kiwanda cha mabomba na ma-*sim tank.* Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja tulitembelea kiwanda hiki, ni kiwanda chenye ubora wa hali ya juu na aliagiza baadhi ya ofisi zetu za Serikali zitumie kiwanda hiki, lakini ma-*engineer* wa Serikali wamekuwa wakikwamisha kiwanda hiki. Wamekuwa wakiagiza mabomba nje ya Arusha, wamekuwa wakiagiza mabomba Dar es Salaam ambapo kwanza ni gharama kubwa sana, wamekuwa wakiagiza wakandarasi wanunue mabomba kwenye viwanda fulani, sijui kuna nini *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo figisu figisu hizo nahisi kuna rushwa. Tumekuwa tunakwamisha Watanzania ambao wanajitokeza kuendeleza viwanda vyao kutimiza kauli ya Rais wetu Tanzania yenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa amri sijui kama kuna amri nyingine zaidi ya Waziri Mkuu. Tujue hawa ma-*engineer* wa Serikali ni kitu gani hasa wanapata mpaka wanatoa amri kwa makandarasi ili waende wakachukue mabomba kutoka kwenye viwanda

vya nje ya Arusha, kwa sababu kwanza ni gharama. Tunasema tunabana matumizi matumizi gani tunabana kama ni hivi? Tunahujumu na tunamhujumu Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Arusha tuna Kiwanda cha *Gypsum* kinaitwa *Saint Gabain Lodhia Gypsum.* Kiwanda hiki kinatumia makaa ya mawe wanatoa Kiwira, mpaka wafike Arusha wanatumia dola 120 mpaka 130. Kiwanda hiki kimekuwa kinatozwa pesa nyingi tofauti na viwanda vingine. Wamekuwa wananunua makaa ya mawe dola 65 mpaka 70; huku viwanda vingine vimekuwa vinatoa dola 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri aangalie sana, tunazidi kukwamisha jitihada za Rais wetu za kuwainua Watanzania. Pia kiwanda hiki kimeajiri Watanzania 450. Hiki cha *plastic* tayari Watanzania 250 wameshapunguzwa kwa ajili ya hawa watu ambao wanatuhujumu. Ninaomba sana kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi nitashika shilingi nisipopata jibu la kiwanda hiki cha *plastic,* nisipopata jibu kiwanda hiki ambacho kinatumia Makaa ya Mawe ya Kiwira. Naomba Mheshimiwa Waziri uje na majibu yanayoeleweka ama sivyo sitakuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alikuja tulitembelea Kiwanda kimoja cha Hans Paul. Yule ni Mtanzania ana kiwanda, anachukua magari Anaya-*design* yanakuwa magari ya kubebea taka. Magari yake anauza shilingi milioni 200 mpaka 220. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe aliona alishaanga sana hakutegemea kama watanzania wanaweza wakawa na ujuzi kama huo. Ni magari mazuri na yana ubora wa hali ya juu. Ningeshauri baadhi ya Halmashauri zetu zitembelee zione kuliko uangize magari kwa bei zaidi ya shilingi milioni 500 huku tunaweza tukapata magari yenye ubora wa juu hapa hapa nchini kwa shilingi milioni 220. Naomba sana tulinde viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Arusha tulikuwa na kiwanda kikubwa sana cha dawa kimefungwa mpaka leo na kimefungwa na Tanzania tuna uhaba wa dawa. Kwa nini kisifunguliwe hata kisaidie hata Kanda ya Kaskazini yote?

Naomba sana Mheshimiwa Waziri uje kunijibu na hili kiwanda cha dawa cha Arusha kimefungwa mpaka leo. Naomba sana kiwanda hiki kifunguliwe Serikali ijipange ifungue kiwanda hiki. Tunayosema Tanzania yenye viwanda haitakuwa yenye viwanda bila kutekeleza haya ninayokuambia Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuna watu ambao walipewa viwanda vilivyokuwa vya Serikali, lakini viwanda vile wameng'oa mashine, viwanda vingi tu havitumiki tena. Tunaomba viwanda hivi mkiweza mvirudishe Serikalini ili vifanye kazi, Watanzania waweze kupata ajira tuweze kutumia na sisi bidhaa zetu. Watu wengi walipwa viwanda lakini wamefanya ma-*godown.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Arusha tunajua ni mkoa ambao unaongoza sana kwa mifugo, ni Mkoa ambao una wafugaji wengi sana. Tunaomba na sisi mtuwekee angalu kiwanda cha ngozi ili tuweze kutumia mifugo yetu na itufaidishe tuweze kutengeza viatu. Ngozi inatengeza vitu vingi sana tunaombasana mtuangalie Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wafanyabiashara, wanakata tamaa wanashindwa kuendelea, tunakwamisha jitihada za Watanzania. Kuna *process* ndefu sana katika kupata vibali cha kuanzisha biashara. Wanapitia sehemu nyingi sana mpaka wanakata tamaa. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wasaidie Watanzania wengi, hiki ni kilio cha watu wengi sana. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri narudia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana mimi leo kweli nitashika shilingi Mheshimiwa Waziri asiponijibu kuhusu Kiwanda cha Plastiki cha Lodhia. Vilevile nilikuwa naomba washirikiane na Waziri wa Maji hata idara zetu za maji mfano kama AUWSA watumie watu ambao wako kwenye mikoa yao maana viwanda ni vizuri, kuna hujuma hapa; na hawa ma-*engineer* wa Manispaa wa mikoa yetu nilitaka nifahamu wenyewe wana nguvu gani kuliko Mheshimiwa Waziri Mkuu? Kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa amri hawaitekelezi wanatuma mabomba wakachukue mabomba Dar es

Salaam inawezekana kweli? Wanapatanini? Kwanza gharama ni kubwa; tunasema Serikali yetu tunabana matumizi naomba tusimuangushe Mheshimiwa Rais ana nia nzuri na Watanzania ana nia nzuri na nchi yetu, ana nia nzuri na chama chake ambacho ndiyo anatekeleza Ilani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi, naunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri nitashika shilingi leo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, Mheshimiwa Gimbi Masaba atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali ajiandae.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kwa siku ya leo ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu. Vilevile nishukuru Mwenyenzi Mungu; amsaidie mwenyekiti wangu wa Kanda ya Ziwa Serengeti Mheshimiwa Heche aweze kupata nafuu ili aweze kuja kutekeleza majukumu yake. Nimeona jinsi ambavyo ameanza kunyemelewa na kashfa na kwa jinsi ambavyo namfahamu mimi siyo muumini wa kupinga maendeleo. Nafahamu hilo yeye ni Mwenyekiti na mimi ni Makamu wake kwa hiyo tunafanya kazi ofisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba tu nizungumze kwamba tunapozungumza Tanzania ya viwanda naamini kabisa hakuna Mtanzania anayepinga Tanzania ya viwanda. Hata hivyo ninachokiona ni kwamba hatuendani na kauli ya Tanzania ya viwanda. Ninasema haya kwa sababu katika taarifa ya Waziri amezungumza mambo mengi sana na mimi kama Mbunge ninayetoka katika Mkoa wa Simiyu tunapozungumza viwanda maana yake tunagusa malighafi za maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu tunalima kila kitu, lakini cha kushangaza sijaona mahali popote

ambapo Mkoa wa Simiyu unazungumziwa kuhusu kupata kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi niliuliza swali ambalo linahusiana na viwanda ambavyo vilikuwepo kwa muda mrefu, viwanda *ginnery* na nilivitaja kama viwanda vitano, *Nasa Ginnery, Ngasamo Ginnery,* Maswa na Malampaka, viwanda vyote hivi vimekufa na nikahoji Serikali inampango gani kuvifufua viwanda ambavyo vimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alisema mkakati wa Serikali na jukumu alilopewa ni kuhakikisha viwanda vyote vilivyokufa vinafanya kazi. Sasa ninataka kujua kauli ya Serikali, hivyo viwanda ni lini vitaanza kufanyakazi ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu waanze kunufanikana na viwanda hivyo vya kuchambua pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia viwanda lazima tulipe kipaumbele zao la pamba. Mkoa wa Simiyu zao la pamba limekufa, wakulima hawalimi tena zao la pamba kutokana na kwamba soko hili la pamba halipo. Wananchi wanatumia gharama kubwa kuandaa mashamba ya pamba kama vile palizi pamoja na vitu vingine lakini cha ajabu wanakwenda kuuza kilo ya pamba shilingi 1,000; jambo ambalo siyo zuri hata kidogo kwa Watanzania wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachotaka kuomba kama kweli Serikali inadhamira ya dhati na kwa kutambua Mkoa wa Simiyu kwamba ni wa wakulima wakubwa sana, ninaomba ipewe kipaumbele kikubwa sana ili kuhakikisha kwamba tunapata viwanda vya kila aina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza wakulima na wafugaji, Mkoa wa Simiyu tuna wakulima na wafugaji. Lakini pamoja na malighafi zote hizi hakuna kinachofanyika kule Mkoa wa Simiyu. Sisi ni wafugaji lakini cha kushangaza hakuna hata kiwanda cha kusindika nyama, hakuna. Wafugaji anapakia ng'ombe kwenye malori kupeleka Dar es Salaam. Mmewahi kuona wapi sisi binadamu tunakwenda

Jiji la Dar es Salaam kutalii ng'ombe nao wanakwenda kuangalia jiji la Dar es Salaam? Ni aibu kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isitengeneze viwanda ili wananchi hawa waweze kunufaika? Mimi niombe sana, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda niko kwenye kamati yako. Kilio changu kikubwa sijawahi kuchangia nikizungumza suala la kimataifa. Mara nyingi nazungumzia Mkoa wa Simiyu na Wabunge wenzangu wanaotoka Mkoa wa Simiyu kila siku tunapiga kelele kuhusiana na suala ya Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalima choroko, tunalima zao la alzeti, tunafuga, bado ndani ya mifugo tunazalisha mbolea, kwa nini sasa tusiwe hata na kiwanda cha kutengeneza *biogas* inatokana na vinyesi vya ng'ombe? Kwa nini kila kitu hakuna? Halafu tunakuja tunasema Tanzania ya viwanda! Sipingani na kauli ya Tanzania viwanda lakini matendo yetu hayaendani na Tanzania ya viwanda. Mimi niombe sana kwamba tuangalie ni namna gani tunaweza kuusaidia mkoa huu wa Simiyu ili tuweze kuendena na kasi ya Tanzania ya viwanda ambayo mnaizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda wewe unatoka Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera unazalisha ndizi, lakini cha kushangaza sisi unatudanganya unatuambia una viwanda una nini, kwako hakuna hata kiwanda cha kuchakata ndizi, hakipo. Naomba uoneshe mfano sasa wewe vinginevyo utaingia kwenye mkumbo wa Mawaziri hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika tumekuwa na changamoto katika historia ya Tanzania. Historia ya Tanzania tumeshuhudia kwamba Serikali imekuwa ikiyakopesha mabenki kutoka Benki Kuu kwenda kwenye benki ndogo ndogo wamekuwa wakiwakopesha. Wakikopesha fedha zile benki wananchi wetu wananufaika kukopa hususan akina mama ntilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwa mara ya kwanza Serikali ya Awamu ya Tano kunyang'anya fedha

kwenye mabenki na kuzirudisha Benki Kuu; jambo ambalo limesababisha sana kuyumba kwa uchumi. Lakini hizi fedha zingekuwa kwenye mabenki ya kawaida mama zetu wangeweza kukopa, lakini sasa hivi wamefungia kule benki tumebaki tunalia; mama analia, baba analia kila mtu analia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge *form one* tuliambiwa kwamba ukiwa Mbunge unakuwa na fedha nyingi sana. Lakini sasa hivi tunalia hata kuliko mwananchi wa kawaida. Jambo ambalo ni aibu kwa Taifa hili. Hata hivyo naamini kabisa kwamba Wabunge tuna hali mbaya lakini tunashindwa kulia kwa sababu ya utu uzima wetu, kwamba unawezaje kulia wakati na mtoto kule analia; kwa hiyo inabidi mama unyamaze kimpya uendelee kuumia polepole. Lakini mimi ninachokiamini kabisa ni kwamba baada ya miaka kadhaa tutajikuta tumepata maradhi ambayo yametokana na *stress* zilizosababishwa na ugumu wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba kusema sasa ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda atakapokuja kuhitimisha hapa nitahitaji kufahamu suala la viwanda vya *ginnery* vilivyokufa, ni lini vile viwanda vitafufuliwa, la pilli, nini tamko la Serikali itakapofika msimu wa kuuza pamba wananchi wauze kwa shilingi ngapi ili tuweze kuendana na kasi ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana Mungu akubariki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masaba. Nilikuwa nimesikia mahali kwamba Simiyu ndio inatoa mfano mzuri wa viwanda ama sijasikia sawasawa. Nimesikia Simiyu mna kiwanda sijui cha chaki, maziwa hebu tusaidie ni kwenu huko tunatakiwa kuja kujifunza au?

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Kiwanda ambacho Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anajifunia nacho ni kwamba kilianzishwa na kikundi cha

vijana kwa ajili ya kutengeneza chaki na Halmashauri ikaingia ikachukua hicho kiwanda. Kwa hiyo, ndicho tunachojivunia nacho. Lakini sisi tunadai viwanda vinavyotokana na pembe za ng'ombe tunaka tutengeneze hata vifungo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa sawa, mimi niliyekuuliza nimekuelewa. Mheshimiwa Nyongo nilikuwa nimemuuliza swali kwa hiyo alikuwa ananijibu mimi sasa hiyo taarifa labda kama unanipa mimi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Raphael Japhary Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuna hoja ambayo imekuwa-*raised* kwamba inawezekana ndoto yetu ya kufikia Tanzania ya viwanda ina mashaka makubwa. Lakini imeonekana kama vile ni uchokozi ambao upande mwingine haukuutaka. Lengo la Kambi ya Upinzani kuonyesha wasiwasi wetu kwa dhana hii kufikiwa, ni vizuri Serikali ikalichukulia hili kama changamoto na isiwe ni sababu ya kuanza kuleta malumbano yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1967 Tanzania ilishaanza hatua hizo za kujijenga katika dhana mzima ya *Industrial Revolution* na bahati mbaya tulienda na dhana hiyo tukiwa na mtu ambaye ni *dedicated* ambaye alikuwa Rais wetu wa Kwanza wa nchi hii. Hata hivyo mwaka 1996 dhana ile tuliiua wenyewe. Na bahati nzuri mwaka 1996 kwa lengo hilo la ubinafsishaji tulikuwa na dhamira kwamba tunaweza tuka-*develop* zaidi kama tutakuwa tume-*adopt* vizuri dhana ya ubinafshaji ambayo bahati mbaya hatukuweza kuifanyia kazi vizuri. Sasa wasiwasi wetu ni kwamba kama *Sustainable*

*Industrial Development Policy* ya tangu mwaka 1996 mpaka leo haijaweza kufanya kazi vizuri, nini miujiza ya kuifanya kwa miaka mitano? Ndio wasiwasi wetu. Sasa nafiki ni vizuri tungeichukua kama changomoto muhimu sana Serikali ilituweze kuifanyiakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kipindi hicho vikwazo vilivyokuwa vinakabili sekta ya viwanda ndiyo ambavyo viko sasa, tangu 1996. Wachambuzi waliokuwa wanatunga hii Sera ya *Sustainable Industrial Development Policy* waliona kwamba tuna vikwazo vya *unfavorable legal and regulatory framework* ambazo zilikuwa ni kikwazo kimojawapo, *limited access of SMEs to finance,* cha pili; cha tatu kilikuwa *infective and poor coordinated institutional support framework;* vitu ambavyo mpaka leo tunavizungumza kwamba ni tatizo katika nchi hii.

Sasa lazima tuone kwamba tuna mahali ambapo panatukwamisha na kwa pamoja tufikiri namna gani tunatoka hapa kwenda mbele ili tufikie hiyo ndoto ya Tanzania ya viwanda. Kwa hiyo ni vizuri mkaichukua kwa uzito wake hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ambalo linafanya tuone mashaka ya viwanda ni soko letu la ndani. Tuna soko la ndani la kiwango gani. Nini uwezo wa watu wetu kununua katika soko letu la ndani, *purchasing power* yetu. Ukizingatia kwamba viwanda anavyovihubiri Mheshimiwa Waziri ni viwanda vidogo sana vyenye kuajiri mtu mmoja mpaka watu watano; viwanda vidogo vinavyofuatia vyenye kuajiri watu watano mpaka watu 49 na viwanda vya kati vyenye kuajiri watu 49 mpaka 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vinategemea sana soko la ndani, soko ambalo hatuna kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano imechukua fedha zote ambazo zilikuwa za Serikali ikaziamishia Benki Kuu na ni sawa tu na hadithi ile ya mtu aliyechukua rupia akaifukia chini ya ardhi. Haiwezekani uchukue fedha zile ambazo zilikuwa kwenye mzunguko uzipeleke benki ukiamini ndio uwekezaji.

Kwa hiyo, matokeo yake tumepunguza sana mzunguko wa fedha katika uchumi wetu, tumepungusa uwezo wa uwekezaji katika uchumi wetu na kwa misingi hiyo *purchasing power* ya watu imepungua, sasa kwa hawa watu wanaozalisha wanakwenda kumuuzia nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio leo tunaambiwa kwamba kuna hata soko la kuuzia bidhaa za kiwanda cha bidhaa za kupambana na malaria zimekosa soko kwa sababu hatuna soko la ndani. Sasa tunafikiaje haya malengo? Hili ndilo suala la msingi la kujadili kwa pamoja ili tuone tunavyoweza kufikia lengo la kuwa na Tanzania ya viwanda. Kwa hiyo ni vizuri tukayachukua haya masuala kwa uzito wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wa ndani kama wengi walivyosema hawana mazingira rafiki ya kibiashara, kuna vitu vingi vya kuwakwaza, ni lazima tuviangalie, tuwapende wafanyabiashara wa ndani. Wafanyabiashara wa ndani tunawaumiza, tunaonekana kama hatuna haja nao, tunaonekana kuvutia zaidi wafanyabiashara wa nje ambao hata wenyewe hatuna vivutio vya kutosha vya kuwavutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri tuone namna gani tunajiweka vizuri katika maeneo hayo ili tufikie katika dhana ya Tanzania ya Viwanda. Kila mtu anaona uthubutu wa kufikia hiyo dhamira ya kuwa na Tanzania ya Viwanda iliyoonyeshwa na Serikali hii, lakini lazima sasa tuone tunafikaje katika hatua hiyo kwa pamoja wote kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na viwanda zaidi ya 15, leo hakuna kiwanda kinachofanya kazi ukiondoa Kiwanda cha Bonite peke yake. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini atahakikisha Kiwanda cha Madawa ya Mimea kinafanya kazi? Kiwanda kile kimewekeza fedha za Watanzania nyingi mno za mikopo lakini kiwanda kile hakuna siku kimefanya kazi na Watanzania wanadaiwa madeni kutokana na fedha ambazo Serikali hii ilikopa lakini

kiwanda kimekuwa pale ni *white elephant* haifanyi kazi yoyote mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aniasaidie ni lini kiwanda kile kitafanya kazi? Ni lini Kiwanda cha *Machine Tools* kitafanya kazi? Kiwanda ambacho katika zama za Mwalimu Nyerere kilikuwa ni kiwanda mama kama vilivyokuwa viwanda vya chuma vya Tanga. Kama ninavyozungumzia Liganga na Mchuchuma, lakini leo kiwanda kile hakifanyi kazi, na ni kiwanda ambacho kilikuwa ni cha tatu katika Afrika, lakini leo hakifanyi kazi; na mnaimba Tanzania ya viwanda, mnafikiaje hilo lengo la kufika Tanzania ya viwanda kama kiwanda mama hamuwezi kukifanya kikafanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa najiuliza kiwanda cha magunia Mheshimiwa Waziri umeorodhesha kwenye hotuba yako Kilimanjaro viwanda vimebinafsishwa havifanyi kazi. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira kwamba anataka Tanzania ya viwanda, kuna kigugumizi gani cha kuwanyang'anya wale watu viwanda ambao hawavifanyii kazi? Nini kigugumizi cha Serikali? Kwa nini hapo mnakosa uthubutu wa kufanya maamuzi magumu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama watu wamechukua viwanda tangu mwaka 1996 mpaka leo hawavifanyii kazi, ni kwa nini mnapata vigugumizi ya kuchukua vile viwanda? Kiwanda cha Magunia kilichokuwa kikiajiri watu wa Kilimanjaro leo hakifanyi kazi, kimekuwa *godown* la kuwekea bidhaa, kwanini tunawalea hawa watu na nyie mnaona ni jambo la kawaida. Bahati mbaya kuliko vitu vyote Serikali yenu haifanyi kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Moshi tumegundua kwamba hamtaki kufufua vile viwanda. Tumeanzisha mipango yetu ya kujiendeleza wenyewe, tumetaka kujenga stendi ya kisasa pale ya kushindana na soko letu lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI hataki kutupa kibali, kwa nini? Kwa sababu ni eneo la

upinzani ama sababu ni nini? Tumeomba kwamba Moshi iwe Jiji ina sifa zote, lakini leo tunanyimwa kwa nini? Sasa mtakuzaje huu uchumi na mnafikaje Tanzania ya viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa nafikiri ni vizuri kama kuna lengo la kufikia Tanzania ya viwanda tuone tunafikaje huko, lakini kuanza kuhujumiana kwa sababu za kisiasa ni jambo la ajabu sana. Kama hamtaki huu mfumo wa vyama vingi vya siasa futeni ili wengine tukafanye biashara zetu zingine kwa sababu hatuwezi kuja hapa kuwawakilisha wananchi, tujenge mawazo ambayo ni *constructive* halafu myakatae *unnecessary* bila sababu yoyote ya kimsingi, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natamani sana nione mlivyo-*link* katika suala la kufikia Tanzania ya viwanda, namna gani mnamsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Bashe amewaambia na Mheshimiwa Zitto amewaambia; namna gani mnamsaidia Rais ili ndoto yake itimie. *Otherwise* mtazungumza kama ilivyozungumzwa tangu mwaka 1967, mtazungumza kama ilivyozungumzwa tangu 1996 mpaka leo na mtazungumza mpaka miaka mingine 40 ijayo mbele hamuwezi kufikia Tanzania ya viwanda. Hatutaki kwamba mfike hapo, hii nchi ya kwetu wote, tunataka tu-*achieve* lengo la kuwa na Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima na nyie mheshimu mawazo ya watu wengine muone kwamba wanaweza wakafanya. Lengo la viongozi ni kuwa wabunifu, ziacheni Halmashauri Madiwani wabuni mipango yao na muwape *support* Madiwani. Acheni kule chini wafanyabiashara wafanye biashara zao vizuri, waacheni wamachinga wa-*develop* ili dhana ya *SME* ifanyike. Sasa msipoyafanya haya mnaifikiaje Tanzania ya viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimependa kuyaonesha haya kwamba Kilimanjaro tuna shida. Kiwanda cha Ngozi leo kinazalisha kidogo; Ofisi ya Makamu wa Rais,

Mazingira itusaidie kuhakikisha kwamba kile kiwanda kinatumia teknolojia ya kisasa; watu pale wanaumia kwa harufu ya kile kiwanda. Sasa hatutaki kifungwe kwa sababu hatuna viwanda, lakini tunataka kilazimishwe kuzalishwa ka teknolojia ya kisasa ili kulinda afya za watu wa Moshi maana kuna watu pale wanapata maradhi, mtawalipa na nini na mtawafidia kwa kitu gani kwa roho za? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba sana ichukuliwe kwamba lengo letu ni jema na ni la msingi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na Tanzania ya Viwanda kweli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana muda wako umeisha Mheshimiwa Japhary. Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nioneshe masikitiko yangu makubwa kwa Wizara ya Viwanda. Kimsingi niseme tu kwamba Kamati ya Bunge ambayo inasimamia viwanda na biashara ni Kamati ambayo inatakiwa imshauri Rais kuhusu mambo ya viwanda lakini kamati hiyo haijawahi kwenda hata gerezani kukagua viwanda wala haijawahi kwenda Kenya, China wala India; sasa sijui inamshauri vipi Mheshimiwa Waziri na viwanda vyake. Kwa hiyo, mimi nioneshe tu masikitiko yangu kwamba jambo hili si sahihi kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hasa nilitaka kuzungumzia maeneo kama mawili ama matatu na hasa nataka kuongelea *Tanzania and China Logistic Centre* ya Kurasini. Mara ya kwanza mradi huu ulizungumzwa katika ile *China-Africa Corporation* mwaka 2009 kule Cairo. Mradi huu mwaka 2012 ulianza kuingia katika Bunge na kuwashawishi Wabunge. Katibu Mkuu wa Viwanda sasa Dkt. Meru alikuwa wakati huo mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara alikuwa haondoki katika Kamati kama vile yeye ni Mjumbe wa Kamati na kuishawishi Kamati ikubali huu mradi wa Kurasini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianza kutathmini ile thamani ya wale watu ambao wanatakiwa kulipwa fidia, uthamini ule. Uthamini wakati huo ukawa shilingi bilioni 60, tukashawishiwa kwamba lazima tufanye uthamini haraka haraka ili muda usije ukaongezeka huyu mwekezaji akakimbia. Hata hivyo tukakaa kwa miaka mitatu baadaye, tulipokuja kulipa shilingi bilioni 60 tukaambiwa fedha zimeongezeka shilingi bilioni 40 tena. Kwahivyo, tumelipa shilingi bilioni 101 badala ya shilingi bilioni 60; lakini baadae tukaambiwa mradi huo haupo, mradi huo umekwenda wapi ooh yule mbia kaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna shilingi bilioni hizo zote zimelipwa wala huo mradi wenyewe haupo na tukashawishiwa kuambiwa kwamba mradi huu utaingiza ajira za moja kwa moja milioni 25 na ajira *indirect* zaitakuwa laki moja. Kwa hiyo, sisi tukaingia katika malumbano makubwa na Serikali kwenye jambo hili kutaka *EPZA* wapewe pesa ili huu mradi uweze kwenda. Mheshimiwa Mwijage mradi uko wapi? Mradi huna. Ukisoma huu mpango wa mwaka mmoja huoni hasa kipi ni kipi na Serikali ya China wakati ule ilisema kwamba itatoa shilingi bilioni 600 tukilipa shilingi bilioni 60, jambo ambalo mmetudanganya, hakuna kitu kinachoendelea baada ya miaka minne. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwijage nataka ujibu hasa, usije ukatuambia maneno ya ajabu ajabu, uje ujibu hasa kwa nini mradi huo haupo na fidia imetolewa na fedha zimeongezeka na lini mradi huu utaanza na upo katika mpango wa mwaka mmoja, sidhani kama katika mpango huu tunaweza kuona jambo hilo, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia *Mini Tiger Plan* ambao mimi nina *interest* kwa sababu mradi ule ikiwa utasimama basi na Zanzibar itafunguka kiuchumi. Kwa hiyo, huu ni mradi kila siku nilikuwa ninauombea dua, ulikuja nao mwaka 2002. Ule mradi ukasema kwamba una awamu mbili; awamu ya kwanza ni kulipa fidia hekta 2500 lakini tufanye kwa ujumla, mpaka sasa kumelipwa shilingi bilioni 26.6; zinahitajika kulipwa shilingi bilioni 51.1 lakini mradi haupo

na baadhi ya watu 1700 wamelipwa fidia na wengine hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujua kwamba huu mradi upo? Ukitizama kitabu chenu cha Mpango wa Maendeleo ya mwaka mmoja utakuta kwamba hata huyo mwekezaji hayupo. Wakati ule tulikuwa tukiambiwa Oman na China wapo watakuja, na lakini Mheshimiwa Rais pia mwenyewe kasema kwamba hiyo sio *priority* yake. Pale palikuwa pana mradi wa bandari na viwanda lakini humu ndani mnasema kwamba mtajenga barabara katika eneo hilo la Bagamoyo, reli, umeme na maji. Ni reli gani itakayokwenda kule kwa mwaka mmoja? Jamani tuwe *realistic* katika mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, Mheshimiwa Mwijage utujibu, na huu mradi upo? Isije ikawa kama tulivyofanyiwa Kurasini, watu walikuwa wana *deal* yao wakalipwa fidia na baada ya kulipwa fidia mradi ukapotea na huku mnataka muwalipe watu fidia halafu mradi upotee kama ambavyo mmetufanyia huku. *Safari hii tunazaa na wewe Mheshimiwa Mwijage. (Makofi)* **[Maneno Haya Sio Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha za *CBE* shilingi milioni 400 ambazo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali kwa ajili ya kuweka kumbukumbu vizuri hebu ondoa hayo maneno yako ya utazaa na Mheshimiwa Waziri.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeondoa hayo hayana tatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, milioni 400 *CBE* zimetafunwa na Mkurugenzi wa Fedha pamoja na Mkuu wa Chuo. Jambo hilo alilisema Mheshimiwa Waitara mwaka wa jana hapa, lakini hakuna ripoti yoyote. Badala ya kwenda kufanya ukaguzi Dar es Salaam ambapo ndiko zilikoliwa ninyi mkaenda mkafanya ukaguzi Dodoma na Mwanza, inawezekanaje?

Fedha zimeliwa kwa wengine mnakwenda kufanya ukaguzi kwa wengine... *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa anayechangia kwamba jambo hilo lilikuja Bungeni bajeti iliyopita 2016/2017; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Katibu Mkuu wanalijua. Katibu Mkuu aliandika barua ya terehe 19 Mei, 2016 kuomba ukaguzi akataja vyuo vinne Dar es Salaam *CBE* ambayo kuna shilingi milioni 400 anasema na utumishi mbaya wa madaraka, Mwanza, Dodoma na Mbeya. Taarifa zilizopo ni kwamba ukaguzi umefanyika Mwanza na Dodoma peke yake na Dar es Salaam taarifa haipo. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa kamili iliyopo na makablasha yapo hapa na Mheshimiwa Waziri anayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ngwali nakupa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea taarifa hiyo kwa upendo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende sasa katika misamaha ya kodi. Nakubaliana na alichosema jana ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba kuhusu misamaha ya kodi na kodi ambazo zinasumbua hasa upande wa *Tanzania Investment Centre*. Lakini ukija sasa kwenye maeneo ya uwekezaji *SEZ* misamaha ya kodi ambayo ipo haina haja ya kuongezwa tena, ni mingi sana. Naomba nisome baadhi ya misamaha ya kodi ambayo inawavutia wawekezaji katika eneo la uwekezaji la *SEZ.* Msamaha wa malipo ya kodi ya ushuru kwa mashine, vifaa, magari ya mizigo, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine yoyote ya mtaji mkubwa itakayotumika kwa madhumuni ya maendeleo ya miundombinu ya

uwekezaji katika maeneo maalum ya *SEZ*, huo ni msamaha wa kwanza. Lakini msamaha wa pili ni msamaha juu ya malipo ya kodi kwenye kampuni katika kipindi cha miaka kumi, msamaha wa tatu ni msamaha juu ya malipo ya kodi ya zuio la kodi, gawio na riba kwa miaka kumi, msamaha juu ya malipo ya kodi ya malipo kwa miaka kumi, msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine; msamaha wa malipo ya ushuru wa *stamp* kwenye vyombo vyote vinavyofanya hivyo na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upendeleo ya uhamiaji hadi wa watu watano katika kipindi cha mwanzo cha uwekezaji na baadae wakizingatia masharti wataongezwa; msamaha wa malipo ya *VAT.* Kwa hiyo, kuna misamaha katika *SEZ* ambayo ni mingi sana *EPZA,* hakuna haja ya kuongeza misamaha kwenye eneo hilo. Tuangalie zaidi kwenye *TIC* tujue ni namna gani tunafanya*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kuhusu *PVoC;* tunazungumza ile *Pre-shipment Verification of Conformity*. Eneo hili ilipitishwa programu ya kuzuia bidhaa bandia kuingia ndani ya nchi, tukapitisha hiyo na *TBS* ikapitisha. Lakini jambo la ajabu toka mwaka 2012 bidhaa bandia zimezagaa katika Tanzania, *TBS, FCC* na *FDA* wapo. Sasa namna gani bidhaa zinazagaa? *TBS* aidha hawafanyi kazi yao vizuri kwa sababu kwanza kuna tatizo, tatizo lililopo ni kwamba *TBS* wanazuia *sub-standard* lakini hawana uwezo wa kuzuia *fake* kwa sababu s*ubstandard* na *fake* ni vitu tofauti*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikiwa chini ya kiwango na kitu *fake* vinatofautiana kabisa, kwamba ikiwa chini ya kiwango maana yake ni kwamba kile kitu sio halisia lakini halisia, unaweza kitu *original* kimetengenezwa na Kampuni ya *Sony* akakitengeneza mtu katika eneo vile vile kuliko kile lakini hicho kikawa ni fake na si *sub-standard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bidhaa bandia Mheshimiwa Mwijage kila kona ya Tanzania inatusumbua. Mkiulizwa kila siku mnasema mnawafanyakazi kidogo na kuna vituo vingi, maana kuna vituo 38 au 48 lakini mnadhibiti

vipi bidhaa *fake*? Hiyo ndio *issue* yetu tunataka. *TBS* wamekwenda mbali Tanzania mpaka tunaingiza mafuta machafu, *TBS* wanakwenda kukagua wanaruhusu mafuta machafu yanaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi leo nilikuwa na hayo lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mwijage... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngwali. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake wameandaa hotuba nzuri sana ambayo nadhani imetupa changamoto ya kuijadili hapa ndani. Vilevile ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, yeye ana jina lake ambalo kule mtaani katika vile viunga vya viwanda tunamuita mzee wa *sound,* halafu anasema kwamba yeye mke wake anamwita ni *handsome boy.* Kazi yake ni nzuri sana Mheshimiwa *handsome boy,* Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuzungumzia masuala makuu matatu. La kwanza, kuna haja kubwa sana sasa ya kujaribu kuoanisha vizuri sana kazi anayofanya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na kazi ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaifanya, kwa sababu pale ndipo tunapoanzia kutofautiana. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anafanya kazi kubwa sana ya kupiga debe na kuhakikisha hii *philosophy* ya uchumi wa viwanda inaanza kwa kasi sana hapa nchini, lakini bado kuna *hiccup* kubwa sana upande wa Wizara ya Fedha; kwa sababu huyu

ataweza tu kuwa na *philosophy* ya uchumi wa viwanda kama na mambo yote yanayohusu mambo ya kodi na vivutio kwa wawekezaji yanakwenda samabamba. Vinginevyo itakuwa ni wimbo ambao utaendelea kuimbwa na hatutapata majibu ya haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimuombe Mheshimiwa Waziri atoe tafsiri zaidi anaposema viwanda, kwa sababu tumekuwa tukichangia hapa tunasema mimi kwangu hakuna kiwanda, viwanda vimesimama sijui magunia na kadhalika. Tafsiri ya kiwanda kutoka kwa *industrial economist* ni kitu chochote ambacho kinaweza ku-*transform* bidhaa moja kwenda kuwa bidhaa nyingine inayoweza kutumika. Kama ni mbao kuwa kitu au meza na kadhalika, kama ni kuchanganya dawa basi iweze kutumika kama dawa na kadhalika, *from chemicals to drugs.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika hali ya kawaida bado tunapata ukakasi kwamba ni namna gani tunazungumzia dhima nzima ya uchumi wa viwanda. Ukiangalia Serikali inajaribu kuweka miundombinu na mazingira ya kumfanya mfanyabiashara au biashara iweze kufanyika hapa nchini.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu kwa miaka mitano iliyopita, Tanzania tumeweza ku-*export* nje, India bidhaa zenye thamani ya dola bilioni 1.12, Kenya dola milioni 793, *South Africa* dola milioni 698, China dola milioni 620, Japan dola milioni 370. Lakini tumeweza ku-*import,* Saudi Arabia peke yake ni bidhaa za zaidi ya shilingi bilioni 5.6, China shilingi bilioni 2.23, India shilingi bilioni 1.24, Uarabuni shilingi milioni 789 na *South Africa* shilingi milioni 567. Kwa hiyo, ukiangalia Tanzania tumeweza ku-*export* lakini tumeingiza zaidi na hii ndiyo changamoto ambayo inaanzia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika sura nzima, maeneo ya msingi lazima tuangalie namna ya kuweza kuongeza uwekezaji utakaoondoa ukiritimba wote na kuongeza ajira na tija kwa Watanzania, bila kufanya hivyo tutaimba wimbo huu hatutafanikiwa kuufikia. Hii nasema kwa

sababu kumekuwa na tatizo kubwa sana sasa hivi hasa la wawekezaji. Wenzangu wamesema, nisingependa kurudia kwamba nchi yetu lazima tuweke utaratibu utakaoweza kuwa rafiki kwa wawekezaji kuwekeza hapa nchini. Mtu hawezi kuwekeza hapa nchini kama kuna *uncertainties* na *unpredictable tax regimes,* haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninachoomba sana katika hili tumsaidie Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, si la kwake peke yake; na Bunge hili tuna jukumu la kuishauri Serikali yetu, kwamba ni namna gani masuala haya yanaweza kuoanishwa na kuhuishwa kwa ajili ya kuchochea uwekezaji hapa nchini. Sisi si kisiwa, Tanzania tuna vivutio vingi sana, tuna maeneo mengi sana ya kuwekeza lakini sisi na wenzetu tuna-*compete* hivyo lazima tuweke mazingira ambayo yatajenga *assurance* kwa mwekezaji anapokuja hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutambue uwepo na ushiriki kamilifu wa sekta binafsi, hili ni suala la msingi sana. Najua tumekuwa na kasumba kwanza kutokutaka kuipenda *private sector,* lakini Waheshimiwa Wabunge, bila kuipenda *private sector* na kuipa nafasi ya ushiriki vizuri hatutaweza kutoka hapa tulipo. Acha Serikali iwekeze pale ambapo panatakiwa huduma itolewe na pengine pasipo faida, lakini maeneo ambayo yanahitaji kupata faida tuwekeze zaidi kwa hawa wawekezaji binafsi na tuingie utaratibu wa *PPP*, huu utasaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kutumia fedha zake katika kuwekeza na matokeo yake tuisaidie *private sector* iweze kuwekeza zaidi, Serikali inachotakiwa pale ni kuvuna kodi. Mimi naomba sana hili tuweze kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuangalie mustakabali mzima kwamba Watanzania tunatoka hapa tulipo namna gani, uwekezaji huu unakuwa na tija gani kwa Mtanzania, lazima tupate tija ya uwekezaji huu katika huduma za afya, elimu na kadhalika. Hata hivyo tatizo lililopo sasa hivi ni mitaji, *liquidity* sasa hivi kwenye *economy* imekuwa *so tight, lending rates* zimekuwa kubwa, watu wanashindwa kukopa fedha na kuwekeza. Njia pekee ni ku-

*attract* mitaji kutoka nje ili kusaidia kuwekeza hapa nchini lakini tutafanya vile kama wawekezaji hawa tutawawekea mazingira mazuri ya wao kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na hadithi ya Mchuchuma na Liganga miaka nenda-rudi. Mheshimiwa Waziri, hebu tusaidie, pale ambapo unadhani kabisa kwamba inakushinda naomba Bunge hili likusaidie ili utusaidie tutoke hapa tulipo tuache kuimba nyimbo na ngonjera za kila wakati. Ukiangalia ufanyaji biashara hapa Tanzania kila kukicha unakuwa ghali zaidi. Kwenye sekta ya utalii peke yake kuna kodi zaidi ya 36, hivi kweli mtu atawekeza kwa kodi hizi 36? Haiwezekani! Mimi sitaki kuzisoma, ni nyingi sana. Kitu ambacho ninaomba sana Serikali yetu ijaribu kuwa sikivu, na hasa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita niliwahi kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie na kusaidia maana yake ni kwamba ajaribu kuwa kiungo na si mtenganishi wa masuala ya uchumi katika nchi. Nina imani kabisa kwamba Watanzania kama tutafuata msingi mzuri wa uwekezaji, tutasonga mbele. Dhima na dhana aliyonayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ni nzuri, tunamsikia kila mahali anazunguka, hata ukikutana naye ukamwambia Mheshimiwa nataka kiwanda, anakwambia ntakupa kiwanda, anakupa hata matumaini hata kama hana, hiyo inatosha Mheshimiwa Waziri, unatupa matumaini. Hata hivyo ninaomba utuambie hapa vizuri zaidi tafsiri ya viwanda ili tuweze kuelewa kwa sababu unapotuambia viwanda tunawaza viwanda vikubwa tu. Kuna viwanda vidogo, vya kati na vikubwa, lakini kunakuwa na *linkage* ambayo inakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunasifika kwa kuwa na uchumi unaokuwa pamoja na sera nzuri au tulivu za uchumi. Hizi lazima ziwe *translated* katika mahitaji ya Watanzania. *Level* ya umaskini Tanzania bado ipo katika kiwango cha juu na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais anasema sitaki kuona wananchi masikini wanateseka, *he is for the poors,* lakini sisi tunafanya nini kusaidia kauli mbiu hii.

Mheshimiwa Rais amejitahidi sana na kwa muda mfupi tunaweza kuona kwamba nchi sasa inaanza kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanzisha na miradi ambayo ni mikubwa yenye kusimika uchumi wa nchi, kwa sababu bila kuwa na *logistics and division systems* huwezi ukapanua nchi yako. Lakini sisi kama Tanzania, leo ujenzi wa reli ni mardi mkubwa sana, unahitaji gharama kubwa sana lakini pindi utakapokwisha utakuwa ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Janeth Mbene ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi siku ya leo kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa jitihada mbalimbali zinazofanyika katika kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inafikiwa. Pia ninashukuru kwa sababu dhana hii inapozidi kuzungumzwa sana, mwisho wa siku inatafsirika na watu wanaamini na wanaingia katika uwekezaji wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu hiyo Mheshimiwa Waziri mimi nijielekeze, najua unajua nikisimama kuzungumzia kiwanda siwezi nikazungumza mambo mengine nikakiacha kile kilichopo pale kwangu Manonga, *Manonga Ginnery.* Mheshimiwa Waziri toka nimekuwa Mbunge na siku yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya Bunge, nimezungumzia suala la Kiwanda cha Pamba ndani ya Wilaya yetu ya Igunga. Kiwanda hiki ni cha zamani sana,

toka enzi za mkoloni mpaka juzijuzi kikabinafsishwa akapewa Rajan, Rajan amekiendesha mpaka na yeye akakishindwa akakiacha, amefikia hatua amefariki, amemuachia mtoto wake, mtoto wake yuko Uingereza mara sehemu mbalimbali. Tumezungumza tukakwambia wapo Igembensabo wanakitaka hiki kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki asilimia 80 anamiliki Rajan, asilimia 20 anamiliki Igembensabo. Igembensabo anataka kukinunua hiki kiwanda, ameweka mezani shilingi milioni 500 lakini Rajan amekinunua shilingi milioni 700 anataka kukiuza shilingi 1,500,000,000, kiwanda kimesimama anataka kukiuza kama vile kinafanya kazi, kinaingiza faida na huyu ni mbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, lakini tulikuomba uwakutanishe hawa watu wakae chini, wao wako tayari. Umetuahidi mara nyingi hawa watu utawakutanisha wakae chini wazungumze Igembensabo yuko tayari, hata wao wako tayari, *issue* yako kama Waziri ni kuwaita hawa ofisini kwako. Juzi juzi hapa katika majibu umesema umefanya jitihada mbalimbali, umetuambia kwamba huyu mtoto wa Rajan yuko Uingereza anakuja baada ya miezi sijui sita au saba, anachelwa. Hivi Serikali hii ya Dkt. John Pombe Magufuli ikitaka kumuita huyu kijana itashindikana kweli? Yaani akakae Uingereza na kiwanda chetu huku, kama hataki kukiendeleza si akiachie wapewe watu wengine waweze kuki-*run*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siamini kwamba Serikali hii imeshindwa kumuita, haiwezekani na siamini. Inawezekana, labda Mheshimiwa kwa sababu wewe unasema unapiga-*sound* inawezekana na mimi kijana wako unanipiga *sound,* nielewe kwamba hiyo ndiyo sehemu ya kupigana *sound,* lakini mimi siamini kwamba wewe zile *sound* unazosema unapiga unamaanisha kwamba unanipiga *sound* kweli. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, hebu muite huyu kijana ikiwezekana, kama inashindikana si mkitaifishe sasa, mmeshamuita amekataa. Inawezekana hamjamtafuta na wao wako tayari kuja. Mheshimiwa Waziri tunakuomba, na

Mbunge mmoja wa Simiyu amesema eti zao la pamba limekufa, si kweli, halijafa, uzalishaji wake umepungua na si kufa. Maana yake ukisema kufa maana yake watu hawalimi kabisa, haiwezekani, kulima tunalima ila si katika kiwango ambacho Serikali ama nchi inataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli uzalishaji wa pamba umepungua si tu katika eneo letu la Wilaya ya Igunga ama Simiyu, katika nchi yetu ya Tanzania uzalishaji wa pamba umepungua; na Serikali haijawekeza vya kutosha na kama hivyo viwanda, *ginneries* zipo nyingi zimetajwa, na moja wapo ya *ginneries* kongwe hii ya Manonga ni *ginnery* kongwe. Katika Mkoa wa Tabora ukizungumza Manonga hakuna ambaye hajui, hakuna Rais ambaye hajui *ginnery* hii, lakini sijaona Serikali ama Waziri ukiwekeza katika kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinafanya kazi. Waweke chini hawa watu wafanye mazungumzo, watauziana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Tabora uangalie hizi fursa. Sisi tunalima sana maembe Mkoa wa Tabora, tuna nyuki, tumbaku, ngozi nyingi sana, hasa kwa sababu tuna ng'ombe wengi. Hivi Mheshimiwa katika makabrasha haya hauhamasishi katika uwekezaji huku kwetu? Maana kila siku ninasikia tulikuja mpaka *airport* wawekezaji wameondoka tena, hivi wawekezaji wa kuishia *airport* kweli? Hawa walikuwa wawekezaji au wasanii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri, hebu sukuma hili jambo ili kila mkoa uwe na fursa maana ukizungumza viwanda hapa vingi viko pwani na sisi huko kwetu Bara tunahitaji viwanda hivi vije, maana viwanda vikiwepo vitapunguza msongamano wa vijana kuwepo Dar es Salaam. Ndiyo hii unasikia kila siku Dar es Salaam vijana wanavuta bangi, wanavuta dawa za kulevya, hizi vurugu zote zipo Dar es Salaam huko na miji mingine huku kwetu haipo katika kiwango hicho. Hebu tuletee hivi viwanda huko vijana wasikimbie vijijini ama wasikimbie wilayani wakakimbilia mikoa ya pwani huko. Hii itasaidia sana kwa sababu leo hii wanabaki bibi zetu kule nyumbani kwetu wanaonekana vikongwe hawa ama wachawi. Hebu

muache kuleta hii dhana, leteni hivyo viwanda ili kupunguza, vijana wawepo wawasaidie wazazi wao, waendeleze maisha na itasaidia kuokoa maisha yetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hili suala la ngozi limekuwa linazungumzwa sana. Ni kweli tunataka tuwe na viwanda vya ngozi ndani ya nchi yetu, sasa ngozi imekuwa nyingi kiasi kwamba wanunuzi hawapo. Tumeweka kodi ku-*discourage* ku-*export* ngozi yetu nje ya nchi, lakini sasa hawa ambao tulionao viwanda vyetu havitoshelezi kununua ngozi, mwisho wa siku ngozi zinabaki kwenye machinjio, watu wananunua wanaacha katika maeneo yao. Hebu tupunguze kodi ama tuwa-*encourage* hawa watu ili kama tumeshindwa kununua ngozi yote badala ya kuharibika wai-*export* tupate hizo dola ambazo zinatoka nje ya nchi ziingine ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Waziri nafikiri hilo utakuwa umelisikia na utawasaidia hawa wafanyabiashara wa ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine mimi ninalotaka kulizungumzia ni hii *issue* ya *One Stop Center.* Leo tunaona mtu anapokuwa na kiwanda chake wanakuja watu wa *OSHA, NEMC,* madubwasha yako mengi. Kwa nini isiwe kwamba mtu yeyote anayetaka kuanzisha kiwanda aende sehemu moja, kama ni *TRA* alipie madubwasha yote, yeye pale apewe karatasi au *sticker* moja ambayo ndani yake yumo *OSHA, NEMC, TRA* na watu wote ili akija mtu wa *NEMC* iwe ni kujiridhisha tu. Sasa mtu ana kiwanda anaki-*run,* siku mbili anakuja *OSHA* anampiga faini anamwambia funga kiwanda, mtu amewekeza kwa gharama kubwa halafu anaambiwa funga kiwanda. Hebu tuwe sehemu ya ku-*encourage* viwanda vyetu na tuwe sehemu ya kuwasahihisha wenye viwanda ili waweze kuendelea kufanya hii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi viwanda vinasaidia kutoa ajira kwa vijana wetu na hii inasaidia kupunguza tatizo la vijana mitaani. Unapo-*discourage* watu wa viwanda unasababisha hawa vijana warudi mtaani wanageuka majambazi, wanageuka vibaka na hatimaye hawa hawa wanageuka kuwa watu ambao si watu wema katika jamii. Tuombe Serikali iwasaidie wenye viwanda hata kama wana

matatizo ninyi muwe sehemu ya kutatua matatizo yao na msiwe sehemu ya kuzuia kufanya miradi au kazi zao. Niombe Wizara, nafikiri mtakuwa mmelisikia hilo; naomba sana muwasaidie wafanyabiashara, maana yake tafsiri ya mfanyabiashara sijaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachojua, mfanyabiashara ni Mtanzania yeyote ambaye anaanza kutafuta kipato chake, mkulima ni mfanyabiashara. Kuna mkulima gani ambaye anazalisha chakula halafu asikiuze? Huyo si mfanyabiashara. Mkulima ni mfanyabiashara kwa sababu anazalisha, anauza. Mwalimu anafundisha, ama sisi Wabunge hapa, wengine tuna hoteli, tuna *guest houses,* tunafanya biashara, maana biashara ikiharibika mpaka kwenye hoteli zetu biashara zinaharibika huko. Humu ndani ya Bunge katika asilimia 100, asilimia 99 ni wafanyabiashara, tunatofautiana biashara gani tunafanya. Unaweza ukawa Waziri ukawa mfanyabiashara. *(Makofi)*

Suala lingine kabla sijafika mwisho, nafikiri muda wangu utakuwa si rafiki; kuna mtu alichangia jana hapa akasema Rais wa Kenya amepata chakula kutoka Mexico na chakula kile kinagawiwa kwa bei ya kutoka shilingi 3,000 ya Tanzania kwa maana ya *Kenyan shilings* 150 kupunguza kwa shilingi 90 ya Kenya sawa na 1,800 ya Tanzania. Hivi kwa saa 24 inawezekanaje Rais akatoa tangazo halafu bei ikashuka kwa kiwango hicho, inawezekana kweli au tunaleta propaganda ndani ya Bunge hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hata kule alikosema kwamba ametoa chakula kile, Mexico, kwanza tutambue, Kenya sasa hivi kuna Uchaguzi Mkuu, Uchaguzi Mkuu ni *pressure* kwa Rais aliyepo hata kwa wapinzani. Kwa hiyo kinachofanyika ndani ya nchi ya Kenya ni siasa, tunachozungumza leo Balozi wa Mexico amekanusha amesema kile chakula hakijatoka Mexico, kwa hiyo tusidanganyane. Mtu analeta taarifa za kutoka huko anasema kwamba eti Kenya wameshusha bei ya chakula, chakula kingi kiasi kwamba..., tuzungume ukweli pale ambapo panastahili ukweli... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, muda wako umekwisha Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, viongozi hawa wameutendea haki Mkoa wa Pwani. Kwa nyakati mbalimbali wamefika kutufanyia shughuli mbalimbali za uwekaji wa jiwe la msingi, ufunguzi na hata ukaguzi wa viwanda mbalimbali vinavyoendelea kujengwa katika Mkoa wetu wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoto ya Mheshimiwa Rais ambayo imeelezewa kinagaubaga kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwangu mimi naiona ina mwelekeo mzuri wa kutimia. Kwa nini nasema hivyo, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ninampongeza sana kwa kazi nzuri kama nilivyotangulia kusema, katika ukurasa wa 16, tofauti na hotuba ya mwaka jana ameeleza kinagaubaga miradi ya viwanda tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo wa 16 mpaka 29 katika moja ya aya kwenye hotuba yake, ameeleza viwanda vikubwa 393 vyenye jumla ya mtaji wa dola za Kimarekani milioni 2000, kama shilingi trilioni 5,000 na ameeleza; ukisoma hotuba yake na ukisoma viambatanisho

vyake, majedwali kuanzia 7(b), 7(c) na 7(d) utaona kabisa ni aina gani ya kiwanda, mwekezaji, ajira ngapi zitatekelezeka na ni *investment* ya kiasi gani. Kwa hiyo, mimi nadhani kwa maelezo yale inatosha kabisa kutoa dira kwamba sera hii ya uchumi wa viwanda inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naomba nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa wa Pwani, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi kwa kuandaa mazingira wezeshi ya viwanda vyetu. Hapa naomba nisemee viwanda vya chuma vilivyopo Kibaha, cha Kilua, Kibaha Mjini na Mkuranga na ninaomba pia nijielekeze kwenye viwanda vya usindikaji matunda vilivyopo Mboga ambacho kinakaribia kukamilika, Bagamoyo pamoja na Mapinga.

Vilevile naomba nijielekeze, na nipongeze naweka kumbukumbu kwenye *Hansard* na mimi mwenyewe binafsi baadhi nilivitembelea, Kiwanda vya Vigae kilichopo Mkuranga ambacho ni kikubwa sana, kinatarajia kutoa ajira 4,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ninaomba nijielekeze kwenye eneo letu la viwanda la *TAMCO* na nimeona nia ya Serikali ni njema, na ukiangalia hata bajeti ya maendeleo ya Wizara hii imeongezeka. Mwaka wa jana tulilalamika hapa zilitengwa shilingi bilioni 40, lakini Serikali imeonesha dhamira, imetenga shilingi bilioni 82, ni zaidi ya mara mbili ya pesa ambazo imetengwa mwaka wa jana. Ndani ya pesa hizi zimetengwa kwa ajili ya eneo la viwanda la *TAMCO,* Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, eneo lile kama ambavyo limeelezwa na Kamati yenyewe, kama ambavyo Serikali imeeleza namna gani eneo lilivyopangwa, upembuzi yakinifu umekamilika, ramani yake imekamilika, tunatarajia viwanda vya nguo, kuunganisha magari, dawa za binadamu pamoja na viwanda vya aina mbalimbali. Pia ninaiona dhamira ya Serikali, hasa kwa kutumia mifuko ya hifadhi ya jamii kujenga viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizoea mifuko hii kujenga nyumba mbalimbali ambazo tunaziona sasa hazina soko, lakini dhamira ya kutumia mifuko hii, tumeona ni namna gani mifuko hii inavyoshirikiana ikajenga kiwanda kikubwa cha sukari Mkulazi, naunga mkono. Vile vile tumeona namna gani mifuko hii inayoshirikiana na *MSD, TIRDO, Tanzania Investment Bank* kujenga viwanda vinavyotumia mazao ya pamba. Kwa hiyo, unaiona dhamira ya Serikali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba niulize; Wilaya yetu ya Rufiji ina maeneo ambayo tuliyatenga kupitia *RUBADA* na kuna maeneo yalikuwa yanatolewa na tulikuwa tunatarajia kujenga viwanda vya sukari, Mheshimiwa Waziri sijaona mahali popote alipotaja juu ya ujenzi wa viwanda hivi katika Wilaya yetu ya Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, pia Wilaya ya Kisarawe tulipima eneo *(Kisarawe Industrial Park),* lipo tayari na tulijitahidi kama Halmashauri na Serikali Wilayani mpaka miundombinu, lakini pia sijaona litajwe popote. Lile eneo lipo sehemu nzuri, limepitiwa na reli ya kati, limepitiwa na reli ya *TAZARA*, lipo karibu na viwanja vya ndege Dar es Salaam na pia lipo karibu na bandari. Kwa hiyo, unaona mkoa wetu umekaa kama mkoa wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali, mwekezaji yeyote atahitaji athibitishiwe usalama wake, lakini pia anahitaji vivutio mbalimbali. Nina imani baada ya mkutano wa Mheshimiwa Rais na Baraza la Biashara pamoja na sekta binafsi, nina imani majadiliano yatakayoendelea ndani ya Bunge hasa itakapofika wakati wa *Finance Bill,* vikwazo mbalimbali vya kisheria, vya kodi na vya vivutio nadhani vitapatiwa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza kwenye mchango wangu kwamba wawekezaji wetu hasa wa Mkoa wa Pwani wanahitaji ulinzi wa mali zao. Naiomba Serikali, pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea, lakini kuimarisha ulinzi wa maeneo yetu. Naamini wawekezaji pamoja na nia waliyoonesha, lakini kwa matukio

yanayoendelea pamoja na kazi nzuri ya Serikali, yanaweza kabisa kufifisha jitihada hizo za uwekezaji katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote haya yanakwenda sambamba na namwomba Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo ameonesha kushirikiana na Waziri wa Wizara ya Maji, basi Wizara ya Kilimo na Mifugo, Wizara ya Fedha, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Miundombinu na Wizara nyingine za kimkakati zijitahidi kufanya kazi kwa pamoja na Wizara ya Nishati na Madini ili kuonesha yale mambo yanayotegemeana na viwanda ili yaweze kufanyika kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sisi kama Wabunge, binafsi mimi ninayetokea Mkoa wa Pwani, naamini wajibu wangu ni kuhamasisha wananchi wa maeneo haya kutumia fursa ya viwanda vizuri. Viwanda vyetu vitahitaji rasilimali, niwaombe vijana, wanawake na wananchi wa Pwani kutumia fursa ya viwanda vizuri. Tulime kilimo ambacho kitaleta tija, tujitoe kufanya kazi katika hivyo viwanda ili ajira inavyosemekana, nimepiga mahesabu, ajira katika viwanda vyote vinavyotarajiwa Mkoa wa Pwani ni kama 10,000 zile za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo ajira chache. Fursa hii isije ikaonekana kwamba viwanda vinajengwa lakini ajira nyingi zinakwenda nje; sitarajii kwamba iwe za Pwani tu peke yake, lakini wote ni Watanzania, tuzitumie fursa hizo lakini wenyewe pia wa Mkoa wa Pwani tuzitumie fursa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimalizie kwa kuomba Wizara ya Viwanda na Biashara ulipaji wa fidia. Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo amezungumza leo na hili jambo kwa kweli katika maeneo yale; na maeneo haya ya kimkakati kwa uwekezaji yanasaidia mno, ni maeneo maalum. Tulitembelea eneo maalum la Benjamin Mkapa *(Special Economic Zone),* tumeona viwanda vya nguo vilivyo pale, tumeona ubora wa bidhaa wanazozitengeneza,

tumeona namna gani hata viwanda vile vilivyopo pale Benjamin Mkapa *(Special Economic Zone)* havijaweza kukidhi soko. Zaidi ya asilimia 30 bado halijakidhi soko la nje. Kwa hiyo, nina imani Serikali ikilipa fidia katika maeneo yote yaliyotengwa nchi nzima na kwa wakati na wawekezaji wakapatikana, uwezo wa kuzalisha bidhaa na kuzisafirisha nje ya nchi upo na masoko yapo.

Mheshimiwa naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa na naendelea kuamini Sera ya Viwanda, Uchumi wa Viwanda itawezekana. Naendelea kuamini changamoto zilizopo zinaweza zikatatuliwa mezani; na naendelea kuamini Mheshimiwa Rais ana nia njema na ipo siku tutashuhudia mapinduzi makubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Janet Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa ya kuiona siku hii ya leo, lakini vile vile naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mwijage, Waziri wa Viwanda, kwa kweli ametutendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hotuba kwa mtu ambaye anataka kuisoma na kuielewa, kwa kweli hakupaswa hata kuwa na maswali humu ndani. Nampongeza sana kwa kuwa hotuba hii imesheheni kila aina ya taarifa. Kuna takwimu, kuna maelezo, kuna mchanganuo; sasa sijui mtu unalalamika kuwa dhana ya viwanda huioni, unataka uione vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, safari hii huu mkakati

jamani utafanyika. Kwa vielelezo hivi vilivyomo humu ndani ni wazi kabisa viwanda vitakuja kufanyika. Mifano, tumeshaiona, viwanda vipya vimeshajitokeza vingi sana; someni haya majedwali jamani! Kama hamtaki kusoma hii *literature* yote kubwa, nendeni huku nyuma kwenye majedwali, yameainishwa kiwanda kipi, wapi, ukubwa gani, kwa faida ipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niipongeze sana Serikali yangu, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wote walioko chini yake. Kwanza tunaambiwa kabisa katika maendeleo yoyote ya uchumi duniani, nchi lazima iwe na *political commitment. Commitment* tumeiona kwa kupitia Rais wetu na Marais wengine wote waliopita. *Commitment* ya kuwa na viwanda nchi hii imekuwepo na sasa hivi ndiyo imetiliwa mkazo zaidi kwa kuweka kabisa mkakati wa kuwa sasa hivi tunaelekea kwenye maendeleo ya viwanda peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala linalofuata ni taasisi. Tunaambiwa kabisa ili nchi iendelee au ionekanae kuwa inaendelea inapaswa kuwa na taasisi muhimu. Taasisi hizo zinahusiana na masuala ya hatimiliki. Sisi chini ya Wizara hii tuna Taasisi ya *Property Rights*, tuna Taasisi zinazosimamia ubora wa mazao au bidhaa, tuna taasisi zinazosimamia miundombinu ya viwanda vidogo na vikubwa, tuna taasisi zinazoshughulikia usuluhishi wa migogoro kwenye biashara, tuna taasisi ambazo zinakwenda kujenga ufanisi wa viwanda kuanzia vidogo kabisa hadi vile vikubwa; tuna sheria ambayo inasimamia, tuna mkakati wa kimaendeleo wa viwanda wa tangu 1996 mpaka sasa hivi ambao umerejewa na sasa hivi umeboreshwa. Sasa zaidi ya hapo tunawezaje kusema kuwa hatuna mwelekeo wa viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoka hapo tunakuja kwenye masuala mazima ya utekelezaji wa huo mkakati mzima wa viwanda nchini mwetu. Tunaona jinsi ambavyo kwa sasa hivi kwa mtazamo huu wa Serikali ya Awamu ya Tano kuwa sasa hivi viwanda hivi vinakwenda kuwajumuisha wananchi wengi zaidi. Kama zamani ilikuwa inaonekana

viwanda viko sehemu chache tu za nchi, sasa hivi viwanda vinakwenda mpaka vijijini kwetu, vinakwenda mpaka kwenye Wilaya zetu, vinakwenda kwenye Halmashauri zetu, maeneo ya mikoa na wilaya ambayo yako tayari kwa ajili ya viwanda yameainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu wote wana ufahamu na uelewa kuwa wanahitaji kuwa na viwanda; tuna *program* zilizokuwepo chini ya Wizara hii zilizokuwa zikisema kila Wilaya iainishe zao moja ambalo wanaliona hilo ndiyo litakuwa linafaa kwa ajili ya kuendelezwa hadi kufukia *level* ya kiwanda; na hayo yamefanyika. Tuna Taasisi muhimu za kusimamia kama *SIDO;* kila mtu aliyesimama hapa amezungmzia *SIDO,* ni kwasababu ameuona umuhimu wake. Sana sana tutakachoweza kusema kwenye Serikali ni kuwa *SIDO* iwezeshwe zaidi kwa maana ya mitaji, kwa maana ya wafanyakazi, kwa maana ya *program* za kwenda kusambaza katika kila eneo kama ambavyo sera inasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazungumzia *BRELA. BRELA* zamani ilikuwa inasajili majina ya Makampuni kwa maana ya wakubwa. Sasa hivi hata akinamama zangu kule kijijini wanaweza kusajili majina ya Kampuni zao au shughuli zao wanazozifanya. Hii imerahisishwa kiasi kwamba hata hawana haja ya kutembea kwenda Dar es Salaam au kwenye Kanda yoyote, hata kwa kutumia mitandao tu ya simu, Mabenki ambayo yameunganishwa. Sasa jamani unalalamika kuwa eti sijui urasimu; urasimu umepunguzwa kwa kiasi kikubwa. Ni sisi sasa kama viongozi katika Halmashauri zetu kuhamasisha wananchi kuwaelewesha jinsi gani ya kutumia nyenzo hizi ambazo Serikali imeziweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Jamani, nani atakayeendelea kubisha sasa kuwa huo siyo mfumo ambao umewasaidia sana wakulima kupata bei bora kwa ajili ya mazao yao? Tuombe sasa mfumo huu wa stakabadhi uenezwe Tanzania nzima maana yake ulikuwa kwenye mazao machache, lakini vile vile haukuwa kila mahali. Wale

wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo na wengi wao wakiwa ni wanawake wangependa sana na wao sasa kujumuishwa katika mfumo huu na kwa hali hiyo haya maghala na huu usimamizi upelekwe mpaka kwenye Wilaya zetu ili sasa wananchi wetu waache kurubuniwa na madalali wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia sera. Jana kuna mtu alikuwa anakashifu Sera ya Viwanda ya 1996 ambayo inaisha mwaka 2020. Mambo mawili makuu ambayo sera hii ilikuwa imelenga; kwanza ilikuwa ni kusambaza viwanda nchi nzima. Jamani, sera ikiwa inasema kitu kama hicho, ina ubaya gani? Inazungumzia *inclusiveness* ya viwanda nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera hii vile vile ilikuwa inazungumzia kueneza viwanda kwenye maeneo ya pembezoni. Mimi natoka kwenye eneo la pembezoni; Ileje ni Wilaya ya pembezoni na kwa muda mrefu sana tumekaa kwa kweli hatuna maendeleo makubwa sana zaidi ya kuwa ni wakulima wazuri, tunazalisha vitu vizuri. Sasa hivi naona Mkoa wa Songwe na wenyewe uko katika maeneo ya kuja kuwekezwa kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ktika Wilaya yangu, tayari *SIDO* wameshakuja kupata eneo na wako tayari kuja kuanzisha viwanda; Wilaya yangu sasa hivi inakwenda kubadilika, siyo ile Ileje ambayo mlikuwa mmezoea kuisikia. Wengine hata mlikuwa hamjui Ileje iko wapi? Sasa hivi mnaijua Ileje iko wapi. Ileje inaenda kupata barabara ya lami kubwa itakayofungua uchumi ule kwa kiasi kikubwa sana. Ileje kwa uzalishaji wake, sasa hivi inaenda kupata miundombinu ya Kituo cha Forodha mpakani na Malawi. Haya yote ni maendeleo. Tunaenda kupata Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda, yote haya ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema mimi, kilimo chetu sasa hivi kinaenda kufanya usindikaji wa hali ya juu. Nasema barabara ile itakapoanza tu, Ileje itakuwa kama

mzinga wa nyuki, shughuli zitavyoanza pale. Sasa hivi tu tayari tuna watu wengi sana wako tayari kuja Ileje, wanavizia barabara ikifunguliwa tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, anisikilize. Afanye kazi kwa karibu sana na Waziri wa Maji ambaye namshukuru Mungu safari hii ametuwekea fedha ya kutosha kuboresha miundombinu ya maji Ileje. Mheshimiwa Mwijage, Ileje tunalima sana mazao mengi; nafaka, mazao ya biashara kama pareto, tunalima soya, alizeti, mihogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbene muda wako umemalizika.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba viwanda Ileje nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri mara nyingi, maeneo yapo tunamkaribisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, najua hii hoja naweza nikaizungumza kutwa nzima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kabisa katika ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kama Waheshimiwa Wabunge wengine, ambavyo wamempongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli inaonesha matumaini ya hili suala tunalolizungumza juu ya Serikali ya viwanda inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ya kipekee kwa kutambua umuhimu wa kuwa na viwanda ambavyo ndiyo unaweza kuwa msingi wa wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufahamu huu tulionao wote, lakini pamoja na hii ambayo ndiyo kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais kwa sasa, bado tunayo kila sababu ya kuhakikisha vyuo vyetu vya *VETA* na mitaala tuliyonayo inatambua umuhimu wa Serikali hii au Taifa hili kuwa na viwanda ili viweze kuchukua sehemu kubwa sana ya vijana kama ajira lakini ya uzalishaji mali na mazao ambayo yatakuwa yanatumika zaidi kwa wananchi hawa wanyonge lakini na kuuza nje ya nchi kama ambavyo tunatarajia kupata kipato kikubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua, nami leo nitajikita sana kwenye viwanda ambavyo, pamoja na utaratibu huu tunaoufikiria sasa wa kuwa na viwanda vipya au ujenzi wa viwanda vipya katika maeneo mbalimbali ya nchi hii lakini nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba tunayo kila sababu viwanda hivi tunavyovijenga kwa sasa ni lazima tuwe na kipaumbele na viwanda tunavyovihitaji kwa ajili ya maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu muda wa miaka mitano ni mchache sana; tukisema miaka hii mitano tunaondoka na viwanda 100, 200, 3,000 au mia ngapi, bado tutakuwa tunajidanganya, tutakuwa na ma-*carpenter* wengi, hatutakuwa na *SIDO* nyingi halafu tunahisi tuna viwanda vikubwa ambavyo vinaweza vikasaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona mfano; tunapozungumzia uhaba wa sukari nchi hii, tunazungumzia moja kwa moja uzalishaji hafifu wa viwanda vyetu tulivyonavyo hapa nchini. Pamoja na uhafifu huo, tunayo mifano; Kenya, Uganda na nchi nyingine zinazotuzunguka, nataka tufikirie kuwa na viwanda vyenye vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchache huu, leo Mheshimiwa Waziri anaweza akajinadi na ana kila sababu ya kujisifu; hata bei ya sukari tunayolalamika sisi iko chini, huwezi kulinganisha na nchi za majirani zetu kama Uganda na Kenya. Sasa maana yangu ni nini? Unapokuwa na viwanda vya sukari vyenye kuweza kuzalisha zaidi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tulikuwa tunazungumza naye pale, wamekamata sukari ya Kilombero inaingizwa Kenya kule kwa magendo; na sababu ni moja tu; inawezekana uhaba huu tulionao bado sukari yetu inavushwa nje. Sasa maana yangu ni nini? Nataka tuwe na viwanda vyenye vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukiwa na viwanda yenye vipaumbele kwa miaka hii mitano, tutajikuta tunafanya kitu ambacho kitakuwa kinaonekana kwa Watanzania kuliko kubaki na historia ya ujenzi wa viwanda lukuki ambavyo havina vipaumbele kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine; nimesema mbali ya kuwa na viwanda vya kipaumbele, lazima sasa tuangalie, tunapiga hatua 100 mbele kufikiria viwanda vipya, tuna mawazo gani juu ya viwanda tulivyokuwanavyo toka zamani na leo tulivibinafsisha na haviwezi kufanya kazi yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mwanza tunavyo viwanda vya *Tanneries,* tunacho kiwanda cha *MWATEX* lakini tunavyo Viwanda vya Samaki. Kiwanda cha *MWATEX* ambacho toka mwaka 1995 kilibinafsishwa, wafanyakazi zaidi ya 1,720 ambao waliachishwa kazi na mpaka leo hawajalipwa, lakini kiwanda kile pamoja na mambo yake mengi, hivi tunavyozungumza, uwezo wa kiwanda hiki kuzalisha hata asilimia 30 ya yale yaliyokuwa yanazalishwa miaka karibia 12 iliyopita, hakijafikia malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *MWATEX* kila mmoja anafahamu, kila mmoja anajua umuhimu wa viwanda hivi; ni wakati gani tuko tayari kurudi kwenye viwanda hivi na tushughulike navyo viweze kuzalisha kama

zamani? Mbali ya ajira kubwa ya zaidi ya watu 2,000, lakini vilikuwa na uwezo wa kuzalisha na tutasafirisha nje kwenye nchi za majirani na kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeongelea Kiwanda cha *Tanneries.* Kiwanda cha *Tanneries* kimebinafsishwa. Kiwanda hiki sasa Mheshimiwa Jenista pamoja na Wizara yake wameanzisha mafunzo muhimu kutoka nchi nzima vijana wanapelekwa pale zaidi ya 1,000. Hawa vijana wakimaliza kujifunza pale wanakwenda kufanya kazi wapi? Kiwanda hiki tangu kibinafsishwe hakijawahi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba na hiki na chenyewe tukiangalie. Hawa vijana wanaotoka *DIT* kwenye mafunzo ya utengenezaji wa mikanda, viatu na mikoba, kiwanda hiki ikiwezekana kama siyo kurudishwa; na Mheshimiwa Rais aliahidi, tuangalie uwezekano wa kurudisha kiwanda hiki kije; vijana wanaotoka kujifunza hawa badala ya kwenda mtaani, watakuwa wanazalisha mali zilizokuwa na ubora. Wafanye kazi kwenye kiwanda hiki, wazalishe mali zenye ubora, tuuze ndani na nje ya nchi kwenye majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni viwanda vya samaki. Tuna viwanda saba vya samaki. Hii ni lazima Mheshimiwa Waziri akubali kuungana na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili waweze kuona. Miaka minne iliyopita kiwanda kimoja peke yake kilikuwa kinakata *shift* nne, watumishi zaidi ya 1,400, kikiwa kinakata tani 280 za samaki kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kiwanda kimoja kinaitwa *Vicfish* kimeshafungwa; na hivi vilivyopo kimoja kina uwezo wa kuzalisha tani sita mpaka 12 kwa siku, kimepunguza wafanyakazi kutoka 1,400 mpaka 300 mpaka 150. Tafsiri yake ni nini? Tunaongeza Machinga, tunaongeza wafanyabiashara ndogondogo, ajira hakuna na kumbe tunaweza kushirikiana tukatengeneza ajira nyingi zaidi kama

viwanda hivi vinaweza vikaboreshwa upya. Kazi inayofanyika ni nzuri, lakini lazima tunapokwenda mbele tukumbuke na tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mpango wa sasa, viwanda tutakavyovijenga Mwanza, vinategemea kuzalisha ajira 1,004. Hawa tunaozungumza viwanda vilivyokufa, zaidi ya ajira 2,900 zimepotea. Tafsiri yake, tunahitaji viwanda hivi viangaliwe upya na ushirikiano kati ya Wizara mbili au tatu ni lazima uwe wa karibu ili kujenga msingi wa viwanda tunavyozungumza viweze kufikia malengo yake tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda lazima akubali kushirikiana. Watumishi hawa ambao miaka 12 hawapo, leo wapo mtaani, wengine wameshakuwa wazee, tunahitaji kujua ni lini watalipwa mafao yao ambayo hawajawahi kuyapata miaka 12? Tukifanya hivyo itatusaidia, tutakwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na wachangiaji ambao watachangia kwa dakika tano, tano. Mheshimiwa Jadi Kadika halafu Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira ya dhati ya kuleta viwanda nchi nzima. Sera ya Viwanda ni sera nzuri sana ambayo kimsingi, yeyote atakayeipinga ni yule ambaye hajui umuhimu wa viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sera hii imeoanisha mazingira mazuri kwamba kila mkoa ni lazima kuwe na viwanda ambayo vitawasaidia wananchi wetu kuweza kukuza uchumi ndani ya maeneo yao. Nzuri zaidi ni pale

ambapo sera hii inaonesha maeneo ambayo yalisahaulika hasa pembezoni, yapewe kipaumbele ili yaweze kunufaika na mpango wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri tu Serikali kwamba, katika sera ambayo imewekwa, Sera ya Viwanda ni vyema wakaangalia mazingira ili tupeleke viwanda mahali ambapo uhitaji wa viwanda unafanana na mazingira yenyewe. Leo hii unapopeleka kiwanda cha kusindika ngozi kwenye maeneo ambayo hayana hata mifugo, hujawasaidia wananchi pale, hasa wale ambao wanatoka kwenye maeneo ya ufugaji. Ni vyema vile viwanda ambavyo vitakuwa vinahusiana na Sekta ya Mifugo, tukawapelekea kwenye maeneo husika ya uzalishaji ili viweze kutoa ajira kwenye maeneo ambayo wananchi wenyewe wanahusika na kulengwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulikuwa tunaomba kuangalia mazingira ya kuboresha Sekta ya Viwanda hasa viwanda vidogo vidogo. Kwenye maeneo haya ni vema Serikali sasa wakawa na mipango thabiti itakayokuwa inaunganisha nchi nzima na kwa kuwashirikisha Wakuu wa Mikoa ili waweze kutenga maeneo ambayo yatakuwa rafiki kuwasaidia wananchi ambao kimsingi tukiboresha kwenye Sekta ya Viwanda vidogo vidogo, tumewasaidia wananchi walio wengi. Huko ndiko ambako ajira zinatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, lazima aje na mpango mkakati wa kuwashirikisha Wakuu wa Mikoa ili kuhakikisha maeneo ya viwanda vidogo vidogo yanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itusaidie mikoa ya pembezoni; kule tunazalisha. Mkoa wangu ulishatenga maeneo ya uwekezaji. Nafikiri kila kitu kipo sawa, lakini tunaomba sasa ielekeze suala zima la kuwekeza kwenye mazao yanayozalishwa na wananchi hasa kwenye Sekta ya Kilimo. Tukielekeza huko, tutawasaidia sana wananchi ambao ni wengi. Mazao ya mafuta yanayozalishwa, tukiweka mipango mikakati mizuri, kwamba yale mazao ya

mbegu za mafuta ambayo yanazalishwa, tukajenga viwanda vidogo vidogo huko, tutakuwa tumewasaidia sana wananchi ili waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao ya chakula. Mkoani kwangu tunazalisha chakula kingi na tunauza mazao ambayo bado hayajasindikwa. Naiomba Serikali, pale ambapo tunafikiria mikoa ya pembezoni; Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma ni vema sasa tukawa na viwanda ambavyo vitafanya kazi ya kuwasaidia wananchi kwenye maeneo hayo na eneo hilo likawa na ukuzaji wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna mazao ya biashara; tuna zao la tumbaku kwenye Mikoa hiyo ya Tabora, Kigoma na Katavi. Hatujakuwa na kiwanda maalum ambacho kitasaidia kukuza zao hili. Ni vema sasa Serikali ikaja na mpango ambao utasaidia maeneo hayo ili kupata kiwanda ambacho kitasaidia kukuza uchumi ndani ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo mazuri ya kivutio cha uwekezaji. Lipo zao la miwa, kama Mkoa wa Kigoma wangepewa fursa, wana mabonde mazuri. Mfano, bonde la Mto Malagarasi; katika Mkoa wa Katavi, Rukwa vile vile; tunahitaji tupate Kiwanda cha Sukari kwenye maeneo haya ili tuweze kupunguza bei ya sukari kwenye maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naiomba Serikali iandae mazingira ya kujenga Kiwanda cha Saruji kwenye maeneo haya; ni maeneo ambayo bei za saruji ni kubwa kweli kwa sababu viwanda vingi vimeelekezwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Pwani lakini maeneo ya pembezoni hakuna. Naiomba Serikali iweze kutengeneza mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie dhamira ya Serikali. Serikali imeonesha wawekezaji wengi kwa kushirikisha Mifuko ya Maendeleo ya Jamii; *NSSF, PPF, PSPF*

na mengine, mashirika ambayo tukiweka ubia yana nafasi ya kuweza kusaidia kukuza uchumi. Ni dhamira nzuri ambayo Serikali imeweka; ni vizuri sasa tukawa na uwiano kwenye maeneo yote yasiwe yanaelekezwa kwenye maeneo maalum tu hasa Kanda ya Mashariki. Naomba Serikali iangalie mazingira haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie eneo ambalo watu wengi wamekuja wanafananisha bei za chakula nchini Kenya na bei za kwetu hapa. Niwaambie wananchi tu kwamba, zipo propaganda ambazo zinaenezwa. Tukiangalia uhalisia, bado bei ya sukari kwa nchi yetu ipo chini kuliko bei ya sukari kwenye maeneo ya nchi ambazo ni jirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya leo hii bei ya sukari ni Sh.3,195/=, Uganda ni Sh.3,550/= mpaka Sh.4,000/=, Burundi ni Sh.3,700/= mpaka Sh.4,000/=. Tanzania bei ya sukari ipo kati ya Sh.2,700/= mpaka Sh.3,000/=. Bado maeneo mengine yote yanayotuzunguka yanahitaji kutoka kwetu kupata bidhaa muhimu kama hiyo. Ni vema sasa watu wakaacha kutumia *propaganda* ambazo kimsingi wenzetu sasa hivi wanazitumia kwa masuala ya kisiasa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge watakaotajwa wanachangia kwa dakika tano, tano. Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Frank Mwakajoka. Kama muda wetu utakuwa bado upo, Mheshimiwa Yosepher Komba atachangia.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema

na kuweza kusimama na kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, imejipanga katika uchumi wa viwanda; na ina nia nzuri tu ya kutoa ajira kwa Watanzania. Nchi yetu kama mtajenga viwanda vingi kama utitiri, lakini ikiwa havina usimamizi na wataalam waliobobea kiuweledi mkubwa, basi viwanda hivi vitakufa kama vilivyokufa vilivyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nichangie ujenzi wa Viwanda vya Minofu ya Samaki katika Ukanda wa Pwani. Nchi yetu inayo maeneo makubwa ya bahari, lakini hakuna kiwanda hata kimoja. Viwanda vyote vinaelekezwa kwenye Ukanda wa Ziwa. Kwa hiyo, naishauri Serikali ijenge viwanda kwenye eneo la bahari kama vile Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mtwara, Pemba na Unguja. Ujenzi huu utatoa ajira na utainua maisha ya wavuvi na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja kwenye Viwanda vya Mabati. Viwanda hivi vinazalisha mabati chini ya kiwango katika baadhi ya viwanda, yakiwemo mabati ambayo yanaingia kutu haraka, mabati mengine yanachakaa haraka na pia yanavuja siku za mvua. Pia bei ya mabati hayo iko juu, kulingana na bei ya saruji ambayo kwa sasa imeshuka. Kwa hiyo, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia ubora wa viwango vya mabati na pamoja na kudhibiti bei? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa feki zimezungumzwa na wenzangu wengi hapa, lakini nami nataka nizungumzie kuhusu bidhaa feki. Kuna bidhaa feki nyingi zinazoingizwa katika nchi yetu. Maziwa ya watoto yana madhara makubwa juu ya kutumia maziwa haya. Nyaya za umeme zinaunguza majumba yetu, zinapelekea maafa. Matairi kupasuka kwa muda mfupi tu na kusababisha ajali nyingi barabarani. Vipodozi vinaharibu ngozi za akinamama na wengi wanapata kansa. Je, Serikali inatuambiaje kuhusu suala hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wanawake wengi tuko ambao huwa tunatumia vipodozi na tunaharibika ngozi na wengi wanapata kansa, wengine wanakufa, uzuri wao umepotea. Kwa hiyo, hili suala linatakiwa lishughulikiwe kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nazungumzia kuhusu viwanda. Vimo viwanda vingi tu, *SIDO,* lakini hata vikiwekwa viwanda vikubwa kwa kuwaboreshea wakulima mazao yao, itakuwa ni bora zaidi. Nashauri kila kiwanda kiwekwe kila mkoa ili wazalishaji waweze kutumia viwanda hivi kwa kuyaokoa mazao yao; kama vile mananasi,maembe, machungwa, mazao kama nyanya na mazao mengine mengi tu yanaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naona muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni, naona umeshangiliwa sana na Mheshimiwa Waziri hapa. Nadhani ameandika yote uliyokuwa unayasema. Vipodozi vinavyotokana na maganda ya korosho, jana tumeambiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kuwasilisha hotuba nzuri ambayo imetoa ushauri wa kutosha na tumemshauri sana Mheshimiwa Mwijage kwamba ajitahidi sana kutumia hotuba hii ili aweze kutekeleza malengo ya Serikali ya Viwanda katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho nataka kukizungumza hapa, kwanza nianze kabisa na mazingira

mabaya kabisa ambayo yako katika nchi yetu kwa ajili ya kuendeleza biashara katika nchi hii. Wote tunafahamu na wote tunajua kwamba katika nchi yetu kumetokea na wimbi kubwa sana la wafanyabiashara kufunga biashara zao yakiwemo maduka, mahoteli, lakini pia na wanaoendelea kuuza biashara zao hizo, wanafunga na hawafanyi tena biashara kutokana na mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunauliza sana ndani ya Bunge kwamba Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inanusuru tatizo hili ambalo linajitokeza la wafanyabiashara kufunga biashara zao? Sababu kubwa ni nini? Wafanyabiashara wengi wamekuwa wanalalamika kwamba mazingira ni mabaya, Serikali inawabana tofauti na jinsi inavyotakiwa. Wajibu wa Serikali siku zote ni kuhakikisha kwamba inatengeneza mazingira mazuri ya wafanyabiashara kuendelea kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inatoa majibu ndani ya Bunge inasema kwamba kuna watu wanafunga, lakini kuna watu wengine wanafungua. Hayo majibu hayawaridhishi kabisa Watanzania. Hivi ni kweli Serikali inataka kwenda kwenye Serikali ya Viwanda, inaona biashara zinafungwa na inasema kwamba wacha zifungwe, nyingine zitafunguliwa. Kwa hiyo, tafsiri ni kwamba biashara nyingine zifungwe na nyingine zifunguliwe! Naona tunafanya biashara ya sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana Serikali hii ikagundua na ikashughulikia matatizo ya wafanyabishara. Lazima tuzungumze hapa ndani ya Bunge hili, kwamba mazingira ya kuanzisha viwanda katika nchi hii, kama wafanyabiashara wa ndani wanashindwa kufanya biashara na biashara zao zinafungwa, ni mwendawazimu gani mfanyabishara kutoka nje anaweza kuja kuwekeza na kufanya biashara katika nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima kwanza tuangalie mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu ndani ya nchi hii wanafanya biashara

vizuri na biashara zao zinaendelea, ndipo watu kutoka nje watakuja kufanya biashara ndani ya nchi hii. Kama hatuwezi kuangalia matatizo ya wafanyabiashara wetu ndani ya nchi, halafu tukafikiria kwamba kuna wawekezaji watatoka nje waje kuweka biashara zao hapa, hili jambo tulisahau, halitaweza kutekelezeka hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane kabisa kwamba nchi hii kumekuwa na matamko mengi sana ya vitisho. Juzi nilikuwa nasikiliza Taarifa ya Habari, wanasema kwamba hata wakulima sasa hivi wanaopata mazao mengi ni lazima waanze kulipa kodi. Nashangaa sana, yaani wanataka kutuambia kwamba wakulima hawa hawalipi kodi. Hakuna Mtanzania yeyote katika nchi hii ambaye halipi kodi. Tunalipa kodi katika njia tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wanalima mazao haya kwa kutumia fedha zao na Serikali haiwasaidii hata kidogo. Tumeendelea kuzungumza kuhusiana na pembejeo za kilimo hapa, zinafika kidogo; lakini leo Serikali inafikiria kwamba ni lazima iwakamue wakulima hawa, eti hawalipi kodi. Hilo siyo jambo la kawaida. Ni kwamba kodi zinakusanywa katika maeneo mbalimbali, siyo lazima ukachukue kodi kwenye yale mazao, lakini kodi zinakusanywa. Yule mkulima akishalima anakwenda kuuza, analipa kodi. Bado pia yule mkulima anakwenda mbele zaidi, anakwenda kununua mizigo ambayo tayari imeshalipiwa kodi, anakuwa ameshachangia Taifa lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana, ni lazima Serikali iwe inafika mahali, inapotaka kuanzisha jambo fulani lazima ifikirie. Tunajiuliza sana kwamba mahusiano kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha, kuna mahusiano gani hapa? Maana tunaona sana kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na watendaji wake wa Serikali wamejipanga sana kuhakikisha kwamba nchi inakuwa ya viwanda; lakini Wizara ya Fedha inakwamisha kutokana na sera na mipango mbalimbali ambayo inafika mahali inakuwa inapingana na dhana nzima ya kuanzisha viwanda katika nchi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima Wizara ya Viwanda na Wizara nyingine zinazofuatia na Wizara ya Fedha lazima wakae pamoja kupanga na kukaa, kuangalia ni namna gani wanaweza wakapunguza kero ambazo zinasababisha viwanda visianzishwe katika nchi hii. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi chetu cha asubuhi. Mchana tutamalizia wachangiaji wachache waliobaki. Mheshimiwa Musa Bakari Mbarouk, kwa dakika tano; Mheshimiwa Yosepher Komba, kwa dakika tano, Mheshimiwa Joyce Sokombi, kwa dakika tano; Mheshimiwa Devotha Minja; kwa dakika tano; na Mheshimiwa Dunstan Kitandula kwa dakika kumi.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili, Mheshimiwa Waitara aliacha kitabu cha Hisabati cha Kidato cha Pili, ambacho ni cha maswali na majibu ya mitihani iliyopita. Anaomba aliyekichukua, tafadhali amrudishie. Maswali na Majibu, Hisabati, Mitihani ya Kidato cha Pili. Anaomba arudishiwe kitabu chake.

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kwamba leo saa 8.00 mpaka saa 10.00 lile tangazo la jana kwamba leo Wakandarasi wa *REA,* awamu ya tatu wanakuja.

Kwa hiyo, wanaomba mwende eneo linaloitwa *Treasury Square.* Muda ni saa 8.00 mpaka saa 10.00 mkashuhudie namna ambavyo Wakandarasi wa mikoa yenu wanakabidhiwa mikataba. Kwa hiyo, maswali kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nadhani baada ya

leo watu watakuwa hawasimami wengi humu maana watapata majibu kule pengine. Kwa hiyo, mnakumbushwa hivyo, mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 10. 00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wachangiaji wachache kabla mtoa hoja hajaja kuhitimisha. Tutaanza na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Yosepher Komba na Mheshimiwa Joyce Sokombi, ajiandae, dakika tano tano, Makatibu.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Nami nichukue fursa hii, kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo katika enzi ya viwanda na uchumi wa kati, lakini kiukweli kabisa ni kwamba yanahitajika maandalizi thabiti. Sasa ni maeneo mengi ambayo tumekusudia kuyafanyia kazi. Jambo la kwanza kabisa ili tuwe na viwanda vya uhakika, ni lazima vilevile pia tuwe na umeme wa uhakika. Sasa ni mara nyingi tumekuwa na tatizo la umeme. Mheshimiwa Waziri atakapokuja naomba atuthibitishie, ni kweli tutakuwa na umeme wa uhakika? Kwa sababu viwanda bila umeme inakuwa ni kama kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Tanzania sisi ni wa tatu wa idadi kubwa ya mifugo; kama sikosei, baada ya Ethiopia na Botswana ni sisi tunaofuatia Tanzania. Ukiangalia wenzetu wa Botswana, ng'ombe anapoingia katika kiwanda cha kuchakata nyama, hakuna kinachotoka. Ngozi ina shughuli yake, nyama ina shughuli yake, pembe ina shughuli

yake na kwato zina shughuli yake. Sisi Watanzania pamoja na mifugo tuliyokuwa nayo, bado hatujaweza kuitumia mifugo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, tutafute wawekezaji wenye uwezo wa kujenga viwanda vya kusindika nyama. Vilevile pia wenzetu wa Ethiopia, kwa mwaka 2016, wamepata takriban Dola 186,000 kutokana na ngozi peke yake. Wanatarajia mwaka 2017 kupata vilevile Dola za Kimarekani kuongeza idadi ya Dola 90,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, mpaka 2017 ikimalizika watapata zaidi ya Dola 276,000,000. Sisi Watanzania badala ya kuitumia mifugo vizuri, imekuwa tunazalisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine iliwahi kutokea hapa kwamba Maafisa wa Wanyamapori, wakagombana na wafugaji, ng'ombe wakapigwa risasi, wafugaji wale wakadhalilishwa, hadi kupelekea baadhi ya Mawaziri kujiuzulu katika Serikali ya awamu iliyopita. Kwa hiyo, naishauri Serikali tutumie mifugo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Watanzania tumekuwa tunashindwa na baadhi ya nchi ambazo zimekuwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe. Tukumbuke Ethiopia waliwahi kuwa na vita na Djibout, lakini baada ya kumaliza vita, wamekaa wamepanga mambo mazuri namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, ng'ombe pia wanazalisha maziwa, lakini Watanzania tumeshindwa kuyasindika. Matokeo yake tunaagiza maziwa ya kopo kutoka nje. Tunaagiza *Nido*, *Lactogen*, *Nan;* hali ya kuwa maziwa ya ng'ombe yangepakiwa vizuri, yangeweza kuwasaidia wananchi wetu. Kwa hiyo, naishauri Serikali itafute wawekezaji wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala zima la viwanda; tuna matunda. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Tanga, Lushoto ni wazalishaji wa matunda na

mboga mboga za aina nyingi. Muheza kuna kilimo kikubwa cha machungwa, lakini pia unakuta tunaagiza *juice* za *Ceries* kutoka *South Africa* na Saud Arabia ambayo ni nchi iko jangwani. Inakuwaje sisi ambao tunazalisha machungwa *by nature* lakini tunashindwa kuyachakata tunaagiza *juice* kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali tutafute wawekezaji wa uhakika. Tusizungumze suala la viwanda kisiasa; tuwe na dhamira ya dhati na ya kweli. Viwanda hivyo vitakapojengwa wananchi wetu watapata ajira lakini vilevile Serikali pia itapata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililotaka kuzungumza, moja ya matatizo yanayofanya wawekezaji wasije Tanzania, ni mifumo mibovu ya kodi, umeme usiokuwa wa uhakika, lakini vilevile pia kuna kitu kinaitwa urasimu. Mtu akitaka kuwekeza kiwanda Tanzania, atahangaishwa, itafika miaka miwili. Wenzetu Uganda ndani ya masaa 48 ukitaka kuwekeza unapata kila aina ya msaada unaotaka na Serikali inakwambia, kama unataka kuongezewa mtaji pia iko tayari, lakini Tanzania hilo hatulifanyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe kwanza inaweka miundombinu rafiki, mifumo mizuri ya kodi, lakini tuondoe urasimu. Vilevile pia nataka kuiambia Serikali...

*(Hapa kengelee ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Mheshimiwa Yosepher Komba atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Sokombi na Mheshimiwa Devotha Minja ajiandae. Dakika tano, tano.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda ku-*declare interest* angalau haiko kwenye hela lakini mimi nimetokea Tanga na mnajua historia ya Mkoa wa Tanga katika suala la viwanda. Mnajua Tanga miaka ya

1980 ni kati ya Mkoa ambao ulikuwa maarufu sana kwa viwanda kwa Tanzania hii. Tunavyoongea sasa hivi, viwanda vingi vimefungwa, vilivyobinafsishwa, vimekufa, watu wameiba vifaa, viwanda Tanga hakuna tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga tumejaliwa kuwa na bandari, viwanja vya ndege na reli ambayo mpaka sasa hivi hatujajua Serikali lini itaamua kutujengea kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia natokea Muheza, Wilaya ambayo ni maarufu sana kwa kilimo cha matunda hasa machungwa. Wilaya ambayo ina hali zote za hewa tunazozijua; kuna hali ya baridi na joto, kiasi kwamba tunaweza kulima mazao yanayotokana na baridi na mazao yanayotokana na joto.

Mheshimia Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Viwanda niliwahi kumgusia suala la Muheza nikaomba kwamba atafute mwekezaji kwa ajili ya machungwa yetu yanayozalishwa Muheza. Wakulima wamekuwa wakipata hasara sana ya machungwa yanayozalishwa pale, yamekuwa yakioza. Wamekuwa kama wana uwezo zaidi kutegemea soko la Kenya lakini Tanzania hakuna kiwanda karibu; Tanzania, Muheza hakuna kiwanda wakulima wanapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tunajua lengo la Tanzania ya viwanda ni jema, lakini kama tusipokuwa makini hatuwezi kufikia huko. Kama hamkujiandaa, tafuteni namna nyingine ya kuliweka sawa. Kwa nini nasema hivyo? Waziri wa Viwanda yeye kama yeye hawezi kufikia lengo la viwanda kama Wizara nyingine hazijaonesha ushirikiano kwako. Yeye kama yeye hawezi kufikia kwenye viwanda, kama Wizara ya Fedha haijaamua kuona kama suala la viwanda ni muhimu. Pia hawezi kufikia lengo kama Wizara ya Ardhi na Wizara ya Usalama na mambo mengine hazijamsaidia. Kwa hiyo, inatakiwa suala la viwanda liwe ni la nchi, siyo Wizara. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na miundombinu mizuri kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee viwanda na wanawake. Sensa ya viwanda inaonesha asilimia 99.15 ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Kwa haraka haraka ukiangalia katika sensa hii, utaona viwanda vidogo sana ni kati ya mtu mmoja mpaka wanne; viwanda vidogo ni kati ya mtu mmoja mpaka 50. Ukiangalia kwa undani zaidi utakuta hivi viwanda vidogo vingi vinamilikiwa na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, sijaona popote kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ambapo ameonesha namna ambavyo atamsaidia mwanamke aingie kwenye uchumi wa viwanda akiwa anajiaamini. Tunajua hali ya kipato cha wanawake wengi wa nchi hii ni cha chini. Wizara haijaandaa utaratibu wowote kumwezesha mwanamke ambaye kwa asilimia kubwa ndio amewekeza kwenye hivi viwanda vidogo aweze kujikwamua. Kwa hiyo, tuna viwanda vingi vya mtu mmoja mpaka watano, tutafika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kitu kingine tunapoongelea Tanzania ya viwanda, lazima tukubali na tuamue tunataka viwanda vya aina gani? Hatuwezi kuwa na viwanda nchi nzima kwa mara moja. Lazima tutenge maeneo, lazima tuwe na *point* ya kuanzia. Tanzania tunataka viwanda ndiyo, tunataka viwanda vya aina gani? Tunataka viwanda vya kutumia malighafi gani? Tutakapokuwa tumefanya hayo maamuzi, itakuwa ni rahisi. Hatuwezi kujenga viwanda nchi nzima, lazima tuamue baada ya miaka 10 miaka 15 tunataka katika viwanda Tanzania ijulikane katika kitu gani? Ziko nchi ambazo zinajulikana kwa ajili ya kuzalisha *products* za maziwa peke yake. Tanzania tunataka tujulikane kwenye nini katika viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongee suala la *VETA.* Tunajua inatakiwa kuwe na elimu na ujuzi wa kutosha ili tuingie kwenye viwanda tukiwa tunajiamini. Kumekuwa na tatizo kubwa sana katika Vyuo vyetu vya *VETA,* siyo tu udahili lakini pia vifaa na mashine zinazotengenezwa *VETA* zina bei ghali kuliko sehemu nyingine yoyote. Sasa kwa namna hii

hamwezi ku-*encourage* viwanda wakati watengenezaji wetu wa ndani wanapitia mazingira magumu katika kuanda hizo zana za kufikia kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali isaidie wale wataalam wa *VETA* ambao wanatengeneza mashine ambazo zinaweza zikatumika kwenye nchi yetu, wapunguzieni kodi ambazo ni mzigo kwa wafanyabiashara wengi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Mheshimiwa Joyce Sokombi, atafuatiwa na Mheshimiwa Devotha Minja, na Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema. Kabla ya yote, napenda tu pia kumpa pole Mwenyekiti wangu wa Kanda, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mheshimiwa John Heche kwa kuumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine pia napenda nisemee kitu kidogo, imesemewa hoja yake iliyotolewa hapa asubuhi; ni mbaya sana kumsema mtu ambaye anaumwa, yuko hoi kitandani. Ni vizuri mkamwacha akapona ndiyo aje aambiwe hayo maneno anayoambiwa ili ayajibu yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mbunge hajakataa kiwanda kisijengwe Tarime, isipokuwa utaratibu ufuatwe unavyotakiwa na mwende mkawashirikishe wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuishauri Serikali kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara ni vizuri ikaungana

ikawa pamoja na Wizara ya Kilimo, kwa sababu bila kuwa na Wizara ya Kilimo, viwanda haviwezi kufanya kazi zozote kwa sababu wanaendesha viwanda kwa kutoa malighafi wapi? Maana malighafi inatoka kwa wakulima. Kwa maana hiyo basi, ni vizuri hizi Wizara zikaungana ili yale mazao yanayopatikana kutoka kwa wakulima yaende yakafanye kazi katika viwanda. Maana huwezi kusema mnafanya kazi katika viwanda kwa kutegemea mazao ya wakulima halafu Wizara yenyewe inajitegemea yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, viwanda vya mafuta; huwezi kuchenjua mafuta bila kutoka kwenye vitu kama karanga, mbegu za pamba, ufuta au alizeti. Kwa hiyo, basi ni vizuri hizi Wizara mbili zikaungana. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mara tulikuwa na viwanda vingi sana, karibu viwanda kumi na kitu, lakini sasa hivi ni viwanda vitatu tu vinavyofanya kazi; na ni viwanda vya watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Waziri wa Viwanda na Biashara kwa nini asivifufue vile viwanda vya Mkoa wa Mara? Kwa mfano, kile Kiwanda cha *MUTEX,* kile kiwanda kilikuwa kinasaidia kutoa ajira nyingi sana kwa wakazi wa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimshauri tu Mheshimiwa Waziri na Mkoa wa Mara una sifa kuu kubwa moja ambapo ametokea Baba wa Taifa. Ili kumuenzi Baba wa Taifa ni vizuri ikaonekana kwamba kuna kitu ambacho kinaleta manufaa kwa wananchi wake katika Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini atavifufua vile viwanda vya Mkoa wa Mara? Maana tulikuwa na Kiwanda cha Mara *Oil* ambacho sasa hivi hakifanyi kazi; kuna Mugango *Ginnery*, tuna *Jarif Ginnery*, *ORAM Ginnery;* hivi vingine vilikuwa vya watu binafsi na Buramba *Ginnery*, vyote hivi havifanyi kazi.

Pia tulikuwa na viwanda vya samaki; na hivi viwanda vya samaki, sasa hivi kinachofanya kazi ni kiwanda kimoja

tu ambacho ni cha *Musoma Fish*. Sasa Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu kwamba wale wavuvi wanapovua samaki, kwa nini wasiwe wanapeleka kwenye kiwanda kuchenjua minofu ya samaki ambayo inasafirishwa kupelekwa nje ili wasilete usumbufu wowote, wawe wanachambulia pale pale Mkoani Mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kikubwa, ni lazima iwepo mikakati ya Wizara hizi mbili ili izingatie namna ya kumsaidia mkulima pamoja na kuweza kuwasaidia vijana wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sokombi, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Devotha Minja, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Olenasha ajiandae.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu kwa maisha na maendeleo ya Watanzania. *Vision* ya viwanda, Mwalimu Nyerere aliwahi kuiona na ilikuwa *implemented* kuanzia miaka 1967, ambapo mikoa mbalimbali ilionesha kwa vitendo kwa kuwa na viwanda na vilikuwa vikifanya kazi. Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa Mikoa ambayo ilinufaika na *vision* hiyo kwa kuwa na viwanda zaidi ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunavyozungumza viwanda vilivyokuwa vimewekeza katika Mkoa wa Morogoro kwa miaka hiyo ya 1960 viliwezesha wananchi wa Mkoa wa Morogoro kupata fursa za kupata ajira. Ilikuwa siyo rahisi kwa Mkoa wa Morogoro kupata *house girl;* ilikuwa siyo rahisi kwa Mkoa wa Morogoro kupita kukuta watu wanacheza bao; ilikuwa siyo rahisi kwa Mkoa wa Morogoro kupita kukuta Wamachinga; ilikuwa siyo rahisi

kupita Mkoa wa Morogoro ukakuta watu wamekaa vijiweni, kwa sababu kulikuwa na viwanda na viwanda vile vilikuwa vikitoa ajira kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo sasa, namwomba Mheshimiwa Waziri, nimejaribu kupitia sana katika taarifa yake hii, iko wapi mikakati ya kufufua viwanda vya Mkoa wa Morogoro vilivyokufa? Ubinafsishaji wa viwanda badala ya kuongeza *efficiency,* ubinafsishaji wa viwanda umekuwa ni wa kunufaisha watu wachache ambao wamechukua viwanda kama *collateral* kwenda kukopa katika mabenki, kunufaika wenyewe na wananchi kukosa ajira. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, atuambie uko wapi mkakati halisi wa kuvirudisha viwanda vya Mkoa wa Morogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Morogoro hivi sasa kuna viwanda, kwa mfano, Kiwanda cha *Canvas* ambacho kilikuwa kikinua hata pamba kutoka kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa, lakini hivi sasa wameacha kulima pamba kwa sababu kiwanda kimekufa. Kipo kiwanda cha Asante *Moproco* cha Mafuta; kiwanda hiki wananchi walikuwa wanalima alizeti kwa sababu walikuwa na uhakika wa sehemu ya kuuza. Hivi sasa wananchi hawalimi alizeti kwa kuwa hakuna kiwanda. Kipo kiwanda cha Komoa, kipo kiwanda cha C*ERAMIC,* Morogoro *Leather Shoe*, *UNNAT* cha Matunda ambacho kilikuwa kikinunua matunda ya wananchi wa Mkoa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe mkakati wa kufufua viwanda hivi. Siyo hivyo tu, atuambie Serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua wawekezaji hawa ambao kwa makusudi waliviua viwanda hivi? Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha watu hawa ambao wengine kwenye viwanda vile wameuza vipuri, hivi sasa yamebaki kuwa magodauni na wengine wanachunga mbuzi. Je, ni sahihi kwa watu hawa kutumia *collateral* kupata faida lakini wanaviua viwanda badala ya kunufaisha? Atuambie, Mheshimiwa Rais alipita Morogoro akasema atalishughulikia, tunataka kuona kwa vitendo kwamba

hawa wamiliki wa viwanda ambao wameziweka ajira za wananchi wa Mkoa wa Morogoro mfukoni, wanachukuliwa hatua gani kama kweli mna nia ya kuleta viwanda kwa nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la nyumba. Wakati wa ubinafsishaji zipo nyumba ambazo zilikuwa zinamilikiwa na viwanda vile na zilikuwa ni nyumba za Serikali. Zile nyumba hivi sasa zinamilikiwa na watu ambao ndio waliobinafsishiwa viwanda, lakini hivi sasa wafanyakazi wa Serikali hawana nyumba, hawana pa kuishi. Wale watu wamepeana nyumba zile kinyemela, hawalipi pango na hawalipi kodi. Maofisa wanakosa mahali pa kuishi lakini watu waliobinafsishiwa wanang'anga'nia kuishi kwenye nyumba hizi. Hii siyo sahihi kabisa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri amulike, aangalie ili hatua mahususi ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia biashara ya mwendokasi; mabasi ya Dar es Salaam, tuna mengi ya kujiuliza. Biashara hii imekuwa kama ni ya watu wachache. Serikali imeamua kuleta mabasi ya mwendokasi kwa lengo la kusaidia kupunguza msongamano, lakini kuna wazawa, kuna Watanzania ambao walikuwa wakifanya biashara za daladala ambao nao walikuwa na uwezo wa kupata fursa ya kuwekeza katika mwendokasi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Dunstan Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa William Olenasha na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye hotuba hii ya Wizara ya Viwanda. Namshukuru sana Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza katika

Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kusema naiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, nikiwa na *reservation* kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta hamasa kwa Watanzania kuona umuhimu wa kumiliki viwanda. Amefanya kazi kubwa ya kuwahamasisha Watanzania kubadili mitazamo ya uwekezaji ili wajielekeze kwenye kumiliki viwanda; viwe viwanda vidogo, viwanda vya kati, lakini vile vile viwanda vikubwa. Hongera sana, ameitendea haki taalum yake ya Masoko. Naomba sasa hili lisiwe jukumu lake peke yake, Wizara ilichukue hili kwa ujumla wake. Ongezeni nguvu katika kuhamasisha Watanzania wabadilishe mitazamo katika umiliki wa viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nataka nieleze masikitiko yangu; pamoja na nia nzuri ya kuanzisha viwanda, lakini yapo mambo yanakwamisha sana ukuzaji wa viwanda katika nchi yetu. Ukifuatilia mijadala na sisi tunaopitia pitia tafiti zinazofanyika katika nchi hii, moja kubwa ni *lack of coordination.* Kuna maeneo tunakwenda hatua moja mbele, tunarudi hatua mbili nyuma; na nitatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nizungumzie Sekta ya Maziwa. Utafiti wa wenzetu wa *ESRF* unaonesha kwamba mwaka 2010 tulikuwa tunaingiza maziwa kutoka nje takriban lita milioni 40 zenye thamani ya dola milioni 20. Ilipofika mwaka 2014 uingizaji wa maziwa ukaongezeka kutoka lita milioni 40 ukapanda mpaka lita milioni 70 zenye thamani ya dola milioni 40. Unaweza kuona ni jinsi gani tunapoteza fedha kwa kuingiza maziwa kutoka nje. Wakati tukiingiza maziwa kwa kiasi hicho, sisi tunazalisha takriban lita bilioni mbili, lakini zinazosindikwa hazifiki lita 150,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 62 ya maziwa tunayoingiza yanatoka Kenya, asilimia 32 yanatoka *South Africa*, asilimia nne Uganda. Hata haya yanayopitia *South*

*Africa,* kuna walakini mkubwa. Tunaambiwa ni uchochoro wa kukwepa kodi. Nitayasema baadaye haya. Masikitiko yangu ni yapi? Kiwanda cha *Tanga Fresh* ambacho ndiyo kinazalisha kwa wingi sasa, kinazalisha lita 50,000 kwa siku. Ni kiwanda ambacho tulitakiwa kukilinda kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki miaka minne iliyopita, walitaka kuongeza uzalishaji kutoka lita 50,000 kwenda lita 120,000 na tulikuwa tumepata *grant* ya kuweza kufanya jukumu hilo. Wenzetu wa Bodi ya Ushindani wakawapiga faini ya shilingi bilioni nne wakisema walinunua *assets* kinyume na utaratibu. *Assets* zilizonunuliwa zilikuwa za kiwanda kilichokufa, kwa hiyo, hoja ya kuua ushindani haipo. Tumeminyana, faini ile imepungua mpaka sasa hivi bado imeng'ang'aniwa shilingi milioni 400. Hiki ni kiwanda ambacho kingeongeza uzalishaji katika nchi yetu. Fedha ile imepotea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanga Fresh* wameamua kukopa sasa. Wanataka kutumia *assets* zao, majengo yao waende wakakope. *TRA* wanakuja wanazuia wanasema hawawezi kutumia majengo yale kukopa kwa sababu aliyewauzia hakulipa kodi stahiki. Vitu vya ajabu sana! Yaani aliyekwepa kodi yupo, anajulikana; anaendelea kufanya biashara kwenye nchi hii, *TRA,* hawaendi kumbana, wanaenda kumbana *Tanga Fresh* ambaye hahusiki. Mambo ya ovyo sana! Tunashindwa kukuza viwanda vyetu kwa mambo ya ovyo kiasi hiki! Leo hii ninapozungumza, vituo 28 vya kukusanya maziwa kule Morogoro vimefungwa, wananchi hawana sehemu ya kuuzia maziwa yao kwa sababu hayawezi kupokelewa *Tanga Fresh*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanga Fresh* wananunua maziwa Mkoa mzima wa Tanga; *Tanga Fresh* wananunua maziwa kutoka kwa wakulima Mkoa wa Pwani; *Tanga Fresh* wananunua maziwa kutoka Morogoro. Hivi ninavyozungumza, *Tanga Fresh* wameombwa na wakulima kutoka Mbeya wanunue maziwa yao, wanashindwa! Maziwa yanamwagwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingiza maziwa ya mabilioni haya kutoka Kenya, halafu tunakuja hapa tunasema tunataka kuendeleza viwanda, hii haiwezi kuwa sawa. Napiga kelele kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwa sababu sera ya ukuzaji wa viwanda iko kwake, lakini najua mchawi wetu hapa ni Wizara ya Fedha. Najua jitihada alizofanya ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage ili jambo hili liishe, lakini barua ile aliyoandika mpaka leo imekaliwa pale Wizara ya Fedha hakuna kinachoendelea. Tutaendelea namna hii namna gani? Lazima tubadilike. Naiomba Serikali yangu jambo hili lishughulikieni, tuondoleeni aibu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kichekesho kingine, tulipitisha hapa Sheria ya *VAT* kwenye bidhaa za maziwa, tuliingizwa mkenge na wenzetu Kenya lakini Kenya wananchi walipopiga kelele, wenzetu wakafuta kodi ile, sisi tumeendelea nayo. Wabunge tukisimama tukisema hapa, tunaonekana vituko. Tuliyasema hapa kwenye Sekta ya Utalii hatukusikilizwa, Sekta ya Maziwa nayo imeingiliwa, hebu tuwe *smart;* tunapokubaliana na hawa wenzetu, tukiona wamekiuka makubaliano, mara moja na sisi tugeuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu korosho; nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, kipindi kilichopita, tuliahidiwa viwanda sita vya Korosho, leo hii havipo. Ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage, taarifa za Bodi ya Korosho wanatuambia mwaka huu, tani zilizouzwa korosho ghafi, tani 260,000 tusiendelee kuangalia jambo hili, tutumie Mfuko ule wa *Export Levy* kujenga viwanda. Nendeni mkafanye utafiti tujue, kama tunataka korosho yetu ibanguliwe hapa, angalau nusu ya tani hizi, tunahitaji viwanda vingapi, tutengeneze Mfuko wa Mikopo kutokana na *Export Processing Levy* tuitangaze, watu waje wakope fedha zile tujenge viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukurani zangu kwako kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ambayo ni miongoni mwa Wizara muhimu katika Taifa letu.

Pili, natoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa matayarisho ya kitaalam ya hotuba ya Wizara hii. Nawaomba wazidi kushirikiana ili kufanikisha malengo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta binafsi ni sekta muhimu katika nchi yetu. Sekta hii inawagusa wananchi wa kipato tofauti wenye azma ya kujiendeleza kiuchumi. Sekta hii inakabiliwa na matatizo kadhaa, kama vile upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji ambayo huwa yanawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwaondolee urasimu huu ili kuwawekea mazingira rafiki ili iwe kama ni vivutio kwa sekta hii. Aidha, Serikali iwapunguzie tozo ambazo hazina ulazima. Tozo nyingi huwa zinaidaiwa kwa sekta binafsi mapema kabla ya mwekezaji binafsi hajaanza kazi. Ni vyema tozo *(tax)* zidaiwe baada ya uwekezaji kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa viwanda nchini; naipongeza Serikali yetu kwa azma nzuri ya kujenga viwanda, ujenzi wa viwanda utaongeza tija katika nchi na kuongeza nafasi za uajiri. Ujenzi wa viwanda unahitaji matayarisho mengi kabla ya kuanza. Kwa mfano, huwezi kujenga kiwanda mahali ambapo hakuna umeme, maji na miundombinu ya barabara. Naiomba Serikali kuchukua juhudi za makusudi kuimarisha miundombinu hii ambayo itawashawishi wawekezaji wa nje na ndani kuweka katika

Sekta ya Viwanda. Aidha, naomba Serikali ipunguze baadhi ya kodi kwa wawekezaji wakubwa wa nje na ndani ili pia iwe ni kivutio kwa wawekezaji wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matayarisho ya rasilimali watu; Serikali ina azma nzuri ya kufikia na kukuza uchumi kwa kupitia Sekta ya Viwanda. Sekta ya Viwanda ni ya kitaalam ambayo inahitaji weledi wa kupanga na kuendesha sekta hii. Naishauri Serikali kuchukua juhudi za makusudi kuanza kuwatayarisha Watanzania kwa kuwapatia mafunzo ya kila ngazi ili kujiweka tayari kuendesha sekta hii. Aidha, ni vyema kuwafundisha na kuwapa kipaumbele wazawa na kuepuka kabisa kutumia wataalam kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imepania kuwa na Tanzania ya viwanda, naiomba Serikali ianzishe au itafute wawekezaji kwa ajili ya Mkoa wa Njombe. Njombe ni katika mikoa inayozalisha kwa wingi chakula kama vile mahindi, ngano, alizeti na matunda. Hivyo, naiomba Serikali itafute wawekezaji kwa ajili ya kiwanda cha kusindika matunda, unga wa mahindi na unga wa ngano Mkoani Njombe. Pia naiomba Serikali ianzishe au itafute wawekezaji kwa ajili ya viwanda vya karatasi, lami, kiwi na *toothpicks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa Mkoa wa Njombe unazalisha viazi kwa wingi, naiomba Serikali itafute wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza bidhaa zinazotokana na viazi kama *crisps*, katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wafanyabiashara wananyanyasika sana na *TRA* kutokana na

kuwa na tozo nyingi, naiomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wafanyabiashara wasikatishwe tamaa kwa kukimbizwa na tozo nyingi na hasa kwa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo (wajasiliamali) wa Njombe watafutiwe eneo rafiki kwa ajili ya kufanyia biashara zao. Napendekeza eneo hilo liandaliwe maeneo ya stendi mpya iliyopo Mji Mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ya bajeti nzuri na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mkakati wa ujenzi wa viwanda ili Tanzania ifikie hadhi ya nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025. Ni jambo la tija sana kwa uchumi wa nchi yetu na ukombozi kwa suala la ukosefu wa ajira kwa vijana na wananchi wetu. Serikali imezuia eneo la *SEZ* Bagamoyo jumla hekta 9,080. Mwaka 2008. Serikali ilitathmini eneo lenye ukubwa wa hekta 5,742 katika Vijiji vitano vya Zinga, Kondo, Pande, Mlingotini na Kiromo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafidiwa walioainishwa ni 2,180 na fidia ya wakati huo ilikuwa ni shilingi bilioni 60. Mpaka hii leo hekta 2,399 zimetwaliwa, wafidiwa 1,155 wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 26.4. Wananchi 1,025 hawajalipwa mpaka leo; miaka 10 sasa tangu mwaka 2008! Wananchi hawa wanadai jumla ya shilingi bilioni 51 (pamoja na *interest*).

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa wamesubiri miaka 10 kulipwa fidia na wamepata madhila mengi. Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atuambie, lini wananchi hawa watalipwa fidia zao? Kwa vile mwekezaji ameainisha eneo atakalotumia kuwa hekta 3,000 tu: Je, hekta zilizobaki zitalipwa na nani? Lini? Kwa bajeti ipi? Mtindo huu wa kumtaka mwekezaji alipe fidia ya ardhi

inapunguza vivutio vya uwekezaji katika nchi yetu, Serikali irudishe utaratibu wa Serikali kulipa fidia ili kushawishi wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bandari Bagamoyo ni sehemu ya *SEZ* ya Bagamoyo. Ila katika mradi kuna wananchi 687 ambao wamepunjwa fidia zao. Sasa wameshahakikiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Serikali iwalipe fidia zao halali wananchi hawa. Mbona katika bajeti hii ya 2017/2018 haina kasma kwa ajili ya malipo ya fidia hii? Mheshimiwa Waziri awape jibu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa ujenzi wa bandari Bagamoyo utahamisha kaya zinazofikia 2,000. Wananchi hawa waliahidiwa makazi mapya katika shamba la Kidogoni - Bagamoyo. Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda ni shahidi wa jambo hili, yeye alilisimamia alipokuwa *DG, EPZA*. Nyaraka mbalimbali za *EPZA* zinaonesha mpango na ahadi hiyo. Kwa vile Mwekezaji yuko tayari kulipa fidia, naiomba Serikali ifanye maongezi na mwekezaji afidie shamba la Kidogoni ili wananchi wahame eneo la bandari haraka.

Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atueleze ni lini wananchi wanaopisha mradi wa bandari watapewa eneo la makazi yao mapya? Kuhusu mradi wa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, Serikali yetu imesaini mikataba ifuatayo: *MoU* Septemba, 2012; *Framework Agreement,* Machi 2013; na *Implementation Agreement,* Desemba, 2013. Kutia saini *Fremework Agreement* kulishuhudiwa na Rais Mstaafu Mheshimiwa Kikwete na Rais wa China Mheshimiwa Xi Jingping.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni mwaka wa tano. Kwa vile *CMPort Holding* na mbia wako Oman wana mtaji na uzoefu; na kwa vile *CMPort* watalipa fidia ya ardhi, naiomba Serikali yangu Tukufu Iharakishe majadiliano na Mwekezaji huyo ili ujenzi wa bandari ya Bagamoyo uanze mapema. Tangu tumeanza majadiliano mwaka 2012, *CMPort* wamekamilisha mikataba ifuatavyo:-

(i) Sri Lanka, tayari wanaendesha *Colombo International Container Terminal (CICT).*

(ii) Nigeria, tayari *CMPort* inaendesha *Tin-Can Island Container Teminal.*

(iii) Togo, tayari, *CMPort* inaendesha *Lome Port Container Terminal*.

(iv) Djibouti, tayari *CMPort* inaendesha bandari ya Djibouti na *Container* Terminal.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zinatuacha nyuma! Mheshimiwa Waziri akija kufanya majumuisho atuambie ni lini Serikali itakamilisha Mikataba na *CMPort Holding*? Ni lini ujenzi wa Bandari, Bagamoyo utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na msimamo wa Wizara katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Wizara itasaidia upatikanaji wa Kiwanda cha Matunda Wilaya ya Muheza; kwa kuwa wafanyabiashara na wakulima wa Wilaya Muheza hawanufaiki na zao la matunda hasa machungwa? Katika Wilaya ya Tanga Mjini Kata ya Kiomoni, kuna Kampuni inaitwa *NEEL KHANT Lime Limited Tanga*, kinachomilikiwa na Bwana Rashidi Liemba.

Kiwanda hiki kimekuwa na madhara makubwa kwa wakazi wanaozunguka eneo hilo hasa wanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari Kiomoni. Wizara inafahamu changamoto hiyo? Iko tayari kushirikiana na *NEMC* kufuatilia usalama wa raia wa eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini *Tanga Special Economic Zone (SEZ)* imetengewa fedha kidogo; shilingi bilioni 2.7 katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 - 2020/2021 wakati Tanga ni Mkoa wa

Viwanda? Katika historia ya nchi, Tanga ndiyo mkoa wa kwanza ndani ya nchi hii kuwa na viwanda vingi miaka ya 1980.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke na viwanda. Sensa ya Viwanda inaonesha asilimia 99.5 ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Kwa takwimu hizi, ni wazi viwanda vingi vidogo vinamilikiwa na wanawake. Je, Wizara imejipangaje kuhamasisha wanawake kujiunga katika Sekta hii ya Viwanda?

Je, Serikali kupitia Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa viwanda vinakuwa *gender sensitive* katika *product* na ajira?

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Changamoto tuliyonayo kubwa inayokabili viwanda nchini ni pamoja na ukosefu wa mitaji na teknolojia ya uzalishaji kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kubwa ni kutokuwa na uhakika wa umeme na maji ambayo inafanya viwanda vyetu kutoimarika, hivyo nashauri kuwa ili viwanda viimarike nchini, Serikali ihakikishe umeme na maji vimepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mwenendo usioridhisha kutoa fedha za miradi ya maendeleo, hivyo kuchelewesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie namna bora ya kuiwezesha Benki ya Rasilimali Tanzania *(Tanzania Investment Bank)* ili ifungue matawi mikoani hasa Mkoa wa Kagera, hatua ambavyo itasaidia mikopo kuwafikia Watanzania walio wengi. Kuna changamoto ya kukosekana kwa soko kwa baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa nchini kwa sababu ya kukosa ubora unaotokana na gharama za uzalishaji kuwa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, husuSan kwa wawekezaji wa viwanda vya madawa ya kilimo na mifugo kutozwa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*, unapunguza ushindani wa bidhaa zinazoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe Kiwanda cha *Kagera Sugar* ili kiweze kutoa sukari kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya Watanzania hasa waliopo Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Kagera *Sugar* kipo Mkoani Kagera, lakini wananchi hawanufaiki na kiwanda hicho kwa sababu sukari inakuwa ni ya bei ya juu sana. Hivyo, naiomba Serikali iweze kutusaidia wananchi wa Kagera kupata sukari kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza ugumu katika hatua ya kuanzisha biashara kwa kuongeza tozo za usajili. Jambo hili linaathiri juhudi za kuongeza ajira kwa vijana. Pia inafanya wajasiriamali wasifanye shughuli rasmi za kuingiza mapato ya Serikali na kupunguza ajira zitokanazo na biashara rasmi.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imedhamiria kuwa nchi ya uchumi wa kati ambao unategemea uimarishaji wa viwanda. Tanzania tulikuwa na viwanda vingi miaka ya nyuma lakini tulifika mahali tukauza au kuvibinafsisha vingine, tena kwa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kurudi nyuma katika kipindi kile cha uuzaji wa viwanda, kuangalia mikataba ile yote ili kubaini ni vipi tunaweza kurejesha viwanda mikononi mwa Serikali. Ujenzi wa viwanda ni ghali sana na ni bora na rahisi kufufua vile vya zamani kuliko kuweka viwanda vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda maana yake ni ajira kwa vijana wetu. Serikali hii ina mipango mizuri kwenye

makaratasi, lakini kwa kweli kiuhalisia bado kabisa viwanda havionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuanzisha viwanda vile ambavyo malighafi yake inaweza kupatikana nchini. Tunayo mazao ya mashambani, tunayo mifugo mingi sana na pia tunayo madini mengi. Viwanda pia vilenge katika kukuza uzalishaji wa mazao hayo ya hapo juu. Ni jambo la kuhuzunisha, kwani mazao yanalimwa hapa nchini lakini yanasindikwa nje. Mfano, nchi yetu inazalisha korosho nyingi lakini inabanguliwa nje. Huku ni kukosesha Watanzania ajira na pia kupoteza mapato ya Serikali.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Kamanda wake Mahiri Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri na ya wazi ya kupeleka nchi yetu katika uchumi wa viwanda. Juhudi za wazi zinajionesha, kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu wa uongozi wake, viwanda vimeanza kuchipuka, *SIDO* imekua sana na wananchi wamekuwa wakijitokeza kuanzisha viwanda katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika. Mheshimiwa Waziri, pamoja na juhudi zote hizi zinazofanyika, bado Mkoa wa Ruvuma, Serikali na Wizara yake, haijatoa msukumo wa kuingiza Mkoa wa Ruvuma katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kuingiza viwanda Mkoani Ruvuma? Kipo Kiwanda cha Tumbaku ambacho mwezi Januari, 2016 Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikitembelea na kujionea mwenyewe hali ya kiwanda hicho na alitoa maelekezo ya namna ya kufufua kiwanda hicho. Je, ni mipango gani ya Wizara ya kufufua kiwanda hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Songea hawana kiwanda chochote na hivyo kukosa ajira na manufaa yatokanayo na uwezo wa viwanda. Tegemeo letu

kubwa ni pale ambapo Serikali ilionesha dhamira ya kuanzisha viwanda kwa kutenga eneo la *EPZA* pale Songea Mjini, lakini ni masikitiko makubwa kwamba hadi sasa eneo la *EPZA* limepimwa na watu wamehamishwa, lakini hawajalipwa fedha zao za fidia kutokana na ardhi na mali zao katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa hadi sasa, hawana mahali pa kwenda, umaskini umewapata, maana hakuna ardhi ya kilimo, hawana makazi wala hawana maendeleo wanayoweza kuyafanya kutokana na kushindwa kupata maeneo ya kufanyia shughuli za maendeleo. Pia wanazuiwa kuendeleza maeneo waliyokuwa wakiishi na kutakiwa kupisha shughuli za *EPZA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatukatisha tamaa sana kwa namna tunavyoona wale wananchi wakipata shida katika eneo ambalo walikubali kulitoa kwa dhamira nzuri ya shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, tunawapatia lini wananchi hawa fidia zao wanazozidai? Ni imani yangu kuwa kuwalipa fidia wananchi hawa kutafuatia juhudi za kazi za Serikali kuanza kulitangaza eneo hili la Songea Mjini kwa wawekezaji waanze kuwekeza viwanda katika Mkoa wa Ruvuma.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mwijage, kwa hotuba nzuri ya bajeti yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuweka mbele mapinduzi ya viwanda. Juhudi hizi tumeanza kuona matunda chanya na Tanzania ya viwanda sasa inaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kisiwa cha Mafia wamehamasika katika kilimo cha miwa na kwa kiasi

kikubwa wamefanikiwa kupata mazao mengi, lakini tatizo limekuwa ni kutokuwepo na kiwanda cha kuchakata miwa ili kupunguza ukubwa wa mzigo na kujirahisishia usafirishaji wa mazao. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri kupitia Shirika la *SIDO,* aangalie uwezekano wa Mtaalam kuja na kiwanda rahisi kusaidia wakulima wa miwa wa Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisiwa cha Mafia pia ni maarufu kwa ulimaji wa zao la nazi. Kwa kuwa zao la nazi linatoa mafuta na tui kwa matumizi ya mwanadamu, nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kutupatia kiwanda kitakachochakata mazao yatokanayo na nazi ili kusaidia kukuza kipato cha mwananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais mwaka anazindua Bunge hili la Kumi na Moja alionesha masikitiko yake ya kukosekana kiwanda cha kusindika samaki kwa ukanda mzima wa Pwani kuanzia Mkoa wa Tanga mpaka Msimbati Mtwara. Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa ukaribu suala hili la kiwanda cha kusindika samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijadili suala Kitaifa la viwanda. Niiombe tu Serikali yangu kwenye kuelekea viwanda, mkazo uwekwe kwenye kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi badala ya Serikali kujenga viwanda vyake yenyewe. Serikali haifanyi biashara, Serikali isubiri kutoza kodi na kupata fursa ya kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, naomba Serikali ianzishe vyuo aina ya *VETA* katika makambi yetu ya Jeshi la Kujenga Taifa. Aina ya viwanda inayokuja sasa, lazima tuandae vijana wetu kwenye kada za kuendesha mashine *(Machines Operators).* Hii itasaidia kwao kupata ajira kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuoanisha uanzishaji wa viwanda na kilimo chetu. Sisi mazao yetu mengi ya matunda yanaoza mashambani kwa kukosa kiwanda cha kusindika matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba tuna kiwanda cha Azam pale Mkuranga, lakini kiasi kikubwa wanaagiza matunda *concentrate* kutoka nje ya nchi. Hii inatokana na ukweli kwamba matunda yetu hayalimwi kitaalam na kupelekea shamba moja kutoa matunda yenye ladha tofauti na kushindwa kutengenezwa *juice.* Kilimo cha kisasa ndiyo namna pekee ya kuoanisha ladha ya mazao haya ya matunda ili yaweze kutumika kutengeneza *juice*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kazi nzuri, kadhalika na Watendaji wa Wizara hii. Suala la Makaa ya Mawe, Mchuchuma na chuma cha Liganga, Ludewa ni la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna maelezo yanayojitosheleza kuhusu utekelezaji wa mradi. Kila kipindi cha bajeti, maelezo ni hayo hayo ya Kamati ya Watalaam kupitia mapendekezo ya mwekezaji. Serikali ieleze Bunge lako Tukufu tatizo la uwekezaji Mchuchuma na Liganga. Tunajenga reli tunahitaji chuma! Tutaagiza chuma kutoka nje ya nchi wakati Mungu katujaalia chuma Liganga!

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAMARTEC* ni kiwanda kinachotengeneza zana za kilimo. Hata hivyo, vifaa vya *CAMARTEC* havipatikani kwa wingi kwa wakulima; wangeweza kufanya kazi kubwa na kwa wepesi zaidi kwa kutumia vifaa vya *CAMARTEC*; vifaa vya kupandia, kupalilia, kuvunia na kuchakata mazao. Kwa kuwa viwanda vingi vya hapa nchini vinategemea malighafi ya mazao ya hapa nchini, naomba Serikali kuhakikisha kuwa vifaa vinavyoweza kumrahisishia mkulima kazi, viuzwe kwa wingi na kwa bei nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tunatamani kuwa na viwanda vingi kila Wilaya au kila Mkoa, lakini je,

tumejiandaa vipi kuhusu malighafi, barabara, umeme, mifugo bora, mazao bora na yanayolimwa mwaka mzima na kadhalika? Maandalizi yanahitajika sana kwa wananchi kulima mazao bora yanayolimwa mwaka mzima, ufugaji wa kisasa na umeme usio na shaka kwa wenye viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiamini Serikali ya Awamu ya Tano, hivyo ni kukumbushana mambo muhimu kwa maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliouziwa viwanda na kuvigeuza maghala na vingine havitumiki kabisa: Je, Serikali inasema nini juu ya viwanda hivyo? Naomba maelezo ya Kiwanda cha Maziwa Utegi, Rorya kilichobinafsishwa na kilikuwa na mali nyingi na mpaka sasa hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna mifugo ya kutosha na tungeweza kuuza bidhaa/mazao ya mifugo na kuingiza fedha nyingi nchini. Tatizo letu ni viwanda vya mazao ya mifugo. Hatuna viwanda vya nyama, ngozi, maziwa na kadhalika. Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, maziwa na ngozi? Viwanda vilivyopo vya watu binafsi havikidhi mahitaji ikilinganishwa na mifugo iliyopo. Naamini tukitumia vizuri Sekta ya Mifugo kelele/ugomvi kwa wakulima na wafugaji ungekwisha kwa amani na kwa urahisi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafanya kazi nzuri kwa maendeleo ya Taifa hili. Mifuko hiyo imejenga majengo makubwa mazuri katika miji yetu; na kwa sababu mifuko hiyo, inatarajia kujenga viwanda katika maeneo mbalimbali. Kwa taarifa zisizo rasmi, Mfuko wa *PSPF* haupo vizuri sana kifedha: Je, utakuwa na uwezo wa uwekezaji kama Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inavyojieleza ukurasa wa 170?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kiti chako, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inahusisha pia uwekezaji ambao kwa kiasi kikubwa uwekezaji bado haujapewa kipaumbele. Kwa kiasi kikubwa hotuba ya Waziri Mheshimiwa Mwijage imejikita katika kuzungumzia viwanda ambavyo kwa kiasi kikubwa ni mbwembwe kuliko uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zote za Umma zenye mitaji ya umma ilitakiwa tuelezwe, kwa kuwa taasisi hizi, mfano Mifuko ya Hifadhi yote inajikita katika uwekezaji. Kwa kiasi kikubwa uwekezaji huu hauna tija. Nilitegemea hotuba ya Mheshimiwa Waziri ieleze juu ya uwekezaji butu unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii pamoja na Taasisi za Serikali kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa viwanja bei ni za juu, hifadhi za Jamii kama *LAPF* wamenunua Kiwanja Mwanza *Square metre* moja kwa Sh.255,000/= kitu ambacho siyo kweli. Kuna harufu ya matumizi mabaya ya Ofisi. Mtwara wamenunua kiwanja eneo la Rahaleo *Square metre* moja ni Sh.155,000/= eneo ambalo mimi nalijua. Niliwaambia haya, wakasema *valuer* ameruhusu. *Valuers* wanacheza *deal* na wahusika. Tunataka uwekezaji wenye tija kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeingia mkataba wa miaka 50 na mwekezaji kutoka Botswana. Huu mkataba unampa mamlaka ya kukusanya kila anachokipata na kuipa Serikali asilimia 10% tu. Hali hii haikubaliki. Kibaya zaidi, anajenga vibanda na anakusanya billions o*f money.* Hivi baada ya miaka 50 vibanda vile vitakuwa na thamani kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri apitie uwekezaji unaofanywa na Taasisi za Umma sio kuwaza viwanda vya watu ambao yawezekana wasije kabisa kujenga. Hivi vilivyopo vifanyiwe uhakiki wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Waziri, Mheshimiwa Mwijage, Kiwanda cha Mbolea Mtwara kina tatizo gani? Kwa nini hakijengwi wakati mwekezaji yupo tayari? Kwa nini hawawezeshwi kujenga kiwanda hicho? Kwa nini hawampi rasilimali anazotaka ili ajenge kiwanda Mtwara? Kila kitu kipo mpaka kwenye eneo, kigugumizi cha nini au Mheshimiwa Waziri hataki maendeleo ya Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara Mjini kulikuwa na Viwanda vingi vya Korosho, vyote sasa hivi havipo. Baya zaidi kilikuwepo kiwanda cha *OLAM*, mwekezaji aliwekeza Mtwara Mjini na kiwanda hiki kilikuwa kinaajiri wananchi wengi sana, lakini Serikali ilimwekea mazingira mabaya ya kodi; huyu mwekezaji, amehamisha kiwanda na kukipeleka Msumbiji. Kwani kuna nini wawekezaji wa Mtwara hamwataki wawekeze Mtwara? Au Wizara inataka Mheshimiwa Rais aje tena Mtwara atamke aliyotamka tarehe 4 Machi, 2017? Naomba wawekezaji wenye nia ya kuwekeza Mtwara wapewe mazingira rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *third party* katika ajira, *UCC Dangote* Mtwara; kuna usumbufu mkubwa kiwanda cha Dangote kwa kuwa kuna mtu kati anaitwa *UCC* ndio anayesimamia na kuajiri watu, baadaye anampa mahindi na mahindi anampeleka Dangote. Hawa watu wakati wanapokonya haki za waajiriwa kiwandani, wananyanyasika sana, wafanyakazi hawana utaratibu, wanadhulumiwa haki zao wakidai mwajiri anasema hawamhusu na anamwambia *UCC* wafanyakazi kadhaa hawatakiwi na wanafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza, Serikali ilitoa waraka mwaka 2014 wa kuzuia mtu kati kutoa ajira ya mawakala, umefikia wapi?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi sana kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa juhudi zake nzuri za kufufua na kujenga viwanda katika nchi yetu ya Tanzania. Tumeona jitihada kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano. Nakubaliana kabisa

kuwa nchi ya Tanzania ni tajiri sana, ina kila kitu, lakini tatizo kubwa ilikuwa ni maamuzi magumu tu. Sasa tumepata Rais mwenye maamuzi magumu na sahihi. Serikali haijengi viwanda, lakini Serikali inasaidia katika kutoa miongozo ya kujenga viwanda na kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mufindi Kusini tuna viwanda vingi sana kwa mfano, Kiwanda cha Chai (*Uniliver Tea Company Limited*), *Mufindi Paper Mill Limited (MPM)*; *Mufindi Tea Company Limited. (MTL),* Kiwanda cha Pareto, Kiwanda cha Mbao *(Sao Hill);* pia kuna viwanda vidogo vidogo vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Serikali, naomba Serikali ijenge miundombinu ya barabara, umeme na maji ili kuwezesha wawekezaji kufanikisha uzalishaji wa bidhaa bila matatizo. Viwanda vinashindwa kusafirisha bidhaa kwa sababu ya babaraba mbovu. Barabara hiyo ni Mafinga hadi Mgogolo, Nyololo hadi Mtwango. Kuna tatizo kubwa la stendi ya reli pale Mgololo ili bidhaa ziweze kusafirishwa kwa njia ya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. Ahsante.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, Ukerewe ni moja kati ya maeneo ambayo yana rasilimali za kutosha kwa ajili ya malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzalishaji mkubwa wa samaki na matunda (mananasi, machungwa na maembe), Wizara ielekeza wawekezaji kwa ajili ya viwanda vya kuchakata samaki na matunda katika eneo hili ili kuokoa matunda mengi kuharibika kwa kukosa soko. Jambo hili litasaidia pia kukuza uchumi wa wananchi hasa vijana na akinamama kwenye visiwa hivi vya Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na uzalishaji mkubwa wa samaki katika Visiwa vya Ukerewe, litakuwa

jambo lenye maslahi kwa Taifa iwapo vitajengwa viwanda vya kuchakata samaki kwenye maeneo haya badala ya kuwasafirisha kuwapeleka katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye sekta ya viwanda kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itafute wawekezaji wa kufufua viwanda vilivyotaifishwa na Serikali na kuwakabidhi wawekezaji wazawa ambao wameshindwa kuviendeleza.

(ii) Serikali itafute wawekezaji kwenye viwanda vidogo vya matunda, viungo (nyanya - *tomato sauce*), viwanda vya juisi za machungwa, maembe, nanasi (*simple machines*) kwenye maeneo yanayozalisha matunda ya nyanya na pilipili.

(iii) Viwanda vinahitaji umeme wa kutosha na wenye uhakika na wa gharama nafuu. Haiingii akilini kuwa na umeme wa gharama kubwa wakati tunazalisha kwa gesi ya Mtwara.

(iv) Kuimarisha sekta ya kilimo kutasaidia upatikanaji wa rasilimali/malighafi za viwanda. Hivyo basi kilimo endelevu ni cha kumwagilia na matumizi bora ya pembejeo. *Agriculture - Raw materials - Industrial goods/ product.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara napenda kuchangia yafuatayo:-

(i) Biashara zinafungwa nchini kwa sababu ya mazingira ya kufanya biashara kutokuwa rafiki. Serikali inawabana sana wafanyabiashara kwa kuweka kodi nyingi sana za uingizaji wa bidhaa toka nje. Hii ni hatari kwa uchumi.

(ii) Mfanyabiashara mpya na hasa wale wadogo wanawekewa makadirio makubwa ya kodi *TRA* hata kabla hajaanza kuzalisha. Serikali iruhusu waanze biashara kwanza kisha itoze kodi tena inayokubalika.

(iii) Leseni za biashara ndogo hazitolewi mpaka mfanyabiashara akalipe kodi *TRA* apewe *tax clearance* ndipo akakate leseni ya biashara Halmashauri. TRA hawako *efficient/ available* hasa vijijini kama Wilaya ya Kakonko, hawapo mpaka mfanyabiashara aende Kibondo, Mtambo wa *TIN* haupo Kakonko wala Kibondo mpaka Kigoma sawa na km.300. Hivyo wafanyabiashara wanashindwa kwenda Kigoma (300km) ili kupata *TIN number*. Nashauri wafanyabiashara hawa wakate leseni za biashara za Halmashauri ili nazo zipate fedha wakati *TRA* ikiweka utaratibu wa kutoa *TIN* vijijini.

(iv) Machinga kuuza bidhaa zao holela hasa maeneo ya Kariakoo soko la wafanyabiashara wakubwa. Hii ni kwa sababu wao hawalipi kodi hivyo huchukua bidhaa za wafanyabiashara dukani na kuziuza bila ushuru wowote. Hivyo wenye maduka Kariakoo hawalipi kodi kwani bidhaa zao zinauzwa nje na machinga, kwa sababu zina bei ndogo na wenye maduka kutotumia *EFD machines*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa wawekezaji, nashauri wapewe masharti nafuu ili wahamasike kuja kuwekeza nchini. Mazingira rafiki na ya kuvutia yatawakaribisha wengi, *invite more coming on board.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda na elimu. Kulingana na umuhimu wa kuwa na viwanda nchini kwetu, ni lazima kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuanzisha viwanda na faida zitakazopatikana baada ya kuwa na viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha kilimo. Kulingana na utaratibu wa viwanda ni vyema wananchi wakabadili

utaratibu wa kilimo cha mazao na badala yake walime au kuanzisha kilimo chenye tija kwa ajili ya kuhudumia viwanda vitakavyokuwa vinazunguka maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda na ajira kwa vijana. Ili suala la viwanda lifanikiwe ni vyema elimu ikatolewa zaidi kwa vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa ambao watanufaika na viwanda badala ya kuchukuwa vijana wa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha elimu ya viwanda mashuleni. Kulingana na umuhimu wa suala la kuanzisha viwanda ni vyema kama wanafunzi katika masomo wakawa na elimu au mada juu ya kuanzisha na kuendeleza viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwawezesha wakulima. Kwa kuwa viwanda vingi na kwa asilimia kubwa vinategemea kilimo na ili suala hili la viwanda lifanikiwe ni vema wanawake wakulima wawezeshwe kuanzisha viwanda hata kama ni vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda na mazao ya biashara. Ni vema Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa na mkakati wa kudumu na endelevu kwa kuwa na viwanda bora vya kuandaa mazao ya biashara ili kilimo kiweze kuwakomboa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha vyuo vya *VETA* Mkoa wa Rukwa. Vyuo hivi vitasaidia vijana kupata ujuzi utakaosaidia kuendesha viwanda vitakavyoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ni tatizo kubwa kwa wakulima hasa wa Mkoa wa Rukwa mpaka wanaelekea kukata tamaa kutokana na changamoto hii. Naomba Serikali ishughulikie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ifufue viwanda vilivyokufa vya nguo, nyama, maji na kilimo (pembejeo).

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Wizara hii na kwa viongozi wake wote. Natambua Wizara hii ni kiungo muhimu kati ya wafanyabiashara na Serikali. Bila Wizara hii kufanya kazi kwa umakini na uweledi, basi ndoto ya Serikali yetu ya kuwa na viwanda itakuwa ndoto isiyotimia. Kwa sababu kumekuwa na kila aina ya matamko na sheria za ovyoovyo za kuua biashara ndani ya nchi hii hasa kutoka katika mamlaka zilizopo kama *EWURA, TBS, NEMC*, *SUMATRA* na zinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ili mtu apate leseni ya *NEMC* ya *Petrol Station*, kwanza lazima apate *consultant* ambaye amepitishwa na *NEMC* na baada ya hapo asajili mradi, *consultant* pekee analipwa shilingi millioni saba (Sh.7,000,000/=) na kusajili mradi napo fedha. Ukimaliza *consultant,* ili watu wa *NEMC* waje kukagua ripoti ya *consultant* nao unalipa gharama zao za kuja *site.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo wakiridhika kukupa leseni, unalipa shilingi milioni kumi (Sh.10,000,000/=) na baada ya hapo utaendelea kulipa ada ya kila mwaka shilingi laki tatu (Sh.300,000/=). Utakuta inagharimu zaidi ya shilingi milioni ishirini na tano kupata Leseni ya *NEMC* kwa kituo kimoja na bila kujali kipo kijijini au mjini. Je, kwa faida ya Sh.90 kwa lita kuna biashara hapo, bado gharama za kodi, upungufu wa mafuta, mishahara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nimetoa mfano kwa kituo cha mafuta lakini ndiyo hivyo hivyo kwa hoteli au viwanda ukitaka kupata leseni ya *NEMC*. Kwa mfano huu mdogo, Wizara hii inachukua hatua gani kuhakikisha mamlaka zilizopo zinafanya kazi zake kwa ufanisi na siyo kuwa wakusanya faini na watoza kodi au Wizara hii ni jina tu? Kwa nini chochote kinachofanywa na mamlaka kuhusu biashara ndani ya nchi hii kisihusishe Wizara kwanza kabla ya sheria na kanuni zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa viwanda na biashara katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Zipo changamoto nyingi katika kutekeleza sekta zilizopo chini ya Wizara husika hasa changamoto ya urasimu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda nchini. Wawekezaji ni lulu inayosakwa na mataifa mbalimbali duniani ni lazima kuwa makini. Nashauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kwamba *Tanzania Investment Centre (TIC)* inatoa huduma zote zinazotakiwa kwa mwekezaji katika sehemu moja hasa suala la vibali na uhakiki ufanyike *under one roof*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara ni Wizara mtambuka inayopashwa kufanya kazi zake kwa kushirikiana na wadau na Wizara zingine kama vile Wizara ya Fedha kupitia sekta za mabenki, bima na *TRA*. Benki zinapofanya kazi zake vizuri na kuwa na riba rafiki katika uwekezaji mitaji katika sekta ya viwanda na kodi mbalimbali zinazotozwa zikiwa rafiki zitasaidia katika sekta zilizoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanda nchini kunategemea kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa malighafi kama vile chuma na umeme wa uhakika. Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa kwa uwepo wa kiwango kikubwa madini ya chuma na makaa ya mawe na kwa kuwa makaa ya mawe yanapatikana Mchuchuma na Chuma cha Liganga, katika zoezi zima la uzalishaji chuma, makaa ya mawe hutumika na kinachozalishwa huwa ni chuma pamoja na umeme.

Nashauri Wizara kupitia Shirika la Maendeleo Nchini *(NDC)* lifanye kila linalowezakana kuhakikisha kwamba uzalishaji wa chuma Mchuchuma na Liganga unakamilika

kwa sababu upatikanaji wa chuma na umeme nafuu utarahisisha uwekezaji katika viwanda nchini. Pia uwepo wa usafiri madhubuti wa reli na barabara na huduma bora katika bandari zetu hasa bandari ya Dar es Salaam kwani hili ni lango kuu la shughuli za kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini kutasaidia ukuaji wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara inao mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya viwanda vya nguo katika Ukanda wa Ziwa ambako zao la pamba linazalishwa kwa wingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya nguo na ukamuaji wa mafuta, kwani uongezaji thamani wa mazao yetu utaleta tija kwa wakulima wetu na kuboresha maisha yao na kuchangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

**MHE HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya katika Wizara hii muhimu lakini anaifanya peke yake bila hata kuwa na Naibu Waziri wa kumsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuonesha malalamiko yangu juu ya kukosekana kwa soko la uhakika la zao la ufuta. Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili ili tupate soko la uhakika la zao la ufuta, wakulima waweze kupata fedha stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu suala la kuwezesha wakulima wa chumvi kupata uwezeshaji wa kupata mkopo wa mashine ya kusindika chumvi ili kuinuna kipato chao. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuwaunganisha wakulima hao wa chumvi na *SIDO* ili *SIDO* iwapatie mashine hizo hata kwa mkopo ili tuweze kufungua kiwanda cha kusindika chumvi hivyo wakulima hao waweze kujiongezea kipato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutambua miaka michache iliyopita kulikuwa na taarifa ya uwepo wa Kiwanda cha Simenti pale Mchinga. Taarifa za kiwanda hicho zilikuwepo tangu wakati Jimbo la Mchinga linaongozwa na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir lakini hadi sasa hatuna taarifa zozote kutoka katika mamlaka husika. Tunaomba kujulishwa kiwanda hiki kimefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu hatua ya viwanda vya *LNG*. Tunasikia kuwa kuna watu wanataka kuhujumu jambo hili, je, taarifa hizi ni kweli au la?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu viwanda vya korosho ambavyo vimebinafsishwa lakini watu waliovichukua wanavigeuza kuwa ni maghala tu badala ya kuvitumia kwa ajili ya kuongeza thamani ya korosho kwa kuzibangua. Mheshimiwa Waziri tunaomba wale wote waliochukua viwanda vyetu vya mtama, Nachingwea, Newala na kadhalika wanyang'anywe na viwanda hivyo wapewe watu ambao watavitumia kwa lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunipa uhai na nguvu za kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pia namshukuru Mungu kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa moyo wake wa dhati wa kusimamia ahadi ya kufanya Tanzania kuwa ya viwanda ili kuinua uchumi wa viwanda. Nchi zilizoendelea kiuchumi ziliwekeza sana katika uchumi wa viwanda maana hapo ndipo penye mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwijage, Katibu Mkuu na Watendaji

wengine kwa kusimamia kikamilifu sera ya Tanzania ya viwanda, kweli kasi inayoendelea inaonekana. Nawashauri wasikatishwe tamaa na kelele za wasioitakia mema nchi yetu.

MheshimiwaMwenyekiti, ili kuinua uchumi wa nchi yetu haraka na kuwanufaisha Watanzania wengi, nashauri Wizara kuwekeza sana katika viwanda ambavyo malighafi zake zinapatikana hapa nchini mfano malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Pia nchi yetu imejaliwa kuwa na madini mengi sana tuombe Serikali kuwavutia wawekezaji kuwekeza viwanda ambavyo tutatumia madini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano Kyerwa tumejaliwa madini ya tini ambayo yanapatikana maeneo mengi ya Wilaya. Madini haya yamekuwa yakinufaisha nchi majirani zetu kwa njia ya magendo. Niombe Wizara kuwavutia wawekezaji kuwekeza Kyerwa kwa sababu mahitaji ya mabati ni mengi na hii itainua uchumi wa nchi yetu na kuwapa ajira wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera na mkakati wa Serikali yetu ni kuwawezesha wananchi kwa kuwawekea mazingira rafiki wakulima wetu ili wanapolima wawe na uhakika na soko la bidhaa zao. Wananchi wetu wanajitahidi sana kulima lakini hakuna soko la uhakika. Jimbo langu la Kyerwa liko mpakani, Serikali imekuwa ikikosa mapato kwa sababu ya biashara ya magendo ya kupeleka bidhaa nchi jirani kwa sababu wananchi hawana sehemu ya kuuza bidhaa zao. Ili kuepuka kuikosesha Serikali mapato na kuwaondolea wananchi usumbufu na wale wanaopoteza maisha Mto Kagera kwa biashara ya magendo, naiomba sana Serikali kufufua masoko ya Kimataifa yaliyojengwa Murongo na Nkwenda ambayo yametelekezwa bila kukamilika na mpaka sasa hatujui nini kinaendelea na nani msimamizi wa masoko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko haya yakikamilika wananchi wetu watakuwa na soko la uhakika kitu ambacho

kitainua kipato chao na uchumi wa nchi yetu utaongezeka na tutaepusha biashara ya magendo na madhara wanayoyapata. Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha awaambie Wanakyerwa nini hatma ya haya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe na kuishauri Serikali yangu tunayowavutia wawekezaji kuwekeza ufugaji na viwanda vya nyama, mfano Mkoa wa Kagera tuna mifugo mingi niwaombe Wizara kuwakaribisha wawekezaji wawekeze Kyerwa kiwanda cha nyama na maziwa tunao ng'ombe wengi, mbuzi na mifugo mingine ili kuwainua wananchi wetu kimapato na uchumi wa Taifa letu utaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Watanzania waendelee kuwa sawa lazima tuwavutie wawekezaji maeneo yote ili isionekane maeneo fulani ndiyo tumewekeza nguvu halafu maeneo mengine yameachwa. Nasema hili kwa sababu inaonesha mfano Mkoa kama Kagera umesahaulika kiuwekezaji wakati kuna fursa nyingi na ndiyo wazalishaji wakubwa wa ndizi, uvuvi, madini, ufugaji na kadhalika. Mkoa wa Kagera tumejaliwa kila kitu na tunaweza kulima na kuvuna zaidi ya mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwekeza kwenye viwanda vikubwa ambavyo vinaajiri sehemu ndogo ya Watanzania lakini pia tuweke kipaumbele katika kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi kama viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana ndani mfano kahawa, alizeti, pamba, korosho na kadhalika. Kwa kufanya hivyo tutainua kipato cha wananchi wetu na uchumi wa Taifa na tutapata baraka maana hapa wataguswa Watanzania wengi na watanufaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri hakika kazi anaiweza sana tumuunge mkono Watanzania kwa umoja wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii hasa kwenye eneo la uwezeshaji na uwekezaji. Katika Jimbo la Mlalo, Halmashauri ya Lushoto, wakulima wadogo wameanzisha kilimo cha mazao ya mchaichai ambacho kina tija kubwa kwa sababu ni malighafi ya bidhaa mbalimbali. Tatizo kubwa ni udhaifu mkubwa wa Idara ya Biashara ya Halmashauri kuziona fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa soko pekee tunalolitegemea ni Kisiwani Pemba ambalo ni soko la kati na siyo soko la moja kwa moja kwa mlaji. Tunaomba kwa dhati, Wizara hii iwatafutie wananchi wa Mlalo masoko ya moja kwa moja ya bidhaa ghafi ya mchaichai ili waweze kukuza uchumi na kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mdau wa ndani wananchi wa Mlalo wamethubutu kukopa mtambo wa kusaga na kukamua majani ya mchaichai kuepuka adha ya kusafirisha majani ghafi kwenda Pemba ambako kwa sasa ndiko soko la kati lilipo. Kupitia kampuni ya kukopesha mitambo ya *EFICA* mdau ameweza kukopa mtambo na sasa wananchi wamepata hamasa kubwa ya kuchangamkia fursa hii adhimu tatizo pekee sasa ni soko la moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Kusindika Chai cha Mponde kule Bumbuli bado ni changamoto. Wawekezaji teule wa Mfuko wa Hifadhi wa *LAPF* bado hawajaonyesha dhamira ya dhati ya haraka ya kufanikisha zoezi hili. Kata zaidi ya 15 zinategemea chai kama zao kuu la kiuchumi, tozo za Halmashauri zinapatikana kupitia chai, tunaiomba Serikali ilione hili kwa jicho la huruma sana kuwasaidia wananchi wa Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *AFRITEX* Tanga kinachotengeneza nguo pale Tanga mjini kimefungwa kwa sababu ya kodi. Tafadhali naomba tufuatilie ili kuona tatizo hili ambalo limefanya ajira zaidi watu 2,000 za moja kwa moja ziwe hatarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *RHINO CEMENT* kimeshusha uzalishaji baada ya kukosa malighafi za kutosha za makaa ya mawe kutoka Liganga na Mchuchuma. Napendekeza sana wapewe mrahaba kama waliopewa wawekezaji wa Dangote ile waweze kupata malighafi ya kutosha. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha saruji tani 20,000 kwa mwezi lakini upatikanaji wa malighafi ni chini ya tani 1,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuelekea uchumi wa kati unaotokana na uchumi wa viwanda, bado hatupaswi hata kidogo kupuuza matatizo ya viwanda vilivyopo. Kiwanda cha Sabuni cha Foma, *TIP Soap Industries* vyote vimekufa, Tanga kunani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada zake za vitendo kuhakikisha nchi yetu inakuwa ya viwanda. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya kufufua na kujenga viwanda, huku akihamasisha wawekezaji kuingia nchini na kufanyika kwa biashara ya kiushindani kwa maendeleo ya wananchi wetu. Natoa pongezi za dhati kwa Wizara hii kwa jinsi wanavyojitoa kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa ni wakulima bora na wazalishaji kwa ziada kubwa na kuchangia chakula kwa Taifa letu. Mkoa wa Rukwa tuna viwanda vidogo vinavyoendeshwa na sekta binafsi na tangu 2015 hadi sasa tuna viwanda 137 vyenye ajira ya 411 (mpya).

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wanapata mfumuko wa bei ya unga pamoja na kuwa na mahindi ya kutosha. Hivi sasa bei ya unga Mkoa wa Rukwa sokoni kilo moja ni Sh.1500, kilo tano ni Sh.8,000/= na kilo 25 ni Sh.37,000/=. Naomba Serikali kuwawekea mazingira bora hawa wenye viwanda hivi vidogo kuzalisha kwa wingi na kupelekea kuteremsha bei ya unga. Pia mahindi yaliyomo

ndani ya maghala ya Taifa ya miaka iliyopita yatolewe na kuuziwa wenye viwanda vya unga (sembe) kuliko kuharibika. Tunaomba wawekezaji waelekezwe Rukwa tupate ajira kwa vijana wetu na kuteremsha mfumuko wa bei ndani ya soko kwa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wengi wanakimbilia kufanya biashara mbalimbali ila hawana uelewa wa uendelevu wa biashara zao. Tatizo ni upungufu wa rasilimali watu katika maeneo yetu, Maafisa Biashara kuwa wahusika na leseni za biashara badala ya kuwainua wafanyabiashara kuwa na biashara zenye tija. Naomba Serikali kutoa ajira kwani tunao vijana waliohitimu kwenye vyuo vyetu vya *CBE* ili tupate wataalam wa kukidhi mahitaji, tupate wafanyabiashara watakaoendana na ushindani wa kiulimwengu na wa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwamba kwa kuwa tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, ni vema maeneo kama Rukwa tuhakikishe tunawaimarishia Chuo cha *VETA* na kuboresha Kituo cha *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waziri wa Viwanda kutuangalia sisi wa mikoa ya pembezoni kwa bidhaa kadhaa kuwa na bei za juu mfano sukari kilo moja ni Sh.2,200/=, sementi mfuko ni Sh.14,000/=. Kutokana na maeneo ya ujenzi wa viwanda yapo, tunaomba kuelekezewa wawekezaji wa kujenga viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka wa pili sasa tangu Serikali ya Awamu ya Tano ijinasibu kuwa hii ni Tanzania ya viwanda. Kwanza kabisa, napenda kuzungumzia juu ya rasilimali tulizonazo. Gesi asilia iligundulika kwa mara ya kwanza katika visiwa vya Songo Songo, Mkoani Lindi mwaka 1974. Ikagunduliwa Mtwara Vijijini (Mnazi Bay mwaka 1982 na Ntorya mwaka 2012), Mkuranga Mkoa wa Pwani mwaka 2007 na Lindi, Kiliwani mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha gesi asili iliyogunduliwa katika maeneo haya inakadiriwa kuwa futi za ujazo trilioni nane. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwa na kasi kubwa ya utafutaji mafuta na gesi asilia uliojikita zaidi kwenye maji ya kina kirefu cha bahari na kiasi cha gesi asilia iliyogunduliwa katika kina kirefu cha maji ni takribani futi za ujazo trilioni 33.7. Jumla ya gesi asili iliyogunduliwa nchi kavu na baharini inafika takribani futi za ujazo trilioni 41.7. Rasilimali hii ya gesi asilia inaweza kutumika katika maeneo mbalimbali yakiwemo kuzalisha umeme, malighafi ya kuzalisha mbolea na kemikali, nishati viwandani, majumbani na kwenye taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Mkoa wa Lindi hauna hata kiwanda kimoja cha kuzalisha mbolea za viwandani licha ya gesi kuwepo mkoani hapo. Ni wakati sasa wa Serikali kutafuta na kuelekeza wawekezaji wa kuzalisha mbolea katika Mkoa wa Lindi ukizingatia ukamilikaji wa barabara ya Masasi-Ruvuma kupitia Tunduru utafanya usafirishaji uwe rahisi wa mbolea hiyo hasa ukizingatia Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo watumiaji wakubwa wa mbolea hiyo ya viwandani. Ujenzi huu wa viwanda utasaidia vijana wa Lindi ambao zaidi ya asilimia arobaini (40%) hawana ajira, jambo ambalo litapunguza kama si kuondoa kabisa tatizo la ajira kwa vijana Mkoani Lindi na Kanda ya Kusini kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia juu ya usindikaji na kuongeza thamani mazao. Mkoa wa Lindi unazalisha kwa wingi mazao kama korosho, ufuta, muhogo, mbaazi na mengine mengi. Kwa sasa duniani kote faida ya kilimo chochote kiko kwenye usindikaji na uongezaji thamani ya zao husika. Mkulima wa Lindi na Mtwara bado hajanufaika na anachokizalisha kwa kuwa mteja wake mkuu ni mlanguzi ambaye ananunua kwa mkulima na kuuza kwenye masoko na makampuni makubwa kwa bei itakayompa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Lindi kulikuwa na viwanda vya korosho ambavyo vilikuwa na mashine za kubangua korosho lakini sasa viwanda hivi havifanyi kazi.

Matokeo yake korosho zinauzwa bila kuongezwa thamani na kupelekea kupunguza kipato. Naiomba Serikali ijikite katika kufufua viwanda hivi Mkoani Lindi na pia katika kujenga viwanda vingine hata kwa kushirikisha *private sectors* ili kuweza kumnufaisha mkulima, kutoa ajira kwa vijana, kudhibiti walanguzi na hatimaye kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na viwanda vya nguo hapa nchini, vipo wapi sasa? Mitumba leo inapigwa marufuku huku Serikali haijaleta njia mbadala wa kuleta nguo za bei nafuu kuweza kukidhi mahitaji ya *majority.* Makubaliano ya *East African Common Market* ni kwamba mitumba marufuku ikifika 2019. Wenzetu Rwanda wameanza kuwapa mafunzo akinamama kutengeneza nguo za gharama nafuu kwa kutumia *materials* zinazopatikana kwa wingi. Imebaki miaka miwili tu tutapiga marufuku mitumba ya Ulaya badala yake tutanunua za bei rahisi kutoka Rwanda na China. Sisi tutanufaika na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda Morogoro kinaitwa Mazava ambacho kinazalisha *sport wear* lakini bidhaa zote zinapelekwa Ulaya na Marekani wakati Tanzania hakuna *product* yoyote sokoni. Tunahitaji kuwa na viwanda vya nguo vitakavyoweza kuzalisha, kujiendesha pia wakati huo huo nguo ziweze kuuzwa kwa bei nafuu. Tukiwa na viwanda vyetu vitakavyozalisha kwa wingi itasaidia kushusha gharama za uzalishaji na bei ya kuuza itakuwa rahisi na mwananchi wa kawaida ataweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Kenya wana kitu kinaitwa *Vision 2030*. Kwenye *manufacturing* wana-*target* kutoka kwenye kumiliki soko kwa 7% hadi kufikia 15% ambayo ni zaidi ya mara mbili. Kwa maana hiyo viwanda walivyonavyo sasa wataviongeza mara mbili. Kipaumbele kimoja cha Wizara ya Viwanda na Biashara Kenya ni kutengeneza *skilled technical human resources*.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya vitu vinavyoangusha watu wetu hapa hawana uwezo wa kushindana kimataifa, *skill level* iko chini. Kwa hiyo, hata

tukijenga viwanda bila kuwa na programu maalum ya kunyanyua *skill* za watu wetu, bado *effect* kwenye uchumi wa viwanda itakuwa ndogo maana kazi zitakuja kuchukuliwa na watu wa mataifa ya jirani ambao wameandaliwa Kenya na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri Serikali ijikite katika kujenga viwanda na vilevile kutayarisha vijana kwa kutengeneza *skilled technical human resources* ili waweze kupata ajira katika hivi viwanda. Vilevile Serikali iboreshe miundombinu ili kuwezesha *movement* ya bidhaa zinazotengenezwa, maana kuongelea Tanzania ya Viwanda bila kuwa na uhakika wa miundombinu ya barabara ni sawa na kuongelea mwili wa binadamu bila damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nami nichangie kidogo kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Jimboni kwangu Mikumi kuna kiwanda cha Sukari cha Kilombero ambacho kinafanya kazi nzuri sana ya uzalishaji wa sukari, lakini kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana kutoka kwa wafanyakazi zaidi ya 3,000 waliofukuzwa kazi bila kulipwa mafao yao mwanzoni mwa mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha afafanue ni lini hawa wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi Kilombero *Sugar Company* kabla haijabinafsishwa kwa Illovo watalipwa mafao yao? Pia kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima wa nje *(outgrowers)* ambao wamekuwa wakilalamika kuhusu kupunjwa sana kwenye mzani ambao unamilikiwa na wenye kiwanda. Je ni lini Serikali itawaagiza wenye kiwanda cha Illovo kuweka mzani utakaokuwa wa uwazi ili kuwafanya wakulima kupata haki yao ya kujua mazao yao yanayoingizwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakulima wa miwa wa Bonde la Ruhembe wamekuwa na malalamiko ya muda

mrefu ya kipimo cha *Sucrose* (utamu) ambayo wamekuwa wakipunjwa kwa kuambiwa utamu wa miwa yao ni mdogo sana hivyo kulipwa fedha kidogo sana pia. Wakulima wa bonde la Ruhembe wamekuwa wakiomba sana kwamba pamoja na kulipwa *sucrose* pia walipwe na *molasses* na *buggers* ambazo zinatumiwa na watu wa kiwanda cha Illovo kutengeneza mashudu, mbolea, *spirit* na hata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakulima wa Bonde la Ruhembe wanalia sana bila matumaini kwa nini wanalipwa utamu *(sucrose)* peke yake wakati mazao yao yanatoa pia *products* zingine ambazo wenye kiwanda cha Illovo wanazitumia na kuuza bila kuwalipa tofauti na nchi za jirani kama Kenya na Malawi ambako wakulima wanalipwa pia fedha za *bugger* na *molasses* na kuwasaidia sana kufaidika zaidi na kilimo hicho cha miwa na kuwaongezea zaidi uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja ku-*wind up* atuambie ni kwa nini Serikali haiwaagizi wamiliki wa viwanda kwanza kuwalipa wakulima wa miwa bei nzuri za *Bugger* na *molasses?* Sambamba na hilo kwa nini bado bei ya tani ya miwa kutoka kwa wakulima wa nje bado inasuasua?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kuwa pale Kijiji cha Mufilisi kingejengwa kiwanda kingine kidogo cha Sukari ifikapo mwaka huu wa 2017, lakini mpaka sasa hakuna dalili yoyote ya kujengwa kwa kiwanda hicho cha sukari pale Mufilisi ambacho kingesaidia sana kuleta ajira na pia kurahisisha usafirishaji wa miwa kutoka Kata za Mikumi na Kisanga. Je mpango huo wa kiwanda cha sukari cha Mufilisi kimefikia wapi na ni lini kitakamilika na kuanza kazi? Au ndiyo yale yale ya kwenye utaratibu bila kutekelezeka?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kwenye Jimbo la Mikumi Kata za Malolo, Masanga, Mhenda, Mabuerebuere, Kilangali na Tindiga kuna mazao ya aina mbalimbali tena kwa wingi sana, nadhani sasa Serikali ili iweze kufikia malengo yake ya kuifanya Tanzania kuwa nchi

ya viwanda basi ingeangalia sana umuhimu wa kujenga viwanda vidogo vidogo kwenye Jimbo la Mikumi, ambayo pia vingeenda sambamba na kuhakikisha umeme unafika kwenye kata hizi za Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kurekebisha miundombinu ya barabara, naamini kabisa kilimo kinacholimwa Jimboni Mikumi kitasaidia sana kufanikisha kutoa ajira kwa wananchi wengi zaidi; pia kufikia malengo ya Serikali hii ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, lakini vile vile kufanikisha kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa. Tumebakiwa na ardhi nzuri, kubwa na yenye rutuba na Wanamorogoro wapo tayari kulima kwa bidii; cha msingi ni kuwawekea viwanda ili wapate uhakika wa masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa shamba zaidi ya heka 1000 kwa ajili ya uwekezaji katika Kata ya Kakese, Manispaa ya Mpanda Mkoani Katavi. Shamba hili la kulima mpunga lipo katika Kata ya Kakese, Kijiji cha Mbungani na linamilikiwa na Charles Dofu na Lucas Busanda. Lilimilikiwa 1985, mwaka 1987 walianza kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuchukua eneo hili ilikuwa ni kwa ajili ya uwekezaji ambapo awali lilikuwa la wananchi. Wawekezaji hawa wanachukua mikopo benki na kuilipa kwa kuwachangisha wananchi, wanajipatia fedha kwa kupitia kundi kubwa la zaidi ya wananchi 5000.

Mheshimiwa Naibu Spika, je ni kwa nini Serikali imemuacha mwekezaji huyu *fake* kuendelea kuwalaghai wananchi na kujipatia mikopo mikubwa ikiwepo *NBC* na wanaposhindwa kulipa mkopo wanataka wananchi walipe mkopo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanalipishwa gharama kubwa wanapokodi mashamba. Kwa heka wanakodishwa kwa zaidi ya Sh.500,000/= kwa sababu ni eneo lenye udongo mzuri. Wananchi wanapiga kelele shamba lirudi kwa wananchi na Serikali ya Kijiji ili walime kwa bei ya chini na hivyo wajikwamue kiuchumi. Wananchi hawa wanatishia kuchoma moto shamba hili ambalo lina zaidi ya wakazi 8000. Hatua ya dharura inahitajika kuchukuliwa ili kuvunja Mkataba wa kujipatia maeneo kupitia kuwalaghai wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanataka kuandamana mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri husika; kuna hali ya tafrani katika eneo hili. Ili kunusuru vurugu zisitokee naomba Serikali itatue huu mgogoro mkubwa katika Kata hii ya Kakese. Serikali imekuwa ikitatua kero nyingi katika nchi hii kwa maslahi ya Taifa na amani; mimi nimewazuia wananchi kuja Dodoma kwa maandamano nikiamini kwamba Serikali italifanyia kazi tatizo hili kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walifunguliwa kesi na hawa wamiliki wakatumia rushwa kuhonga polisi. Wananchi wakapigwa ili kuondoka ilihali lilipatikana kutoka kwa wananchi. Je hamuoni kwamba Serikali inaibiwa kupitia wawekezaji hawa wahuni kwa umma? Tunahitaji majibu kuhusu shamba hili; lirudi kwa wananchi, hali ni mbaya, ni mwizi huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niipongeze hatua ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutoa mwelekeo wa bajeti mbadala kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya CCM haina mapenzi mema na wananchi wake katika kuwasaidia vijana kupata ajira kupitia viwanda vidogo vidogo. Tuna wimbi kubwa la vijana waliokosa kazi vijijini kwa takwimu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishwaji wa Mradi wa Viwanda Vidogo Vidogo Vijijini 2016/2017. Serikali imeanzisha

viwanda vipya 161 vidogo vijijini Tanzania nzima na kufanikiwa kuajiri vijana 1,098. Ajira hizi ni chache ukizingatia vijana wengi wako vijijini na hawana elimu. Tulitegemea vijana hawa wangewekewa mkakati wa kuwapatia ajira na si kuwadidimiza kiuchumi vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha mazingira ya uwekezaji ni jukumu la Serikali ili kuhakikisha sheria kanuni na utendaji wa sekta ya umma unakuwa rafiki kwa wawekezaji ili kutoa ajira, kuwalipa vijana kwa wakati, kuacha unyanyasaji kwa vijana wanaofanya kazi migodini katika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Isulamilomo (Nsimbo Katavi), kuna mwekezaji mchimbaji yuko pale na hana leseni; amepora eneo kubwa na vijana wamebaki hawana maeneo. Huyu bwana (Mbogo) Simon Mdandila anazua tafrani na uvunjifu wa amani kwa kuwanyima fursa vijana kupitia kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana zaidi ya 450 wanashindwa kuchimba katika maeneo yao kwa rushwa iliyofanywa na huyu bwana Mbogo. Je Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inawazuia wawekezaji wa aina hii wanaotumia rushwa kuhodhi maeneo katika eneo la uchimbaji na huku vijana wakihangaika kupata ajira? Uwekezaji huu wa aina hii wenye lengo la kuwatesa wananchi pamoja na hali ngumu waliyo nayo usimamiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa Kiwanda cha Kukoboa na Kusaga. Mashine hii ilinunuliwa na Halmashauri ikayeyuka, ilikuwa na thamani ya milioni mia moja lakini leo hii wananchi wakihoji hawapati majibu ya wizi huu wa wazi kabisa. Je Serikali hii kwa kuendelea kuwalea wezi wanaokula fedha za viwanda vya uwekezaji katika Manispaa ya Mpanda kwa kutochukua hatua yoyote hamuoni kwamba mnapoteza fursa za vijana kwa kuwalea wabadhirifu hawa bila kuwachukulia hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa viwanda uendane sambamba na ukuaji wa sekta ya nishati na umeme. Je ni mkakati gani wa haraka wa kuuhakikishia uchumi wa viwanda upatikanaji wa umeme unaoenda sambamba na mazingira ya uwekezaji sawia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM bado haijajipanga pia kujiendeleza kiuchumi kupitia viwanda. Bajeti yenye asilimia 0.36 ya pato hili, je, Wizara hii imejipanga kweli kuwasaidia wananchi au utani?

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:**Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru *Allah Subhanahu Wataala* kwa neema ya uhai na afya njema. Nikushukuru wewe pia kwa nafasi hii muhimu sana kwangu ili nitoe mchango wangu ingawa kwa ufupi katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na bidhaa bandia. Pamoja na kwamba Serikali kupitia *(TBS)* imeweka *program* ya kudhibiti bidhaa bandia kutoka nje ya nchi lakini kinyume chake bidhaa bandia zinazagaa kila sehemu ya nchi yetu, wakati mamlaka ya udhibiti *(TBS)* wapo na jambo hili wanalijua na hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa. Jambo hili la bidhaa bandia linaweza kuleta madhara makubwa katika nchi na kwa wananchi wenyewe kwa ujumla. Pamoja na kuzorotesha bidhaa za ndani ya nchi lakini pia wananchi hawana elimu ya kutosha juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu juu ya jambo hili ni kwamba, kwa sababu *(TBS)* wanashughulikia bidhaa bandia, na kwa kuwa *(TBS)* hawana uwezo wa kushughulikia bidhaa bandia na kwa kuwa *(TBS)* hawana uwezo wa kushughulikia na bidhaa *fake* na kwa sababu *(TFDA)* pamoja na mambo mengine inajishughulisha na dawa zilizokuwa chini ya kiwango na kwa sababu *(FCC)* inashughulika na bidhaa *fake*, kwa mantiki hiyo ni bora taasisi hizi kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la ngozi. Tanzania tuna ng'ombe million 21.3; mbuzi millioni 1.5; na

tunao kondoo millioni 6.4. Pamoja na kuwa na mifugo mingi kiasi hiki jambo la ajabu Tanzania tunasafirisha ngozi ghafi katika kiwango ambacho hakiendani na rasilimali tuliyonayo ukilinganisha na Kenya ambayo inasafirisha ngozi ghafi nyingi kuliko Tanzania. Pia Sekta ya ngozi haitengenezi ajira wala haiongezi pato la Taifa kwa hiyo inachangia pato kidogo sana la Taifa. Pamoja na juhudi za Serikali za mara kwa mara za kuongeza kodi mpaka kufikia asilimia 90 ili kuzuia usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mpango huu haujasaidia kwa sababu bado ngozi zinasafirishwa kwa magendo hivyo kukosesha mapato ya Serikali kutokana na kodi iliyowekwa. Pia hata ngozi ingebaki ndani ya nchi zingeoza kwa sababu hakuna viwanda vya ku-*process* ngozi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuokoa sekta hii ya ngozi. Kama si hivyo basi wingi wa mifugo tulionao hautasaidia vema uchumi wa nchi yetu. Tutabaki na changamoto zile zile za siku zote kati ya wakulima na wafugaji kugombania malisho. Naomba tuwe makini kuhusu hili.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Bidhaa zinazoingizwa bila kukidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa vifaa vinavyokamatwa kutoka nchi za nje kama mabati ambayo tatizo lake ni *Specfication*, yaani geji isiyokuwa sahihi badala ya kuviharibu vitiwe chapa ya bei kulingana na hali yake halisi ili vitumike kwa shughuli nyingine kama kujengea mabanda ya mifugo kuwekea fensi pia ujenzi wa nyumba za muda mfupi. Kuviharibu ni kupunguza *level* ya uchumi na vina *impact* kwenye *GDP* kwani kuna fedha zimetumika toka kwa wazawa *(domestic).*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za bidhaa kuwa juu (bidhaa za viwanda vyetu). Wizara hii ishirikiane na Wizara

ya Fedha kulinda bei ya bidhaa inayotengenezwa ndani; kuweka *VAT* kwenye bidhaa inayoanza kuzalishwa nchini na kupandisha bidhaa hiyo kwa walaji wa ndani kwa kuwa inamvutia mzalishaji kuuza nje ya nchi kwa ajili ya *zero rated concept* ya *export* zote. Pia kupoteza ushindani kwa bidhaa inayozalishwa au kuingizwa kutoka nje hususani nje kwenye upatikanaji wa *material* ya bei rahisi, *technology* ya hali ya juu na sera zao juu ya *exports* zao. Nashauri *VAT* itazamwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya pembejeo. Nashauri Wizara iweke mkazo sana kwenye viwanda vitakavyozalisha pembejeo, yaani mbolea, madawa pamoja na vifaa vya kilimo. Pia maduka ya vifaa vya kilimo yawekwe maeneo ya wakulima sambamba na mafunzo kwa wananchi ili wajue au wapate elimu ya umuhimu wa kutumia vifaa vya kisasa kuwawezesha kuwa na kilimo chenye Tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ya kutekeleza adhma ya Serikali ya viwanda. Ombi, Mkoa wa Kagera tunasahaulika kwenye vipaumbele vya *flagship projects* hususan uanzishwaji wa viwanda vinavyoendana na *comperative advantage* za mkoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati ana-*wind up* atueleze Wanakagera ni lini Serikali itasukuma uwekezaji wa kiwanda cha kusindika nyama ili kusaidia kutunza uchumi wa mkoa kwa kuwa unaongoza kwa wingi na ufugaji ng'ombe nchini. Kufanya hivi kutasaidia kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji inayosababishwa na ng'ombe wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itusaidie vijana wa Kagera hususani Wilaya ya Karagwe waweze kuwafikiria na *SIDO's SME guarantee scheme.*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunisikiliza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuunga hoja mkono. Tanzania ni nchi yenye rasilimali nyingi ambapo kama zitatumiwa vizuri katika viwanda vyetu zitaleta manufaa makubwa sana katika Tanzania yetu. Hata hivyo, changamoto kubwa inayovikabili viwanda nchini ni ukosefu wa mitaji, teknolojia, umeme, malighafi zisizokuwa za uhakika pamoja na ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto niliozitaja hapo juu bado hakuna vivutio vizuri kwa wawekezaji kutoka nchi za nje na mlolongo wa kodi nyingi ambazo zinawavunja moyo wawekezaji wa ndani na nje. Ningeshauri Serikali kwa changamoto ambazo nimezitaja hapo hasa za ukosefu wa umeme, teknolojia na maji ni vema sasa Wizara ya Viwanda ikakaa pamoja na kuwa na mikakati ya pamoja na Wizara ya Nishati, Kilimo na Maji ili kuunganisha nguvu kwa pamoja na kuwa na mkakati mmoja kwa kuwa Wizara nilizozitaja hapo juu zina mahusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mlolongo wa kodi ni vema sasa Serikali ikawa na chombo kimoja ambacho kitakuwa na mamlaka ya kutoza kodi ambacho kitasimamia utozaji wa kodi zote kwa wawekezaji. Mkoa wa Singida ni mkoa unaosifika kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Mazao ya biashara ni alizeti, vitunguu, pamba, ufuta, karanga na choroko. Mazao ya chakula ni mahindi, mtama, viazi vitamu na uwele, lakini bado hakuna viwanda vya kutosha. Pia Singida ni wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Mazao yote niliyotaja hapo juu yangeweza kuwa malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika viwanda mbalimbali ambavyo vingeanzishwa Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida ni maarufu kwa ukulima wa alizeti, alizeti inayozalishwa Singida ni maarufu Afrika Mashariki na Kati. Singida ina jumla

ya viwanda 126 vya alizeti, kikubwa kimoja, vitatu vya kati na vidogo vidogo 122. Hivi vidogo vidogo vinategemea mitaji kutoka *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeishauri Serikali yangu kuona uwezekano wa kuwaongezea uwezo *SIDO,* ili waweze kuwakopesha viwanda vidogo vidogo mitaji ya kutosha. Kwa sasa *SIDO* inakopesha shilingi milioni sita. Iwapo itaongezewa uwezo angalu kuwakopesha wajasiriamali wa viwanda vidogo vodogo milioni ishirini itakuwa ni jambo jema sana. Kwani wajasiriamali wadogo wadogo hawana uwezo wa kwenda kukopa kwenye benki na taasisi mbalimbali za fedha kwa kuwa wanatoza riba kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningeomba Wizara hii kuuangalia Mkoa wa Singida kwa jicho la pekee kwa sababu kila Wilaya/Halmashauri tayari kuna maeneo kwa ajili ya kuanzisha viwanda, kinachokosekana ni mitaji, hivyo iwapo Serikali itapata mitaji itasaidia sana kuweka miundombinu ya viwanda kwa kuwa malighafi si za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Viwanda Mheshimiwa Mwaijage kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuleta mageuzi katika viwanda yeye pamoja na timu yake, nawatia moyo waendelee kukaza buti kazi ni nzuri na yenye tija.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa hotuba nzuri yenye kusheheni mambo mazuri na taarifa kwa umma. *MUVI*, imefanya wilaya na mikoa saba tu hivyo basi ni muhimu kuongeza wilaya nyingine na hasa Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Mpanda katika Halmashauri ya Nsimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEDF*. Mfuko huu bado haujasaidia wajasiriamali kwa kuwa bajeti ni ndogo hivyo Serikali itoe kipaumbele kwa kuongeza mtaji ili wananchi wakope.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Biashara katika Halmashauri. Bado hatujaona jinsi Maafisa Biashara katika Halmashauri wanavyotumika kuendeleza kazi za Wizara katika Halmashauri zetu, hivyo basi Sekretarieti ya Mkoa inafaa kupewa majukumu ya kuendeleza masuala ya viwanda katika mkoa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hatua ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Tanga ulikuwa ni mji wa viwanda na biashara pamoja na kilimo cha zao la mkonge (palikuwepo mashamba 72).

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vya Zamani. Tanga ina bandari na reli ambavyo viliweza kusafirisha bidhaa zinazozalishwa viwandani, wakati ule katika miaka ya 1970 -1990 ambapo pia ajira zilipatikana kwa wingi. Viwanda vingi vimelenga kwa ama kubinafsishwa na kupewa (kuuziwa) watu wasio na uwezo wa kuendesha aina za viwanda hivyo. Mfano Tanga, *Steel Rolling Mill* (chuma) kimekufa, hali ya kuwa chuma bado kinahitajika na kina soko kubwa katika ujenzi wa madaraja, nyumba, mabodi ya magari na bidhaa nyingine za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Kamba Ngomeni Tanga kilikuwa kikizalisha kamba zitokanazo na zao la katani ambazo kwa sasa, mkonge umepata soko kubwa katika Soko la Dunia na kwamba bidhaa zitokanazo na katani zinahitajika sana kwa matumizi mbalimbali. Zana/ bidhaa za mkonge zina soko na mahitaji yake ni ndani na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kuwa kutokana na soko kuwa kubwa Serikali itawekeza upya au kutafuta wawekezaji makini na wenye uwezo wa kuendesha viwanda vya korona na viwanda vya kamba kwa lengo la kutoa ajira kwa Watanzania, lakini pia kuiwezesha Serikali kupata kodi na kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga kulikuwa na viwanda vya sabuni kama Foma, Mbuni, Gardenia, mafuta ya nazi *(nocolin)* na kadhalika. Viwanda vyote nilivyovitaja vimekufa katika zoezi la ubinafsishaji mbovu lakini pia ukosekanaji wa umeme wa uhakika; vile vile kodi kubwa zilizopo. Hivyo nadhani kwa sababu nilizozitaja nimeeleweka. Ushauri wangu; viwanda vyote vilivyokufa au vilivyoshindwa kuendeshwa na wawekezaji wanavyovimiliki, vifufuliwe kwa kupewa wawekezaji wapya lakini pia Serikali ihakikishe kunapatikana yafuatayo:-

(i) Umeme wa uhakika na bei nafuu;

(ii) Mfumo wa kodi uwe rafiki kwa wawekezaji *(VAT/CUSTOMs DUTY)*;

(iii) Vivutio vya kibiashara *(Tax Holiday et cetera)*; na

(iv) Sheria ziwe rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda Vipya vya Nyama na Ngozi. Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa kuwa na mifugo mingi lakini nchi yetu haipati/haifaidiki na mifugo hiyo ukilinganisha na nchi kama Ethiopia na Botswana. Vile vile mifugo (ng'ombe) hutoa maziwa ambayo pia tunashindwa kuyasindika na kusimamia na hatimaye tunaagiza nyama za kopo *(beaf tin)* na maziwa ya kopo ya *Lactogen, NIDO, NAN, Kerrygold*, kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ethiopia imepata *USD* milioni 186 (2016) kwa mazao ya ngozi na inatarajia kuongeza US $ milioni 90 (2017) na kufikia *USD* 276 (2017). Je Tanzania inapata *USD* ngapi kwa 2015 – 2020? Zaidi ni migogoro ya wakulima na wafugaji, Maafisa Wanyamapori kuwapiga risasi ng'ombe na wafugaji na kashfa ile na kusababisha Mawaziri kujiuzulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili *(scandal)* ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilisababisha baadhi ya Mawaziri

kujiuzulu. Ushauri wangu, (Serikali itafute wawekezaji wakubwa kuboresha sekta ya mifugo ili viwanda vya nyama na ngozi vijengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kusindika mboga/matunda. Tanzania imejaaliwa na Mwenyezi Mungu katika mikoa na kanda aina mbalimbali za matunda na mboga mboga. Pia Tanzania inayo mito na maziwa yenye maji ya kutosha na kama tukifanya *Irrigation scheme for fruits and vegetables* tunaweza kupata mapato kwa wananchi (kujiajiri wenyewe). Serikali za mitaa zitapata mapato na Serikali kuu pia itapata mapato kutokana na kodi baada ya kulifanyia kazi kikamilifu eneo hili la kilimo cha matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazao ya Matunda na Mboga Mboga Katika Mkoa wa Tanga. Mkoa wa Tanga unazo wilaya nane (8) na kati ya hizi zipo ambazo ni wazalishaji wakubwa wa mazao husika na wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muheza ni Wilaya inayozalisha matunda aina ya machungwa, machenza, madalanzi, malimao, mashuza, mafenesi na mapera, ambayo ikiwa Serikali itatafuta wawekezaji wa viwanda vya kusindika matunda ajira na mapato yatapatikana. Lushoto, ni wazalishaji wakubwa wa aina zote za mbogamboga na matunda (nyanya, vitunguu maji/saumu, *cabages, spinaches,* matango pamoja na pilipili hoho. Aina zote hizi zina soko kubwa katika Soko la Dunia (Europe na America) Serikali ilete wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda bila umeme ni sawa na gari bila mafuta. Umeme ndio *Enquire* kuu za viwanda, bila ya umeme wa uhakika, wataalam waliobobea na wenye weledi na uzalendo hata tujenge viwanda vingi kama utitiri baada ya muda vyote vitakufa tena. Ushauri, Serikali inahitajika kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana, mifumo ya kodi iwe rafiki na tuondoe urasimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii muhimu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Nimefuatilia sana taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji lakini katika hotuba yake hakuzungumza mkakati wa kufufua viwanda vilivyokufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Tanzania ya Viwanda lilikuwepo na Mwalimu Nyerere miaka 1967 alikuwa na *vision* hiyo na a*li-implement* wakati ule kwa kuhakikisha viwanda vingi vinaanzishwa katika mikoa mbalimbali ukiwemo mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro pekee ulikuwa na viwanda zaidi ya 40, lakini hivi sasa viwanda vingi vimekufa vikiwemo viwanda vya *Canvas, Komoa, Asante Moprocco, Ceramic Tanzania, Leather Shoe, Unnats* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aje na majibu, upi mkakati wa Serikali wa kufufua viwanda vya Mkoa wa Morogoro ambavyo vilikuwa vikitoa ajira kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro?

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa viwanda ulikuwa na lengo la kuongeza ufanisi wa uzalishaji na si kuua viwanda. Sasa kwa nini uwekezaji umetumika kuongeza tija kwa mwekezaji na kuua ajira? Wawekezaji kwa masikitiko makubwa wametumia viwanda hivi kama *Collateral* kuchukua mikopo mikubwa katika mabenki badala ya kuendeleza kwenye biashara za malori, mabasi na kuua viwanda hii sio sawa. Tunataka kuona Serikali inachukua hatua mahsusi kwa wawekezaji hao kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Serikali zilizonunuliwa na wawekezaji hata baada ya kuua viwanda kwa nini wawekezaji hawa wasirudishe nyumba hizo zikatumika kwa wafanyakazi wa Serikali? Hawalipi kodi hawalipi pango, huku wameua viwanda; ni kwa nini Serikali isichukue nyumba hizi zikatumika kwa maofisa wa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya Mwendo Kasi Jiji la Dar es Salaam, ni kama imekuwa *monopolized* na watu

wachache. Kabla ya mwendo kasi wapo wamiliki wa mabasi ya daladala ambao walikuwa wakifanya biashara tena kwa mkopo na wengine wakijifunga mkanda kuuza nyumba, mali na kuingia kwenye biashara ya daladala. Serikali imekuja na mpango wa mabasi yaendayo kasi; kwa nini wasiwape fursa wafanyabiashara wa daladala nao kama wana uwezo wawekeze katika mabasi hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mabasi ya mwendo kasi ambayo yalikuwa yanatoa huduma kwenye njia pekee sasa hivi yanafanya biashara kwenye njia ambazo si maalum; wa mfano Mbezi Louis, Muhimbili; hali hii inawaweka pembezoni wafanyabiashara wanyonge wa daladala ambao nao wangeweza kupata fursa hizo kama wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya viwanda sasa itekelezwe kwa vitendo ambapo tunatarajia kuona Serikali inafanya kazi kwa pamoja na Wizara nyingine mtambuka kama vile Wizara ya Kilimo na Mifugo, Nishati na Madini pamoja naWizara ya Maji na Umwagiliaji. Hakuna viwanda bila uhakika wa umeme na malighafi.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Allah kwa kunijaalia afya njema na kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Nchi yetu ni nchi ya kilimo ambapo wakulima huzalisha matunda kama maembe, machungwa, mananasi na mengineyo. Kwa vile tumekusudia kujenga Tanzania ya Viwanda kwa nini basi mazao kama hayo ambayo nimeyataja hapo juu ambayo huzalishwa kwa msimu tunashindwa kuyatengenezea viwanda na kuyasindika kwa matumizi ya baadaye?

Mheshimiwa Naibu Spika, matunda hayo kama yangesarifiwa nina imani kwamba nchi yetu ingeweza kuuza nje ya nchi na kupata fedha za kigeni na hivyo kupelekea kuongeza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunataka Tanzania ya Viwanda ni vema tukaangalia kwa kina nini kilisababisha viwanda vyetu vingi vimekufa, tena vile ambavyo malighafi zake zinapatikana ndani ya nchi yetu. Kama tatizo ni wataalam basi kabla ya kuanzisha ufufuaji wa viwanda hivyo, basi vijana wapewe taaluma inayolingana na viwanda hivyo; lakini lakini tatizo ni uongozi mbovu basi ni vema kukawa na usimamizi wa hali ya juu au wa mara kwa mara ili kugundua hizo kasoro zinazopelekea viwanda kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania yetu ya leo tunazalisha mpira kwa wingi lakini *General Tyre* imekufa na tunaagiza mipira kutoka nje ya nchi. Pia tunazalisha ngozi kwa wingi lakini tunashindwa kuzalisha viatu, mabegi na hata mikanda, vitu vyote hivi tunaagiza kutoka nje ya nchi. Hivi kweli kwa msingi huo tuna lengo thabiti la kuwa na Tanzania ya Viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko yangu makubwa ni kushindwa hata kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vingeweza kusaidia kutoa ajira ndogo ndogo kwa vijana wetu. Leo Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa ufugaji lakini tunaagiza maziwa kutoka nje. Pia maembe yanazalishwa kwa wingi Zanzibar lakini yanasafirishwa katika nchi za kiarabu tena huuziwa hapa nchini kwa fedha zetu za Tanzania. Hili linalikosesha mapato mengi Taifa letu.

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho Masasi kina mwekezaji aliyepaswa kukifufua, lakini kimegeuzwa ghala la korosho; tafadhali tunaomba majibu juu ya hoja hii. Mheshimiwa Waziri mfumo uliopo sasa hauwezi kuwafanya wajasiriamali wenye viwanda vidogo vya ubanguaji kupata malighafi, wasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ili kuchochea ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kusini kuna malighafi ya juisi (mabibo na maembe mengi) mpango wa Serikali ni upi katika uwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake za kuiendeleza nchi katika sera ya Viwanda iliyowekwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli kwa kutekeleza kwa vitendo, kwa kweli viwanda ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba sana Serikali yangu ya CCM kujaribu kulimaliza tatizo la Liganga na Mchuchuma kwa kuwalipa fidia wale wananchi wa Ludewa na kuendeleza yale machimbo na kumtafuta mwekezaji mwenye uwezo kwani ni muda mrefu sasa toka tuseme kuna mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni upatikanaji wa vibali vya uwekezaji wa haraka kwani *TIC* kuna urasimu sana na hivyo kupeleka wawekezaji kuondoka na kufanya uwekezaji kwenda na mwendo wa kusuasua, hivyo tutachelewa kufikia malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na timu yake yote kwa ujumla kwa hotuba yake nzuri inayoonesha matumaini makubwa na zana nzima ya Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika kuwa Wilaya ya Lushoto ni ya Wakulima wa matunda na mbogamboga, na ndiyo biashara inayoipatia Halmashauri mapato makubwa. Pamoja na hayo asilimia kubwa ya matunda yale na mbogamboga vinaoza kwa kukosa soko. Kwa hiyo, niombe pamoja na kuishauri Serikali yangu

iwakumbuke wakulima wa Lushoto kwa kuwawekea kiwanda angalau hata kimoja tu ili mazao ya wakulima yasiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika Tanga ni Mkoa wa Viwanda lakini viwanda vilivyokuwa Mkoa wa Tanga vyote vimekufa, mfano kiwanda cha nondo, kiwanda cha sabuni, kiwanda cha nguo, kiwanda cha katani, kiwanda cha Mkumbara, kiwanda cha mbolea, kiwanda cha chai cha Mponde kimefungwa mpaka leo. Wakulima wa chai wanapata tabu hawajui hatma ya kiwanda kile na maisha yao yamekuwa ya tabu mno na ukizingatia kiwanda kile hakina tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho Waziri alisema kiwanda cha chai Mponde ameshakikabidhi kwenye Mfuko wa Jamii *(LAPF),* lakini mpaka sasa Mfuko huu wa Jamii haujaonekana na wala hawajaonesha nia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba Mheshimiwa Waziri, uwafuatilie watu hao *then* utupe majibu ya kuaminika wawekezaji hawa watakwenda kufungua kiwanda kile. Pamoja na majibu hayo utakayoyatoa pia tungeomba ukayatoe wewe mwenyewe kwa wakulima wale kwani imefika hatua hawatuamini kabisa sisi viongozi wao. Msema kweli ni mpenzi wa Mungu kiwanda kile mpaka sasa kina miaka minne sasa hakuna muafaka, leo tusipopata majibu ya kuridhisha tutashika shilingi juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mwisho kabisa nimwombe Mheshimiwa Waziri, aikumbuke Tanga na aikumbuke Wilaya ya Lushoto.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mambo yote. Pili, nakushukuru wewe binafsi kwa ujasiri wako wa kuliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii angalau kwa uchache kati ya mengi ya Wizara hii

ya Biashara na Viwanda. Viwanda ni kichocheo cha maendeleo katika kila Taifa duniani, viwanda ni mkombozi wa wananchi kupitia ajira na kuimarisha biashara na ustawi wa hali za wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo na uimarishaji wa viwanda katika nchi na duniani kote unapitia hali au hatua mbalimbali, uamuzi wa nchi yetu kuja na mkakati wa kujenga viwanda ni wa busara sana ila kabla ya kufikia huko kwanza kuna hizi hali mbalimbali mpaka kufikia uchumi wa viwanda, lazima zitekelezwe ili manufaa tunayoyafikiria yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vinahitaji wataalam na injinia mbalimbali ili waweze kuviendesha kwa uzalishaji, hivyo naishauri Serikali kujipanga na wataalam wazawa na wazalendo kwa kuwasomesha vijana wa kutosha ili viwanda tuviendeleze viwe na wafanyakazi wazawa na wataalam wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naishauri Serikali ikubali kutenga fedha kiasi cha kutosha ili kutoa nguvu kubwa juu ya kupata elimu kwa wataalam watarajiwa, ambao watafanya kazi katika viwanda hivyo. Lakini jambo la kusikitisha ni bajeti ndogo itengewayo Wizara ya Elimu ili kusimamia mafunzo na elimu ya kuzalisha wataalam, hivyo tumekuwa hatufikii lengo kutokana na bajeti ndogo itolewayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchumi tunaouendea ni wazi kwamba tunahitaji mafundi mchundo wa kutosha ili kukidhi haja ya viwanda vyetu vinginevyo kama Serikali haikutilia mkazo jambo la elimu tutakuwa siku zote wa kuajiri wataalam toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, India ni nchi inayoendelea kama Tanzania lakini sitaki kusema kwamba tuko sawa na India lakini India imelipa uzito mkubwa suala la elimu kiasi kwamba India wanatenga zaidi ya asilimia 10 ya bajeti ya nchi yao kwa upande wa elimu, sisi Tanzania bado tuko

nyuma si zaidi ya asilimia 4.5, hivyo India imefanikiwa kuzalisha wasomi na wataalam wengi sana wametosha India na wanauza wataalam duniani kote. Mfano, katika kampuni kubwa kama *Microsoft ya Bill Gates* takwimu zinaonesha zaidi ya wafanyakazi mabingwa asilimia 10 ni kutoka India. Pia Madaktari Bingwa wengi walioko Marekani na duniani kote ni Wahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siri ya mafanikio hayo ni mkakati wa makusudi wa kuwekeza katika elimu. Kwa hali hii ni lazima na sisi tusiwe nyuma kwa kuiweka elimu kuwa ni kitu cha chini, huwezi kuendelea katika nyanja yoyote duniani bila elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri tena Serikali itilie maanani juu ya elimu katika nyanja zote hasa katika suala zima la utafiti, jambo ambalo halionekani kupewa nafasi kubwa wakati inafahamika wazi kwamba bila utafiti huwezi kuleta ufanisi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakuwa tayari kuiwezesha elimu na sisi tutazalisha wataalam wengi kwa ajili ya viwanda vyetu na ziada tunaweza kuuza nje, vinginevyo kama hatukuwa makini kwa uwekezaji juu ya elimu baada ya kuzalisha wataalam tutakuwa tukizalisha watumishi tu.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kuunga mkono hoja mapendekezo ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aseme ni lini ataenda Jimbo la Mlimba katika Kata ya Namwawala, Kata ya Mofu, Vijiji vya Idandu na Miyomboni ili kuweka utaratibu wa ujenzi na kilimo cha miwa ya sukari na wananchi waweze kunufaika ili kuwaondolea tabu wanazoendelea na kupata miaka mingi sasa bila kuwa na uongozi wa Serikali za Vijiji kwa kuwa ni eneo la uwekezaji wa kiwanda cha sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jimbo la Mlimba ni eneo la kilimo kikubwa cha mpunga, lakini Serikali haijaweka mkakati na uendelezaji wa wakulima kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuwawezesha kuwepo kwa viwanda vya uchakataji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu MPM - Kiwanda cha Karatasi Mgololo. Mara kadhaa nimeongea na Mheshimiwa Waziri kuhusu kiwanda hiki na hata nimefikia kumwandikia, kuomba ridhaa ya kuuona na kuupitia mkataba wa ubinafsishaji wa kiwanda hicho ambacho awali kilijulikana kwa jina la *SPM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoenda uchumi wa viwanda jambo ambalo Serikali ilisisitiza ni kuhakikisha kuwa wote waliopewa viwanda kuhakikisha vinazalisha katika uwepo na malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, MPM wanazalisha katika *stage* fulani kisha wanasafirisha *material* kwenda kufanya *finishing* Kenya, kisha karatasi zinarejeshwa kuja kuuzwa hapa nchini, hapa kuna *double loss*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, hawazalishi *end product* kwa maana ya karatasi, tunapoteza sehemu ya ajira kwa sehemu ya *finishing* kwenda kufanyiwa Kenya, lakini pia tunapoteza mapato maana tungeweza kupata fedha za ndani na kigeni kwa kuuza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya masuala ya *East Africa Community* kuhusu *rules of origin*, *MPM* inatuletea karatasi kutoka Kenya na ushuru unaolipiwa *is only* 10% na siyo 25% maana sote tupo ndani ya *EAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, kiwanda hiki kinauziwa magogo nusu ya bei 14,300/= kwa *cubic meter*, inapewa magogo hayo na Serikali *(Sao Hill Forest*). Je, kina sababu gani ya kutozalisha *finished product* kwa maana ya karatasi? Kusimamia na kuhakikisha kuwa ile *machine* Na.1 inafanya kazi italeta tija na kuipa Serikali heshima kuwa ina

maanisha ilichosema kuwa, itahakikisha wote waliopewa viwanda wanatenda kadri ya malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *One Stop Centre*, Uanzishwaji biashara za kati na za chini ni suala lenye malengo marefu kiasi kwamba inasababisha biashara nyingi kutokuwa rasmi. Ushauri, tuwe na *one stop centre,* mfano wa *TIC* kila Mkoa, kuliko ilivyo sasa mara *BRELA*, mara *TIN,* mara OSHA. Tuki-*centralize* katika *level* ya mkoa itarahisisha suala zima la kuanzishwa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya masuala ambayo ukizungumza na Jumuiya ya Kibalozi (*Diplomatic Community*) ni suala la *Double Taxation* na *Protection of Investments,* wanasema mahusiano katika dunia ya sasa ni kuhusu kuimarisha fursa za kibiashara (*Trade Opportunities*) na ili kuzifaidi fursa hizo ni lazima pawepo mazingira bora ya kufanyia biashara na uwekezaji. Mazingira hayo mojawapo ni hili la *double taxation* na *protection of investments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nchi nyingi mfano Oman, Kuwait na za *South East* Asia, kama Korea, Japan na hata China ziko tayari kushawishi watu wao kuja kuwekeza hapa nchini, lakini ukakasi upo kwenye *assurance* yao hususani katika masuala hayo ya *double taxation* na *protection of investments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tupunguze woga, tupo na mashaka mno, kila jambo tunahisi tutaibiwa au kudhulumiwa, naamini tunao wataalam ambao watatufanya tufikie ile tunaita *win win agreement*. Hivyo ili yafanikiwe ni lazima Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Fedha, ambao *focus* yao ni kukusanya tu pasipo kuangalia kuwa bila ushiriki wao katika suala zima la *double taxation*, itakuwa haileti tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa Biashara. Katika mchango wangu bajeti iliyopita niligusia suala hili, kuwa tunapoenda uchumi wa viwanda na *reflection* yake

kiuwekezaji kama lilivyo jina la Wizara, Muundo wa Kada hii kuendelea kufichwa ndani ya Idara ya Fedha katika Halmashauri zetu sio sahihi. Ikiwa Nyuki tu ni Kitengo kwa nini hii isifanywe Idara au angalau Kitengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Biashara wamebaki kufanya kazi ya kukagua leseni, wapo vijana ni wasomi wazuri lakini wako *under utilization,* kwa sababu hata Wakurugenzi wanajikuta wanawapangia kazi ambazo sio za utaalam wao. Ni wakati sasa kada hii, ninyi Wizara muongee na Utumishi na TAMISEMI muweze kuipa nguvu kimuundo ili watumike ipasavyo hasa katika suala zima la biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafinga Mjini na Uchumi wa Mazao ya Misitu (Mbao). Mji wa Mafinga ni kitovu cha shughuli za kiuchumi na uzalishaji katika Wilaya ya Mufindi na Mkoa wa Iringa. Hata hivyo watu hawa hawajapata fursa ya kupata huduma mbalimbali na changamoto wanazokutana nazo hasa katika sekta ya mbao, uzalishaji wa nguzo na milunda. Ombi langu, naomba waje hapa Dodoma kutokana na Waziri na Watendaji ili msikie maoni na ushauri wao kwa namna gani mnaweza kuwasaidia kushiriki ipasavyo katika suala zima la kuelekea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SIDO*, inafanya kazi vizuri lakini *SIDO* wamejikita *level* ya Mkoani tu, Mafinga ina fursa yingi, tungependa *SIDO* ishirikiane na Halmashauri ya Mji wa Mafinga katika suala zima la kuwepo ama kutenga *Industrial clusters* kama walivyofanya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Industrial Cluster's*, jambo hili lilijitokeza mwaka 2016/2017, hata hivyo nikifanya tathmini ni Halmashauri chache zimelitekeleza. Nashauri, kwa kushirikiana na TAMISEMI, Halmashauri zipewe maelekezo maalum kutenga maeneo hayo na ikibidi wapewe *deadline* maana hatuwezi kuwa na viwanda pasipo kutenga hizo *Industrial Cluster's.*

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa jitihada kubwa anazofanya kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii nikiamini kabisa nchi yoyote duniani ambayo ina viwanda imara vinavyozalisha, uchumi wa nchi yake utakuwa imara. Nchi yetu ina fursa pengine kuliko nchi zilizo jirani nasi je, tutapataje fedha za kigeni bila kuuza nje? Tuna maeneo mengi ambayo yana fursa ya mali lakini tatizo ni usimamizi ambao siyo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ya nchi yetu miaka ya nyuma yalikuwa na viwanda, mfano Mkoa wa Tanga lakini viwanda vimekufa, japo nimeona jitihada za kuvirejesha hali hiyo kwa kuona ujenzi wa viwanda vya sementi katika mkoa wetu. Tanga tuna reli inayoanzia Tanga kupitia Moshi, Arusha baadaye Musoma, tukijenga viwanda vingi Tanga na uwepo wa reli ya Tanga tutarejea mafanikio makubwa kwenye fikra ya nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya nchi yetu kuelekea kuwa nchi ya viwanda, bado kuna tatizo la wawekezaji wetu kukosa mazingira au ushirikiano kutoka baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara, hili litazamwe sana. Mfano yupo mwekezaji ambaye anataka kujenga kiwanda cha mabati, Wilaya ya Mkuranga ameshindwa kuanza uzalishaji kutokana na Baraza la Mazingira *(NEMC)* kutompa kibali, hili lifuatiliwe kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine juu ya ugawaji wa fursa hizi katika maeneo ya nchi yetu, baadhi ya mikoa ya nchi yetu ina viwanda vingi kuliko mikoa mingine na si kwa sababu tu maeneo haya yana fursa zaidi kuliko mikoa mingine bali kuna tatizo la kutotoa fursa sawa. Nashauri sana tena sana tutoe fursa sawa kwa kila eneo muhimu, fursa ipatikane eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, Wilaya ya Kilindi ni eneo lenye shughuli kubwa za kilimo, pamoja na shughuli za mifugo. Naomba sana nasi tupewe fursa katika maeneo hayo. Mfano tunaweza kupewa kiwanda cha uchakataji wa siagi kwa sababu tuna mifugo mingi, aidha tunaweza kupatiwa kiwanda cha ngozi kwa sababu tunayo mifugo ya kutosha. Naomba Mheshimiwa Waziri achukue ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuangalia kilimo na elimu kuwa kipaumbele cha kwanza ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi kutoka kwa wakulima wetu ili kukuza uchumi wa kaya. Nishauri Serikali kupitia sera zake za viwanda kuzihuisha ili ziendane na wakati wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashauri Serikali itunge sheria na adhabu kali zinazotokana na uharibifu wa mazingira, hasa utiririshaji maji ya viwandani ambayo yamekuwa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri Serikali kurejesha viwanda vyote vilivyobinafsishwa kutumika kinyume na mkataba wa awali. Mfano, Kiwanda cha Korosho Kibaha kimegeuzwa mahali pa kutunzia bidhaa, hivyo matumizi yaliyoainishwa wakati wa mkataba kukiukwa. Naishauri Serikali kupunguza urasimu katika kusajili biashara na kupelekea wawekezaji kushindwa kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda na wanawake, naishauri Serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma wasaidiwe ili kuweza kupata mikopo ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Mfano, viwanda vya vyakula vya kuku na mashine za kutotolea vifaranga ili waweze kujikwamua kiuchumi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** *May your Table be pleased to read my contribution in English as it is research based, it should also be read with Intoxicating Liquour Act. of 1968/ 1966 and 1981.*

*Justification for cashew value addition in Tanzania. Cashew Apple Processing: In Tanzania, cashew apples are under utilized. In most cashew-growing areas, small quantities of cashew apples are consumed as fruits, though they are not sold in markets as there is no demand for them. A few cashew apples are locally used in production of alcoholic and non alcoholic beverage, but the majority of cashew apples are left to not in the field. Some farmers in Brazil plant cashew primarily for its fruits and the nut is a secondary product which is thrown away, yet they realize a very good profit.*

*It should be noted that Cashew apple have vitamin C, five times than that in citrus fruits, have high carotene and hence they have good health benefits.*

*The estimated amount of cashew apple produced in Tanzania is over 1,300,000 tons in major cashew growing areas based on current National cashew production levels. Assuming that only 10% of it (Approximately 130,000 tons) is utilized for production of juice at extraction rate of 70% about 91.000 tons (approximately 91 million liters) of cashew apple juice will be produced. If each liter is sold at a farm-gate price of $o.5,about $45.5 million will be realized in a season.*

*Equally, if 90% of the remaining cashew apples (Approximately 1,100,000 tons) is used to produce cashew gin (Nipa), farmer could earn even more money than the amount obtained in juice above.*

*It should be noted that Farmers are already knowledgeable in the production of cashew gin, but they are not aware if there is a law that allows them to distill alcohol as long as they have a valid distilling license from relevant authority. As a result, they produce gin (Nipa) in hiding and once they are caught by Police they face prosecution. This*

*calls the need to create awareness to our farmers. Nipa is called illegal illicit alcohol simply because the producers do not have a licensed to do so. The law is clear that gin (Nipa) can be produced but the producer must have a valid license.*

*The institute has done a research on cashew apples processing into juice, Jam and Wine. They are in the final stage of commercializing the value addition to juice and wine. Equally the institute has also undertaken research on cashew butter production. They are also in the final stage of studying shelf life of the cashew butter. Broken cashew kernel are sold at Tshs 6,000/kg. Once the 1kg of broken kernels is processed into butter it will produce three jars (each 330 mls) and will be sold at Tsh 6,000 per jar making a total of Tshs18,000.*

*It should be noted that Cashew kernel is cholesterol free or zero cholesterol therefore it is good for health. These health benefits are the main reason why cashews are quite expensive worldwide. Cashew farmers can double their income if they will add value to cashew kernels, cashew shells and cashew apples.*

*Convincing farmers to produce Gin (Nipa) for value addition into Ethanol and Methanol will give them more income. The reason for further processing is due to the fact that Nipa has about 2% methyl alcohol which is not good for health. It makes people blind but it is mainly used in hospitals (popularly) known as methylate spirit). This means adding value to Nipa will make our people more health and equally farmers will tend to sell to get more money.*

*Naliendele Research Institute is in the process of installing a small scale cashew distilling plants to be specific Fractional Distillation Equipment to separate Nipa into methyl alcohol and ethyl alcohol. The objective is to undertake economic analysis to find out how much more farmer can gain if they sale their Nipa to authorize agent. It is estimated that at moment the Nipa is sold at about Tshs 500 per Fanta bottle which is approximately 330 mls. This means Nipa will be sold at about Tshs 1500 per litre. On the other hand, 100*

*mls of the methylated sprit (methl alcohol 70% v/v) is sold between Tshs 1,000-2000 in pharmacies.*

*Naliendele Research want to establish how much can be obtained from the Nipa if it is fractionally distilled. Data from this study will show how much more farmer can get from cashew apples which are sometimes thrown away or under utilize. It is no doubt that they will earn more than selling the Nipa at Tshs 1,500 per litre. Another advantage of adding value to cashew apples in creation of employment in the entire cashew value chain.*

*Reviving Cashew Processing is Possible; Cashew processors in Tanzania complains that they cannot compete with foreign buyers in buying raw cashewnuts in the warehouse because they hardly get raw cashewnuts when bidding. On the other hand, they also complain that they do not make profit due to high prices. One of the reason why they do not make profit is due to the fact that they depend on only one product when processing and these are the cashew kernel. The cashew shells are not value added. They can produce Cashewnut Shell Liguid(CNSL) and shell cakes to be used as fuel.*

*The CNSL also can produce several products as follows:-*

- *Brake linings*
- *Lubricant is high temperature areas*
- *Cosmetics*
- *Insecticides to fumigated buildings*
- *Ceiling boards for high moisture conditions*

*Cashewnut produce the following:-*

- *Kernels (20-25% by weight of raw cashewnuts*
- *Cashew shells (70-80% by weight)*
- *Cashew shell produce CNSL –(20-25%) of weight of raw cashewnuts*
- *Cashew shell cake for fuels (50-60%) by weight of raw cashewnuts*

*It is important for the local processors to be given a high priority in buying cashewnuts in the auction though warehouse receipt system. Arrangement can be done to make sure the local processors do not need go to the auction. They need to be allocate 20-25% of the amount the cashewnuts which was given the highest price during auction.*

*When a foreign buyer bid and get a certain amount of cashewanuts, 20-25% will be allocated for local processors to buy at the same market price. In this way, farmer will continue getting higher prices while the local processors will have an access to the raw cashewnuts until they satisfied.*

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wameendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kupitia Wizara hii, hakika naiunga mkono Tanzania mpya ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri mwenye dhamana na kwa weledi mkubwa, juhudi na jinsi anavyojituma kupitia Wizara hii, hakika ni Waziri mchapakazi. Pia niipongeze sana timu ya Wizara kwa jinsi ya utendaji wao na kuwapatia Watanzania tumaini la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *General Tyre*, naomba ufafanuzi wa kina wa kiwanda cha *General Tyre* kwani maelezo yanayotolewa ama maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa ndani ya Bunge hili na maelezo ya hotuba ya leo yanakinzana. Maelezo kuhusu Kiwanda cha *General Tyre* kwenye Hotuba za bajeti kwa miaka 2015/2016 na 2016/2017 ni tofauti (kila mwaka yanaletwa maelezo mengine mapya. Naomba ufafanuzi wa kina, maelezo gani ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa mtoa hoja anifafanulie wakati anahitimisha hoja yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Tate Olenasha, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, dakika 10.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mapema kabisa kuanza kuiunga mkono hoja iliyopo mezani ili nisije nikasahau. Vilevile nitumie nafasi hii kutoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa hotuba nzuri, lakini vile vile kwa jitihada kubwa ambayo ameonesha katika kutupeleka katika nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeyote yule anayebeza jitihada za Mheshimiwa Waziri na Timu yake, najua atafanya hadharani lakini nina hakika kimoyo moyo anampongeza. Kwa sababu haiwezekani kwamba ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu tu tayari tunashuhudia uanzishwaji wa viwanda zaidi ya 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia, wameibua masuala yanayogusa kilimo ambayo ningependa kuyatolea ufafanuzi kwa muda mfupi nilionao. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusiana na biashara ya chakula na bidhaa zinazotokana na kilimo katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki, wakiashiria kwamba wangetaka na sisi tufuate kinachofanyika kwenye nchi nyingine kuagiza chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na changamoto ya chakula tuliyopata katika mwaka uliopita, lakini ukifananisha na picha tuliyonayo katika ukanda wetu wa Afrika Mashiriki, nchi yetu imeendelea kuwa na hali nzuri ya chakula kuliko nchi yoyote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua baadhi tu ya bidhaa za chakula tutaona picha kuhusiana na hali halisi ya bei kwa sasa. Tukichukua zao la mahindi, bei ya wastani

Uganda tunavyozungumza leo ni Sh. 96,000/=, wakati Kenya ni Sh.114,000/=; Rwanda ni Sh.88,000/=, Juba au Sudani ya Kusini ni Sh.135,000/=, Burundi ni Sh.152,000/= wakati kwetu bei ya wastani kwa leo ni Sh.95,000/=. Kwa hiyo, unaweza ukaona tumekaaje katika mizania ya kikanda ikija suala la bei ya mahindi. Hata zile nchi nyingine ambazo zinaelekea zina bei nzuri kama Rwanda ni kwa sababu wao wameagiza kutoka Brazil. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tukiangalia zao la mchele au basi chakula cha mchele, tunaona kwamba bei ya wastani Uganda kwa leo ni Sh.203,000/=, Kenya ni Sh.267,000/=, Rwanda ni Sh. 204,000/= lakini Burundi ni Sh.236,000/= na kwetu bei ya wastani wa mchele kwa leo ni Sh.174,000/=. Unaweza ukaona kwamba bado sisi tukiangalia kikanda tuko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile imezungumzwa sana kuhusu sukari. Ukiangalia bei ya sukari katika Nchi za Afrika Mashariki, utagundua kwamba nchi yetu bado tuko katika hali nzuri ukifananisha na nchi za jirani. Bei ya wastani Burundi kwa leo ni kati ya Sh.3,700/= mpaka Sh.4,000/=; Uganda kati ya Sh.3,500 mpaka Sh.4,000/=; Kenya ni kati ya Sh.3,500/= mpaka Sh.5,000/=. Kwa hiyo, ukiangalia sisi Tanzania tuko katika hali nzuri bei ya sukari ni kati ya Sh.2,500/= mpaka Sh.3,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi nilipata wasaa wa kuongea na Ma-*DC* wa Wilaya za mpakani za Kakongo, Misenyi, Ngorongoro, Rombo na Tarime, kujaribu kuangalia hali ya chakula na kimsingi wote wanasema kwamba sisi kama nchi bado tuna hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanataka na sisi tuagize chakula kutoka nje, wangeshauriwa vizuri zaidi kuhusiana na athari ambazo nchi yetu ingeweza kupata kwa kufanya kama hivyo. Kimsingi Kenya na Rwanda wao wameagiza chakula kutoka nje kwa

sababu wao wana changamoto kubwa ya chakula, hali yao ya chakula siyo nzuri; wakati sisi mwaka uliopita tulikuwa na ziada ya tani milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tathmini ambayo tumeifanya karibu mikoa yote inatuonesha kwamba mwaka huu inaelekea kwamba tutapata chakula kingi zaidi. Sisi hatuna haja ya kuagiza. Kenya wameagiza chakula kutoka *Mexico* kwa sababu hali yao ni mbaya, lakini kawaida wao wanategemea Tanzania na Uganda katika kupata chakula.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Sospeter Muhongo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie hoja iliyoko mezani. Kimsingi hoja hii ni ajenda ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tunapojadili hoja hii, tunapaswa kuwa Watanzania ili tuunge mkono jitihada anazofanya Mheshimiwa Rais, kiu ambayo Watanzania wamekuwa nayo kwa siku nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala huu tunaojadili, ukiangalia haraka haraka, unaweza tu ukaingalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini ukaacha kuangalia uamuzi wa makusudi ambao Serikali imeufanya kwa nia

njema ya kutekeleza Sera yake ya Tanzania ya Viwanda. Ni bahati mbaya sana Watanzania tulio wengi huwa tunapenda matokeo ya haraka haraka kama ya kamari vile, kwamba unacheza halafu unapata matokeo; kama umepatia, umepatia; kama umekosea, umekosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo tunalolizungumzia leo, siyo jambo linaloota kama uyoga, ni jambo ambalo linahitaji utengenezaji wa vitu vingi sana ndiyo matokeo yake uweze kuyaona. Kwa mfano, leo hii tunavyoongea, tangu muda mwingi sana Serikali iliondoka kwenye sera ya kujenga viwanda, lakini leo tunapoongea kwenye Awamu ya Tano, Serikali imeweka mkono wake kwenye kujenga viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa na ni utekelezaji wa vitendo wa dira ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa Kampeni, wakati wa kuzindua Bunge, lakini pia na kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine mnasema Waziri anahamasisha, anahamasisha, lakini Serikali ilisema itajenga viwanda; mimi niwakumbushe, Serikali imetafuta dirisha ambalo itaweka mkono wake wa kujengea viwanda. Hivi leo tunavyoongea, Taasisi ama Mashirika ambayo yako chini ya Serikali kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwa Dira ya Mheshimiwa Rais, yamebadili mwelekeo ambao yalikuwa yakifanya kwa muda mrefu ambao haijafanyiwa tathmini na ikaingia kwenye utekelezaji wa ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea, *PPF* walishaingia mkataba na Magereza wa kufufua kiwanda cha viatu kule Karanga na mwelekeo na maelekezo tuliyoyapata na ambayo tumekubaliana kama Wizara, wateja wa kwanza tutakuwa watumishi wenyewe wanaopatikana kwenye vyombo vyetu vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na tutakwenda na kwenye Taasisi nyingine ambazo wanahitaji viatu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa tathmini ya haraka ni kwamba soko la bidhaa hizo zitakuwepo na hivyo itawezesha kiwanda kuwa endelevu. Maana yake lilikuwepo swali lingine kwamba ni namna gani mtahakikisha kwamba viwanda mnavyovijenga havitakufa? Kwa hiyo, moja ya sifa, utakuwepo upatikanaji wa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumeongelea hiki alichotoka kukielezea Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu mambo ya sukari. Ni kweli sukari bei yake imepanda ukilinganisha na miaka kadhaa iliyopita. Hata hivyo, Tanzania siyo kisiwa; panapokuwepo na bei za juu sana kwenye nchi zinazotuzunguka, ni kanuni za kiuchumi kwamba lazima na sisi tutaathirika na bei zitapanda. Ukiangalia kwa mfano, Uganda kwa bei ya Kitanzania sukari inakaribia Sh.5,000/=, ukienda Kenya inacheza kwenye Sh.4,300/= hadi Sh.5,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kama tuna sukari kwetu huku na wao bei yao iko juu namna hiyo, ni lazima itaathiri bei kwa sababu watu watatorosha. Hatua za muda mfupi na za muda mrefu tunazochukua, kwanza tunakataza utoroshaji wa sukari na nimeelekeza taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuchukua hatua kwa wale wote watakaofanya zoezi la kutorosha sukari na kusababisha upungufu na kusababisha madhara ya bei katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaishia kuchukua hatua za mpito hizo za kuzuia za kuweka doria, Mheshimiwa Rais ameelekeza na dira hiyo inafuatwa na Wizara zinazohusika ikiwepo kinara Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kazi, Wizara ya Mambo ya Ndani; hivi tunavyoongea, ndani ya wiki chache utekelezaji kwa maana ya kupata mtengenezaji wa kiwanda katika Gereza la Mbigili utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za awali sasa hivi za utengenezaji wa mradi huo zilishatekelezwa na kiwanda hicho kitaweza kuzalisha sukari kati ya tani 30,000 mpaka 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelekezo ya Mheshimiwa Rais, haijaishia hapo; kutakuwepo na mradi mkubwa wa Mkulazi ambao tuliuweka kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais na kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha na kwenye Hotuba ya Waziri mwenye dhamana ya Viwanda, katika vipindi vyote ambavyo amekuwa akisemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili unaona kwamba litaenda kutuondolea kabisa upungufu uliokuwa unajitokeza katika eneo hilo na liko katika hatua za mwisho za kwenda kwenye utekelezaji. Maandalizi ya eneo katika utekelezaji huo uko katika hatua za juu kama ambavyo atabainisha Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ambayo ni tathmini ya jumla ya ajenda ya viwanda, wengine walikuwa wanasema kwamba mwekezaji atawekezaje wakati vivutio tumeviondoa?

Waheshimiwa Wabunge, siyo siku nyingi sana kwenye mijadala yetu, ukichukua *Hansard* za Bunge lililopita, mijadala yetu ilikuwa inajikita kwamba vivutio tunavyovitoa siyo vyenyewe. Kwa kuwa tulikuwa tunasema vivutio tunavyovitoa siyo vyenyewe, sababu tulizokuwa tunatoa ni kwamba baadhi ya nchi bado zinatuzidi kwenye wawekezaji ilikuwa ni aina ya vivutio. Sasa Mheshimiwa Rais amelenga kwenye vivutio vyenyewe ambavyo vinatumika Kimataifa, vinavyoondoa vikwazo kwenye uwekezaji na kuleta sifa halisi ya mwekezaji kuweza kuvutiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vitu ambavyo vinavutia kwa kiwango kikubwa na Serikali imechukua hatua kubwa, Mawaziri wenye Sekta watasema kwa kirefu, mojawapo ni kasi kubwa inayofanyika kwenye umeme. Mojawapo ni kasi kubwa inayofanyika kwenye barabara; mojawapo ni kasi kubwa ya ujenzi inayofanyika kwenye reli na nyingine ni vita kubwa inayopiganwa ambayo Mheshimiwa Rais ameiishi kwenye maneno na kwenye vitendo ya mambo ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye nchi nyingine utasifia kwamba wamefanikisha mradi kwa haraka, lakini utakuta wametumia vibaya fedha za walipa kodi wa nchi zao. Sisi tunaenda katika utaratibu ambao tunapata mradi ukiwa umejumlishwa na matumizi bora ya fedha za walipa kodi. Kwa mwekezaji yeyote asiye mbabaishaji, atapenda sifa hizo kwamba pana umeme, pana amani, pana muunganiko wa kusafirisha bidhaa, lakini pia pana matumizi bora ya fedha za walipa kodi katika nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vyote lazima vitaongeza ufanisi, vivutio vingine ambavyo tulikuwa tunavisema vya rejareja vinatumiwa zaidi na wawekezaji wababaishaji, lakini katika nchi zao ambako na nchi ambako tunatumia kama mifano walikowekeza vivutio vikubwa ambavyo ni *standard* katika uwekezaji, huwa ni vya aina hiyo na ndivyo ambavyo mwekezaji asiye mbabaishaji angependa avikute katika Taifa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa dira yake hii na kwenye historia za nchi yetu Marais hukumbukwa watakapokuwa wameshaweka alama. Kwa hiyo, hizi kelele nyingi, miezi mitatu tu baada ya kumaliza awamu zake mbili, watakuwa wakiona mwekezaji mbabaishaji amepewa fursa, wanasema enzi za Mheshimiwa Magufuli hili lisingetokea. Watakuwa wakiona rushwa imetokea mahali wanasema enzi ya Magufuli hili lisingetokea hili, watakuwa wakiona viwanda vinaanza kufa, ama ndege zilizokuwa tano zinaanza kurudi kuwa nne, watasema enzi ya Magufuli hili lisingetokea. Sasa kwa sababu Tanzania itaendelea kuwa chini ya CCM, tuna hakika haya anayoyafanya Mheshimiwa Magufuli yanatengeneza viwanja kwa ajili ya nchi yetu kuweza ku-*take off.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania wote wafunge mikanda, tuiandae nchi yetu, kwa dira ya Mheshimiwa Rais ili tuweze kuiona Tanzania ya viwanda na hiyo ndiyo itakayotengeneza ajira nyingi na sisi tutakuwa

wauzaji wa bidhaa na sio waagizaji wa bidhaa kama ambavyo kwa kipindi kirefu tumeishi katika mazingira hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya pacha wangu na huku nikimshukuru kwa kuwekeza kwenye Gereza la Karanga ambako ukiondoa viatu vyako na vya Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi humu Bungeni mimi ndio nimependeza zaidi viatu vilivyotoka Gereza la Karanga, vimetengenezwa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, dakika kumi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, huwezi ukatenganisha viwanda na umeme. Umeme, tuna siku mbili; wiki ijayo, Alhamisi na Ijumaa, tunzeni maswali yenu yote, hebu leo tushughulikie viwanda tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje. Kama unalipenda Taifa lako, ni lazima utapiga marufuku makaa ya mawe na *gypsum* yaani *jasi* isitoke nje. Twende kwa takwimu; ni kwamba tulikuwa na mtaalam mmoja tu, bahati mbaya amefariki Dkt. Semkiwa, alifanya *Ph.D* yake *University* ya Colon Ujerumani, Profesa wake alikuwa wa kutoka Australia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa wakati huo miaka ya 1990 wamepiga mahesabu kwamba tuna mashapo *deposit* ya bilioni tano ya 'B', ya baba. Miaka mitatu nyuma alivyoendelea na utafiti akasema, tunaweza tukafika bilioni kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unayesema turuhusu makaa kutoka nje, nawe tupatie takwimu za kuonesha

kwamba hatuna makaa ya kutosha, lakini bila takwimu, msimamo wa Serikali ni kwamba bado tutazuia makaa yasitoke nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi, Ngaka walikuwa wanayumbayumba, wanazalisha tani 80,000 kwa siku; Magamba wanazalisha tani 1,000 kwa siku; Kabulo ambayo ni ya *STAMICO* wameanza tarehe 30 mwezi wa Nne sasa hivi wana tani 500. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu ana kiwanda cha saruji anakudanganya kwamba makaa hayapo, mwambie aje Wizarani kwangu aende Ngaka, aende Magamba, aende Kabulo, makaa ya mawe tunayo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa Lindi na Mtwara wamelalamika kwamba hakuna viwanda huko. Sehemu pekee kwenye Taifa hili kwa miaka kumi au ishirini inayokuja ambayo itaendelea kwa kasi, nasi wote tutahamia huko, ni Lindi na Mtwara. Mikoa mingine itabaki ni Mikoa ya kizamani; ya pamba, korosho, na dhahabu, mikoa ya kizamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Lindi hakuna uwekezaji mkubwa ambao umeshafanyika wa kihistoria kama ambao utafanyika Lindi wa *LNG;* ni bilioni, bilioni, bilioni tena ya 'B'; bilioni 30 ambayo ilikuwa inazidiwa na reli ya *TAZAMA* ikafuata bomba hili, inalofuata ni pale Likong'o Lindi. Utasemaje kwamba Lindi imesahaulika ina uwekezaji wa bilioni 30. Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua viwanda vikubwa vikubwa, hivyo vidogo namwachia Mheshimiwa Mwijage ndio anaviweza mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kiwanda cha Mbolea kitajengwa Lindi tena mmoja nadhani sikuwepo, alitoa kauli mpaka Balozi wa Ujerumani amenipigia simu jana anasikitika sana, sijui alipata wapi taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaeleze, tuna viwanda viwili vitajengwa; cha mbolea cha Kilwa kitajengwa na Kampuni ya Ferrostaal**.** Hizi ni kampuni za Kimataifa na kile cha Mtwara kitajengwa na kampuni ya Helium nayo ni ya Ujerumani. Hayo ni makampuni ya Kimataifa, eeh! Sikiliza sasa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, hii ya Kilwa Ferrostaal Balozi huyu aliyemaliza muda wake kabla hajaondoka tunataka kwenda kuzindua *groundbreaking ceremony.* Siyo kuweka nini; ile tunaenda kabla ya tarehe 1 Julai, uwekezaji wake ni bilioni 1.92. Bilioni 'B'! Utasemaje kwamba Lindi na Mtwara imesahaulika? Itazalisha mbolea *Urea* tani 2,200 kwa siku; *Ammonium* tani 3,850 kwa siku ya *Urea*. Utasemaje Mbeya wamesahaulika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa Mtwara, nitamwachia ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage aongee ya *cement* ya Dangote, lakini kuna kiwanda kingine cha mbolea cha *Helium*, haya ni makampuni makubwa! Nenda u-*search* u-*google* mwenyewe utayaona. Ni uwekezaji wa bilioni ya 'B' siyo milioni 1.26 na itazalisha tani 3,700 kwa siku. Utasemaje Lindi na Mtwara imesahaulika? Lindi na Mtwara ndiyo Mikoa mipya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme nimesema tuonane wiki ijayo. Nakuja suala la Liganga. Bado nina dakika tano! Niongeze *speed* eeh!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni wakati tunafanya utafiti, hatukujua namna ya kutenganisha *iron, titanium* na *vanadium. Ph.D* alifanya Profesa Mahinda, mimi nilikuwa bado mwanafunzi Dar es Salaam Chuo Kikuu, tulikuwa tunapigania chuma tu, lakini dunia sasa imebadilika, hii chuma haina thamani kubwa kuliko *titanium* na *vanadium.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu mwekezaji kazi moja kubwa anayoifanya ni ya kutenganisha *iron from titanium, from vanadium.* Hiyo inataka muda, inataka vivutio; na hivi vivutio vinataka sheria zije humu zibadilishwe. Huwezi

ukaweka vivutio kwa ajili ya Liganga na Mchuchuma peke yake, kwa hiyo, inamaanisha tupitie vivutio vyote; hata vivutio vilivyopo vya *TIC* uwekezaji wa umeme unahesabika sio *strategic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu tukubali kwamba hatujachelewa na hii itafanyiwa kazi. Kingine ambacho ni muhimu ilikuwa ni mchuchuma, yaani kwenye makaa ya mawe. Wenyewe wakati wanatengeneza mradi, tulikuwa na matatizo ya umeme wakataka wauze senti 13 kwa *unit* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mahesabu yao yote ya kuchimba chuma na makaa kuzalisha umeme, yalijikita kwenye senti 13. Kwa kuwa tuna umeme mwingi, huo sasa hivi tunauita umeme wa bei mbaya. Kwa hiyo, inabidi waje kwenye *model* ya senti saba au nane kwa *unit.* Hiyo *model* nayo inataka muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msiseme kwamba vitu havifanyiki. Ameshafanya *experiments* kubwa sana za kujaribu kutenganisha *iron, titanium, vanadium*, lazima aje na *model* wa senti saba mpaka nane wa kuzalisha umeme wa Liganga. Kwa hiyo, Waheshimiwa ni kwamba kazi zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaoneshe, wenyewe tunataka kuzalisha tani milioni moja; vile vile tunabadilisha mawazo. Mawazo yalikuwa kuzalisha chuma kusafirisha nje ya nchi, lakini sisi ni kama wachezaji, ni kama tunachezea njugu. Wapo wasafirishaji wakubwa. Kwa hiyo, lazima tubadili *concept* hiyo. Kwa mfano, Australia mwaka 2016 chuma iliyozalishwa duniani, ilikuwa tani bilioni 3.4. Imewatosha?

**MBUNGE FULANI:** Inatosha!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Haya ahsante. Jamani hili la Liganga Mchuchuma, mwache, ni mambo ya kitaalam, linaenda vizuri. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Muhongo, ulikuwa unataja hapo hizo bilioni. Ni dola au ni hela za Kitanzania? Zote tu ulizotaja hayo mabilioni ni hela za Tanzania ama ni dola?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kuwaeleza, miradi yangu yote huku ni dola. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, leo naona tumepewa changamoto. Ameanza na sisi Waziri wa Afya asubuhi ametupa misamiati mikali hapa, tumemalizia na Waziri wa Nishati na Madini. Nadhani inabidi tukatafute *google* iko wapi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, mtoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote nguvu na afya njema ili kuweza kujadili hii bajeti yetu kwa siku mbili. Hii ndiyo bajeti inayobeba Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wenye dhima ya kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Nawashukuru sana Wabunge wote mlivyojadili bajeti hii, napenda niseme mmeitendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa; yeye na Kamati yake kwa jinsi walivyoichambua bajeti yangu na kwa jinsi walivyosimamia Wizara yangu, mpaka kutupelekea kuandika hii bajeti ambayo kila anayeisikia, anaomba nakala halisi pamoja na kwamba iko kwenye mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nimshukuru kipekee Waziri kivuli wangu, Mheshimwa Antony Komu kwa hotuba yake ya kufikirisha ambayo inakufanya ufikirie miaka mingi mbele, uende maili nyingi. Waziri Kivuli nakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na ushauri mzuri, uliotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, Wizara na taasisi zilizoko chini yake imepokea pongezi nyingi kwa kuweza kutekeleza masuala ambayo wananchi wamekuwa wakiyatarajia. Hakika pongezi hizo zinatupa hali ya moyo ya kujibidiisha zaidi katika kubuni, kupanga na kuboresha mbinu za utendaji ili Taifa na Watanzania kwa ujumla wanufaike zaidi na matunda ya fursa zilizomo. Nami nawaahidi kuwa tutaendelea kujibidiisha na wala hatutawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Waliochangia kwa kuongea moja kwa moja ni Waheshimiwa Wabunge 44; waliochangia kwa njia ya maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 48; waliochangia Wizara hii kwa kina katika bajeti za Mawaziri wenzangu waliotangulia ni Waheshimiwa Wabunge 10, ujumla wake watu 101 wameiunda upya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijitahidi kujaribu kuweka sawa kwa mujibu baadhi ya hoja, lakini ni kweli wataalam wangu wote wako hapa, wamejiandaa watatengeneza majibu ya kina; na kama nilivyosema, mtazamo wetu katika kujenga uchumi wa viwanda mmeujenga upya. Kwa maneno rahisi, mmeuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na swali la kwanza, *the misconception, what is not,* mawasiliano ya kati na ndani ya Serikali siyo mazuri; *the misconception,* siyo kweli. Mawasiliano ndani ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni mazuri. Sina muda wa kuzungumza zaidi, nitawapa vielelezo. Serikali hufanya kazi kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Taarifa ya Wizara yangu ambayo nimemwandikia Waziri wa Fedha baada ya yeye kunitaka kwa maandishi kwamba ni vivutio gani unavitaka ili wawekezaji wako waweze kuwekeza unavyotaka, iko

hapa. Akaenda zaidi, ni kodi gani ziongezwe au zishushwe ili mambo yaende vizuri? Ndiyo hayo! Kwa hiyo, mawasiliano ni mazuri na Serikali inafanya kwa makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watu wasipate wasiwasi kwamba nchi hii inaingia vitani, hapana! Tunafanya kazi vizuri na nakumbuka, bahati mbaya simu zangu nimezifungia, mawasiliano ya mwisho alinipigia akiwa Marekani kwamba hakikisha andiko hili linapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimempa maelekezo Katibu Mkuu wangu anayeshughulikia biashara na uwekezaji, anayeshiriki kwenye chombo cha Kitaifa kinachopitia bajeti kabla ya kwenda kwa Mheshimiwa Waziri kwamba yale niliyoyapendekeza mimi msiongeze wala kupunguza chochote. Kama mnakataa, andika mmekataa, kusudi siku ya siku waje waone tunavyoshirikiana. Serikali hii ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, nimeelezea hivyo, lakini nitatoa mifano mingine zaidi. Tunawasiliana!

Waheshimiwa Wabunge, zimekuwepo hoja na mmesema ukweli kwamba kasi ya kujenga uchumi wa viwanda inakwenda taratibu. Napenda nikiri na nitambue mchango wenu, lakini nyie sio wa kwanza. Kuna wakati mimi na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikuwa hatuangaliani machoni; nikawauliza Wasaidizi wake, vipi? Wanasema, haoni viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Samia kuna wakati aliniiita nyumbani kwake, akasema Mwijage nataka viwanda vya madawa! Bahati nzuri Mheshimiwa Ummy amekwenda kutafuta viwanda hivyo, hayupo hapa. Tajiri huyo ndio alikuwa hataki kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitambue mchango wa Mheshimiwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Kijazi, nikamwambia mzee nifanyaje? Akasema kama hawakuelewi andika! Nikaandika kitabu hiki kinaitwa *strategy*

*for fast tracking in industrialization in Tanzania.* Yote mliyoyasema yako humu. Wakakipeleka kwa tajiri. Tajiri namba moja; wewe unalinda duka tu, tajiri ni mmoja tu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijuaje kwamba Mheshimiwa Rais ameona kitabu hiki? Tulipowaita wawekezaji, Mheshimiwa Rais alitamka kwamba wakati wa kuwekeza ni sasa na atakayetaka vivutio, aje aniambie. Nikajua ugonjwa umepata dawa. Nimewasiliana, Serikali inawasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni vielelezo viwili kwamba *the Government is coordinated;* na kitabu hiki siyo changu tena, kimeshapelekwa kwenye Kamati ya Wabunge wote na kinakwenda kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, Serikali inawasiliana. Naweza kutoa ushuhuda, Mheshimiwa Mpina alizungumza nini, tulibishana nini kuhusu hii; na vile vikwazo vyote na *gear* zote za kwenda kasi, zimezungumzwa humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa Sekta Binafsi na Serikali. Viongozi wa Sekta Binafsi wako pale; *Tanzania Private Sector Foundation, CEO* wao Dkt. Simbeye yuko pale. Jana mliona uwanja wote ulijaa suti za bei mbaya! Hao ni wawekezaji hao! Walikuwepo hata wale akinamama wa *VICOBA*, wote ni wawekezaji. Tungekuwa na mahusiano mabaya wasingekuja. Kwa hiyo, mawasiliano yetu ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu tukiwa Bungeni, mimi na Mheshimiwa Mpango tuliitisha mkutano wa wawekezaji wote, mliona; uwanja wa ndege wa Dodoma ulionekana mdogo, ulijaa ndege! Wawekezaji wa Madini walikuwepo; wa umeme walikuwepo, tukakutana, tukajadiliana; na tukawekeana maazimio. Tumekubaliana kila miezi mitatu tuitishe mkutano mkubwa. Sekta Binafsi na Serikali tunafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngazi ya Kitaifa, Baraza la Biashara la Taifa ambalo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa

Rais, tumekutana juzi. Wale mnaotumia mitandao, ndiyo ile *clip* ya Millard Ayo inayozungumza, ikichukua yale maneno matatu aliyoyasema Mheshimiwa Rais, wakati wa kuwekeza ni sasa. Atakayekukwamisha njoo uniambie. Ukitaka vivutio, nitakupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Mheshimiwa Rais anasema ukitaka vivutio nitakupa, wewe unaogopa nini kumfuata? Si anaonekana! Amekwambia ukitaka vivutio atakupa. Nenda kamwambie sasa akupe, si yupo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu ni viwanda vilivyobinafsishwa. Mheshimiwa Devotha, wewe bado ni rafiki yangu. Usidhani urafiki wangu ulikufa kwa sababu ulifanya hivyo, hapana, bado ni rafiki yangu. Tatizo la Morogoro halipo tena. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mnitendee haki. Msome kitabu changu, kina majibu ya kila kitu. *Moro Canvas* karibu mambo yake yatakwisha. Kutoa kiwanda kwenye *ownership* moja kwenda *ownership* nyingine kuna mambo ya kimikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie nimetumia nguvu zangu zote na muda wangu wote, mimi nina maslahi. Nimekwambia Mheshimiwa Devotha urafiki wangu na wewe hautakufa. Nilikasirika kipindi, sasa hasira zimekwisha, eeh! Kuna wakati alibadilisha mwelekeo wetu na mimi nikakasirika, sasa nimetulia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *MOPROCO* inaanza mwezi wa Sita. Matatizo ya *MOPROCO* yamekwisha na nimeshaeleza kwenye kitabu changu kwamba pamoja na ku-*crush* mbegu ita-*crush* hata mashudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *MOPROCO* inaanza, haina tatizo na Moro *Canvas* inaanza. Hivi vingine viwanda vya *Ceramic,* siyo tatizo, tutavishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye viwanda vilivyobinafsishwa, nimeandika kwenye mambo nitakayoyafanya kwamba mfumo wa sasa wa kushughulikia

viwanda vilivyobinafsishwa utabadilishwa. Lazima tumhusishe Mkuu wa Mkoa, tuhusishe Wizara ya Kisekta, tumhusishe kikamilifu *Attorney General* na lazima tuihusishe Wizara yangu kama anavyosema bosi wangu wa zamani, jeshi la mtu mmoja. Kwa hiyo, viwanda vilivyobinafsishwa ndiyo hatma yake.

Mheshimiwa Japhary rafiki yangu, Mheshimiwa Rais amekuja juzi anasema viwanda vya Moshi vifanye kazi. Kama Mheshimiwa Rais anasema, mimi nitapingaje? Juzi mtu mmoja amenipigia simu, anataka Kiwanda cha Viberiti. Kwa nini Kiwanda cha Viberiti kilikufa? Mlikuwa mnaagiza viberiti kutoka Pakistan vya bei rahisi wakati vya hapa mnaviacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza Waziri wa Mambo ya Ndani, atanisaidia kuhakikisha *smuggled items* haziingii nchini. Mheshimiwa Mwigulu nami itabidi niende lindo. Ni hilo naweza kuwaeleza kwenye viwanda vilivyobinafsishwa. Azma ya Serikali ndiyo hiyo, tunaongeza nguvu, kazi ya *Treasury Registrer,* Wizara za Kisekta, twende pamoja. Mama, viwanda vya Korosho ni *chapter* inajisimamia yenyewe; tutazalisha na ile kitu ambayo ukiiona unasema *astaghfiru Allah. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nne; mazingira ya kufanya biashara. Mazingira ya kufanya biashara naomba nilizungumze hili na Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, unajua mtu akitusikiliza, lakini hiki ni kikao cha wakubwa, ndiyo maana hata mitandao mingine hairuhusiwi kusikiliza. Kwa hiyo, wakubwa mnaponyukana huko chumbani, mnanyukana mtu wa nje asisikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akitusikiliza atadhani Tanzania hapafai kuwekeza, hapana! Ni kwa sababu tunakopataka siyo hapa. Kwa hiyo, muumini mkubwa wa mazingira mazuri ya kuwekeza ni mimi namba moja. Nikipata muda nitawasimulia. Niliwahi kupoteza kazi yangu nzuri kwa sababu ya mazingira mabovu ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *report* ya dunia ya mwaka 2017, wepesi wa kufanya shughuli, Tanzania tuna nafasi ya 132, tulipoanza tulikuwa 139 katika nchi 190. Mzazi yeyote akipeleka mwanaye shule, hawezi kufurahi kwamba mwanawe awe wa 132; lakini siyo sababu ya kupiga kelele au ya kulalamika kana kwamba kuna mtu kafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie sababu moja inayofanya Tanzania kuwa ni sehemu ambayo siyo nzuri ya kuwekeza. Wale wanaotupima, wanaangalia wepesi wa watu kulipa kodi na ule mfumo wa kodi. Sasa watu wengi wanaojadili wanaangalia upande ule unaolipisha kodi, wanaangalia madhaifu ya *TRA,* lakini hawaangalii wepesi wa mtu kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine zilizoendelea ambazo ziko *better ranked,* namba moja, namba kumi, mtu anadai risiti, anasema lazima unipe risiti, unioneshe kodi. Hapa, unamwambia andika kwamba hii bidhaa ya shilingi milioni moja, niandikie laki moja halafu, basi, basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wepesi wa kulipa kodi ni kigezo. Kwa hiyo kama ningekuwa mhubiri kama ambavyo mdogo wangu Bashe anaamini ningewaambia tujitazame, tuwe wepesi wa kulipa kodi na tuwaambie wapiga kura na ndugu zetu tuwe walipa kodi wazuri kusudi wawekezaji waje. Mwekezaji makini hawezi kuwekeza katika nchi ambako mmoja analipa kodi, mwingine halipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu pale Mnyampala anasema, mbona makampuni yamekufa? Mbona biashara inakufa? Mbona maduka yanafungwa? Inaitwa *paradigm shift.* Kama ulizoea kuleta bidhaa yako hulipi kodi, sasa utaratibu ni kulipa kodi, uta-*collapse.* Kama ulikuwa unalipa chumba Kariakoo kwa kodi ambayo ni kubwa kuliko London, haiwezekani chumba Kariakoo kikazidi London, huo unaitwa uchumi bandia. Sasa ni uchumi halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hao wataondoka. Sasa tutahesabu shilingi kwa ya pili, tutajenga uchumi imara na mfanyabiashara atakayelipa kodi ataweza kustawi. Huo ni upande wa pili wa sisi walipa kodi. Upande mwingine ambao walio wengi na mimi nikiwa Mbunge tunausemea ni upungufu wa *TRA.* Nawaahidi, mimi ni sehemu ya Serikali, tutaishughulikia. *TRA* ina upungufu, tutaiboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma taarifa ya Wizara yangu aliyosimamia Profesa Mkenda, wepesi wa kufanya shughuli Tanzania, walipotu-*rank* Wazungu na sisi tukaji-*rank;* unajua mtu akikwambia wewe ni *handsome boy,* kajiangalie kwenye kioo, kweli wewe ni *handsome* au anakudanganya? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wazungu walipotufanyia *ranking,* nasi tukajifanyia *ranking* wenyewe. Tukatengeneza zoezi la wepesi wa kufanya biashara. Katika kitabu hiki alichokiongoza Profesa Mkenda, kimehusisha Watendaji wa Wizara zote za Serikali, wote wamehusishwa. Kwa hiyo, *NEMC* kama anakosea, tunasema anakosea; *TBS* ana makosa, ana makosa; *TFDA,* ana makosa, ana makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu hiki shangazi, kodi 25 za Kagera zimeandikwa. Rafiki yangu Gimbi anasema umefanya nini nyumbani? Nimepigana kodi 25 zitoke, ngoja aje Tizeba kesho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kitabu hiki kinaeleza kwamba kila Waziri aliyepewa mamlaka, yale mambo ambayo kutokana na *regulations* anaweza kuyabadilisha, ayabadilishe. Ndivyo inavyosema. Kwa hiyo, kero zote tutaziondoa moja baada ya nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nashukuru mmepaza sauti. Mlitupa jukwaa kama lilivyo, tumeshughulikia. Tuliyoyaona ndiyo hayo, *fast tracking of industrialization* lakini vikwazo viko hapa, tumemaliza. Kilichobaki ni utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *point* tatu hizi katika 25 nitakazozisema, Waheshimiwa Wabunge kwa *point* tatu nawaomba mjiandae kwa heshima na taadhima na bashasha na nderemo kunipitishia Bajeti yangu niende kuitekeleza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Viwanda. Hapana, kwanza niwaeleze viwanda ni nini? Halafu nije niwaeleze Sera ya Viwanda. Mheshimiwa Nape na Waheshimiwa Wabunge wengine wametaka kujua tafsiri ya viwanda. Shughuli yoyote, viwanda vina tafsiri mbili; ile tafsiri inayohusisha mambo ya *construction,* uzalishaji wa gesi kwamba ni viwanda, mimi siitumiii. Naitumia ile ya *manufacturing,* ya kuongeza thamani ya kuchukua mawese yakatoa mafuta, mbegu za alizeti kutoa mafuta, *cotton* kutoa suti nzuri kama niliyovaa leo hii. Hivyo ndiyo viwanda unavyovihesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ngoja niwaeleze, kiwanda kidogo sana ni kiwanda kinachoajiri mtu mmoja mpaka wanne; na kiwe na thamani isiyozidi shilingi milioni tano. Kiwanda kidogo sana! Watu wanakwenda zaidi, wanasema ukiwa na vyerehani vinne ni kiwanda kidogo. Najua kuna Mbunge mmoja hapa alianza na vyerehani vinne, leo ana vyerehani 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Katani, amekuwa mkweli. Amesimama akawaambia, Mwijage alinielekeza nimekwenda, nimeona nimetekeleza. Waheshimiwa Wabunge, tuambizane. Kama kuna kasungura, umwambie na mwenzako.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ninayemsema Mheshimiwa Mbunge, alianza na vyerehani vinne, leo ana vyerehani 30 na cherehani kimoja ni shilingi milioni tatu, *ninety million,* anaajiri watu wa kutosha. Kiwanda kidogo kinaajiri watu watano mpaka 49 na kina thamani ya milioni tano mpaka 200. Hivyo ndivyo sisi Wabunge tunavimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha kati kinaajiri watu 50 mpaka 99. Shilingi milioni 200 mpaka shililngi milioni 800 na hivi Wabunge tunavimudu. Ndiyo vile viwanda vya akina Mheshimiwa *Captain* Rweikiza vya kutengeneza nyanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye viwanda vikubwa, vinaajiri watu 100 na vinatumia shilingi milioni 800 na kuendelea, ndiyo viwanda vya akina Mheshimiwa Salum, vya Jambo, ndiyo viwanda vya akina La Cairo, vimo humu. Kwa hiyo, hivyo ndivyo viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaeleze Sera ya viwanda ambayo nilizungumza mimi na Mheshimiwa Mama Lulida, shangazi yangu. Ni shangazi yangu kweli, tumetoka mbali shangazi Lulida na wengine waliochangia. Sasa niwaeleze, sifa ya Sera kama walivyosema Wabunge na nimshukuru mtangulizi wangu Mheshimiwa Mama Mary Nagu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera yoyote ina sifa moja kubwa, lazima iishi muda mrefu, lakini na nyie mmechangia, kwamba sera mbona zinabadilika? Kumbe mlisahau, mnataka sera inayoishi muda mrefu, sasa ya 1996 mpaka 2020 huu ni muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa sera hii kuliko yote, inazungumza mambo mawili ambayo mmeyasema. Inasema viwanda visambae Tanzania yote. Nani hataki viwanda visambae Tanzania yote? Kama imepitwa na wakati, kwa hiyo, tuibadilishe viwanda vikae sehemu moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inasema kwamba mikoa ya pembezoni ipewe vivutio; kwamba pamoja na vivutio kwa wawekezaji wote, lakini mikoa ya pembezoni ipewe *more incentives.* Kuna ubaya gani? Huwezi kwenda kuwekeza Kigoma bila kupewa *incentives* za ziada! Ni mbali sana! Uipiganie ndugu yangu Wamugabwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo hiyo Sera ya Viwanda ya Mwaka 1996 mpaka 2020. Kutokana na Sera hii, tumetengeneza mkakati wa *integrated* au fungamanisho la maendeleo ya viwanda, kutokana na Sera hii tumetengeneza *vision* ya 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka wakati huo mimi nilikuwa *officer,* Mwenyekiti wangu wa Bodi Profesa Mwandosya akiwa yeye anashiriki kwenye timu iliyotengeneza *vision* ya 2025, tumetoka mbali. Nilikuwa nabeba mkoba, sera hii inatengenezwa. Sasa ni mimi, Mr. mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msambao wa viwanda. Viwanda vina namna mbili. Sera inasema viwanda visambae; wawekezaji wanapokuja, Serikali au Waziri uwezo wangu wa ushawishi kiwanda kiende wapi ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanaokuja siyo mbumbumbu, wawekezaji wanaijua Tanzania kuliko tunavyoijua sisi. Akija Mjerumani anajua madini yako wapi. Labda wamwondoe Profesa Muhongo mtaalam wa miamba, lakini mwingine anakuja anakuonesha dhahabu ziko hapa. Ndiyo maana kila mara wanakuja wanajidai kwenda kuangalia makaburi ya babu zao. Wanaangalia yake mambo waliyoyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, viwanda viko vya namna mbili, *FDI,* nina *influence* kidogo ya kueleza ziende wapi. Kuna *LGI (Local Grown Industries),* ndipo tunapokwenda kwamba unaanza na kiwanda kidogo sana, unakilea kinakwenda kuwa kiwanda kidogo, kinakuwa kiwanda cha kati na kiwanda kikubwa. Mdogo wangu Mheshimiwa Kitandula, ni mdogo wangu kabisa, tumefanya kazi wote, nimemlea, nimemfundisha kazi, tumefanya kazi wote. Pole sana na *Tanga Fresh.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Kitandula angeniambia kwamba barua yake iliyokwenda Hazina hawakushughulikia ningeshakwenda mimi. Naomba anikumbushe nitakwenda Hazina huyo aliyekata aniandikie mimi, *I am a Minister,* kwa nini alinyamaza? Mimi nilisema mtu huyu hana hatia afunguliwe, yeye akakaa na barua akanyamaza. Angeniambia ningemwambia Mzee Mpango, huyu ni mtu wa Mungu anaelewa. Unajua Mheshimiwa Mpango watu hawamwelewi, unamtegea wakati anatoka kusali unamwambia shida yako, atakusainia tu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, viwanda vidogo sana, vidogo na vikubwa ndivyo viwanda tutakavyokwenda navyo ila watu wanavidharau kwa neno la viwanda vidogo. Waheshimiwa kiwanda cha shilingi milioni 200 kinazaa sana. Angekuwepo Mheshimiwa Katani angewaeleza mchanganuo na namshukuru sana Mheshimiwa Katani hata usiku nimemuota. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Katani, amenikumbusha Profesa Aba Mpesha, Baba Mchungaji wa kutoka Michigan University aliyenifundisha biashara ndogo na viwanda vidogo, aliyefanya utafiti wa korosho, watu wa korosho, wanasiasa wa Mtwara ndiyo waliomwekea mtimanyongo. Kama mnamtaka naweza nikampigia simu akatoka Michigan akaja, lakini kama mmejirekebisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaeleze, wawekezaji wanakuja kule kwenye Mikoa na Halmashauri mnawawekea mtimanyongo kama ile kesi yangu ya Tabora. Mwekezaji ametoka China yupo uwanja wa ndege watu wakapiga figisu, wakamwambia umekuja Tanzania hupaswi kwenda Tabora, Tabora siyo Tanzania, yule Mchina akashangaa akarudi kwao. Inabidi niwaambie kusudi mwelewe tunayoyapata. Nichukue nafasi hii kumwombea kijana wangu Mheshimiwa Heche apone vizuri aje afanye kazi, tunafanana sura lakini ana pilikapilika nyingi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie suala la Heche limekwisha, wale wawekezaji watakuja, mkitaka taratibu nitasimamia mimi wawekeze Tarime. Yale yamekwisha na nikitoka hapa nakwenda Dar es Salaam nikazungumze naye, mwambie afanye kazi moja mambo yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niwaeleze Wabunge kuwapata wawekezaji ni shida, msiwaseme neno baya na Tanzania si nchi peke yake ya kuwekeza. Mimi napoteza wawekezaji wanakwenda Zimbabwe, Mozambique, Ethiopia, Rwanda na baya zaidi wanakwenda kuzalisha Rwanda kusudi sisi tugeuke soko, msiniumize.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaeleza *FDI* na *LGI*, *LGI* ndiyo inaweza kusambaa nchi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Tawala za Mikoa, tutafanya nini? Nimewaahidi kwenye hotuba yangu tunamalizia mwongozo, Wakuu wa Mikoa tutawapa mwongozo. Hii imetokana na nini? Baadhi ya Wabunge wananilaumu kwamba mimi napendelea mikoa fulani na mingine naiacha, tarehe 28 nakwenda Tanga. Niwaeleze Wabunge wa Tabora, Mheshimiwa Mwanry ameshafanya *booking* kwamba nikapige kongamano kule. Mjiandae Waheshimiwa wa Tabora, tupige kongamano na nimemweleza Mheshimiwa Maige rafiki zake wa Geneva awaambie na wenyewe waje watuletee viwanda twende Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naleta mwongozo kwa sababu imekuwepo kutolingana kati ya mkoa na mkoa. Ukifungua *Facebook* ni Simiyu, *WhatsApp* ni Simiyu, sasa tunataka kuwaambia Wakuu wa Mikoa wote waingie kwenye *Facebook* na *Instragram* na mitandao yote.

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeee. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Ndiyo, wawekezaji wanatafutwa, kwa hiyo, nitatoa

mwongozo wa kuweza kutekeleza hilo. Kwa hiyo, mwitikio wa mikoa haulingani lakini haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutaandika mwongozo, nitauweka dibaji mimi, ataweka dibaji Mheshimiwa Simbachawene na Mkuu yeyote ataweka dibaji twende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya ujenzi wa viwanda, nimeilezea *fast tracking.* Jukumu la ujenzi wa viwanda linatafsiriwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda seti kubwa na ujenzi wa viwanda vya *subset.* Sekta binafsi ndiyo itajenga viwanda, Serikali inaweka mazingira wezeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaeleza katika kipindi ambacho Mheshimiwa Rais yupo madarakani, viwanda vya sekta binafsi kwa *address* humu yaani mpaka wenye viwanda nimewawekea simu zao, wamejenga viwanda kwa mtaji wa shilingi trilioni tano, una mashaka wapigie simu, lakini nimeweka picha na *beacon* za mahali walipo unaweza kwenda *ku-trace*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda niwaambie mimi siyo saizi ya kuzalisha viwanda vya shilingi trilioni tano kwa mwaka mmoja, *I want more*, ndiyo maana nikaleta *fast tracking,* ndiyo maana nikazungumzia kuweka mazingira bora ya biashara. Kwa hiyo, nashukuru na nyie hamridhiki sio saizi yetu tunapaswa kukimbia. Hatupaswi kuwa soko la watu wengine, tunapaswa kuzalisha tuwauzie watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa viwanda. Niwashukuru Waheshimiwa wote waliozungumzia kuhusu ulinzi wa viwanda. Sitaki kurudi nyuma, nimeshampongeza Kivuli changu, unajua ukiona Kivuli kina mashaka hata na mtu mwenyewe ana mashaka, sasa Kivuli changu ni kizuri siwezi kusema zaidi, lakini Nunua Tanzania inaendelea. Mwaka jana ilipigiwa sana kampeni na Mheshimiwa Makamu wa Rais alipozindua 620GS1 lakini tulipokwenda kutoa *award* za *Brand* 50 mshindi akawa *Alaska Rice*, huyo mama *Alaska Rice* ni mke wa Mheshimiwa Bashungwa, Mbunge mwenzetu, anatengeneza *branded product* zinapendwa Dar es Salaam

*Supermarket* zote. Hata pilipili, watu wanaokwenda kununua wanasema nataka ile pilipili ya Alaska, *branded* na Mheshimiwa Mbunge. Jamani Wabunge muwe mnaambizana tunaishi vipi siyo tunakuona unaendesha mtambo mkubwa hutuambii, tuambizane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ulinzi wa viwanda tunauzungumzia. Ulinzi wa viwanda upo chini ya *TBS*, *Fair Competition* na upo chini ya Polisi. Niwahakikishie taasisi zilizopo chini yangu zitafanya kazi sasa kuliko wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimehakikishiwa niseme ninachopewa na mimi nimekwenda kuwaambia wakubwa, bidhaa feki inapita, nimezungumza wakaniambia sema unachotaka nimewaambia, kwa hiyo, tutafanya kazi. Niwaeleze wawekezaji wengi kwa mfano kwenye sukari walikuwa wanakataa kwa sababu ya sukari inayokuwa *smuggled in,* kwa sababu ya mchele ulikuwa *smuggled in,* sasa watu wana *confidence* baada ya ku-*control.* Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mwigulu tu-*control* zaidi bado, bado, bado. Kwa hiyo, vitu vya feki na *quality* tutalizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie fungamanisho la viwanda na sekta nyingine. Waheshimiwa Wabunge kuna fungamanisho kuliko maelezo. Ukisoma mkakati wa pamba mpaka mavazi ni fungamanisho. Ndiyo maana Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwigulu huwa ananiita pacha. Ni kwamba mimi ndiye niliyebuni mradi wa viatu wa Karanga lakini mwenye dhamana ni Waziri wa Mambo ya Ndani. Nilijua tukitengeneza viatu Magereza vitasambazwa katika majeshi yote na yule mzalishaji anapata soko la kuanzia, kuna fungamanisho hapo. Soma mkakati wa pamba mpaka mavazi kuna fungamanisho, soma mkakati wa alizeti kuna fungamanisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maziwa, soma Ripoti ya *SAGCOT* inazungumzia mradi wa maziwa. Nikiri kwa masikitiko kwamba hatufanyi vizuri kwenye maziwa, lakini

mambo ya *Tanga Fresh* tutayashughulikia na viwanda vingine vianze. Niwaeleze jambo moja, *ASAS* ana kiwanda chenye uwezo wa kuchakata lita 50,000 kwa siku lakini maziwa anayopata ni lita 12,500. Kwa hiyo, kuna haja ya kuweza kuwasaidia watu wa Nyanda za Juu Kusini kuweza kuzalisha maziwa zaidi na chini ya hapo atakuja aeleze Waziri wa Kilimo ndiyo tunakuja na mpango wa *SAGCOT* wa kuleta *IFAD* kutoka Ulaya kusudi waende kule. Sitaki kusoma hotuba ya mwenzangu ngoja aje aseme mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kipaumbele, nitafika baba ikibidi nitaomba muda. Ipo hoja ameuliza Mheshimiwa Mbunge, jina lake nimelisahau kidogo ila ame-*declare interest* kwamba yeye ni mwana Tanga na mimi Tanga nakwenda tarehe 28, kwa hiyo, huenda tutakutana huko. Nakwenda kupiga, mnaita *sound*, kuhamasisha viwanda, anasema tuwe na kipaumbele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Saruji cha Simba, kimeongeza uwezo kwa tani 750,000, ndiyo alichokizungumza Mwenyekiti wa Kamati yangu kwamba ile nafuu waliopaswa kupewa haijatoka. Mwenyekiti wa Kamati na wewe ni sehemu ya Serikali waambie watu wa Tanga walete karatasi zao tutakwenda Hazina wanieleze mimi kwa nini hawatoi. Kama mtu amewekeza na tani zinaonekana kwa nini msimpe? Halafu unajua watu sijui kwa nini, mkikwama huko mje kwangu, mimi ndiyo Waziri mwenye dhamana nitawapeleka huko mnakoshindwa kufika. Wanasema huwezi kwenda kwa Baba mpaka upite kwa Mwana, Mwana ni mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukisoma mkakati wa fungamanisho la viwanda, Mheshimiwa Mbunge aliyesema hatuna kipaumbele, kwenye mkakati wa fungamanisho la viwanda imeelezwa na hicho kiwanda kingine cha Tanga kitazalisha tani milioni saba, kitawaajiri watu milioni nane na 60% ya saruji itauzwa nje ya nchi, sisi tutabaki na 40%. Kinawekwa jiwe la msingi, kwa sababu sina mamlaka ya kutamka kinawekwa jiwe la msingi mwaka huu, kitapata vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa aliyesema kwamba hatuna vipaumbele asome mkakati wa fungamanisho la viwanda liko kwenye *website* yangu. Tutaweka kwenye viwanda vya sukari, Mkulazi tani 2000, Mbigiri 30,000, tutapanua Kagera Sugar na Kilombero. Juzi mbele ya Mheshimiwa Rais nimemueleza Mheshimiwa Zuma kwamba aisaidie Ilovo iongeze *Kilombero One* na *Kilombero Two* waache kutonunua miwa ya wananchi, kwa hiyo tumeyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hilo kuna pamba, mafuta ya kula ya alizeti, ngozi na bidhaa za ngozi na matunda. Kwa matunda ndiyo tunazungumza na Kiwanda cha Matunda cha Sayona. Nimewasikia Ndugu zangu wa Tanga, tunazungumzia Kiwanda cha *Eveline* lakini tunazungumzia Kiwanda cha Matunda cha Handeni, kwa hiyo, tunaendelea na imeainishwa. Tunazungumzia maziwa, tunaweza kuwa hatujatekeleza kama alivyosema Mheshimiwa Kitandula lakini ndiyo dhamira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumziwa viwanda vya nyama, watu wa Manyara mwambie yule mwana mama aliyekuwa na matatizo ya kiwanda chake cha nyama, matatizo yake yameainishwa kwenye Ripoti ya Profesa Mkenda. Wale waliokuwa wanamkwamisha, sitaki kuwasema wasijisikie vibaya wakashindwa kula, dawa yao imeshapatikana aje tumpeleke wampe nyaraka zake. Unamkwamisha mtu na kikaratasi asitengeneze kiwanda cha nyama, ng'ombe wanakwenda Kenya wanarudi, ningependa tuwe wawazi tuambizane. Hicho ni kiwanda cha *Chobo Investment* kipo Mwanza, anachinja ng'ombe 600 kwa siku, kijana amejaribu. Matatizo yako yote watayasema kesho kwenye Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya chakula na katika hili niwaeleze, nimekuwa nikisema hapa Bungeni, nikiwaambia Waheshimiwa Wabunge hakuna sababu ya kutoa mahindi Katavi kuyapeleka Dar es Salaam, msage mahindi kule, mfanye *packaging* vizuri, muweke kwenye maroli mpeleke sokoni. Ndiyo maana nachukua fursa

hii kumpongeza Mheshimiwa Aeshi ametengeneza kiwanda kikubwa sana cha kusaga nafaka na zitakuja sokoni. Waheshimiwa tuambizane, kama umewekeza mwambie mwenzako wewe umepata wapi namna, tuelezane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na rafiki yangu mmoja Kenya nilipotaka kuingia kwenye siasa nikamuaga aliniuliza Mwijage utaziweza siasa. Nikamwambia nitaziweza, *I can talk*. Akaniambia *politics is not about talking.* Akaniambia ninyi Watanzania mna tatizo moja. Akaniuliza adui yenu ni nani? Nikamwambia umaskini. Akaniambia mbona mnaogopa utajiri? Ukikutana na mwanasiasa wa Tanzania ukimwambia wewe tajiri anasema mimi maskini bwana, hapana! Mheshimiwa Aeshi amejenga kiwanda cha mfano cha kutengeneza nafaka, tunataka hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema sembe nzuri inalimwa Ileje. Mheshimiwa Mbunge wa Ileje, jasiria, *SIDO* wanakuja weka kiwanda Ileje, mjini tunataka watu waondoke warudi shamba, zile *by-product,* mmetoa mfano mzuri wa pumba zibaki kule. Akinamama wapepete mahindi, wafanye *packing*, wakaangalie watoto wakimaliza pumba wawape mifugo, nazungumzia mifugo ng'ombe sizungumzii *astaghfiru Allah*. Unajua kuna wengine pumba wanamlisha *astaghfiru Allah,* hapana. Wamlishe ng'ombe akamuliwe maziwa, akikamuliwa maziwa mama auze na mtoto anywe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maamuzi ya Serikali ni kwamba ziliko rasilimali ndiko vitajengwa viwanda. Ndiyo maana Mheshimiwa wa Simiyu, maamuzi yamefanyika kiwanda cha vifaa tiba vitokanavyo na pamba nimeandika kwenye ripoti kitajengwa Simiyu kitatumia pamba tani milioni 50 na kitatuokoa na aibu ya kuagiza vifaa pamba toka nje. Tuna aibu nyingi na tutazimaliza. Tunaagiza hata *drip* ile ya kumwekea mgonjwa kutoka Uganda, hizo aibu zote tunazifuta. Soma ripoti hiyo, mimi aibu zote nimezianika kusudi mnione halafu mnipange vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema yote haya ili Waheshimiwa Wabunge wasiwe na tatizo la kuangalia vifungu ila wakubaliane tupitishe moja kwa moja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ni *petrol chemicals*. *Petrol chemicals* ni vile viwanda vya Mheshimiwa Muhongo. Kiwanda cha *Ferrostaal* Mheshimiwa Muhongo amekwenda zaidi mpaka ametaja tarehe ya kwenda Kilwa na mimi nimeshapata mwaliko kutoka Ujerumani, Profesa nitakuwa karibu na wewe. Unajua watu siku hizi wananichanganya na mimi wananiita Profesa, kwa hiyo, tutakuwa wote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kiwanda Ferrostaal karibu kitaanza na kiwanda cha *Helium* kitaanza, kwa hiyo ni *petrol chemicals* zimeandikwa. Nawaeleza vipaumbele mvijue kwa sababu uwekezaji katika kiwanda cha mbolea utatuwezesha kuzalisha mbolea tani 2,600,000 katika viwanda viwili wakati mahitaji ya mbolea Tanzania mnatumia tani 400,000. Kwa hiyo, *is a break through* tutatumia mbolea zaidi, tutapata tija na viwanda vitafufuka. Ni kwa uwekezaji wa namna hiyo kuongeza tija *ginneries* zitafufuka, akina Manonga watafufuka pamba ikizalishwa kwa wingi na tukawa na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya uwekezaji, *Kurasini Logistic Centre.* Kama nilivyoeleza kwenye ripoti yangu inatengenezwa. Mheshimiwa Ngwali, *Kurasini Logistic Centre* haiwezi kufika mwezi Julai. Nichukue fursa hii kuwaeleza watendaji ninaofanya kazi nao, mimi huwa nasema wazi, nimeshamwambia Waziri Mkuu kwamba *performance* ya *EPZ* si nzuri kwenye *Kurasini Logistic Centre.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaandikia *memo* Makatibu Wakuu wangu kwamba *I am not happy* na *speed* ya *EPZ on Kurasini*, nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya hapo ni kwenda kwa tajiri. Naitaka *Kurasini Logistic Centre* ianze, namna nilivyokaangwa hapa na rafiki yangu Mheshimiwa Ngwali siwezi kukubali mimi ni mtu mzima. *Kurasini Logistic Centre* tutakuwa na nafasi nzuri kabla

ya Bunge kuwaambia ni kitu gani kinafanyika, ikibidi kuitisha Bodi nitaitisha Bodi. Naitaka *Kurasini Logistic Centre,* mimi ni mtu wa Temeke nani asiyejua bwana, Mbunge wangu yupo hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Bagamoyo Special Economic Zone*, bandari ipo na itachimbwa na mwekezaji. Nimeulizwa kwa nini tumetaka *private sector* ilipe fidia? Mimi wazo hili nimelipeleka kwa wakubwa nikajenga hoja wakanikubalia. Wewe mtu umemthamini mwaka 2008 unamlipa kidogo kidogo huwezi kuona, tena Kamati yangu ndiyo iliniambia kwamba Mwijage itakuhitaji miaka 30 kumaliza, basi nikawaomba wakubwa tutafute *private sector* wameingia lakini malipo yote tutayasimamia sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze nimepata barua sasa hivi, kuna mwekezaji nguli kutoka China ananifuata hapa anataka nimpe eneo la kuweka *Special Economic Zone*. Nimeshawaeleza watu wote tunaofanya kazi pamoja, watu wa *EPZA*, Makatibu Wakuu mnahusika, huyo Mchina hata asiponiona mimi mpelekeni Bagamoyo, mpelekeni Kibaha, ninazo hekari 5,000 Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze watu wa Pwani, Mheshimiwa Subira Mgalu na Wabunge wote sijawahi kuona ukarimu kama wa Pwani. Mkuu wa Mkoa anachosema ndicho anachosema Diwani. Unajua ngoja niseme niokoke na nitakayemsema msimchukulie hatua yoyote. Watu wa Morogoro waliniangusha na nimemwambia Mzee Mbena. Nimemleta mwekezaji toka Singapore amefika pale Madiwani wanatokea huku wanakwenda huku, tumepoteza viwanda vitano kutoka Mauritius juzi vyenye kuweza kuajiri watu 7,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwaambia nina kiwanja Morogoro, wakienda Morogoro wanatokea hapa wanaingia hapa, mara umeme mara nini. Umeme hauwahusu, umeme mniambie mimi, mimi Mzee Muhongo naongea naye wakati wowote, *substation* ni shilingi bilioni tatu, mbele ya kuingiza wawekezaji watano wanaozalisha ajira 7,000 ni kitu gani?

Mheshimiwa Devota nisaidie hilo, acha longolongo na mambo ya *master plan* tunataka eneo lile. Kwa hiyo, Bagamoyo itatekezwa na watu watalipwa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAMCO* Kibaha, tunaendelea kutekeleza. Maeneo ya mikoani, Kigoma na Songea kwenye bajeti nimewaweka. Kwenye bajeti inayokuja naomba mnitendee haki msome vitabu vyangu. Mheshimiwa *Special Economic Zone*, nimesaini kwa mkono wangu *Special Economic* Zone nane za sekta binafsi, kwa hiyo, Serikali inapenda sekta binafsi. Nitambue nafasi ya Waheshimiwa Wabunge walioniahidi kunipa maeneo, Mheshimiwa Bashe taratibu, kama sikuwekeza leo na kesho ipo, wewe niombe nibaki kwenye nafasi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha *SME*, *SIDO*, *TBS* na *TanTrade* wamekuwa wakiwezesha *SME*. Ninachotaka kuwaambia hatutalegeza viwango hasa kwa wale watengenezaji wa chakula, *TFDA* atashirikiana na *TBS* hatutalegeza viwango. Ila katika maelekezo ya Serikali za Mikoa mnapotenga maeneo wale akinamama, watu wamehoji nimesema nini kwa akinamama, akinamama muwajengee mabanda ambayo *TBS* atawapa mafunzo. *TBS* atakupa mafunzo na *certificate* na gharama za *certificate* atalipa yeye mpaka utakapokuwa mjasiriamali mwenye nguvu. Nimetoa maagizo na mamlaka inaniruhusu kufanya hivyo, akinamama niwapende zaidi ya hapo niwapende namna gani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza hisa kwenye makampuni. Jambo ambalo nimekuwa na ushawishi nalo ni Urafiki. Mwekezaji wa Urafiki amekubali kupunguza hisa zake alikuwa na hisa 51. Majadiliano yanaendelea, wanafanya *valuation* na tumeshapata wawekezaji wa Tanzania. Kwa hiyo, hicho ndicho naweza kusema kuhusu Urafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TANALEC,* sina mamlaka nayo ila mimi nawashawishi *TANALEC* waende kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange.* Hata hivyo, katika

kulinda uchumi wa viwanda Mheshimiwa Muhongo alishasema na kwenye tenda zake amesema *transformer* na *cables* zote zote kwenye *REA* Awamu ya Tatu zitanunuliwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, orodha ya viwanda ni kubwa, kuna kiwanda kimejengwa Tanzania cha kutengeneza waya, kina uwezo wa kutengeneza kilometa 100 za waya kwa masaa nane kiko Mwenge. Viko vitatu kimoja kiko Nigeria, kingine kiko Mwenge na kingine kiko South Africa, ni kijana mdogo ukimwona hutaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya makaa ya mawe. Mheshimiwa Profesa Muhongo amezungumza lakini mojawapo ya faida ya kutumia makaa ya mawe ya Tanzania yamechangamsha uchumi. Pale wanapopita wenye malori, mama ntilie anapika lakini spea na *mechanic* wanatengeneza Watanzania. Naomba mtuelewe, tumefanya hivyo kwa nia nje lakini hali hiyo imefanya wenye migodi waone kwamba kuna soko wamefungua migodi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie korosho. Maelezo aliyozungumza *comrade* Mwambe, unajua ukiwa *comrade* hata ukijipaka matope mtu akikuangalia tu michango yako ni ya ki-*comrade* tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, michango yake Mheshimiwa *comrade* na mchango wa Profesa Masawe wa Naliendele tutaufanyia kazi na tutamuunganisha na *COSTECH* kusudi zile bidhaa zinazotokana na korosho tuweze kuzitumia. Suala ni *research* na Profesa Masawe amefanya *research,* kuna bidhaa nyingi, *brake lining* na kile kinywaji ambacho wewe ukikiangalia unasema *astaghfur Allah* lakini kinaingiza pesa. Kwa hiyo, vyote hivyo tutavishughulikia na naomba tuendelee kufanya kazi wote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kipekee kuna faida kwa kuchambua korosho hapa ndani

tunaposhughulikia viwanda vilivyobinafsishwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Kitandula zile *export levy,* mabilioni yale, tutakaa tuwaulize wenye dhamana kama tunaweza kuchukua viwanda vya kuanzia kusudi msimu unaokuja tuweze kuanza na baadhi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *CBE*. Mheshimiwa Mwita ameleta suala la *CBE* akalipitisha kwa Mheshimiwa Ngwali akaona haitoshi akalipitisha kwa Mheshimiwa Mwambe akaona haitoshi, ikanipa shida. Nikaenda kutafuta Ripoti ya *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Waitara ni kwamba waliokwenda kukagua *CAG* hakukagua Dar es Salaam. Nakala niliyo nayo iliyowekwa lakiri na *CAG* anasema yeye *CAG* alikagua Dar es Salaam, lakini kwa mamlaka ya kiutawala, Waziri nikishapata ripoti, siruhusiwi kufanya lolote kwa watendaji napitia kwenye Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waitara najua yeye amesoma sayansi mambo ya utawala hayajui. Ukiingilia moja kwa moja watendaji bila kupitia kwenye Bodi akienda mahakamani anakushinda. Kwa hiyo, mimi nimepata ripoti yangu nitaiandikia Bodi na itachukua *action* isipochukua *action* ndio mimi kwa mamlaka niliyonayo au kwa mamlaka ya uteuzi naweza kuchukua hatua. Nimhakikishie *I have the report* anaweza kuisoma, nimemshikilia kwa sababu imeandikwa siri na yeye siyo mmoja wa siri, sisi ndiyo watu wa siri, kwa hiyo mambo ndiyo hayo *CBE* Dar es Salaam ilikaguliwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *Tanga Fresh…*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Umeshalizungumza.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Nimeshalizungumza, ahsante sana kama mmeridhika. Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru kwa namna ya kipekee Waheshimiwa Wabunge na kupitia kwenu Watanzania wote ambao tunawawakilisha kwa ushirikiano mnaotupa katika kuendeleza sekta yetu na hususan ujenzi wa uchumi wa viwanda. Wizara daima itaendelea kuwa sikivu, kupokea mchango wa mawazo na ushauri katika kuboresha utendaji wa Wizara na sekta kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kuendelea na ushirikiano huo katika kuhakikisha kuwa rasilimali tunazozipata zinatumika kwa umakini mkubwa ili mipango na mikakati ya sekta iweze kuleta matokeo chanya katika kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025. Ni dhahiri kuwa ushiriki wa sekta binafsi na uthubutu wao ni nyenzo muhimu katika kuleta mageuzi na matokeo yenye ushindani utakaotokana na juhudi za uendeshaji na uanzishwaji wa viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu letu tukiwa ndiyo wawakilishi wa wananchi wetu kuwajengea ufahamu wa mipango, sera, mikakati mbalimbali ya kisekta ili kuwaongoza ipasavyo katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono japokuwa nilitaraji kwa makofi yale Bunge zima lingekuwa limesimama. Tutaendelea na taratibu zinazofuata, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA- KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 - Viwanda**

Kif.1001- *Administration and HR Management*..........................Sh.11,838,840,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri na nina orodha ndefu kabisa hapa ya watu wanaotaka kushika shilingi. Tutaanza na Mheshimiwa Deo Sanga, huyu anatoka CCM.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali lakini masikitiko yangu ni kwamba, yale niliyochangia jana yaani hapa nilipo hata machozi yanataka kutoka, kweli kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali kwa fidia niliyosema jana ya wananchi wa Makambako ambao wameteseka kwa muda mrefu zaidi ya miaka 16 hawajalipwa fidia yao. Kama nilivyosema kwamba kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017, waliwekwa kulipwa hizi fedha ambazo muda unakwisha Juni ambayo ni kesho kutwa tu. Kwenye bajeti hii ambayo tunaipitisha leo hapa ya mwaka 2017/2018 hawajawekwa. Kwa hiyo, naomba kauli ya Serikali ni namna gani watalipwa fidia kama nilivyosema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilisema jana pia tunaomba tupate kauli ya Liganga na Mchuchuma ni kitu gani kimekwamisha kwa mwekezaji huyu ambaye tayari yuko pale na fedha za kulipa fidia zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo kupata kauli ya Serikali naomba mniunge mkono nashika shilingi. Naomba kauli ya Serikali, Waziri wa Fedha yuko hapa, nimesema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu kuhusu mshahara wa Waziri, Kanuni ya 101(3) ili tusipate tabu kipindi hiki nitawasomea kwa haraka inasema hivi:-

*"Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri, ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahususi la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja". (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwenye mshahara wa Waziri kwanza ni jambo moja lakini pia liwe la sera. Sasa Mheshimiwa Sanga hapa amezungumzia mambo mawili la kwanza halikuwa la sera, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri endelea na suala la pili.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alikuwa amesimama.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** *It's okay.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Sanga hakuwepo labda wakati nilikuwa naelezea suala la Liganga. Jamani kwanza hapa kuna suala la teknolojia ilivyobadilika. Mara ya kwanza sisi Watanzania tulitaka chuma kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi,

tukawa tunang'ang'ania *iron.* Sasa ukichukua madini yale ni kwamba kuna *iron* ndani yake kuna *titanium* halafu kuna *vanadium*, hivi vitu vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *model* wakati sisi tunaanza tulikuwa hatujui kwamba *vanadium* na *titanium* itakuwa na faida kubwa sana duniani. *Titanium* sasa hivi ukienda kwenye mambo ya ndege ndiyo ipo, *vanadium* vilevile ndiyo inatengeneza hata dawa za *blood pressure* hata mambo ya moyo. Hii *titanium* yenyewe ni nyepesi lakini ni ngumu kuzidi hata chuma. Kwa hiyo, huyu mwekezaji muda mwingi aliouchukua ni namna ya kuja kutenganisha, hizi ni *melting point* yaani atenganishe *titanium*, *vanadium* na *iron*, hilo ni la kwanza linachukua muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lilikuwa ni kwamba, kwa sababu miradi iliungaishwa pamoja na makaa ya mawe yeye akawa na *model* kwamba atatumia yale makaa ya mawe kwa ajili ya *smelting,* vilevile atauza umeme. Kwa hiyo, kwenye mahesabu yake ilikuwa atengeneze fedha kutokana na umeme aje kuweka kwenye mgodi. Sasa ndiyo maana tukamwambia, wakati huo hesabu zake alizozileta zilikuwa *US sent* 13 kwa *unit* lakini duniani tunajua umeme wa makaa ya mawe ni kati ya senti sita mpaka nane, kwa hiyo, inabidi arudi kwenye hiyo *model.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine alikuwa anataka kuzalisha megawati 600, 300 atumie na 300 aweke kwenye *grid*. Kwa hiyo, tunachokisema inabidi vilevile tu-*revisit,* turudie vile vivutio tulivyompatia lakini vile vivutio tulivyompatia ni lazima tuje hapa Bungeni tubadilishe sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa. Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri bado nakusudia kushika shilingi kwa sababu katika maelezo yake hajaeleza sasa namna ambavyo wale walivyokuwa tayari kulipa fidia na fidia nazo wamesimamisha kwa sababu ya kufanya utafiti

huo ambao ameelezea Waziri? Kwa sababu wale wananchi walikuwa tayari wanasubiri kulipwa fidia ambayo mwekezaji alikuwa tayari kuilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naendelea kushika shilingi naomba wenzangu mniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga hoja iliyoko hapa Mezani sasa hivi ni ile ya Mchuchuma na Liganga kwa sababu hiyo ya fidia haikuwa ya kisera. Sasa kama unashika shilingi utoe maelezo sekunde thelathini kuhusu hoja ya Liganga na Mchuchuma kwamba ndiyo unashika shilingi baada ya maelezo ya Profesa. Hiyo hoja nyingine haipo mezani sasa hivi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni lugha tu jambo ni lile lile. Ni namna gani Mchuchuma itaanza, naomba kauli ya Serikali hapa ndiyo maana nimeomba wenzangu mniunge mkono, naendelea kushika shilingi.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja haijaungwa mkono.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imeungwa mkono.

**MWENYEKITI:** Inaungwa mkono na idadi ya Wabunge kadhaa, sasa hapa mlisimama sijui mko wangapi, naona ndiyo mnaanza kuota kidogo. Kama mnataka kuunga mkono hoja mnasimama wote, kwa sababu huwezi kuwa unasimama mmoja, mwingine na mwingine. Sawa, hoja imeungwa mkono, naomba wale ambao hawahitaji kuchangia wakae ili tuone akina nani wataweza kuchangia.

Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Profesa Muhongo na Naibu Waziri wa Fedha. Tunaanza na Mheshimiwa Deo Ngalawa.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii na naunga mkono hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga ni mkataba ambao tayari ulishaingiwa kati ya Serikali ikiwasilishwa na *NDC* pamoja na mbia. Mheshimiwa Waziri amejaribu kuzungumzia suala la utenganifu wa madini ya *titanium* na *vanadium*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naungana na Mheshimiwa Mzee Sanga hapa ni kwamba, sisi tulifuatilia hili suala, tulichoambiwa ni kwamba, *Government Notice* haijatoka, mwekezaji yupo na ana pesa za kutosha ili aweze kuendelea na uwekezaji. Sasa leo tunasikia tena kumbe kuna masuala ya ku-*separate* kati ya chuma na madini mengine. Tunaomba *commitment* ya Serikali, lini watatoa hiyo *Government Notice* ili huu mradi uweze kufanya kazi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sanga kwa sababu mwekezaji ambaye yupo tumemchagua kutokana na uwezo wake wa kutenganisha *titanium* na *vanadium* kutoka kwenye *iron* na ana uwezo huo jamani, ila sasa yale mambo ya *incentive* yamalizike na *iron* ianze kutengenezwa. Hatuwezi

kuwa nchi ya viwanda bila kuwa na chuma na chuma hiki jamani duniani hakipo, kipo karibu na mkaa. Naomba tusipoteze muda na sisi tutarudisha hiyo shilingi kama *commitment* ya Serikali itatoka ya kutoa *Notice.* Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Naomba tu nimwombe Mheshimiwa Deo Sanga, kutokana na maelezo ya kitaalam aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, aachie shilingi. Nimwambie ni azma ya Serikali yetu kuhakikisha kwamba uchumi wa viwanda unakamilika na unasimama ndani ya nchi yetu. Pamoja na mambo ya kitaalam aliyoyasema Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, lakini katika masuala ya kodi Serikali inaendelea kufanya *analysis* kwa umakini wa hali ya juu kuhakikisha suala hili linakaa vizuri kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu katika Sheria ya *VAT,* mwekezaji tunayemsema kwa sasa alitaka aruhusiwe kukusanya na kutumia Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa miaka 15, kisheria hili suala halipo. Ndiyo maana tunasema tupate muda Serikali, tunaendelea kulifanyia kazi, masuala ya kisayansi, masuala ya kisheria za kodi na Serikali yetu ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha suala hili linafika mwisho mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tu kumuomba ndugu yangu, mtani wangu Mheshimiwa Deo Sanga aiachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri tutakapoyakamilisha masuala haya tutaendelea kama nilivyosema mwanzo dhamira ya Serikali yetu ni njema kabisa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudi pale pale. Huwezi ukabadili kitu

kimoja ukawa na *model* uliyokuwanayo kwa miaka 10 ni lazima uibadili, ukibadili kimoja lazima uende na kingine. Kwa mfano, bei ya chuma duniani ilikuwa chini Dola 50 kwa tani, juzi ndiyo imepanda imefika karibu 80. Hata kwenye *uranium* mnaona tumesimamisha leseni kwa sababu bei ya *uranium* iko chini, yule anayewekeza hatapata faida na Serikali haitapata faida, ndiyo maana ya kufanya hivi vitu na *models* siyo kwamba wameshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine na Mheshimiwa mwenyewe anajua ni kwamba, mwanzoni mawazo yetu yalikuwa kusafirisha chuma nje, sasa tumeamua tutatumia kwa sababu huyu mtu hawezi kupambana na *production* ya China ambayo ni *1.38 billion tones per annum,* ana-*produce* Mchina. Wachina hii chuma yote unayoiona, chuma imekuwa nyingi China ndiyo wanaileta huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tubadili *models* kwamba chuma ya Liganga sasa ni yetu sisi kuitumia ndani ya nchi badala ya kufikiria kuisafirisha. Sasa hizo *models* ni lazima twende kwenye vile vivutio na vingine kubadilishwa ni lazima tuje tena Bungeni hapa. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ni kwamba tutakamilisha vivutio na tutawaletea Wabunge wapitishe kusudi mradi uanze. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Serikali yanayoridhisha ambayo yanaonekana yana nia njema na Liganga na Mchuchuma, nami nitakuwa jirani kufuatilia. Kwa maelezo haya, basi narudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo. Anayefuata ni Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya hoja ya

Mheshimiwa Waziri, lakini naomba nipate maelezo ya kina ya namna ya kufungamanisha sekta hii ya viwanda na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo yake amejitahidi kutoa mifano, lakini hata katika hotuba yake sijaona kwa kina maelezo ya ufungamanishaji wa sekta hii ya viwanda na sekta kama vile maji, barabara na miundombinu mingine na nikizingatia vipo viwanda katika maeneo mbalimbali vimefunguliwa, lakini vina changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara, maji pamoja na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutueleza kwa kina na kama sitaridhika na maelezo yake nitatoa shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Subira Mgalu, Mbunge kutoka Mkoa wa Pwani, ambao punde hapa nimewapongeza kwamba ni watu wazuri sana kwenye kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uchumi wa viwanda, niliwahi kuwaona Waandishi wa Habari wanasema Mheshimiwa Magufuli apanga bajeti ya viwanda ya shilingi trilioni 29. Maana yake ni nini? Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kuna kitu kinaitwa viwanda, lakini kuna miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. Miundombinu wezeshi, unapozalisha bidhaa katika kiwanda kuna *cost of production,* unapohamisha bidhaa ama malighafi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kuna gharama zile zinaitwa *transaction cost.* Ili uweze kupata nguvu ya kiushindani sokoni lazima *production cost* iwe ndogo na *transaction cost* iwe ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungamanisho la uchumi wa viwanda ndiyo maana Mheshimiwa Rais anapigana

kutengeneza *standard gauge rail* kusudi mawese ya Kigoma yakija kuchakatwa Dar-es-Salaam yaje kwa gharama ndogo kuliko kuchukua *CPO* kutoka Malaysia. Ndiyo maana tunasema barabara zinazokwenda kwenye malighafi, kwa mfano kiwanda changu cha Mkuranga kinachotengeneza vigae *square meter* 80,000 kwa siku, barabara zote zinazokwenda kwenye vyanzo vya madini yale zote zitatengenezwa na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunazungumza kwamba, iwepo miundombinu wezeshi ya *ICT* kuwezesha mawasiliano kufanyika. Ndilo hilo fungamanisho, ila nililizungumza kwa haraka, unajua unapokuwa pale na ninyi Wabunge mmetulia, nakuwa na wasiwasi. Mheshimiwa Mbunge wala usiende mbali sana fungamanisho lipo, miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo yake naendelea na hoja yangu ya kutoa shilingi ili Mheshimiwa Waziri abaini ukubwa wa tatizo hili. Mimi najielekeza kwenye vile viwanda ambavyo vimeshaanza uzalishaji. Amekitaja kiwanda chetu cha *tiles* cha Mkuranga, naomba nimtaarifu kiwanda kile kimetumia zaidi ya shilingi bilioni 110 lakini kiwanda kimeanza kazi kinatumia malighafi maeneo yale ya Mkuranga, Mkamba, Kimanzichana, Kisarawe lakini barabara haipitiki mpaka sasa imetitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri anaposema ni kweli hiyo mikakati ipo lakini, je, viwanda vilivyoanza kazi, anafahamu kwa mfano, Kiwanda cha Sayona kilichopo katika Kijiji cha Mboga kinatarajia kuanza kazi hakina maji na yeye mwenyewe amekitembelea amekiona? Sasa kwa jitihada za namna hiyo zinafifisha moyo wa wawekezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ilia one ukubwa wa tatizo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ili ijadiliwe na Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, hoja imeungwa mkono. Wale ambao hawatataka kuchangia wakae ili tuone nani anataka kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Zaynabu Vulu, Mheshimiwa Ngonyani, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Tutaanza na Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuunga mkono Mheshimiwa Subira katika hoja yake ya fungamanisho ambayo kwa kweli jambo la namna hii ndiyo maana nilisema tunapiga hatua moja mbele tunarudi hatua mbili nyuma na nikatoa mfano kwenye sekta ya maziwa. Kwa miaka mitano *Tanga Fresh* wanaomba kibali waweze kupanua kiwanda chao lakini tu kwa sababu kuna watu ndani ya Wizara ya Fedha, hususan *TRA,* wanazuia bila sababu za msingi, hivi hii nia ya viwanda kweli tutakwenda kwa mpango huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaynabu Vullu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niseme kwamba, pamoja na nia njema ya kutuletea viwanda ambavyo vitatusaidia kupata bidhaa kwa bei nafuu lakini pia vimesaidia kutoa ajira, hofu iliyokuwepo ya mtoa hoja ni kwamba miundombinu iliyokuwepo ni hatarishi kwa maana ya kwamba zile *raw*

*materials* zinaweza zisifike kwa wakati kwenye viwanda na uzalishaji usiwepo, Serikali ikapata hasara, dhamira ya awamu ya viwanda ikawa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ituambie barabara ambazo zinachukua malighafi, mfano Kiwanda cha *Tiles* ambacho kiko Mkiu, Mkuranga, malighafi zinatoka Wilaya ya Mkuranga na Wilaya ya Kisarawe lakini barabara ni mbovu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Zaynabu Vulu, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii na nimpongeze mtoa hoja kwa kuikumbusha Serikali juu ya miundombinu mibovu iliyopo kule Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumwomba arudishe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwanza yeye kama mjukuu wangu, pamoja na Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, wanapaswa waipongeze Serikali kwa kufanya jitihada za kupeleka viwanda vingi sana Mkoani Pwani katika Awamu hii ya Tano. Hakuna mkoa umepata viwanda vingi vipya katika Awamu ya Nne na hii ya Tano kama Mkoa wa Pwani. Kwa hivyo, hata ule uwezo wetu kama Serikali wa kujenga miundombinu kwa haraka kadri ambavyo viwanda vinaingia kwa wingi, umekuwa mdogo kwa sababu, viwanda ni vingi mno Pwani na vitaendelea kuwa vingi kwa sababu ni karibu na bandari, ni karibu na jiji kubwa la kibiashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, niwaombe sana waipe Serikali muda, wampe Waziri muda afike kwenye maeneo yale aangalie changamoto za kutatua kwa haraka na ndiyo hizo aanze nazo kuliko kutoa shilingi na kumkatisha tamaa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa kumwomba Mheshimiwa aliyeshika shilingi aiachie kwa sababu, Mheshimiwa Mama yangu pale Mheshimiwa Mgalu alishauliza maswali siku za nyuma, tulishayajibu na majibu tuliyoyasema yalionesha *commitment* ya Serikali inaenda wapi. Labda tu mengine ambayo wakati ule sikusema, niyaongezee leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo tumeelekezwa na Serikali, sisi Wizara ya Miundombinu ni kuhakikisha kwamba tuna-*facilitate* uanzishaji wa viwanda nchi nzima. Kwa hiyo, katika *priority* kwa zile fedha wanazotugawia kitu cha kwanza tunachoangalia ni kuondoa madeni, kama ambavyo mara nyingi naongelea wakati najibu maswali mbalimbali, tunaondoa yale madeni ambayo yanamaliza hela zetu kuwalipa watu wakati wamekaa *idle,* ni kwa sababu tu wamecheleweshewa kulipwa. Kwa hiyo, *priority* namba moja ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *priority* namba mbili ni maeneo ya viwanda.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata nafasi hii. Moja kwa moja nianze kumwomba mtoa hoja aondoe shilingi kwa sababu zifuatazo...

**WABUNGE FULANI:** Arejeshe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Arejeshe, arejeshe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arejeshe shilingi kwa sababu zifuatazo. Amezungumzia Kiwanda cha Sayona ambacho kinajengwa pale Chalinze, kwanza hakijaanza kazi lakini pili ni kwamba pale Chalinze tumefanya miradi mitatu,

mmoja ndiyo bado haujakamilika, jumla ya hiyo miradi mitatu ambayo inatoa maji kutoka Mto Wami inakaribia shilingi bilioni 168. Mwaka huu wa fedha Serikali ilitenga shilingi bilioni 915, mpaka sasa hivi tumeshaingia mikataba ya shilingi bilioni 710 kwa ajili ya kuleta huduma ya maji, tukiwa tunatambua kwamba kiwanda bila maji hakiwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu, tayari tumeshaongea na Sayona ambaye ndiyo mwekezaji pale Chalinze, tumefikia makubaliano. Jana nimetoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo kwamba tunamalizia taratibu, mashine zimenunuliwa, kinachopitiwa na wataalam ni masuala ya *specification* tufunge ili Sayona apate maji kazi ianze kufanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo tatizo la Wizara hii, ni lazima Watanzania tukubali tuna udhaifu wa mipango ya maendeleo. Mtu anaamua kwenda sehemu, cha kwanza akishapata ardhi tu anaanza kujenga kiwanda lakini haangalii maji na umeme yako wapi. Kwa hiyo, kusema kweli kumlaumu Waziri wa Viwanda unamwonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hicho kiwanda cha Mkuranga, sisi wenyewe tumefanya kazi mchana na usiku kuwapatia gesi na Mheshimiwa Ulega anajua. Kila siku tukionana nao gesi lakini kabla ya kuweka kiwanda hawakuweza kutuona sisi. Vilevile Dangote wameweka pale kiwanda hawakutuona kutuambia kwamba wanahitaji gesi, tukafanya kazi mchana na usiku. Kwa hiyo, tukubali kwamba, mtindo wetu sio mzuri, mtu akipata ardhi anaanza kujenga nyumba, hajui kwamba ana umeme au maji. Hata hivyo, kwa mambo ya umeme mimi nadhani nisitoe hotuba yangu, tusubiri mpaka Alhamisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na nashukuru nimesikia majibu ya Mawaziri mbalimbali. Nimalizie aliposema Mheshimiwa Muhongo, namheshimu sana, lakini naamini kibali cha ujenzi wa viwanda kinatolewa na Wizara husika na Wizara inapotoa kibali inakuwa imejiridhisha na si suala la mjenzi wa kiwanda kung'amua kwamba sehemu anayojenga kiwanda kuna maji, umeme na kadhalika. Hata hivyo, nimeridhika na majibu ya Mawaziri wengine, nimeona *commitment* zao, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwa kazi yake nzuri. Nataka tu ajue ukubwa wa tatizo kwamba ujenzi wa viwanda uendane na kufanya kazi kwa vizuri kwa kila sekta ili mapato yapatikane. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unarudisha shilingi?

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimerudisha shilingi yake ili aje tena Pwani. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakusudia kushika shilingi kama majibu ya Waziri hayatakuwa yanaridhisha katika eneo ambalo nataka nili-*address*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la nchi hii kila wakati tunalipigia debe viwanda vipya lakini vile vya zamani hatuvilei. Kwa hiyo, inaonekana Wizara hii inapiga *sound* kwa ajili ya viwanda vipya lakini vile vya zamani hawavilei, hawaangalii vina shida gani mwisho wa siku viwanda vingi sana vinafungwa. Sasa hivi kila mkoa unaozunguka viwanda vimefungwa. Sasa tutakuwa kila mwaka tunahubiri vipya na huku vya zamani vinafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe tamko nini wanafanya kuhakikisha kwamba viwanda vilivyopo

vinaendelea kulindwa na kutoa huduma kama ambavyo tunakusudia? Kama sitaridhika na majibu nakusudia kutoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya majukumu yangu ni kulea viwanda. Imeandikwa hivyo kwenye bajeti yangu ya mwaka huu tunaomalizia na nimerudia kuwaelezea kwamba mimi nitalea viwanda na nimekuwa nikivilea acha hivi vipya mjomba mimi siachi chungu cha zamani kukimbilia chungu kipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie katika *speech* yangu nimeelezea nilivyohamasisha *brand* 50 za bidhaa za Tanzania. Ninapokuja kuhamasisha *brand* ya Tanzania ina maana natambua kwamba hawa watu wanafanya kazi na vigezo ninavyopitia kuja kuitambua kwamba hii ni *brand* naangalia anajiri watu wangapi, anahifadhi vipi mazingira, analipa kodi kiasi gani na vitu kama hivyo, hiyo ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninazo taasisi zangu ya *TBS* na yangu *TIRDO* wanakwenda viwandani si kama mapolisi, wanakwenda viwandani ili kwenda kuwafundisha wazalishe bidhaa zenye ubora zinazokidhi masoko ya Tanzania na masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, navilea viwanda kwa namna hiyo na nina imani viwanda vyangu vinaendelea vizuri na ndiyo maana Tanzania mnaweza kuona bidhaa ya Tanzania. Zaidi ya hapo mwaka jana na nitarudia na mwaka huu, niliitisha maonyesho ya viwanda vya Tanzania tu na vilishiriki na yalifanyika maonesho pale Sabasaba na mwaka huu mwezi Novemba, nitaviitisha tena chini ya Kauli Mbiu ya Tanzania sasa tunajenga viwanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda mimi na Mheshimiwa Waziri tunaishi Tanzania tofauti, yeye ana ya kwake na mimi nina ya kwangu. Kwa sababu anaposema analea viwanda viko wapi Viwanda vya *KIBO MATCH, MOPROCO, Sungura Tex*, *Kili Tex*, *Mbeya Tex, Tabora Spinning,* hapa tunazungumzia viwanda vyote nchini ambavyo vilikuwepo tangu enzi za Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza leo Tanzania viwanda tunasahau kwamba wakati wa Mwalimu Nyerere viwanda hivi vilikuwa vimetapakaa mikoa yote hapa nchini. Sasa Mheshimiwa Waziri anaposema analea viwanda ni viwanda vipi anavyovilea na hivi ninavyovitaja vyote vimegeuka kuwa ma-*godown*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na Wabunge wenzangu waniunge mkono tuweze kulijadili jambo hili tusiwe tuna nadi viwanda vipya wakati vya zamani vinakufa. Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Wale ambao hawachangii wakae ili tuanze kuandika wachangiaji. Mheshimiwa Shahari Mngwali, Mheshimiwa Japhary, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaanza na Mheshimiwa Shahari.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niunge mkono hoja ya baba mkwe wangu Mheshimiwa Shangazi kwamba, *we are serious* lakini *we have to be more serious.* Kwa sababu haya mambo ambayo tunaambiwa tu tutafanya, tutatekeleza lakini bila kuwa na mwonekano wa wazi kwamba kweli vinatekelezwa na hapa maelezo kwamba hivi viwanda vilivyokufa vinafavywaje, maelezo yanatolewa kiujumla ambayo hata hivyo yalishatolewa miaka mingi iliyopita wimbo ni ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa sasa wanasema tujiongeze ili tukijadili tujadili. *Failure* ya ile *integrated* bajeti niliyoisema mwaka jana ndiyo hii hapa sasa. Ile hoja ya mwanzo ni hiyo kwamba kila mtu kipande chake halafu tunalazimisha kuungana haviungani. Viwanda vyote ambavyo vimekufa huyo mlezi hatumwoni anavilea vipi na wale watoto waliokufa sijui kama watafufuka hatuelewi. Naomba itoke kauli yenye kuthibitika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono Mheshimiwa Mbunge Shangazi kuhusu mkakati thabiti wa Serikali wa kuhakikisha kwamba viwanda hivi ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa kama havifanyi kazi vinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wakati Mheshimiwa Rais anajinadi pale Moshi alisema apewe siku 37 tangu atakapochaguliwa viwanda vile vyote vya Moshi vitakuwa vimeshafufuka. Mwaka mmoja na nusu sasa hata kiwanda kimoja hakijafufuka na kimojawapo kikiwa kiwanda cha vibiriti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba na kumuunga mkono Mheshimiwa Shangazi ni kupata *commitment* ya Serikali kwamba ni lini sasa hivyo viwanda vitachukuliwa kwa hawa ambao wameshindwa kuviendesha, virudi katika mikono ya watu sahihi wa kuviendesha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niunge mkono hoja na Mheshimiwa Shangazi. Mheshimiwa Mwijage anapozungumza suala la ulezi wa viwanda najiuliza ulezi upi? Juzi juzi tu hapa nilipouliza swali linalohusiana na Kiwanda cha Nyuzi Tabora, akajibu kwamba kila mtu atabeba mzigo wake sijui kama amesahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa na viwanda hivi vinakufa. Juzi juzi aliinuka msemaji mmoja hapa akasema kwamba kile kiwanda bado ni *godown.* Viko wapi viwanda vya kusindika nyama kama cha Shinyanga na vinginevyo. Mimi huu ulezi anaouzungumzia Mheshimiwa Mwijage sioni kama upo. Namuunga mkono Mheshimiwa Shangazi kwa hoja yake ya kushikilia shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami namuunga mkono Mheshimiwa Shangazi kwa sababu licha ya kuanzisha viwanda vipya lakini viwanda vya zamani ni vizuri vifufuke. Kwa mfano Mkoa wa Morogoro ulikuwa ni mkoa wa viwanda lakini kama tulivyochangia jana viwanda vingi vimekufa. Kwa mfano, Kiwanda cha Ngozi, Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha *Ceramic* (cha vyombo), vingi vimekufa. Kwa hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Shangazi tuanzishe viwanda vipya lakini na vile vya zamani viweze kufufuka na kufanya kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Niendelee kurejea azma ya Serikali yetu ni kuchochea uchumi wa viwanda. Hiyo lazima ikae hiyo na hatuwezi kuchochea uchumi wa viwanda bila kulea viwanda vilivyokuwepo na bila kuangalia vile vilivyokuwepo kwa nini vilikufa ili tuje na mkakati sasa wa kuhakikisha viwanda hivyo vinapofufuka kama alivyosema dada yangu Mheshimiwa Riziki kwamba tutakapovifufua visife tena, hiyo ndiyo dhamira ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hili Msajili wa Hazina alifanya tathmini, uhakiki na *research* ili sasa aje kuieleza Serikali ni kwa nini viwanda hivi viliishia njiani. Baada ya kujua ni matatizo gani tulikumbana nayo tuje na mpango na mkakati mzuri wa kuhuisha viwanda vyetu na kuweza kuwa na viwanda endelevu na kuhakikisha kwamba kama

alivyosema Mheshimiwa Rais wetu Tanzania ya Magufuli ni ya viwanda na tuna uhakika ndani ya miaka mitano viwanda vyetu vyote vitakuwa vimeuhishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa William Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi sana Mheshimiwa Shangazi aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri, asimpunguzie kasi andelee kwenda kufanya kazi ambayo ameifanya kwa uzuri sana kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inajaribu kuhimiza uchumi wa viwanda siyo tu kwamba tunahimiza ujenzi wa viwanda vipya lakini vilevile kuangalia vilivyopo lakini ikiwezekana kurudi nyuma na hata kuangalia vile vilivyokufa kama kuna haja au uwezekano wa kuvifufua. Katika kufanya hivyo ni vizuri kuangalia mambo kadhaa, kuna viwanda vingine vimekufa ambavyo ukijaribu kuvifufua inawezekana ukatumia fedha nyingi zaidi na jitihada kuliko ukianzisha kipya. Vilevile kuna vingine *technology* imekuwa *obsolete* huwezi kusema tu nirudi kwenye teknolojia ya zamani kwa sababu mambo sasa yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimfahamishe tu Mheshimiwa Shangazi kwamba kuna jitihada kubwa za Serikali kufufua baadhi ya viwanda, nitavitaja tu baadhi kwa mfano Kiwanda cha *Triple S* (Shinyanga), Kiwanda cha *General Tyre* (Arusha), Kiwanda cha Nyama (Mbeya), Kiwanda cha Chai (Bumbuli) na viwanda vingine. Kwa hiyo, jitihada zipo lakini lazima tuangalie mazingira ya kila kiwanda kabla ya kusema tu tunafufua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Shangazi arudishe shilingi na kwamba Mheshimiwa Waziri amepokea *concern* ya kufufua viwanda nikielewa kwamba hicho ndicho alichomanisha. Kwenye swali lake alikuwa anaongelea kulea na akataja viwanda vilivyokufa, Waziri halei makaburi ya viwanda ambavyo vimekufa ila analea viwanda ambavyo vipo na ulezi wake anaoufanya utaona katika sera alizotoa Waziri wa Fedha akishirikiana na Waziri wa Viwanda wanafanya *control ya damping* ya bidhaa kutoka maeneo mengine ambapo huwa zinachangia kuua viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mmeona vitabu ambavyo ametuonesha ambapo wengine tumeshavisoma ambavyo ameelezea mikakati ambayo italea vile viwanda vya ndani. Pia mmeona jitihada kama Naibu Waziri wa Kilimo kama ambavyo ameelezea viwanda ambavyo vimefufuliwa. Kufufua kama alivyoelezea Naibu Waziri wa Kilimo si tu jambo la kwenda kufufua kama unainua uzio kwa sababu lazima uangalie kitu gani kilichokuwa kinafanyika, ni kitu gani kilichosababisha kifeli na je, mabadiliko ya teknolojia yanaendana na kufufua vyuma vilivyokuwepo, lakini mpango nzima unakuwa wa kuwa na viwanda vinavyoendana na *raw material* ambazo zipo na ambazo zitaweza kupata soko na ushindani wa bidhaa zinazotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Shangazi aridhie mpango mkakati wa Serikali kwa ujumla wake ambao Wizara inayoongoza kutoa mpango wa viwanda imeshatoa, Wizara ya Fedha imeshatoa lakini na Wizara zingine za Kisekta tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda kama ambavyo mnaona tunawekeza kwenye Kiwanda cha Viatu kule Moshi pamoja na Kiwanda cha Sukari Mbigili ambavyo miaka iliyopita vilishakufa. Kwa hiyo, hizo ndiyo jitihada ambazo Wizara inafanya na ndiyo dira ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwenye Serikali ya viwanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mengi lakini bado hayajajibu yale ambayo nilikuwa nakusudia. Teknolojia inapobadilika siyo kwamba inakuja kuondoa uhitaji wa kitu, hapo tunachozungumzia, kwa mfano zamani tulikuwa na kiwanda kama Zana za Kilimo Mbeya, je, sasa hivi hatuhitaji majembe, mabeleshi na mikokoteni, ni vitu ambavyo bado vinahitajika. Kwa hiyo, kama teknolojia imebadilika ni kuviboresha tu lakini siyo kwamba uhitaji haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nimwonee tu huruma nimrudishie shilingi yake lakini bado eneo hili linahitaji usimamizi makini ili yale malengo ya Mwalimu Nyerere aliyoyapanga kutawanya rasilimali za Taifa nchi nzima yaweze kuendana na Taifa letu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 104, naongeza nusu saa. Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba maelezo ya Serikali kuhusiana na marufuku aliyotoa Waziri Mkuu kwenye vifungashio vya pombe aina ya viroba na kama maelezo hayatakuwa ya kuridhisha basi nitatoa shilingi ya Waziri na nitaomba Bunge liniunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ieleweke wazi kabisa kwamba na mimi ni mmoja wa watu ambao siungi mkono matumizi ya ile pombe ambayo ilikuwa inafungashwa kwenye viroba. Ninachosema ni kwamba baada ya marufuku hii Serikali ilitoa maelekezo kwamba wale wenye *stock* ya pombe ile katika vifungashio hivyo vilivyopigwa marufuku ifanyiwe *stock taking* na Polisi walifanya hivyo, *TRA* na *TFDA* walikwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, Serikali ilisema itatoa maelekezo ili vikafanyiwe *repacking* lakini leo ni zaidi ya miezi miwili tokea jambo hilo lifanyike na kama

jana nilivyosema limewagharimu watu sana kwa sababu wana ma-*godown* wanayalipia, wanapaswa kufanya marejesho katika benki, wako wengine wenye mtaji unaozidi shilingi milioni 300 na kadhalika. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali au maelezo ya Serikali juu ya jambo hili ambalo kwa kweli liko kila mahali katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa unyenyekevu kujibu hoja ya Waziri Kivuli wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Masikitiko yangu ni kwamba tulikuwa hatujawasiliana mimi na yeye lakini wazalishaji wote ambao wote kimsingi, ningejua ningekuja na barua wanakubaliana na maamuzi ya Serikali ya kuzuia vifungasho vya namna hiyo, wote kwa barua na ninazo na bahati mbaya hiyo sikuijua wameshapewa maelekezo ya hatua za kufanya. Mojawapo ya hatua za kufanya ni ku-*pack* bidhaa hiyo kwenye chupa maalum ambazo zitaondoa vishawishi na ile *easy portability.* Tumewasiliana na *Megatrade* ya Arusha na *TBL* namna ya ku- *handle* bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii na ndiyo *commitment* ya Serikali, yeyote ambaye bidhaa yake itakuwa ilizuiliwa, iko kwenye ma-*godown* mikoani aende Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira aonane na Katibu Mkuu, Profesa Kamuzora ili ampe maekelezo namna ya kutoa bidhaa kutoka *point* moja kwenda *point* ya pili na kuhakikishia zile bidhaa zinakuwa *handled* katika hali ambayo haitakwenda mtaani. Kama alivyosema yeye kwamba vitoke kwenye makatarasi ziwekwe kwenye chupa ya lita moja, lita tano hata lita kumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri yanaridhisha sana kwa hicho kipande cha kwamba wakamwone Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu ya Rais. Hata hivyo, kuna jambo moja tu ambalo kwa sababu ya muda ukimruhusu tena akaji-*commit* basi nitamaliza hii biashara hapa hapa. Hizo gharama za kurudisha kwenye kiwanda ni nani atazishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huruma yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huruma hiyo umeipata maadam hujatoa shilingi. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu hoja ya Mheshimiwa Waziri Kivuli, hawa ni wadau wetu tunaelewana na ndiyo maana nikasema waende wakamwone Katibu Mkuu, Profesa Kamuzora watapewa *logistic* zote. Ngoja niseme zaidi, tumetoa maamuzi, kutoa bidhaa kutoka *godown* moja kwenda nyingine italindwa na ulinzi wa Polisi. Tuko *serious* na jambo hilo kuhakikisha kwamba hakuna kiroba kitaingia mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuko *serious* waende wapewe maelekezo, hatuwezi kumwaga mtama kwenye kuku wengi. Maelekezo ndiyo hayo, kuna ulinzi mkali kutoa bidhaa kutoka kwenye godown moja kuipeleka kiwandani. Pia tutasimamia vile viwanda vinavyokwenda kutoa kwenye makatarasi kuweka kwenye chupa. Hiyo dhamira ya Serikali kuhusu viroba bado iko pale pale. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba litatekelezwa na katika hili nitaomba msaada wake tusaidiane kusudi tusirudi nyuma twende mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony Komu kikanuni hapo tena tutakuwa tumetoka nje. Mheshimiwa Waziri, nadhani swali la Mheshimiwa Komu ilikuwa ni kuhusu gharama za kubadilisha kutoka kwenye kale kamfuko kuelekea kwenye chupa, nani hapo anahusika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Waziri sihusiki na mambo ya kiutendaji, nazungumza ninachokiamini na msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Ndiyo maana nikasema Katibu Mkuu anayeshughulikia anajua yote hayo na hawa wajasiriamali mnaowasema wanawasiliana na Katibu Mkuu huyo. Nimemsema *TBL* na Mheshimiwa rafiki yangu tukitoka hapa nikakuoneshe barua, nimemsema *Megatrade,* tumefikia hatua mpaka ya kuwapa *model* ya ku-*bottle* na kuwapa namna ya kuweza kuweka alama za siri za ku-*protect* hiyo vitu, hiki kitu ni *sensitive,* watu wamekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uliache kati yangu mimi na yeye ndiyo kivuli changu nitashughulikia. Gharama watazibeba wenye mzigo ule. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia zaidi suala la *TBS* kuhusu bidhaa bandia na nikasema kwamba *TBS* tunatekeleza programu ya *PVoC* ambayo tuliianzisha mwaka 2012 sasa ni miaka sita haionekani athari yake na tukayapa makampuni *SGS* wakati ule na *Intertek* wapo pamoja na *Bureau Veritas.* Sasa toka tuanze hiyo programu ya kuzuia bidhaa bandia kutoka nje zisiingie Tanzania bidhaa bandia ndiyo zimeingia kabisa. Kwa hiyo, niseme kwamba kama hoja yangu hii haikupatiwa majibu sahihi ya Serikali basi nina kusudio la kutoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokisema bidhaa bandia ambazo ni *substandard* zipo kila eneo na Mheshimiwa Waziri anajua na mnasema kwamba mmeshindwa kuzuia bidhaa bandia kuingia kwa sababu kuna vituo bandia vya bahari kama vituo 36 pamoja na mipakani. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuzuia bidhaa bandia zisiingie nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu rafiki yangu Mheshimiwa Ngwali kuhusu bidhaa bandia na bidhaa zisizokidhi viwango. Niwaombe tena Waheshimiwa Wabunge mchukue muda mkisome kile kitabu changu ambacho watu wengine wamekiita kitabu cha rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa bandia zinaingia Tanzania mojawapo ya njia zinazoingiza bidhaa hiyo ni hizi njia za panya, yako majahazi yanaingiza bidhaa hapa, watu wangu waliopo bandarini hawawezi kuziona, nitazizuiaje? Ndiyo maana aliyesimama kuchangia ni Waziri wa Mambo ya Ndani na nimemwomba atanisaidia lakini nitamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais ili ikibidi tupewe nyambizi atakayekuja na mashua na bidhaa bandia tumzamishe, niseme nini zaidi ya hapo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magendo inaingiza bidhaa humu nchini, inaua viwanda na inawaumiza na wananchi. Wanaofanya magendo Watanzania mnawajua, bidhaa zinazoshuka Tanga, Kilwa na Kunduchi mnajua zinatoka wapi. Mzee Ngwali kwa nini unanipa shida kwa tatizo ambalo unalijua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoingiza bidhaa kwa magendo ndiyo ambao wanatupa shida. Wale wanaopitia bandarini nimesema jana kwamba waliopo chini yangu wahakikishe bidhaa haipiti. Mheshimiwa Ngwali ikibidi tutakwenda wote ukakague hizo *PVoC* unazozisema China na Hongkong, siwezi kushindwa nauli ya kwenda mimi na wewe. Nakuhakikishia zikiingia humu ndani kupitia bandarini mtu anaondoka, lakini za magendo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe dakika moja, ngoja niwaambie tulikosa wawekezaji wa sukari kwa sababu sukari ilikuwa inashuka magendo hapa nchini. Tulikosa wawekezaji kwenye kilimo cha mpunga/mchele na hata

*Kilombero Plantation* alitaka kuondoka nchini kwa sababu ya kuleta mchele wa Pakistani wenye miaka 30 kwenye ma-*godown* kwa njia za magendo, tunadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza na rafiki yangu hapa amesema atanisaidia lakini nitakwenda na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa Mheshimiwa Rais, atakayeingiza atapambana na Jeshi la Wananchi. Tukizuia magendo bidhaa bandia na feki haziingii. Mheshimiwa Ngwali usiende mbali wewe ni rafiki yangu na kila mtu anakujua hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali pamoja na ahadi ya kwenda nchini China bado umesimama? *(Kicheko)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili sio la leo, ni jambo la zamani sana na Waziri anataka kutumia polisi, polisi hao ambao wamepewa dhamana kwa muda mrefu na wameshindwa kutekeleza kazi hiyo. Siyo tu bandari bubu lakini pia mipakani bidhaa bandia zinapita. Pia *TBS* wana wafanyakazi wachache kukidhi kupambana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nauliza ni mkakati gani wa Serikali ambao upo sasa kwa sababu *Bureau Veritas* na *SGS* wameshindwa kazi na bado mnaendelea wala hakuna ripoti yoyote. Nataka *commitment* ya Serikali ni mkakati gani mlionao kuzuia tatizo hili?

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi hoja hii ijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, wale wanaochangia ndiyo wabaki wamesimama sasa.

Mheshimiwa Halima Mohammed, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa

Allan Kiula, Naibu Waziri wa Mazingira, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Cosato Chumi. Tunaanza na Mheshimiwa Halima Mohamed.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali azuie shilingi. Nasema hivyo kwa sababu nina mfano hai, kuna miswaki ukiutia mdomoni mara moja tu unakatika, nafikiri mtaniunga mkono Waheshimiwa Wabunge*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri hapa alizuia simu feki lakini bado chaja zipo feki madukani, tunafanyaje Mheshimiwa Waziri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali. Mheshimiwa Waziri suala la vitu feki wala sio la kujadili, linajulikana na lipo wazi. Mheshimiwa Waziri mlitoka kutuambia humu Bungeni kwamba Usalama wa Taifa wako kila sehemu lakini leo Usalama wa Taifa wako kwenye mikutano ya hadhara inayoandaliwa na CHADEMA tu, kwenye vitu feki wewe unasema umeshindwa na unakiri hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda dukani leo unaulizwa unataka feki au *original?* Kweli hilo nalo linahitaji tutafute jeshi kutoka nje kuja kutusaidia? Mheshimiwa Waziri mtueleze ni nini dhamira ya Serikali kusitisha suala la bidhaa feki Tanzania. Mmesema habari ya simu feki, mmewaumiza wananchi, simu zimechukuliwa lakini wananchi walilipa kodi na wananunua vocha na wanaingiza pato la nchi hii kupitia simu hizo feki. Mheshimiwa Waziri tunaomba atupe majibu yanayoeleweka, Watanzania wanaumia sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwombe Mheshimiwa Ngwali rafiki yangu arejeshe shilingi kwa sababu amesema njia za panya ambazo sio rasmi. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Mwigulu aongozane na Mheshimiwa huyu amwoneshe hizo njia za panya ili tuwakamate hao watu kwa sababu watakuwa wanazuia Serikali ya Awamu hii kufanya mambo mazuri ambayo wamekusudia. Mheshimiwa Ngwali achia hiyo shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kidogo jambo hili na nimwombe Mheshimiwa Ngwali amrudishie Waziri shilingi ili aweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mchangiaji aliyepita ni kwamba amesema bidhaa bandia, sasa bidhaa bandia sote tunajua kwamba tuna *porous border*. Sisi mipaka yetu ina njia za panya nyingi sana ambazo bidhaa feki ambazo zinaingia pale. Sasa bidhaa feki hazina uhusiano na kazi ya *Bureau Veritas* kwa sababu *Bureau Veritas* na kampuni nyingine ambazo tumezikasimu kazi hiyo zinakagua na zinakuja bidhaa sahihi. Sasa hizi zinazoingia kwa njia ya panya ndiyo zinaleta matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine sisi kama Watanzania lazima tukatae kununua bidhaa feki. Kama tunanunua bidhaa feki wale ambao wanaingiza bidhaa feki wanaendelea kuingiza, lakini pia tutoe taarifa. Tunaona bidhaa feki hatutoi taarifa, mamlaka zinazohusika zitachukuaje hatua? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ngwali arudishe shilingi lakini pia Wizara husika ijipange ili kuweka mikakati zaidi kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Wizara ya Mambo ya Ndani kuweza kuzuia suala la bidhaa feki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Ngwali arudishe shilingi kwa sababu anafahamu kwamba hivi sasa tumeshaunda timu ambayo ndani yake kuna Wakuu wa Mikoa wote ambao wapo katika mwambao wa bahari na karibuni tutaenda kuunda timu inayohusisha maziwa yote makuu. Hii ni kuhakikisha kwamba tunazuia *operation* za bandari bubu. Huo mkakati tayari upo na tutahakikisha tunausimamia kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja lililotulazimisha tufanye mabadiliko makubwa katika bandari kwa maana ya Mamlaka ya Bandari ni hilo. Kwa hiyo, tumeshaanza kuchukua hatua, tumesafisha uchafu kwenye bandari na tumeweka watu sasa ambao tunaenda nao sambamba katika kuhakikisha kwamba masuala ya bandari bubu hatimaye yanakwisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naibu Waziri wa Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nimkumbushe tu Mheshimiwa Ngwali ambaye yeye alikuwa mjumbe wangu wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara wakati ule tuliyoyafanya sasa hivi amesahau. Makampuni yote dhaifu wakati ule yaliyokuwa yakishughulika na *PVoC* tulimwambia Waziri wa Viwanda na Biashara wa kipindi kile yote yaliondolewa na anajua kabisa kwamba Serikali ilichukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile anajua hatua tulizozichukua katika Kamati hiyo kwamba tuliiambia Serikali iongeze watumishi *TBS* na Serikali ilikubali ikaongeza watumishi zaidi ya 200 na yeye anajua. Leo anasema Serikali

haichukui hatua, Mheshimiwa Ahmed anayakumbuka haya na anajua kabisa kwamba Serikali inachukua hatua katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuthibitisha ni kwamba mapambano ya kuingia kwa bidhaa bandia nchini tumepambana nayo kwa kiwango kikubwa enzi hii ya Serikali ya Awamu ya Tano. Isipokuwa kinachokosekana hapa ni takwimu za kuthibitisha kwamba tumepunguza kiasi gani. Wafanyabiashara tulipokutana nao katika kikao cha pamoja majuzi ambao tuliwaita hapa, waliitwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wote walithibitisha kwamba hali sasa inaendelea vizuri kwa kupungua kwa watu hawa ambao wanaingiza bidhaa bandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la elimu, tumeimarisha sasa hivi kuhakikisha kwamba meli zote zinazotua kwenye bandari zilizoruhusiwa na bandari zisizoruhusiwa zinaonekana na tunazifanyia ukaguzi. Kwa hiyo, Watanzania wanatakiwa watu-*support,* wanapokumbana na bidhaa bandia watueleze zipo wapi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa heshima tuliyopata Watanzania kutoka kwa *Serengeti Boys,* nataka niwape taarifa tumeshinda mechi hiyo. Kwa hilo tu linamfanya Mheshimiwa Ngwali ambaye ni mchezaji mzuri sana akarudisha shilingi kwa furaha aliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba bahati nzuri watu mbalimbali wamechangia lakini *commitment* ya Serikali hasa ukiangalia hii Awamu ya Tano jinsi gani tumefanya, Mheshimiwa Mpina ameelezea suala zima la ajira kwamba kuongeza kikosi kazi kuweza kufanya kazi hiyo. Kubwa zaidi ambalo napenda kulizungumza, katika ajenda hii sasa ukiangalia *mentality* ya Watanzania imebadilika katika suala zima la uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunajipambanua katika uchumi wa viwanda, niseme kwamba Mheshimiwa Rais ametuelekeza sana katika suala zima la uzalendo na hili tulivae sisi Watanzania wote kwamba kwa sababu tunajenga viwanda na tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunapata bidhaa bora suala la elimu lazima liwe jukumu la kila mmoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ngwali kwa sababu Serikali imejenga *One Stop Border Post* na inaweka nguvu kubwa sana katika suala zima la ulinzi, inaajiri watu na Serikali imejizatiti kabisa kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unapanda, hili jambo tulivae wote na tumuachie Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana shilingi yake, lengo kubwa nchi yetu iweze kwenda mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze Mheshimiwa Ngwali kwamba shilingi anakotaka kuichukulia sio mahali pake. Zoezi la uingiaji wa bidhaa feki linasimamiwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Nami nimwambie tu wale wanaoingiza bidhaa feki wala hatuwaombi kuacha kufanya hivyo lakini tunawaambia kwamba tutapambana nao kwa nguvu zote na kuhakikisha kwamba tunatokomeza utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ni vile tu hatujaorodhesha takwimu, lakini utaweza kuona katika maeneo mengi sana tumeweza kufuta kwa kiwango kikubwa uingizwaji wa bidhaa feki. Kama ambavyo tulipata orodha bidhaa feki zilizokuwa zinakuja zilikuwa katika nyanja nyingi sana na zote hizo tumepambana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *commitment* ya Serikali ni kwamba tutapambana kuhakikisha kwamba tunadhibiti, lakini pia tunachukua hatua kwa wale ambao wataweza

kupenya na tukagundua kwamba walishapenya. Kwa namna hiyo, wenzetu wa viwanda wataweza kuinua zaidi viwanda vya bidhaa halali ambazo zinazalishwa kwetu na zina viwango ambavyo ni makini kwa matumizi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Ngwali arudishe shilingi lakini na wao ni viongozi wenzetu tusaidiane kupeana taarifa na kutoa elimu kwa wananchi wetu. Kila mtu akikataa bidhaa feki na yenyewe hiyo ni hatua kubwa ya wale ambao wameingiza bidhaa feki kutokurudia tena kuingiza bidhaa feki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bidhaa feki zinaweza kuleta athari kwa wewe mwenyewe, Mheshimiwa Mwigulu, Mwanasheria Mkuu kutokana na kununua bidhaa feki bila kujitambua, naomba jambo hili tuliamue kwa kura, nazuia shilingi yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa hapo Mheshimiwa Ngwali siyo kwamba majibu unayajua tayari? Haya, nitahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ngwali.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa Ngwali imekataliwa, kwa hiyo, shilingi ya Mheshimiwa Waziri ipo palepale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilimhoji Mheshimiwa Waziri, kwamba wananchi ambao wanapisha Mradi wa *SEZ* Bagamoyo wamesubiri kwa miaka kumi kuweza kupata fidia kwa ajili ya mali zao katika eneo hilo. Ni utaratibu wetu wa

kisheria na kisera kwamba pale ambapo Serikali inalazimika kutwaa eneo la wananchi kwa ajili ya mradi wa maendeleo, basi wananchi hao walipwe fidia zao halali kufuatana na thamani ya soko na kwa wakati. Hata hivyo, katika maeneo mengi nchini mwetu Tanzania ulipaji huu wa fidia umesuasua sana, mifano ni mingi katika mikoa mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni mkakati gani ambao upo wa kuhakikisha kwamba mateso ambayo wananchi wanayapata kwa kusubiri miaka mingi hadi kupata haki ambayo imetajwa kisheria na kisera yanaondolewa na wananchi hawa wa Bagamoyo kwenye Mradi wa *SEZ* waweze kupata fidia zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali kutwaa yale maeneo kwa ajili ya viwanda ilikuwa nzuri na bado ni nzuri. Kama anavyojua yeye, kwa sababu kiti nilichokikalia mimi leo alikuwepo yeye jana, haya maeneo yamechukuliwa miaka ya 2008 na 2010, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwalipa watu fidia na pale inapokuwa imechelewa inawalipa riba lakini kama alivyosema, ni kweli watu wanaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwenye maelezo yangu baada ya kuona kwamba watu wanaendelea kuumia kwa Bagamoyo Serikali mwezi Desemba ilikubali kwamba sekta binafsi iingie ilipe fidia dhamira ikiwa bado ni ileile ya kujenga viwanda. Maslahi ya mwananchi yatasimamiwa na Serikali, mwananchi anaishika Serikali, Serikali inatafuta watu wa kusaidiana naye kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo mengine ya nchi kwenye bajeti yangu humu nimeeleza kinagaubaga namna gani Songea, Kigoma tutaweza kufanya hivyo. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, katika vitu ambavyo vitanipa faraja ni kuona mradi wa Bagamoyo watu wanalipwa fidia. Nimesema, wale wabia wawili wa Oman na China wameshaleta *proposal* na imeshakubaliwa, wataalam wetu wameshaijibu inakwenda kwenye kikao cha Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimezungumza kwamba mwekezaji mwingine wa kwenye *industrial park* amekuja na tumeshakubaliana na Katibu Mkuu, Dkt. Meru, kwamba akija huyu mtu kile kipande kingine kinachobaki cha Bagamoyo agawiwe. Kwa hiyo, nia yetu ni njema, ni kujenga viwanda. Nawasihi wananchi tengeni maeneo, kuna sisi, wanetu na wajukuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa naona ameridhika na maelezo.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya ya Mheshimiwa Waziri na kuhisi nia yake thabiti ya kutatua mgogoro huu, basi naridhika naomba tu Serikali ijitahidi kutekeleza hili vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kabisa kukuza uchumi wa viwanda. Katika mpango huo wa Serikali wa kukuza viwanda, nafikiri kwamba Serikali na *EPZ* wangekwenda sambamba kwa maana ya kulipa fidia kwenye maeneo ya wananchi ambayo wamechukua na wanashindwa kulipa fedha ambazo wananchi wanatakiwa

wapate fidia. Kwenye eneo hili mimi nataka nipate maelezo ya kina ambayo kimsingi kama sitaridhika nayo nipo tayari kuondoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna eneo ambalo liko pale Songea Mjini katika Kata ya Mwengemshindo *EPZ* toka mwaka 2008 mpaka leo wananchi wana kilio kikubwa, hawajalipwa pesa zao takribani shilingi bilioni 2.5 ilikuwa shilingi bilioni nne wakalipa nusu na nusu bado haijalipwa, wananchi hawaelewi nini wafanye mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sekunde thelathini.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe maelezo Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye kitabu changu baada ya kuzungumza na Mheshimiwa Gama, Mbunge wa Songea na kwa kufuatilia wakati natengeneza bajeti, nimepanga pesa ya kumalizia hiyo sehemu iliyobaki. Kwa hiyo, tufanye sala tukusanye mapato, watu walipwe, mambo yawe mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ulipofikia Kanuni yetu ya 104, inataka tuingie kwenye kupitisha Mafungu yote kwa pamoja, Katibu.

**Fungu 44 – Viwanda**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* .....................Sh.11,838,840,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ................. Sh.363,889,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ....................Sh.1,043,882,000/=

Kif. 1004 – *Government Communication Unit*........................Sh.81,701,000/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* ..........................Sh.200,381,000/=
Kif. 1006 – *Legal Services Unit*...........................Sh.96,218,000/=
Kif. 1007 – *Manangement Information System* .......................Sh.259,686,000/=
Kif. 1008 – *Procurement Mgnt Unit* ................Sh.181,304,000/=
Kif. 2001 – *Industry* .....................................Sh.5,078,406,000/=
Kif. 2002 – *Small and Medium Enterprises Division* ....................Sh.5,028,186,000/=
Kif. 3001 – *Commerce* ................................................Sh.0/=
Kif. 4002 – *Commodity Market Development*................Sh.0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji**

Kif. 3001 – *Commerce Division* .......................Sh.991,528,000/=
Kif. 3002 – *Investment Division* ......................Sh.1,603,730,000/=
Kif. 4002 – *Commodity Market Development Division* ..............Sh.15,256,981,750/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 44 – Viwanda**

Kif. 1003 – *Policy and Planning*................. Sh. 71,460,377,000/=
Kif. 2001 – *Industry*......................................Sh.2,380,000,000/=
Kif. 2002 – *Small and Medium Enterprises Division*......................................Sh. 0/=
Kif. 4002 – *Commodity Market Development*...............Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji**

Kif. 4002 – *Commodity Market Development Division*................Sh.6,350,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Bunge kupitisha bajeti yake na wataalam wake wako hapa, tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa yale mliyoyaahidi mwaka huu maana mwakani tutakutana tena hapa na vitabu vitakuwa vitatu vya kuvitazama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mawili kabla sijamruhusu Mheshimiwa Bobali. Tangazo la Kwanza linahusu kikao cha Wabunge wa CCM ambacho kitaanza mara baada ya kumaliza kikao hiki. Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM wanatakiwa kuelekea *White House* na tangazo linatoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kwamba leo kulikuwa na mechi kati ya *Serengeti Boys* na Angola na *Serengeti Boys* imeshida goli mbili na Angola wamepata goli moja. Kwa hiyo, vijana wetu wanafanya vizuri, tuendelee kuwa pamoja nao kwa hali na mali ili waweze kufika mbali zaidi kama ambavyo tumefurahi leo. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Nitaruhusu Mwongozo mmoja kutoka kwa Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuomba Mwongozo wako nikitumia Kanuni ya 68(7) pamoja na Kanuni ya 101 ya Kanuni zetu za Kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mfupi uliopita tulikuwa tunapitisha bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara

na Uwekezaji lakini tumepitisha mafungu kwa mfumo wa kupitisha kwa pamoja *(guillotine).* Mfumo huu umekuwa ukitumika katika Wizara nyingi kama siyo zote zilizopita, jambo ambalo linatunyima fursa Wabunge kuitendea haki hotuba hii. Mimi binafsi nimeipitia, hotuba hii ni nzuri na ina mambo mazuri lakini kuna mambo tulihitaji tupate ufafanuzi kwa kupitia kifungu kwa kifungu badala ya kupitisha vyote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa itakavyokupendeza, naomba Mwongozo wako, kwa nini tusiwe tunachukua ama wawili kutoka kwenye upande wa *Ruling Party* na huku mmoja katika mshahara wa Waziri ili tuweze ku-*balance,* tupate watu watatu tuache kujadili bajeti za mambo mengine kwamba mtu anakuja na sera yake na jambo lake, tujadili hotuba na vifungu vilivyopo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni hizo ambazo nimezisoma. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na Mheshimiwa Bobali. Maelezo ya Mheshimiwa Bobali wote tumeyasikia, yanahusu utaratibu wetu wa kupitisha Mafungu kwa pamoja kwa mujibu wa Kanuni ya 104. Mheshimiwa Bobali anaona utaratibu huu unawafanya Waheshimiwa Wabunge washindwe kupitia mafungu mengine baada ya kuwa muda wote unaishia kwenye mshahara wa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, hizi Kanuni zetu uzuri wake zinazungumza kuhusu kila jambo. Ni sisi wenyewe ndiyo tunaoamua namna tunavyotaka kufanya. Mwongozo huu uliwahi kuombwa na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi na maelezo yaliyotoka wakati huo ndiyo yatakayotoka sasa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 101, Kanuni ya 103 na Kanuni ya 104, ukizisoma hizi kwa pamoja, hasa Kanuni

ya 103 ndiyo inayozungumzia kuhusu kushika shilingi. Sasa, Bunge limeamua kuwa na utaratibu huo, si Bunge kama taasisi, kwa maana ya Wabunge wameamua kuwa na utaratibu huo ama niseme tumeamua kuwa na utaratibu huo, kila mtu anataka kushika shilingi na kila mtu anataka kuchangia hoja ya mtu anayetaka kushika shilingi.

Kwa hiyo, kama tunataka kuyapitia Mafungu yote, tuache kushika shilingi ambayo haishikiki kwa sababu kuna Mbunge anasimama tu hapa anataka kushika shilingi lakini hata jirani yake pale hajazungumza naye kwamba anataka kushika shilingi ili amuunge mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, huu utaratibu tumejitengenezea wenyewe na kwa kuwa tumetengeneza wenyewe na hizi Kanuni ni za kwetu wenyewe basi matumizi yake sisi tuangalie tunataka kuangalia ipi, kama mshahara wa Waziri ndiyo ambao tunaupenda sana basi ni Kanuni ya 103 ndiyo inayotufanya tukae muda wote tukijadili kifungu kimoja. Kama tunaona tunataka kuangalia mafungu mengine, matumizi ya kifungu cha 103 tuyapunguze.

Kwa hiyo, ni sisi wenyewe kwa kweli tunaoamua namna ya kufanya na nadhani Bunge hili limeamua huo pengine ndiyo utaratibu, lakini bajeti ya mwaka jana si kila bajeti ilikuwa inapita kwa utaratibu huu, ilikuwa inapitiwa vifungu lakini safari hii tumeamua kutumia Kanuni yetu ya 103 nayo ipo humu. Kwa hiyo, huwezi kuwazuia watu wanaotaka kushika shilingi kwa sababu na yenyewe ni Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, lakini sasa wapo Wabunge wanaotoa hoja kana kwamba tunaweza kwenda zaidi ya huo muda wa nusu saa ambao Mwenyekiti amepewa mamlaka akiwa kwenye Kamati ya Matumizi kama muda uliosalia haukutosha anaongeza nusu saa. Kanuni yetu ya 104, haitoi fursa hiyo ya kuongeza muda zaidi ya nusu saa. Kwa hiyo, ndiyo utaratibu ambao tumejiwekea.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bobali ametoa hapo na pendekezo kwamba kwa nini uwiano usiende hivi. Sasa uwiano ni namba, kwa hiyo ni sisi wenyewe Wabunge tuambizane, mtu anaposimama kushika shilingi kama haishikiki msiunge mkono kaeni ili hoja yake ife tuendelee na hoja nyingine. Tukisimama maana yake ni sisi wenyewe ambao tunaamua kutumia muda wetu kwenye Kanuni ya 103 badala ya Kanuni nyingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, tarehe 19, Mei, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.18 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 19 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*